

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Sita - Tarehe 12 Mei, 2014**

(Mkutano Ulianiza Saa tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ninataka kuwaambia kwamba tunapowasilisha mezani hizo Documentni lazima ziwepo. Kambi ya Upinzani hakuna document zinazohusika. Kwa hiyo, mnapowasilisha on the table ni vizuri zikawepo, ndicho hasa tunachowasilisha siyo maneno tu.

Tunaendelea, Katibu.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye Maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, atauliza swali hilo.

Na. 33

### Upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. SELEMANI S. JAFO)** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la upungufu wa walimu wa shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kisarawe:-

- (a) Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la Walimu Wilayani Kisarawe?
- (b) Je, Mpango wa posho ya Mazingira Magumu kwa Walimu Wilayani Kisarawe utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwaajiri na kuwapanga Walimu wapya katika shule za Msingi na Sekondari nchini kila mwaka kadiri wanavyohitimu na kulingana na uwiano wa mahitaji ya Walimu katika Halmashauri.

Katika ajira mpya ya mwaka 2014, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe wameripoti Walimu 341 wakiwemo walimu wa Shule za Msingi 178 na Walimu wa shule za Sekondari 163 hivyo kutosheleza mahitaji ya Walimu 780 wa shule za msingi huku shule za Sekondari zikiwa na upungufu wa Walimu wa Sayansi 82. Kwa hali hii, ifikapo mwaka 2017 Serikali itamaliza upungufu wa Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kukabiliana na changamoto zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu nchini kwa kuyaboresha ili kupunguza ugumu wa maeneo hayo badala ya kutoa posho pekee. Katika kutekeleza azma hii mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga shilingi bilioni 20

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi katika Halmashauri 40 zilizobainishwa kuwa na mazingira magumu.

Halmashauri ya Wilaya a Kisarawe ilitengewa milioni mia tano na tayari imeshapokea shilingi milioni mia mbili ambazo zimeweza kujenga nyumba za walimu 19 na kukamilishwa ikiwemo shule za Gongoni, Maneromango, Masaki, Masimba, Kanga na Visegeze.

Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu kupitia program ya mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari (MMEM na MMES) na kupitia ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGCDG).

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kama ambavyo mwenyewe ameeleza kwamba kuna tatizo la Walimu wa Sayansi wanaokaribia 82 Wilaya ya Kisarawe na kwa kweli tatizo hili ni karibu Tanzania nzima. Tuna matatizo makubwa ya Walimu wa Sayansi kwenye shule za Msingi na Sekondari.

Je, Naibu Waziri anaweza kuwambia Watanzania kupitia Bunge hili wamejipangaje ili kumaliza tatizo hili la Walimu wa Sayansi kwenye shule zetu?

Pili, kama ambavyo nimetoa shukurani kwa Naibu Waziri natoa pia shukrani kwa Serikali kwa namna ambavyo wamejaribu kupunguza tatizo la Walimu mwaka huu. Tandahimba katika walimu 374 waliopaswa kuripoti wamesharipoti na hivi sasa ninavyosema ni asilimia 95 ya walimu wote, lakini kuna tatizo kubwa, Asilimia 40 tu ya walimu hao ndiyo wamepata mshahara na kwa sasa wana madeni makubwa wamekuwa wakiishi kwa shida, wananyemelea maisha.

Serikali imeweka utaratibu gani wa kuhakikisha mwezi huu wa tano pamoja na mshahara wa mwezi wa tano na arears zao ili wasiendelee kupata shida na kudaiwa kwa wananchi wale ambayo tayati wamekuwa wakiwasaidia hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, tumejipanga vipi kuendelea kupunguza tatizo la Walimu wa Sayansi.

Kwa sasa tunao mkakati ambao pia unasihamiwa na Wizara ya Elimu kuanzia mwaka huu wa masomo, wale wote watakaoijiunga na kozi za Ualimu kuanzia ngazi ya Stashahada wenye daraja la kwanza watapatiwa rusuku na daraja la pili na la tatu watapatiwa mikopo ili kwenda kusoma masomo ya Sayansi ili kupata idadi ya walimu wengi. Hii ilikuwa ni motisha ya wale wote ambao wataenda kusoma masomo ya Sayansi.

Lakini kama haitoshi, Serikali inao mpango thabitibni ambao utakuja kuelezwa vizuri zaidi na Wizara ya Elimu watakapokuja kuwasilisha Bajeti yao ule wa kurudisha Sub Comb ile ya miaka mitatu kwa Walimu wa Cheti ili kuondoka wakiwa wakiwa wamepata Diploma lakini hasa wanalengwa Walimu wa Masomo ya Sayansi.

Tatu, kuanzia mwaka huu pia wa masomo ya mafunzo rekebishi yanarudishwa kwa ajili ya Walimu wa Shule za Msingi watakaomiliza masomo ya Cheti nao pia ni wale ambao wamesoma masomo ya Sayansi kwa ajili ya masomo ya Sayansi ili kuongeza idadi ya masomo ya Sayansi kwa kujengea msingi kutoka Elimu ya Msingi na kule Sekondari kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka huu kati ya ajira hii ambayo tumeitoa Walimu 36,071 ni walimu 2173 pekee wa Sayansi ambao kwa kweli mgawo wake hautoshelezi ndiyo kwa sababu tuna upungufu mkubwa wa Walimu wa Sayansi. Hivyo huo ndiyo mpango ambao tunao wa kupata walimu wengi wa masomo ya Sayansi na ambayo pia yatasaidia kupeleka kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la mishahara, nilifanua juzi hapa wakati nawasilisha Bajeti ya Waziri Mkuu na nilisema hili litaweza kuwafanya wale wote wapate taarifa kwamba kuchelewa kupata mshahara kwa Walimu wapya una sababu nyingi, lakini chache ni kwamba moja Walimu hawa wanaokwenda kuripoti ni lazima waripoti kati ya tarehe moja na kumi ili kuwezesha mfumo wetu wa TAMISEMI kuwasiliana na Utumishi na Hazina ili ku-effect malipo ukamilike.

Kwa hiyo, wengi ambao hawajapata mshahara ni katika kundi la watu walioripoti kuanzia tarehe kumi na kuendelea. Lakini nilikiri kwamba wako walimu wameripoti ndani ya tarehe hiyo, lakini ni lazima waje na vyeti

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

vilivyothibitishwa na halisi vyenye masomo yao yenye majina ya mtiririko ambapo sisi TAMISEMI tukiingiza kwenye mtandao Utumishi waweze kukiri na kuridhia kwamba hawa ndiyo wenyewe, lakini pia ndiyo watakaota kibali Hazina waweze kulipa.

Tatu, Walimu hawa, ni kweli wengine hawakuingia kwenye mtandao kutokana na uwingi wa Walimu ambao tumewajiri na kwamba kila Halmashauri ina scramble kuingia kwenye mtandao ili waweze kuingia kwenye mishahara.

Jambo hili limeleta ugumu kidogo kupitia mtandao wetu. Lakini nataka niwahakikishie kwamba mwezi huu watapata mishahara yao. Tumetumia utaratibu gani ni kwamba tumeziagiza Halmashauri watafute popote namna ya kuwawezesha walimu wale angalau waweze kuendelea kuishi badala ya kuwaacha wakiwa hawana fedha, jambo hili tumeanza kupata mrejesho kutoka kwenye Halmashaurio zetu kwamba wanaendelea vizuri.

Kwa hiyo, kama kuna Halmashauri ambayo bado hawajatafuta namna ya kuwawezesha walimu wetu kupata namna ya kujikimu waendelee kutumia vyanzo vingine ili kuwawezesha walimu hawa wapate kuishi kwenye maeneo hayo badala ya kuwaacha wakiwa wanahangaika. (Makofij)

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri akimjibu Mheshimiwa Jafo amezungumzia nguvu za Serikali katika kujenga nyumba za Walimu. Lakini Serikali imetoa pesa nyingi tatizo ni kwamba ukija kuangalia nyumba zinazojengwa ni gharama kubwa lakini haina tija.

Kwanini Serikali isiwe inawahuisha wananchi wa sehemu husika kusudi nguvu za wananchi na pesa ambayo Serikali inatoa kwa kuwashirikisha wananchi waweze kujenga nyumba nyingi badala ya pesa nyingi kujenga nyumba ndogo. Muige mfano waAfrican Barrick - Tulawaka ambao kwa kushirikiana na wananchi wamejenga nyumba nyingi Kagera kwa kutumia pesa nyingi na nyumba nyingi zaidi kuliko tunavyofanya sisi Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi tunatumia muda mwangi mno.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa fedha hizi ambazo tumezipeleka kwa Halmashauri ili ziweze kujenga nyumba kwenye shule ambazo zina upungufu. Utaratibu wa usimamizi, utafutaji wa mkandarasi ni wa Halmashauri yenyewe.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, hivyo, kila Halmashauri inao uwezo wa kujenga nyumba hizo kutokana na gharama za materials za ujenzi kulingana na eneo walilomo. Hakuna masharti ambayo yamewekwa na TAMISEMI kwamba nyumba hizo ni lazima zijengwe kwa milioni 40 na kujenga nyumba chache.

Kwa hivyo, ni Halmashauri yenyewe, Wahandisi, na kuwashirikisha Madiwani kwenye Baraza lao na wananchi kule chini wanaweza kujenga nyumba nyingi. Halmashauri nyingine wameanza kufanya hivyo. Kule nyumbani Karagwe wafanye hivyo. (Makofii)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mashishanga.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, tayari nimeshapata jibu kwa sababu nilikuwa nauliza uhaba wa Walimu wa Sayansi. Ahsante sana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa swalii la msingi linahusu upungufu wa Walimu na ni wazi kwamba pamoja na ajira ambazo zimesemwa, bado kuna utata mkubwa sana kwa Walimu waliomaliza mafunzo yao hawajapata ajira na baada ya kuongea na Wizara husika walisema kwamba tatizo kubwa ni kwamba Wakuu wa Vyuo hawakupeleka majina ya wahitimu.

Mheshimiwa Spika, swalii langu ni kwamba, Je, wanafuata mahitaji kutokana na Wakuu wa Vyuo au ni kutokana na selection. Hawa ambao bado hawajaajiriwa, Chuo cha Ualimu St. Mary's Tabata hakuna hata mmoja ameajiriwa.

Je, hawa Walimu ambao bado wapo majumbani ni lini watapata ajira zao hasa ikizingatiwa kwamba kuna tatizo kubwa sana la upungufu wa Walimu Tanzania nzima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi tumetumia dakika zaidi ya kumi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, juu ya jambo hili naomba pia tuelewane kwamba sasa hivi zipo kozi nyingi za education zinasomwa kwenye vyuo vyetu vyaa elimu ya juu. Mahitaji yetu sisi ni Walimu ambao watakuwa wamesomea kozi zenye masomo ya kufundishia madarasani.

Kwa hiyo, idadi kubwa ya vijana ambao sasa wanalamika kutopata ajira ni wale ambao wamesoma kozi ya education with psychology ambako ukienda sekondari huwezi kufundisha saikolojia. Lakini pia kwa eneo ambalo umeliuliza ni kwamba mfumo uliopo ni Wizara ya Elimu inafundisha vijana hawa kozi za ualimu baada ya kumaliza kozi zao wale ambao wamefaulu sasa ndiyo

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanatuletea majina yao kwamba hawa wamemaliza masomo yao na sisi tuliomba kibali cha walimu 36,071.

Kwa hiyo, vigezo vya masomo waliyosomea, kama ana *teaching subject* lakini pia na idadi ya kutosheleza idadi ambayo tunaihitaji ndiyo vigezo vikubwa viliviyotumika, wale wote ambao hawajaajiriwa tumeendelea na ofisi Utumishi kuomba kibali cha nyongeza ili pia tuweze kuwaajiri ikiwemo na ucheleweshaji wa utoaji majina kutoka chuoni na kutoa ripoti kwa Wizara ya Elimu kwamba wamefaulu, Wizara ya Elimu inatuletea hawa ndiyo ambao wamefaulu wanafaa kuajiriwa na sisi tunawaajiri.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo utaratibu ambao tunautumia.

Na. 34

### **Wataalam wa Sheria za Ardhi Kupelekwa Katika Kata**

**MHE. CLARA D. MWATUKA** aliuliza:-

Waendesha Mabaraza ya Ardhi kwenye Kata hawana elimu ya uendeshaji wa kesi za Ardhi na kupelekea vitendo vya rushwa kuongezeka.

Je, kwa nini Serikali haiweki Wataalam wa Sheria za Ardhi kwenye Kata ili kuepusha ukiukwaji wa utoaji haki?

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Kata yameanzishwa na Sheria ya Mabaraza ya Kata yaani *The Ward Tribunal Acts Sura Na. 206 ya Toleo la 2002*. Madhumuni ya Mabaraza ya Kata ni kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu, yaani *to secure peace and harmony* katika maeneo yaliyoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia madhumuni ya kuanzishwa kwa Mabaraza haya na majukumu ya Baraza Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria hii na kuelekeza aina ya watu wanaoweza kuwa Wajumbe na wale ambao hawatakiwi kuwa Wajumbe. Kwa mujibu wa kifungu cha 5 kifungu (1) cha Sheria hii, wafuatao hawatakiwi kuwa Wajumbe wa Baraza la Kata. Wabunge,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wajumbe wa Halmashauri za Kijiji na Kamati za Kata, Watumishi wa umma, Wanasheria, Watumishi wa Mahakama na watu ambao siyo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Bunge wataalam wa Sheria za Ardhi ambao wengi wao ni Wanasheria hawaruhusiwi kuwa Wajumbe kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata yaliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Mabaraza ya Kata ulivyo sasa ni utekelezaji wa matakwa ya Sheria. Aidha hakuna tafiti iliyofanywa na ambayo imebainisha uhusiano kati ya elimu ndogo na vitendo vya rushwa. Kimsingi tatizo la rushwa ni tartizo linalohusu maadili na uadilifu wa mtu zaidi kuliko kiwango chake cha elimu.

Mheshimiwa Spika, endapo Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba kuna haja ya kutafakari upya Sheria hii basi anaweza akatumia taratibu zilizowekwa kwa kufanya jambo hilo. (Makofij)

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini napenda kusikitika tu kwamba mimi hayakuniingia kwamba nilichouiza nilitegemea kwamba majibu yangu nitapata kulingana na swali lile.

Nasema hivyo sababu gani, sasa ukiangalia hao waliopo hao pamoja na utaratibu kwamba wameorodheshwa watu wasiotakiwa hapa. Naona wasiotakiwa hapa ambalo linashikiliwa hilo labda niseme tu wa vyama vya upinazani. Lakini waliopo baadhi yao ni Wajumbe wa Serikali za Vijiji. (Makofij)

Viongozi wengine wapo kwenye Mabaraza hayo. Sasa sijui kama kuna chombo ambacho kinafuatilia kuhakikisha kwamba utaratibu huo unafuatwa. Sehemu ya pili, kulingana na hali hiyo hapa amesema kwamba nia ni kujenga amanii na utulivu katika maeneo yale yaliyoanzishwa.

Kwa kweli ndiyo hapo ambapo nasema sikubaliani nayo. Kwa sababu gani utakuta Mabaraza haya yanajenga chuki, uhasama yaani watu ni kugombana. Anayepata haki kwenye Baraza hizi ni yule mwenye pesa.

Hata kama imeonekana wazi kabisa kwamba huyu mdai ana haki ya kupata haki yake. Lakini kama hana pesa hapati. Sasa je, amani na utulivu ndiyo inapatikana kwa mtindo huu? Serikali inasemaje juu ya hili. Ahsante sana. (Makofij)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Spika, mimi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

naomba nieleze hapa wala mimi hata sijajiliza hivi Mheshimiwa Mwatuka anatoka kwenye Chama gani, ndiyo nasikia hapa sasa hivi. Mimi hapa ninachojibu hapa najibu Sheria na Waziri wangu anafahamu mimi hapa nime-spend about six hours ninatafuta majibu haya. Jana yote nilikuwa nahangaika nayo. Mimi hapa na-quote Sheria ya nchi inavyosema. Kama ina mapungufu hiki ni kitu kingine.

Kama ina mapungufu hiyo ni habari nyininge. *The bottom line is hii Sheria nilioi-quote* hapa ndivyo inavyosema. Mbunge ukitaka kuwa wewe Mjumbe wa ile Baraza huruhusiwi. Diwani akitaka kuwa Mjumbe wa ile Baraza haruhusiwi. Kama una digrii ya Sheria huruhusiwi. Ndivyo inavyosema hii *simple and clear* ndicho ninachokisema hapa. Lakini analolisema hapa anzangumza juu ya habari ya posho zinazotolewa hapa, correct kabisa *Member of Parliament* anasema jambo la msingi.

Wakati tulipokuwa na Mabaraza haya way back kwenye mwaka 1985 Mheshimiwa wakati inakuja kitu kinachoitwa *International Monetary Fund* wakati walipokuja kuleta habari astactoral adjustment program ndiyo walifuta hiyo ruzuku, ikafutwa maana ana-address serious na mimi basi tuwe serious tueleze vizuri. Ikafutwa hiyo na posho ile ikawa haipo na utaratibu haupo. Kilichopokea kazi hiyo, ni Halmashauri kupitia katika *Ward Development Committee*, wao ndiyo wakawaambia kwamba nyinyi ndiyo mtakaotenga hizo hela.

Mheshimiwa anachosema pale ni jambo la msingi sana. Fedha zinazolipwa wale wazee pale ni fedha zinazotokana na zile tozo (*fine*) zinazotolewa pale. Ndicho anachokisema, sasa kama mimi nikienda pale nikalipa laki tano pale *definitely* pale majibu yatakayotoka pale, ndiyo upungufu anaouona katika jambo hili na sisi tunakiri kwamba hilo ni tatizo.

Kwa maneno mengine tulichoagiza tumesema Halmashauri zetu kupitia mapato yake ya ndani ndiyo zitenge hizo na vikao vile viendeshwe kwa msingi kwa hela zinazotokana ya ndani ya Halmashauri na siyo hela zinazopelekwa pale na watuhumiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu huo na mimi nakiri kwamba uko. Lakini mimi hapa nime-quote Sheria na huo ndiyo utaratibu unaotumika ili haki iweze kutendeka hapa lazima Kata zetu na Halmashauri zitenge hela zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo. (*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna mapungufu makubwa katika uendeshaji wa Mabaraza haya hususan uwezeshaji wa kielimu kwa wale watu. Je, Serikali sasa hivi haioni umuhimu wa kuendesha Semina Elekezi na Semina za mafunzo ili kuongeza uwezo wa Wajumbe wa Mabaraza haya ili waweze kuwatumikia wananchi wanaopeleka masuala yao katika Mabaraza hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hii ya kutoa elimu na kutoa Semina, elimu ni afya. Ukipata elimu hivi ukiwa na elimu hivi, si kitu kizuri?

Kwa hiyo, kama kuna haja ya kuwaelimisha watu wetu waweze kufahamu ili hili jambo walielewe vizuri ili tuweze kujua jinsi ya kuendesha haya Mabaraza. Mabaraza haya kwa kifupi Mheshimiwa Spika, kwa kifupi kabisa, yanatakiwa yaendeshwe na watu kawaida kabisa tu. Siyo watu wenye sophistication na madigri makubwa.

Ukimchukua mtu mwenye digrii ukampeleka kwenye haya Mabaraza haya anakwenda pale anamkuta Mwenyekiti pale wa lile Baraza atakuwa ana-influence maamuzi pale.

Kwa hiyo, lakini kutoa elimu watu wakajua. Hii ni sawa sawa na zile gachacha za kule Rwanda, wa-reconcile wakae waelewane pale. Wakimaliza kama ni *fine* pale ni kutoa debe la mbege, kutoa kambuzi kanachinjwa pale. Wanashikana mikono wanaridhiana, wanaelewana, wanaondoka wanakwenda.

Kwa hiyo, elimu hiyo kama itatolewa Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri ili tuweze kueleweshana kuhusu majukumu ya haya Mabaraza. (Makofii)

Na. 35

### **Ukarabati wa Maktaba ya Mkoa – Mara**

**MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y. VINCENT J. NYERERE)** aliuliza:-

Maktaba nyingi ambazo ni za zamani zinahitaji ukarabati kutokana na uchakavu wa majenfgo na samani:-

Je, Serikali itakarabati lini maktaba hizo hususani Maktaba ya Mkoa wa Mara, iliyopo Musoma Mjiji?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA) inaendesha shughuli za maktaba katika mikoa 22 Wilaya 19 na Tarafa mbili. Majengo mengi ya maktaba hizo yalijengwa miaka ya 1960 na 1970 na Serikali na mengine kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA). Hali ya baadhi ya majengo ya maktaba hizo kwa ujumla siyo nzuri na hayaendani na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Maktaba ya Mkoa wa Mara ilitengewa jumla ya shilingi milioni 33,508,274/= kwa ajili ya ukarabati wa awamu ya kwanza. Ukarabati huu ulihusisha kuanza uboreshaji wa paa awamu ya kwanza, kubadilisha dali yaani ceiling board na kupaka rangi jengo lote nje na ndani.

Pamoja na ukarabati wa milango na madirisha na kubadilisha baadhi ya nyaya kwenye mfumo wa umeme na kuweka taa mpya jengo lote.

Awamu ya pili itagharimu shilling milioni 10,342,200/= kazi zinazotakiwa kufanyika ni pamoja na kumalizia kazi ya uimarishaji wa paa. Aidha Serikali katika mwaka wa fedha 2013/2014 ilitenga jumla ya shilingi milioni 100 za kuanza ukarabati maktaba kadhaa kongwe nchini na kazi imeanza katika maktaba ya Mkoa wa Mtwara.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa taarifa nilizo nazo ni kwamba kasi ya ukarabati wa hii maktaba ni ndogo na katika swali la msingi la Mheshimiwa Vincent Nyerere maktaba ya Mara ameitaja kama maktaba mahususi. Lakini swali lake la msingi linahusu maktaba nyingi nchini na ameuliza ni lini.

Sasa katika jibu Mheshimiwa Spika, inaonyesha kwa maktaba ya Mara pekee milioni 43 zimetumika kwa ujumla na pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya maktaba nyingine ni milioni 100 peke yake. Maana yake ni kwamba kwa hizi maktaba nyingi ambazo ni mbovu itachukua miaka mingi sanampaka kukamilika kama kasi hii ikiwa ndogo namna hii. Sasa ningepena Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze orodha ya maktaba nyingine ambazo ziko kwenye matengenezo na lini hasa zitatengenezwa kwa kasi hii ilivyo ndogo ni lini hasa hizi nyingine zitatengenezwa. Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, kwa sababu ya kasi ndogo ya matengenezo ya hizi maktaba na kwa sababu ya uchache wa maktaba ziko kwenye ngazi ya Mkoa tu 22 na 19 kwenye Wilaya. Kwa hiyo Wilaya nyingi hazina maktaba na kuna matatizo ya maktaba hapa nchini.

Ni kwa nini sasa ili kuhakikisha matokeo yanakuwa makubwa kwa haraka Bodi hii ya huduma za maktaba isiweke mfumo vile vile wa kutumia maktaba za mzunguko kwa maana ya *mobile libraries* ili ziweze kufika kwa haraka katika maeneo na taasisi ambazo zinahitaji huduma za maktaba ikiwemo taasisi za elimu na hata katika jumuiya mbalimbali? Ningombwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanzza kabisa naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge nchi yetu ya Tanzania ni kati ya nchi chache sana katika Bara la Afrika na Ulimwenguni zenye mfumo wa maktaba kama tulionao sasa katika nchi yetu na kwa taarifa ya nchi yetu sasa hivi inatimiza miaka 50 toka mfumo huu nzuri wa maktaba umeanzishwa katika nchi yetu ya Tanzania na katika nchi nyingine haupo.

Lakini nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika swali lake la kwanza anasema speed ya ukarabati katika maktaba nilioitaja ni ndogo. Lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge asilimia kubwa asilimia 70 ya ukarabati wa maktaba hiyo imeshakamilika na mimi mwenyewe nimewasiliana na wahusika wa maktaba hiyo na nina mpango wa kwenda pia kuangalia ubora wa ukarabati uliofanyika ili niweze kusimamia ukarabati unaoendelea katika maktaba nyingine.

Lakini swali la pili anasema kwa nini mfumo wa *mobile libraries* usitumike katika nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Spika, wazo hili ni jema sana sana na sisi kama Serikali tutalichukua na kuangalia tunalifanyiaje kazi ili kuweza kuboresha tu huduma za maktaba nchini.

Lakini hata hivyo, Serikali haijalala usingizi Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita tumanza kukarabati maktaba hiyo tulioisema lakini tumeanza kukarabati pia maktaba ya mkoa wa Mtwara na mwaka huu wa fedha tumetenga fedha nyingine tena za kuendelea na ukarabati. Lakini Serikali inaendelea na mpango wa kujenga tena maktaba nyingine katika Mikoa mipyä katika nchi yetu ya Tanzania.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba niwahakikishie Serikali iko makini na inafahamu umuhimu wa maktaba na inafanya kazi kwa kiasi cha kutosha suala hilo. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea tuangalie kama inaendelea kukarabatiwa. Twende Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Desderius Mipata.

Na. 36

**Kuvipatia mawasiliano ya uhakika vijiji vya Kata za Kate na Isale**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Vijiji vya Kate, Nkata, Ntemba, China, Chalatila na Nchenje vya Kata ya Kate na vijiji vya Ntuchi, Msilihofu na Ifungwa, Kata ya Isale havina mawasiliano ya k uaminika ya simu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia mawasiliano ya uhakika vijiji hivi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi la kuainisha maeneo mbalimbali kwa kuangalia idadi ya wakazi, ukubwa wa Kata, kiwango cha mawasiliano na ruzuku inayohitajika vijiji vya Kate, Nkata, Ntemba, China, Chalatila, Nchenje, vya Kata ya Kate na vijiji vya Ntuchi, Msilihofu na Ifundwa vya Kata ya Isale vimejumuishwa katika orodha inayoandalishiwa kwa ajili ya zabuni ya awali ya pili ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kupitishwa kwa mfuko wa mawasiliano kwa wote Kata ya Wampembe na Namanyere katika Wilaya ya Nkasi zimepata mzabuni yaani Vodacom, katika miradi ya awamu ya kwana (a) na (b) sawia ambapo kabla ya mwisho wa mwezi Novemba, 2014 vitakuwa vimepata minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaendelea kuwahimiza watoa huduma za mawasiliano kupeleka huduma za mawasiliano ya simu ya viganjani maeneo yote yenye shida za

mawasiliano yakiwemo maeneo ya vijiji vya Kata za Kate na Isale. Wakati mwingine ucheleweshaji wa kufikisha huduma unasababishwa na mambo mambo mbalimbali yakiwamo ukosefu wa miundombinu muhimu kama barabara na umeme na ukosefu wa fedha kufadhili miradi yote kwa wakarti mmoja. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa majibu mazuri ya Serikali. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Serikali katika awamu yake ya kwanza wametuahidi Wabunge hapa kwamba watapeleka maeneo mbalimbali mawasiliano ya simu ikiwemo maeneo ya Wampembe, Kate na Ninde.

Lakini mpaka sasa kufuatana na majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha ni Wampembe peke yake ndiyo itakayonufaika na nashukuru pia. Lakini nataka kuuliza Kata ya Kala na Kata ya Ninde kuna mpango gani wa haraka na uhakika wa kupata mawasiliano katika Kata hizi? (Makofii)

Swali la pili, kutokana na jinsi nilivyofanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye Wizara hii nimejifunza kwamba kukwama kupeleka mawasiliano sehemu mbalimbali nchini hakujatokana na uzembe wa Wizara badala yake ni mfumo uliopo sasa amba Serikali inategemea wafanya biashara ndiyo wapeleke mawasiliano katika maeneo mbalimbali. Mfumo huu haufai.

Je, kupitia Bajeti hii Serikali imetenga kiasi chochote cha fedha ili kuondoa changamoto ambayo imekuwa ikitabiliwa nayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, anataka kujua mpango wa kupeleka mawasiliano Kata za Mkala na Ninde kwa mpango wa haraka. Mheshimiwa Spika, kwanza mimi ningeomba hata Mheshimiwa Mbunge ashukuru hata kwa jitihada ambazo Serikali imefanya katika kuhakikisha kwamba jimbo lake linapata au Wilaya yote ya Nkasi kwa ujumla inapata mawasiliano kwa sehemu kubwa sana kama tulivyoeleza kwenye majibu yetu ya msingi.

Sasa kupeleka mawasiliano yaharaka kwa maana ya Kata za Mkala na Minde kwa mpango wa haraka hiyo Mheshimiwa Mbunge hatuwezi kuahidi kwa sababu mpaka sasa tumeshafanya jitihada za kutosha sana. Lakini kwa mwaka mwingine baada ya kukamilika kwa awamu hii ambayo tunamwahidi kwamba Mheshimiwa tutakamilisha hayo, basi tutakuwa na mpango sasa kwa ajili ya maeneo mengine yote ambayo yatakuwa yamebaki.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa anasema mfumo wa kutegemea wafanya biashara kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo haufai.

Lakini Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba kwanza siyo kazi ya Serikali kwa maana hiyo, moja kwa moja kutenga pesa kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika maeneo mbalimbali baada ya Serikali kupata maswali ya Waheshimiwa Wabunge tunawasiliana na makampuni ya simu, tunawaeleza umuhimu na wenyewe wanakwenda kuangalia maeneo haya kama kuna umuhimu wa kupeleka mawasiliano ya simu na ndiyo makampuni hayo kama ulivyoona katika swali la msingi makampuni ya Vodacom na Tigo yameitikia kwa sehemu kubwa sana.

Lakini pia tunajua pia tulishaanzisha mfuko wa mawasiliano hapa kwa maana ya UCAF ambao utasaidia kupeleka mawasiliano ya simu katika yale maeneo ambayo hayana tija sana kwa makampuni ya simu. Lakini hata hivyo Mheshimiwa Spika, na mfuko wenyewe huo pia haupati ambao itasaidia kupeleka mawasiliano ya simu katika yale maeneo ambayo hayana tija sana kwa makampuni ya simu.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo na mfuko wenyewe huo pia, haupati pesa za kutosha kupeleka mawasiliano katika maeneo yote kwa wakati mmoja. Lakini nataka tu niseme kwamba, ni mpango wa Serikali kwa kushirikiana na Makampuni haya na Mfuko kuhakikisha kwamba, maeneo mengi zaidi katika nchi yetu, yanaweza yakapata mawasilano ya simu. Ahsante sana. (Makof)

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kutohana na ufuatiliaji wangu katika Wizara hii inaelekea kwanza Mfuko huu unategemea hela ya World Bank ambayo haikupatikana na pili ufadhili wa nchi mbalimbali rafiki wa Tanzania. Sasa, kama alivyouliza mwuliza swali la msingi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Bajeti mahsus kwenye mfuko huu, ili miradi iliyopitishwa iweze kutekelezwa kwa sababu, tumeona kwamba, miradi ni mingi lakini hakuna utekelezaji?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Akunaay, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa anasema kwamba, tumekuwa tunategemea fedha za Mfuko wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupeleka

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mawasiliano na kama Serikali, ina mpango wowote wa kutenga pesa kwenye Mfuko huu wa kupeleka mawasiliano ya simu katika maeneo haya:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata pesa zinazotengwa, sio kwamba, Mfuko haupati pesa, lakini kiwango pia ambacho kinakwenda kwenye Mfuko wenyewe hakitoshelezi kwa ajili ya kupeleka mawasiliano ya simu katika maeneo ya nchi yetu. Lazima tukiri kwamba, nchi yetu ni kubwa hata hivyo, jitihada ambazo zimefanyika na Serikali kwa kushirikiana na Makampuni ya simu bado ni ni kubwa sana kwa sababu, ni maeneo machache sana nchini leo ambayo unaweza ukaenda ukakosa mawasiliano ya simu kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia niwahakikishie Wabunge kwamba, tumetayarisha orodha ya karibu Mikoa yote ambayo inaonesha maeneo yatakayopata mawasiliano ya simu kuanzia mwezi Mei mpaka tarehe 31 Desemba na ninaweza pia nikawapatia nakala hiyo.

Hata Mheshimiwa Akunaay, kule kwako nimeona kuna maeneo mbalimbali ambayo yatapata mawasiliano ya simu, lakini niseme kwamba, ni jitihada za Serikali kuona kwamba, Watanzania wote na mahali pengi wanapata mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ngara napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyomngeza.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nimemweleza Waziri wa Mawasiliano kwamba, Ngara inapakana na nchi za Burundi na Rwanda na mipaka hiyo haina utulivu. Kwa ajili ya usalama tunahitaji usikivu mzuri wa simu kwa hiyo, ni lini Serikali itaweka minara ya simu katika vijiji vya mipakani kama vile Kirusha, Mabawe, Ntobeye, Muganza, Musagamba na Bugarama? Nakushukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ntukamazina, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunapokea rai yake. Tutajitahidi Wizarani tuone kwamba, vijiji vyote vya mipakani katika eneo lake vinapata mawasiliano ya simu, lakini pia niseme kwamba, bado hata katika utaratibu wa kawaida Wilaya ya Ngara inapatiwa minara ya simu katika maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 37

**Kujenga Minara ya Simu Jimboni Lupa**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA**  
aliuliza:-

Tarafa ya Kipembwe ina mzunguko mkubwa wa mapato ya zao la tumbaku, lakini minara ya mawasiliano ipo sehemu ya Lupa tu:-

Je, Serikali itahimiza lini Kampuni za Simu kujenga minara katika Kata za Mamba, Lualaje, Matwiga, Matyeko na Kambikatoto, ili kuboresha mawasiliano katika sehemu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu Swalil la Mheshimiwa Kilasile, Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, inaendelea kuwahimiza watoa huduma za mawasiliano kupeleka huduma za mawasiliano ya simu za viganjani maeneo yote yenyewe shida za mawasilaino. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) inatoa ruzuku kwa makampuni ya simu kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara.

Aidha, Kata za mamba, Lualaje, Matwiga, Matyeko na Kambikatoto zitajumuishwa katika orodha ya Kata za Zabuni ya awamu ya pili (WB Phase 2) inayotegemewa kutangazwa katika mwaka ujao wa fedha, 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kupitia UCSAF mwishoni mwa mwezi Novemba 2014 Kata sita za Wilaya ya Chunya zitakuwa zimepata huduma za mawasiliano ya simu za viganjani ambapo jumla ya shilingi 782,140,928 zitatumika; walioshinda zabuni ni kama ifwatavyo:-

Kata ya Chalangwa, Totowe, Ngwala na Kapalala – Mkandarasi ni TTCL;  
Kata ya Namkukwe – VODACOM; na  
Kata ya Kanga – tiGO.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, nilikuwa na swali dogo la nyongeza, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tatizo hili la Chunya sio Chunya peke yake na limekuwa ni tatizo sugu sana la muda mrefu. Naweza nikasema katika Wilaya zote za pembezoni za Mkoa wa Mbeya. Mwaka jana niliuliza swali langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la Chunya liko katika Wilaya ya Kyela kule, kwenye Kata ya Ngonga, ukipigiwa simu unaambiwa *Welcome to Malawi*.

Liko tatizo hili kule Tarafa ya Bundali katika Wilaya ya Ileje, liko tatizo hili kule Kamsamba ambako Mheshimiwa Naibu Waziri ni Mbunge wa Jimbo, Mbozi, lakini...

**SPIKA:** Swali mama swali, hotuba hiyo.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, orodha imetoka. Na mimi nina kiri kabisa tangu mwaka jana orodha hii ilitoka, lakini mpaka leo jambo hili halijatafutiwa ufumbuzi. Nilikuwa nataka kujua, Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze, ni lini jambo hili litapata ufumbuzi? Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, Viti Maalum Mbeya, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa concerned na Mawasiliano katika Mkoa wa Mbeya, lakini pia kwa maana ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, yeye anasema kwamba, kuna matatizo ya mawasiliano katika Kata za mipakani, lakini kama tulivyosema, Mkoa wa Mbeya ni mionganini mwa mikoa ambayo sehemu kubwa sana ina mawasiliano ya simu za mkononi. Hata kule Kamsamba, Jimbo la Mbozi Magharibi kwa Mhesbhimiwa Silinde, mawasiliano ya simu yanapatikana bila ya matatizo yoyote na mimi nashuhudia na Mbunge hapa ananikubalia kwamba, hakuna matatizo ya mawasiliano ya simu.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sasa maeneo mengine machache ambayo yana matatizo ya simu, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, imejipanga vizuri sana. Ndiyo sababu, ukiangalia orodha ya maeneo yatakayopatiwa mawasiliano ya simu kwa kweli, ni mengi sana na tumeahidi Waheshimiwa Wabunge tutawapa nakala hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, mwaka 2010 Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) uliahidi kutenga fedha kuweka mnara wa simu kwenye Kata ya Kilolambwani, Rutamba na Mipingo. Leo ni mwaka 2014 na orodha hiyo kila mwaka tunajaza, ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri anatueleza hapa. Nilitaka kufahamu je, ni lini sasa mnara wa simu utapatikana kwenye Kata ya Kilolambwani, Kata ya Mipingo na Kata ya Rutamba kwenye Jimbo la Mchinga?

**SPIKA:** Hilo swali mbona jipya kabisa, unamwingiza kwenye mitaa ambayo hakujandaa?

Mheshimiwa jibu tu ka ujumla, maana siyo huko tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Mtanda, Mbunge wa Mchinga, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema ni swali jipya kwa kiwango kikubwa, lakini kwa sababu tuna orodha naomba niwasiliane na yeye baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu, ili niweze kuzungumzanaye kwa undani. Na kama iko haja basi, tuweke jambo lake hilo katika, kama litakuwa halipo kwenye mipango ya sasa, basi tuweke kwenye mipango inayokuja, ili Kata hizo alizozitaja za Kilolambwani, Lupingu na Rutamba ziweze pia kupatiwa mawasiliano ya simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona hiyo orodha muigawe kabisa kwa wote, maana naona wote wanaanza kusimama hapa.

Naendelea Wizara ya Nishati na Madini, muda unaisha. Mheshimiwa Getrude Rwakatare, nataka kuuliza swali hilo, kwa niaba yake Dkt. Haji Mponda?

Na. 38

**Wananchi Kupatiwa Nishati Mbadala**

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA K.n.y. MHE. MCH. DKT. GETRUDE RWAKATARE**  
aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, lakini naomba univumilie kidogo nianze kwa kuwapa pole wakazi wa Ulanga kwa adha na tabu kubwa wanayoipata. Ulanga sasa hivi ni kisiwa, hakifikiki zaidi ya boti moja na mitumbwi ya kienyeji. Maisha kule yamekuwa magumu, maisha yamekuwa ya hatari na majuzi tumeshampoteza mwenzetu mmoja amepinduka na mtumbwi.

Mheshimiwa Spika, bei ya lita...

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa naomba sana, tukifanya tena hiyo dakika 15 ndio hizo, tafuta utaratibu mwingine tafadhali. Nilifikiri unawapa pole, halafu na wewe utakuwa nao, basi sasa na wewe unaanza tena lita za mafuta?

Mheshimiwa, uliza Swalii.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusisitiza tu kilio chetu watu wa Ulanga.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba sasa kwa niaba ya Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, Swalii lake Namba 38, lipatiwe majibuu.

Serikali imetangaza kuwa, ifikapo tarehe 30 Juni, 2011 wananchi hawataruhusiwa kuokota kuni katika Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao ambao hawana nishati mbadala kwa matumizi yao?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa eneo walau kilomita moja, ili litumike na wananchi kwa matumizi ya nishati na kuni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)**  
aliijibu:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji, Dkt. Getrude Lwakatare, lenye sehemu (a) na (b), kama ifwatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TANAPA na World Wildlife Fund (WWF), ilifanya maandalizi ya upatikanaji wa nishati mbadala kwa kipindi cha miaka 10, ikiwemo kuwapatia wananchi miche ya miti bure, ili waweze kupanda katika mashamba yao kwa ajili ya kupata kuni mara hifadhi itakapozua eneo lake.

Aidha, wananchi wamekuwa wakipatiwa mafunzo ya utengenezaji na utumiaji wa majiko banifu, majiko yanayotumia mkaa/kuni kidogo na yanayotumia pumba pamoja na mafunzo ya kilimo mseto.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa wanaendelea kupata nishati ya kupikia baada ya kuzuiwa kuendelea kuokota kuni katika hifadhi hiyo, Serikali itaendeleza mafunzo ya kutengeneza na kutumia majiko banifu na pia upatikanaji wa majiko haya ambayo yanatumia kuni kidogo.

Aidha Serikali inafanya tathmini ya uanzishwaji wa miradi ya bayogesi, ili wananchi wa Udzungwa, hususan wenye mifugo, waweze kukidhi mahitaji yao ya nishati mbadala ya kupikia.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kutengewa eneo la hifadhi kwa ajili ya kuni, ni matumaini yangu kuwa matumizi sahihi ya nishati mbadala ikiwemo matumizi ya LPGE pamoja na umeme vijiji yatasaidia kutatua tatizo la kutegemea hifadhi hii kama chanzo kikuu cha nishati kwa wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Udzungwa.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni lini tathmini hiyo ya uanzishwaji wa miradi ya bayogesi itaanza na kukamilika?

Mheshimiwa Spika, na swali la pili; ninaomba Serikali iwatendee haki watu wao wanaokaa katika maeneo ya Udzungwa. Je, wamefika maeneo yale? Kwa sababu, kilio chao swali lao la pili halijajibiwa vizuri sawasawa, wameuliza na wameomba.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, kuna umuhimu Serikali wanaouona wa kuongezewa angalao kilometra moja kwa sababu, mazingira yale wananchi hawa hawana ardhi ya kutengeneza hiyo misitu? La pili.

Mheshimiwa Spika, lingine wananchi hao mnaozungumza bayogesi, hawana hao ng'ombe. Je, Serikali mko tayari kuwapatia angalao kilometra moja ya ziada, ili wapande miti?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Haji Mponda, Mbunge wa Ulanga, kama ifwatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miradi hii ya bayomasi, bayogesi, ipo katika Wizara ya Nishati na Madini na kuna Kitengo ambacho kinaendelea na kazi za utafiti na uwekaji wa miradi hii katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ameuliza ni lini mradi huu utanza na utakwisha?

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya Bunge hili, niweze kupata majibu sahihi kwamba, mradi huo, hususan katika eneo hilo alilolizungumza, lini utakwisha. Maana miradi hiyo imeshakwisha anza.

(b) Mheshimiwa Spika, nimepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuongeza kilometra moja katika Hifadhi ya Udzungwa. Niseme tu kwamba, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, ambao kimsingi ndio wanaosimamia hifadhi hizi, ili tuweze kuangalia uwezekano kama inawezekana. Na kama haiwezekani tutawajulisha kwa barua na kwa maandishi Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa pia napenda kumuuliza kwa kuwa, hivi karibuni tumeona vijana wakiburuzwa kwenda Mahakmani baada ya kuonekana wanakata miti kwa ajili ya mkaa. Hivyo, nilipenda kujua kwamba, je, Serikali haioni kwamba, wananchi walio wengi mjini wanatumia mkaa, lakini bado bei ya umeme ni nkubwa sana kiasi kwamba, wananchi hawa pamoja na kwamba, wana umeme, lakini hawawezi kuununua kutoptana na bei kubwa.

Je, Serikali ina mpango gani kushusha bei ya umeme, ili wananchi waachane na mkaa watumie umeme? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kwamba, Serikali imekuwa ikinunua na ikitumia umeme wa mafuta kwa muda mrefu. Na hivi karibuni tunakamilisha ujenzi wa bomba la gesi ambalo liko katika 80% mpaka 90% ya utekelezaji. Na malengo yetu kwamba, bomba la gesi litakapofika tutaanza kupata umeme wa bei nafuu kwa maana tutaanza kununua umeme kwa senti 8 mpaka senti 9, ambapo ni tofauti na sasahivi tunavyonunua umeme kwa senti 35 mpaka senti 55 za Dola ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili Shirika la Umeme la TANESCO liweze kumudu shughuli za uendeshaji, ililazimika Serikali kuongeza bei ya umeme, ili huduma iweze kutolewa kwa wananchi. Ni matumaini yetu kwamba, tutakapoanza kununua umeme wa nafuu ambao tunauzalisha wenyewe katika senti hizo nilizozizungumza, 8 mpaka 9, basi Serikali itafikiria wazo la kupunguza gharama za umeme na jambo hilo litafanyika ndani ya miezi 12 kutoka sasa ambapo bomba la gesi na mitambo ya kuzalisha umeme itakuwa tayari ifikapo mwezi wa 12 mwaka huu.

**SPIKA:** Sema hali ikiwa kama kawaida.

Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, swali linalofuata?

Na. 39

**Mfuko wa Maendeleo wa Kampuni ya  
African Barrick Gold (ABG)**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kampuni ya African Barrick Gold imeanzisha mfuko wa kusaidia Miradi ya Maendeleo kwa jamii inayozunguka migodi:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika toka mfuko huu tangu 2009 kusaidia jamii husika?

(b) Je, utaratibu gani unatumika kushirikisha jamii kupata vipaumbele vya miradi ya kuchangiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo (*MAENDELEO FUND*) ulianzishwa na Kampuni ya African Barrick Gold mwezi Septemba mwaka 2011. Lengo la mfuko huo ni kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye huduma za jamii (*Corporate Social Responsibilities*).

Walengwa wa wakuu wa mfuko huo ni jamii inayozunguka migodi yote inayomilikiwa na Kampuni hiyo ambayo ni Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara. Mfuko pia, umelenga kunufaisha jamii iliyopo Kanda ya Ziwa na mahali pengine kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya ABG imepanga kutumia kiasi cha dola za Marekani milioni 10 kila mwaka kupitia mfuko huu, hadi sasa kiasi cha dola za Marekani milioni 18.5 zimetumika kwa kazi hiyo. Miradi inayotekelawa kupitia mfuko huo ni ya afya, elimu, maji, miundombinu kwa maana ya barabara na umeme. Changamoto kubwa katika mfuko huo ni kuwepo kwa mahitaji makubwa ya miradi ya kipaumbele kwa jamii inayolengwa kunufaika na mfuko ukilinganisha na fedha zilizotengwa.

(b) Mheshimiwa Spika, jamii inayozunguka migodi ya ABG hushikirishwa ipasavyo katika kubuni miradi ambayo itanufaika na mfuko wa maendeleo. Baada ya mahitaji ya jamii kufahamika, uongozi wa ABG hukutana kila mwaka na Wakurugenzi wa Halmashauri husika, ili kupanga na kuitisha miradi ambayo itanufaika na mfuko huo.

Hata hivyo, katika upangaji wa miradi hiyo, ahadi ambazo tayari zimetolewa na mgodi kwa jamii husika, hupewa kipaumbele.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, mgodi au kampuni ya ABG ina migodi mitatu hivi sasa yaani mgodi wa Bulyanhuru, North Mara na Buzwagi na kila mwaka imekuwa ikitenga dola milioni kumi kwa ajili ya maendeleo kama alivyosema lakini katika miaka miwili mfululizo toka mwaka 2011 mfuko huu ulipoanzishwa kiasi cha fedha ambacho kimekuwa kikitengwa na kutumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wanaozunguka mgodi mmoja wa North Mara ni zaidi ya asilimia sabini.

Ili hali migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi ambayo inazalisha zaidi ya asilimia themanini hutengewa chini ya asilimia thelathini na maelezo ambayo

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

yamekuwa yakinolewa ni kwamba wananchi wa maeneo hayo ya North Mara ni wakorofi. Sasa nilitaka kujua kama Serikali ipo tayari kuendelea kuruhusu kigezo hiki cha ukorofi wa kupopoa ndege ya Mwekezaji na kutoboa lile bwawa la maji machafu kama kigezo cha kuwafanya wapate fedha nydingi. Kama sivyo, je, Serikali itafanya nini ili kufanya wananchi wa Kahama ambao ni wapole wasiadhibiwe kwa upole wao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Wilaya ya Kahama imekuwa ikidai mgodi wa Bulyanhulu na Buzwagi jumla ya dola za Kimarekani milioni kumi na moja, laki moja na elfu hamsini kama service levy toka mwaka 2001 mgodi wa Bulyanhulu ulipoanzishwa na mara zote mgodi umekuwa ukikataa kulipa kwa kisingizio kwamba inatoa service levy. Nilitaka kujua Serikali iko tayari kuendelea kuruhusu kampuni hii ya ABG iendelee kuvunja Sheria ya Serikali za mitaa ambayo inaruhusu Halmashauri kutoza service levy?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi muda wenyewe umeisha.

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na madini naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ezekiel Maige, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli migodi ya Barrick kupitia Maendeleo Fund imekuwa ikitoa huduma za jamii katika Wilaya ya Tarime na wamejenga shule nzuri na miradi mingine ya kijamii. Kuhusu uwiano wa utoaji wa miradi hii hili ni suala ambalo linapangwa baina ya Halmashauri husika kwa maana ya Halmashauri ya Kahama pamoja na mgodi lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameweka ombi kwa Serikali kuangalia uwiano basi tutaingilia kati tuweze kushirikiana na Halmashauri ya Kahama pamoja na mgodi kuhakikisha kuna uwiano mzuri wa ugawaji wa fedha hizi kwa maendeleo ya maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu service levy Wizara kupitia Halmashauri zetu tumekuwa na mazungumzo na mgodi wa ABG na hivi karibuni tumeweza kusaidia ku-recover fedha ambazo zilikuwa ni service levy zilizoachwa kulipwa miaka ya nyuma wakati migodi imeanza na hivi juzi tu nilikuwa Wilaya ya Tarime ambako jumla ya shilingi dola za Marekani laki nane zimelipwa kwenye Halmashauri ya Tarime ikiwa ni madeni ya nyuma ya mgodi.

Pia kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nzega mtakumbuka kwamba jumla ya bilioni 2.3 zililipwa kutoa mgodi wa Resolute na katika Wilaya ya Geita tumeweza kuhakikisha kwamba 1.4 million dollar zimelipwa kwenye Halmashauri ya Geita. Hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ya Kahama imelipwa jumla ya dola milioni moja za Kimarekani kama madeni ya nyuma ya service levy.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeshaagiza Wizara ya Nishati na Madini kupitia Kamati ya Majadiliano ya Serikali pamoja na Kamati ya Uwekezaji ya Serikali kukaa pamoja na migodi mikubwa ikiwemo ABG na GGM kupitia upya mikataba ya madini na hasa maeneo ambayo yanakinzana na Sheria zetu za nchi ikiwemo service levy. Kwa taarifa tu ni kwamba tumeshakubaliana kimsingi kwamba migodi itahama kutoka kulipa dola laki mbili na sasa itaanza kulipa dola kulingana na Sheria ya Fedha ya Serikali za mitaa itaanza kulipa asilimia 0.3 ya turn over yao katika Halmashauri zetu pale tutakapokamilisha mazungumzo yetu ambayo tumekwisha yaanza. (Makof)

Na. 40

### **Usikivu Hafifu wa Redio ya Taifa (TBC) Mkoa wa Katavi**

**MHE. DKT.PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Redio ya Taifa (TBC) nchini inasikika kwa shida sana katika Mkoa wa Katavi na kutosikika kabisa baadhi ya sehemu za Mkoa huo;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha redio hiyo inasikika kwa uhakika katika Mkoa huo ifikapo mwisho wa mwaka huu (2014) hasa ikizingatiwa na umuhimu wa mawasiliano kwa wananchi?

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu TBC ina mpango wa kufungua vituo vipyta vyta redio na kuboresha baadhi ya vituo vilivyopo katika baadhi ya maeneo ya nchi kwa masafa ya FM ili kuimarisha usikivu wa redio ya Taifa.

Maeneo ambayo yatahusika na kunufaika na mpango huo ni pamoja na Mkoa wa Katavi ambapo mtambo uliopo eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda utahamishwa na kujengwa katika eneo la Company Hill ambalo lipo juu ili kuongeza usikivu wa matangazo ya redio.

Pia mtambo mpya utajengwa Mkoani Katavi katika eneo la Kibaoni. Maeneo mengine ambayo yatadaidika katika mpango huo wa kuboresha matangazo haya ya TBC ni Unguja na Pemba na Mikoa ya Simiyu, Geita,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Njombe, Mtwara na Wilaya za Kilwa pale Nangurukuru, Same, Kilosa na Mvomero.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali kupitia TBC itaendelea kuongeza vituo vipyta na kuboresha usikivu wa redio ya taifa katika maeneo mbalimbali ya nchi mwaka hadi mwaka kulingana na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) pia limeweka mitambo katika mlima wa Matogoro Songea na hivyo kuongeza usikivu katika Mkoa wa Ruvuma vile vile TBC imehamisha mtambo wake wa Radio uliokuwa katika majengo ya Mkuu wa Mkoo wa Morogoro na kuhamishia katika Kilimakola na hivyo kuongeza usikivu wa matangazo ya redio katika maeneo mbalimbali ya Mkoo wa Morogoro. (Makof)

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda tu nionyeshe masikitiko yangu kwa Serikali kwa sababu hili swali lilikuwa ni la mwaka 2011. Bajeti inayoonyeshwa hapa anayoisema Mheshimiwa Naibu Waziri ni ya mwaka 2013/2014 ambayo mpaka sasa hiyo mtambo na hayo anayoyasema aliyoysasema kwenye majibu hakuna lilifanyika.

Mheshimiwa Slkpika, huu ni Mkoo mpya wa Katavi nafikiri vile vile hata Mikoa ya Simiyu, Geita na Njombe, ambayo ni Mikoa mipyas inawezekana haya bado na hayapo. Sasa naomba tu niulize swali dogo.

Je, Serikali inaonaje ikatumia mitambo angalau ya Mikoa jirani ambayo inaweza ikafikia Mikoa hii mipyas kwa mfano labda kama Kigoma inaweza ikatumia kwa Mkoo wetu wa Katavi tukapata mawasiliano kuliko kuendelea kusubiri hiki kinachoelezwa kwamba kitafanyika na ilikuwa ni 2011 na sasa tupo 2014, ahsante sana. (Makof)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mitambo hii bado haijawekwa, lakini tayari tenda imeshatangazwa na juhudzi zinafanyika sasa za kuiweka mitambo ile pale. Ombi lake la kuomba kwamba tutumie ama TBC itumie mitambo ya Mikoa jirani, mitambo hii ina uwezo wa kwenda masafa kiasi fulani si rahisi

mitambo iliyoko Kigoma ikaenda moja kwa moja ikafika mpaka eneo hili la Katavi.

Kwanza mitambo hii ni ya FM na FM ina utaratibu wake wa kusafiri. Kwa hiyo, avute subira tunaendelea kufanya juhudili suala hili la usikivu katika Mkoa wa Katavi liweze kufanyika vizuri, ahsante sana. (Makofisi)

**SPIKA:** Waheshimiwa samahani sana muda umekwisha naambiwa muda abao ulipangiwa kwanza kabisa naomba nitambue wageni tulionao. Tunao wageni kutoka Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa UNDP nao ni wafuatao. Tunaye Mheshimiwa Mrs. Hellen Clerk, Mrs. Hellen Clerk ni Mkuu wa Utawala katika Umoja wa Mataifa UNDP pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa kundi la Umoja wa Mataifa wanaohusika na mambo ya maendeleo.

Lakini Mheshimiwa huyu alishakuwa Waziri Mkuu katika nchi ya Newzealand kwa vipindi vitatu mfululizo na wakati wake Newzealand kulikuwa na tatizo la uchumi, kulikuwa na tatizo la ukosefu wa kazi pia kulikuwa na matatizo ya wale wenyeji asilia pale kwa hiyo kipindi chake alijitahidi sana kurekebisha mambo haya yote na mimi nilikuwa Newzealand mwaka jana tu mwishoni unakuta kabisa hata wale watu asili na wenyeewe wote wanachanganyika wanajaribu kuzungumza lugha moja na dini inakuwa moja basi mambo yake ni mazuri ni wakati yeye alifanya vitu hivi.

Mheshimiwa Hellen huyu alikuwa pia kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika Serikali yake kipindi cha mwaka 1993 mpaka 1999 wakati Serikali yao haikuwa madarakani lakini kwa sababu ya kazi nzuri aliyofanya akawa akaingia madarakani akawa Naibu Waziri Mkuu kipindi cha kati ya 1989 mpaka 1990. Halafu amekuwa Mbunge toka anamaliza shule tu kama akina Mheshimiwa Mkosamali, hivi aliingia kwenye mambo ya siasa akajaribu mwaka 1974 hakupata lakini mwaka 1981 akawa Mbunge mpaka juzi 2009 alipokwenda kugombea nafasi hii ya utawala katika Umoja wa Mataifa.

Nafasi hii ya Utawala katika umoja wa Mataifa ni nafasi ya tatu yupo Katibu Mkuu, halafu yupo Deputy Katibu Mkuu halafu yeye ndiyo watatu duniani kote. Kwa hiyo tunakukaribisha sana Mheshimiwa najua utakutana na makundi mbalimbali pamoja na mimi mwenyeewe *I really welcome you to our Parliament we will have time to discuss some few things in my office after finishing this work.* Lakini amefuatana na Mr. Philippe Ponsort yeye ni Resident Representative UNDP Country Director Tanzania tunamfahamu karibu, ahsante sana yupo na Miss Mandissa Masholubu yeye Deputy Director UNDP Tanzania, yupo Miss Anna Povernessey, Technical Advisor wa UNDP ahsante, yupo Mr. Godfrey Msissa Practice Specialist UNDP ahsante, yupo Anna Harjat Officer huyu akina Anna wapo wengi hapa sasa huyu nimeshindwa kutamka, yupo Miss Pamela Clea Communication Consultant UNDP ahsante.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo, tuna ujumbe mkubwa wa UNDP wamepitia hapa na safari ya Mheshimiwa Hellen Klerk yeye alikuja kujaribu kuelewa suala la Operation Tokomeza na jinsi wanavyoweza kusaidia. Lakini pia kwetu amekuja kuangalia masuala ya akina mama, yanaweza kuangaliwa kwa namna gani katika uso wa siku za baadaye. (Makofij)

Wageni kutoka ofisi ya Makamu wa Rais ambao ni Ndugu Sazili Salula Katibu Mkuu na yuko Ndugu Anjelina Madete Naibu Katibu Mkuu, asante sana. Kuna wageni wa Mheshimiwa Ntukamazina ambao ni Walimu wa Kuu wa shule za msingi kumi na moja zilizofanya vizuri katika mitihani ya darasa la saba Kitaifa kutoka Ngara wakiongozwa na Maafisa Elimu wa Wilaya wawili Ndugu Simon Mdee na Ndugu Julius Nestory, naomba wageni wetu hawa wasimame na tuwapongeze sana kwa kazi nzuri ya kufaulisha watoto na tunaomba uzi uwe pale pale isiwe mgema akisifiwa tembo hilitia maji ahsanteni karibuni sana. (Makofij)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mchungaji Natse ni mke wake kwanza Mrs. Natse na mtoto wao naomba wasimame walipo karibuni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye ni mzee Thomas Mkongolo Mwenyekiti wa kijiji cha Mahambe karibu mzee yuko na Ndugu Machemba Mjengi Mgehwa - Mwenyekiti wa kijiji Ikungi, Tuna Ndugu Wilbroad Peter Salvii Mwenyekiti kijiji cha Damaski ahsante tunashukuru karibuni katika Bunge letu na tuna wanafunzi wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo, wanafunzia mia moja na nne sidhani kama wapo kutoka Shule ya Sekondari ya Dodoma watakuja baadaye.

Shughuli za kazi kwanza kabisa saa tano na nusu Kamati ya uongozi ya Bunge naomba tutakuwa na kikao kwenye Board Room yangu saa tano na nusu (5.30) Wenyeviti wote tutakuwa na kikao kidogo cha dharura. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa William Ngeleja anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa C, Kamati ya katiba na Sheria. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Lembeli anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na robo (7.15) kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi mdogo wa Hazina.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema kutokana na wageni tulio nao nitamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti aendelee na shughuli. Naomba Mwenyekiti aendelee na shughuli.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

# KUHUSU UTARATIBU

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee Kanuni ya 46 kwamba Waziri kushindwa kujibu swali linaloulizwa kikamilifu. Wakati nikiuliza swali la nyongeza namba 33 kuhusiana na ajira za Walimu Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba baadhi ya walimu hawajaajiriwa kwa sababu wamekuwa na somo moja tu la *education psychology* lakini nijuavyo mimi Walimu lazima wasome masomo mawili ya kufundishia na *education psychology* inakuwa ni somo la lazima.

Sasa nilikuwa naomba ni kwa nini Naibu Waziri amelidanganya Bunge kwa sababu najua kabisa huwezi kusoma ualimu bila kuwa na masomo mawili ya kufundishia nilikuwa naomba muongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan baada ya kipindi cha mjadala saa saba nakuagiza uonane na Waziri myamalize hayo.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(8) Mheshimiwa Spika wakati amekalia kitu nilileta maelezo yangu binafsi na yapo hapo mezani kwako. Niliomba uweze kuyapitia ili uweze kuyapatia majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile maelezo yako sijayapata nitakapoyapata nitakupa Mwongozo. Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2014/2015**      **Ofisi ya**  
**Makamu wa Rais**  
**Muungano na Mazingira**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote walioituwezesha kutekeleza majukumu ya ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi kilichopita na ambao wamewezeesa kuandaa mpango wa mwaka wa fedha 2014/2015 na kustawisha hoja ambayo naiwasilishq katika hotuba hii.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wa Kamati za kudumu za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa James Lembeli na ile ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa William Ngeleja kwa kupokea, kujadili na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Vile vile natoa shukurani kwa Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, aliyekuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Masuala ya Mazingira kwa Ushirikiano na Michango yake katika kuboresha hoja hii. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Israel Natse, Mheshimiwa Asa Othuman Said na Mheshimiwa Rashid Ally, kwa kuteuliwa kuwa wasemaji wakuu wa Kambi ya Upinzani kwenye masuala ya Mazingira na Muungano. (Makofij)

Nichukue pia fursa hii kumpongeza ndugu yangu Tundu kwa kuendelea kushirikia nafasi ya Waziri kivuli kwa masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kunipa dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano na pia kuwateua Mheshimiwa Binilith Satano Mahenge kuwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia mazingira na Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu kuwa Naibu Waziri katika ofisi ya Makamu wa Rais.

Nashukuru sana Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano na utendaji wao thabiti na makini katika kutekeleza majukumu ya ofisi. Aidha, natoa shukrani za dhati na za pekee kwa Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, kwa ushirikiano wa dhati alionipa katika kipindi cha miaka mitatu tulipokuwa pamoja ofisini. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuwashukuru Bwana Sazi Salula, Katibu Mkuu Mhandisi Angelina Madete, Naibu Katibu Mhandisi Bonaventure Baya, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Wakuu wa Idara na Vitengo na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri iliyofanywa na wote niliowashukuru hapo juu isingwezekana bila uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi mazingira.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sasa naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi kwa vifo vya Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Said Ramadhan Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutohama na ajali za barabarani na maafa ya mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Vifo na majanga hayo ni pigo kubwa kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii sasa kuwapongeza Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Chalinze, kwa kuchaguliwa na wananchi ili kuwalilisha katika Bunge lako Tukufu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni ambapo zimetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla katika masuala ya mipango ya uchumi, utumishi na utendaji Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na malengo ya mwelekeo kwa mwaka 2014/2015. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaofuata kila jema na ufanisi katika kazi hii inayotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka fedha 2013/2014 na malengo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2010/2015, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010/2015, Malengo ya Maendeleo ya Millennia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa katika utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM na mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na 2015 na nianze na upande wa Mungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Aprili, 2014 Muungano wetu umetimiza miaka 50 tangu kuasiwa kwake. Katika kipindi hicho sote tumeshuhudia wananchi ndani ya nchi yetu wakipata fursa ya kuishi kwa amani na kufanya shughuli za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hali hii inathibitisha kauli isemayo Utanzania wetu ni Muungano wetu, hatuna budi, kuulinda, kuimarisha na kuudumisha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Makamu wa Rais iliahidi mambo kadhaa ambayo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, tuliagizwa kuratibu uboreshaji wa sheria na kanuni za fedha, zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka ya Mapato (TRA)na ZRB ya Zanzibar kwa faida ya pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitekeleza hili Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamekubaliana kuwa kwa vile kodi ya mapato itokanayo na mishahara ya wafanyakazi (*Pay as You Earn – PAYE*) ni suala linalohusu mapato ya Muungano, dai la SMZ kupata fungu kutohama na mapato hayo kwa wafanyakazi wa taasisi za Muungano ofanya kazi Zanzibar litekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 hadi 31 Machi, 2014, jumla ya sh. 36,750,000,000/= zimepokelewa na SMZ. Hata hivyo, marekebisho ya kisheria yanahitajika ili kuweka utaratibu wa wazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliagiza pia kuratibu Uboreshaji wa Sheria, za Ajira kwa Taasisi za Muungano ili kuwa na uwiano. Ofisi imeratibu uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu na ajira kwa taasisi za Muungano ili kuwa na uwiano katika nafasi za ajira. Mwongozo wa ajira katika taasisi za Muungano umeandaliwa kupitishwa. Mwongozo huo unaendana na ibara ya 185 ya rasimu ya mapendekezo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Desemba, 2013 inayozungumzia uwiano wa ajira kwa washirika wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza agizo la kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano, ofisi imeratibu utekelezaji wa masuala yanayoendelea kufuatilia ufumbuzi wake ambayo ni pamoja na hisa za SMZ katika Bodi ya Sarafu Afrika Mashariki na mgao wa faida ya Benki Kuu mafuta na gesi, usajili wa vyombo vya moto na masuala ya kodi kwa wafanyabiasha kama yalivyoelezwa kwenye ibara ya 15 hadi 17 ya kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliagizwa kufanya uratibu ya masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria na mambo yanayohusiana na Katiba katika Muungano. Katika eneo hili ofisi imeendelea kuratibu gawio la asilimia 4.5 ya mapato ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Gawio hilo linajumuisha misaada ya kibajeti yaani GBS, Fedhaya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Kodi ya Mshahara (*PAYE*). Hadi kufikia mwezi Machi, 2004 SMZ

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

imepokea msaada wa kibajeti, sh. 27,190,502,190/= kati ya sh. 32,627,535,000/= zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 SMZ imepokea PAYE ya sh. 15,750,000,000 na fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo sh. 1,243,925,860/=. Vile vile, SMT ilichangia sh. 600,000,000/= kwenda SMZ kwa ajili ya kufanikisha maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hiki masuala ya miradi ya miradi ya kijamii inayofadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo yameratibiwa. Baadhi ya miradi hiyo ni mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Fund - TASAF*) na Mradi wa Maendeleo ya Kilimo pamoja na Mradi wa Maendeleo ya Mifugo. Pamoja na hiyo kulikuwa pia na mradi wa *Millenium Challenge Account* na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Maelezo kamili ya jinsi miradi hiyo inavyotekelawa yako kwenye ibara 18 – 22 ya kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekeleza wa Awamu ya Tatu ya TASAF umeendelea kufanya katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kazi zilizofanyika ni pamoja na utambuzi wa uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo 22 ambapo kaya maskini 113,297 kutoka katika Vijiji na Shehia 1,043 zilitambuliwa; Malipo na utimizaji wa masharti ya elimu na afya kwa walengwa wa mpango yamefanyika; Maaandalizi ya kukusanya takwimu za awali za Mpango wa TASAF awamu ya tatu yamefanyika na Mifumo ya Taarifa za Uendeshaji (*Management Information System*) na masjala ya walengwa imeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo (ASSP) na Program ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo zimetekelawa katika Shehia 253 kwa upande wa Zanzibar. Fedha zilizopatikana kwa program ya ASSP ni sh. 47,138,452 na kwa program ya ASDPL yaani ya mifugo ni sh. 223,684,667. Kati ya fedha hizo sh. 198,494,667 ni mchango kutoka IFAD na sh. 24,190,000 ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia program hizi wananchi wa Unguja na Pemba wamewezeshwa kupata elimu bora ya kilimo na ufugaji. Aidha, program hizi zimesaidia kuongeza uzalishaji wa mazao, kuongeza kipato na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, program ya *Millenium Challenge Account* imejumuisha miradi ya sekta tatu muhimu za usafirishaji, nishati na maji kwa pande zote mbili za Muungano. Utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa na mafanikio makubwa kwani karibu miradi yote imekamilika. Wananchi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wamefaidika na ujenzi wa uboreshaji wa miundombinu na hivyo kusababisha kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelimisha umma kuhusu Muungano, ili kuwe na jamii yenye uelewa ya masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano, Ofisi iliandaa makongamano manane ya kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano. Makongamano hayo yalifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Zanzibar, Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi pia iliandaa na kuchapisha nakala 2,000 za jarida la Muungano Wetu; nakala 7,000 za vipeperushi, nakala 5,000 za jarida maalum la miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na nakala 5,000 za Kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, historia katika picha na kuzisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maadhisho ya 50 ya Muungano, Ofisi imeratibu makongamano mawili, yaliyofanyika Zanzibar moja likiwa ni Mtengamano wa Afrika Mashariki na lingine linalohusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Pamoja na makongamano hayo taarifa ya miaka 50 ya Muungano iliandaliwa na Kamati iliyoundwa na wajumbe kutoka Wizara na Taasisi za Muungano kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Vile vile ofisi iliratibu maonyesho ya miaka 50 ya Muungano, yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano; katika mwaka huu fedha, Serikali zote mbili zilishirikiana katika kukamilisha na kufanikisha maadhisho ya kusherehereka miaka 50 ya Muungano na Mapinduzi. Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na taasisi nyingine za Muungano zilishiriki katika maonyesho ya maadhisho hayo kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu mafanikio na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, mwaka huu tumeshuhudia Muungano wetu ukitimiza miaka 50 tangu kuasiwa kwake. Ni ukweli ulio wazi kuwa Muungano huu upo kwa sababu ya uamuzi makini na wa busara uliofanywa na viongozi waasisi wa Taifa letu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Tanganyika na Mzee Abeid Karume aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. (Makofi)

Tunaposherehekea na kuadhimisha miaka 50 hatuna budi kutambua, kupongezana kuthamini uongozi wao, hasa kwa kuona mbali kuhusu umuhimu wa Muungano na mchango mkubwa walioutoa katika kuasi na kujenga Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na juhudhi za waasisi hao, hatuna budi kuwashukuru viongozi wa Kitaifa katika awamu zote za uongozi wa Jamhuri

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuuenzi Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha miaka 50 ya Muungano wetu kimekuwa n a mafanikio mengi katika nyanja za kiuchumi, ulinzi na usalama, kisiasa na kijamii kama yalivyoainishwa kwenye kitabu cha taarifa ya miaka 50 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya mwaka 2014/2015. Katika mwaka wa fedha 2015, ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya uratibu wa masuala ya Muungano na kudumisha ushirikiano katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika kutekeleza hayo, shughuli za Kamati ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na vikao vinavyohusika vitaratibiwa ili kurahisisha utekelezaji wa masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi itaendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi ya kijamii iliyopo na mipyä inayotarajiwa kuja na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ili kubaini manufaa na upungufu unaopatikana kwa kuwepo kwa miradi hiyo. Vile vile ushirikiano baina ya Wizara na taasisi zisizo za Muungano zenyé kazi zinazoshabihiana kati ya SMT na SMZ utaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu kwa umma litapewa msukumo kwa kushirikiana na Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya ili Watanzania wapate uelewa mkubwa zaidi wa historia ya Muungano na hali ilivyo kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu iko katika mchakato wa kuandika Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ofisi itatekeleza masuala yote yanayohusu Muungano yatakayotokana na mapendekezo au yatakayotokana na Katiba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nielekee kwa upande wa hifadhi ya mazingira na niwasilishe mapendekezo ya ilani ya uchaguzi kwa upande wa mazingira na utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliagizwa kuimarisha zoezi la Kitaifa la kupanda miti, pamoja na miti ya asili katika Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa. Katika kulismamia hilo, ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa kufuatilia utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti milioni moja na laki tano kwa mwaka kwa kila Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, ofisi imepokea taarifa za mikoa 20 kuhusu miti iliyopandwa na kumea mwaka wa fedha huo. Taarifa hizo zinaonesha kuwa miti 209,252,221 maelezo ya kina yanaonekana katika ibara ya 34 na kiambatisho namba moja katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza mikoa ambayo Wilaya zake zimevuka lengo la upandaji miti na nahimiza mikoa mingine kuongeza jitihada ili kulinda mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano ya tuzo ya Rais ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti yameendelea kuhamasishwa nchini katika ngazi ya kaya, Vijiji, Kata, Halmashauri ya Vijiji na Manispaa, Mikoa, shule za msingi na sekondari, vyuo vya utafiti na mafunzo, taasisi za kijeshi, taasisi za vikundi vya uhamasishaji na uwezeshaji na taasisi au kampuni na uhamasishaji na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuzo hii inachelewa kila baada ya miaka miwili na mwaka huu itatolewa tarehe 5 Juni, katika kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani ambapo Kitaifa yatafanyika Mwanza. Mikoa iliyoshiriki katika mashindano haya kwa mwaka huu, ni Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Mwanza, Mara, Mtwara, Morogoro, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu na Tanga. Napenda kuipongeza mikoa hiyo kwa kushiriki katika mchakato wa tuzo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulagiwa pia kusimamia Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa ili zitunge sheria ndogo za kuhifadhi misitu. Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, mwaka 2013/2014, Halmashauri za Wilaya zilizotunga sheria ndogo za kuhifadhi misitu na mazingira ni Halmashauri za Wilaya ya Moshi, Mpanda, Kalambo, Uvinza, Kasulu na Kibondo na pia zimeanza kutumia sheria ndogo katika kuainisha vyanzo vya maji na kuvitunza. (Makofii)

Aidha, Halmashauri za Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma zinaendelea kuandaa sheria ndogo za hifadhi ya mazingira. Vilevile Halmashauri zingine zinaendelea kufuatiliwa na kusisitizwa kuhusu umuhimu wa kutunga sheria ndogo za kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ilituagiza kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe. Ofisi kuitia Baraza la Hifadhi na usimamizi wa mazingira, imeendelea kutekeleza mkakati wa usimamizi kamilifu wa mazingira ya Pwani kama ilivyoainishwa katika aya ya 78 ya kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yaliyotekelizwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, ni ukaguzi na tathmini ya ujenzi kandokando ya Ziwa Victoria uliofanyika katika maeneo ya Mkuyuni, Capri-point na Igombe kule Mwanza na waliojenga kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira walipewa Hati ya Katazo ili wasiendelee kujenga ndani ya mita 60 kutoka fukwe ya ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa awali wa mto Mkundi uliopo Morogoro na eneo la dakio ulifanywa na kubaini uharibifu ulisababishwa na mafuriko. Taarifa za hali ya milima katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara iliandaliwa na tathimini ya hali ya chemichemi za maji za eneo la Themsi Arusha ilifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine lilikuwa ni kuchukua hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi kuitia program ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliwezesha Wizara ya Nishati na Madini kuandaa mpango wa mazingira wa sekta ya Nishati na Madini. Mpango huu utaiwezesha Wizara kuandaa Sera ya Nishati Mbadala. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini inaandaa sera ya uendelezaji wa nishati itokanayo na *bio-fuel*. Sera hizi zitawezesha kupunguza matumizi makubwa ya kuni na mkaa ambayo imeongeza kasi ya uharibifu wa mazingira. Sanjali na zoezi hilo, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara hiyo, inaandaa tathimini ya mazingira kimkakati kuhusu sera ya uendeshaji wa *bio fuel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi itaendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya 1997. Katika mapitio hayo pamoja na mambo mengine suala la nishati mbadala litazingatiwa kama hatua ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ili kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliagizwa pia kupunguza gharama za vifaa vyatuhusu mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijiji watumie nishati hiyo ya umeme badala ya kuni na mkaa na kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeelekeza uamuzi wake wa kupunguza kodi ya ongezeko la thamani katika vifaa vyatuhusu mbadala ili wananchi waweze kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kunusuru mazingira yetu. Katika kutekeleza hilo, Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vifaa vyatuhusu mbadala kama vile upopo na jua ilipunguzwa kwa asilimia 18. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilipunguza gharama za kuunganisha

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

umeme katika maeneo ya vijiji kutoka takribani sh. 500,000/= mpaka kuwa sh. 27,000/- tu kwa lengo la kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Aidha, washirika wa maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Serikali yamekuwa yakichangia jitihada za Serikali kuwezesha upatikanaji wa nishati mbadala vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliagizwa kuimarisha usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Ofisi kupitia Baraza ilifanya ukaguzi wa viwanda, migodi na biashara 105 katika Mikoa ya Mwanza, Morogoro na Dar es Salaam. Hatua za kisheria zilichukuliwa kwa viwanda na shughuli zilizobainika kukiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ikiwa ni pamoja na kutoa notisi za kufanya marekebisho kulipa fine, kufungiwa na kupewa masharti ya kutekeleza, ili kuboresha hali ya mazingira. Ufafanuzi wa kina uko katika aya 95 hadi 102 ya Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi pia iliagizwa kutekeleza mradi wa vijiji vya mfano vya hifadhi ya mazingira. Katika kutekeleza hilo, awamu ya pili ya mradi wa vijiji vya mfano unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya umeanza kutekelezwa kwa gharama ya takribani Euro 8,000,000 sawa na sh. 16,000,000,000/=. Mradi huu unatekelezwa katika kanda za maeneo ya Pwani na ukanda wa chini maeneo ya miinuko yenye mvua nyingi kiasi na maeneo ya kanda kame.

Mchakato wa kupata taasisi za kutekeleza mradi umeanza ambapo taasisi 71 ziliandaa na kuwasilisha andiko la wazo la mradi na taasisi 16 zilifanikiwa kuandaa maandiko yaliyokidhi vigezo na tayari zimetaarifiwa kuandaa andiko kamili la mradi, ambapo miradi sita itakayokidhi vigezo inatarajia kupitishwa. Aidha, kila mradi unakadirwa kuwa na gharama ya takribani Euro 1,000,000 hadi 1,500,000 kutegemea ukubwa wa kila mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais iliagizwa pia kufanya tathimini ya athari ya kimazingira katika miradi ya ujenzi ambapo kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limeendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba miradi ya ujenzi inafanyiwa tathimini ya athari za mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya miradi 935 ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa tathimini ya athari ya mazingira. Kati ya miradi hiyo, miradi 396 ni ya ujenzi na miradi 298 ilipatiwa hati. Miradi iliyobaki imerejeshwa kwa wahusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia maelekezo tuliyopewa katika Ilani ya CCM, naomba sasa njielekeze katika utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015. Pamoja na utekelezaji wa maelezo ya Ilani ya Uchaguzi, Ofisi katika kipindi hicho imetekeliza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Maadhimisho yanayohusu masuala ya mazingira hutumiwa kama ni fursa ya kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira. Maadhimisho hayo ya Kitaifa ni siku ya ozone Duniani, Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Mazingira ya Afrika, Siku ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame na Wiki ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maadhimisho hayo kila mwaka elimu ya mazingira hutolewa kwa kutumia hotuba za viongozi, vipeperushi, mabango, machapisho na vitabu vyenye ujumbe kuhusu masuala ya mazingira. Ibara ya 47 na 48 ya kitabu cha hotuba ya bajeti kinaleza mambo hayo kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Ofisi iliidhinisha tathimini ya mazingira kimkakati kuhusu mpango kambambe wa Taifa wa sekta ya Uchukuzi na biashara nchini. Aidha, Ofisi imeendelea kuratibu tathimini nyingine za mazingira kimkakati kuhusu Sera ya uendelezaji wa bio fuel; Miradi ya Kujaza Eneo la Pwani ya Dar es Salaam; Mradi wa Kuendeleza Mji wa Kisasa katika eneo la Tengeru; Halmashauri ya Meru na Mradi wa Uendelezaji wa Mji wa kisasa katika eneo la Kibada Kigamboni. Katika kuongeza ufanisi wa uandaaji wa tathimini ya mazingira kimkakati, Ofisi imeandaa mwongozo wa uandaaji wa tathimini ya mazingira kimkakati utakaokamilika mwezi Juni mwaka huu 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imetoa ushauri wa kitaalam kwa Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika kuandaa mikakati ya mipango ya kisekta ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Halmashauri za Wilaya 16 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Tanga na Mtwara zimejengewa uwezo wa kutathimini athari za mazingira na zimewezeshwa kuandaa mipango kazi ya usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kutekeleza program ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuandaa kanuni za mbinu za kiuchumi za usimamizi wa mazingira, kanuni za kusimamia kemikali hatari za vimiminika kutoka viwandani, kanuni za kusimamia taka zitokanazo na viwanda vya umeme na kielektroniki, kanuni za uandaaji wa mipango kazi ya mazingira ya sekta na mamlaka za Serikali za Mitaa na Kanuni za kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi yetu pia imeandaa miongozo sita chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambayo ni Mwongozo wa Upangaji Mipango ya Mazingira na Ardhi; Mwongozo wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi Oevu, Mwongozo wa Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Nyanda za Malisho ya Mifugo; Mwongozo wa Jinsi ya Kukabiliana na Maafa ya Kimazingira;

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mwongozo wa Kujumuisha Masuala ya Jinsia katika Mazingira na Muongozo wa Wakaguzi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuanzisha Mfuko wa Mazingira, rasimu ya mwanzo ya kusimamia fedha za Mfuko na rasimu ya mwongozo kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa mfuko zimeandaliwa. Uteuzi wa Majina ya Wajumbe wa Bodi ya Mfuko unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/2015 tathimini ya vyanzo vya fedha ya Mfuko itafanyika na mapendeleko yatawasilishwa Serikalini kwa maamuzi. Aidha, washirika wa maendeleo watahamasishwa kuchangia katika Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inaelekeza uundwaji wa Baraza la Rufaa la Mazingira. Tayari Msajili na Wajumbe wa Baraza wameteuliwa, aidha uteuzi wa Mwenyekiti wa Baraza unashiriki maamuzi ya mamlaka husika. Katika kipindi hiki vigezo vya taratibu za uendeshaji wa Baraza zimeandaliwa na Baraza litaanza kazi rasmi baada ya taratibu hizo kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mchakato wa kuanda ripoti ya pili ya hali ya mazingira nchini umekamilika na ripoti ipo katika hatua za kuchapishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Program ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Kwa mwaka huu wa fedha, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa program endelevu ya hifadhi ya mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika inayohusisha nchi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia. Maeleo ya kina ya utekelezaji ya program hii yapo kwenye Ibara ya 56 hadi 62 ya Kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Baianuai. Ofisi ilifanya uratibu wa maandalizi wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Baianuai kwa kuzingatia mpango mkakati mpya wa Kimataifa wa mwaka 2011-2020. Uratibu wa majadiliano ya wadau kuhusu kuridhia Itifaki ya Nagoya inayohusu kusimamia upatikanaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki na Itifaki ya Nagoya Kuala Lumpur kuhusu uwajibikaji kisheria dhidhi ya athari zitokanazo na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa yalifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Ofisi imekamilisha uandaji wa ripoti ya tano ya Kitaifa kuhusu utekelezaji wa mkataba. Ripoti hii imebainisha hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na uharibifu wa Baianuai katika maeneo ya nchi kavu na majini.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Bainowai pamoja na itifaki zake. Utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena kuhusu teknolojia ya kisasa umeendana na shughuli za kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili mfumo wa usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, maabara za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maabara ya Chakula na Dawa, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Taasisi za Utafiti wa Kilimo Zanzibar na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni zinazohusika na udhibiti na utafiti zimejengewa uwezo kwa kupatiwa vitendea kazi vya maabara hizo vitakavyosaidia shughuli za utambuzi na ung'amuzi wa mazao au viumbe ambavyo vimefanyiwa mabadiliko ya kutumia njia ya uhandisi-jeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi itaendelea kukuza uelewa wa wananchi kuhusu kukuza matumizi salama ya baiteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko wa Itifaki ya Kyoto, Serikali imefanya tathimini ya athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sekta za kilimo, mifugo, misitu na mradi wa majoribio ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi katika sekta hizi tatu, utatekelezwa katika Wilaya za Singida Vijijini, kwenye Vijiji vya Mgoli, Mguga na Unyampanda. Aidha, miradi minne ya maji ya majoribio kwa ajili ya kuhimili mabadiko ya tabia nchi katika Wilaya za Mbanga, Igunga, Misenyi na Nungwi- Zanzibar ilikamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo ya Pwani ya Dar es Salaam wenyе thamani ya takribani dola za Marekani 5,000,000 umeanza kutekelezwa kwa kufanya tathimini ya athari za mazingira, kuandaa taarifa ya awali ya mradi na kuanzisha Kamati Elekezi ya Usimamizi wa Mradi. Kazi za mradi zitatekelezwa katika mwaka wa fedha ujao kama inavyoonyeshwa katika ibara ya 73 ya kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi inatekeleza mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari. Mradi huu wenyе dola za Marekani 3.3 unahuisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar. Maafisa 20 kwa kila Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo na Rufiji walipatiwa mafunzo kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabia nchi. Kazi hii itaendelezwa pia katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mkataba wa Nairobi kuhusu hifadhi ya mazingira ya bahari. Tanzania imeendelea kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa mkataba wa kipindi cha mwaka huu 2013-2017. Katika kutekeleza mpango huo, Ofisi kwa kushirikiana na UNEP imeanza mchakato wa kuratibu utekelezaji wa mkakati kwa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari ukanda wa Pwani, maziwa, mito na mabwawa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Maafisa Mabonde. Shughuli hizi zitaendelezwa pia katika mwaka ujao wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mazingira Duniani kupitia UNDP ilifadhili miradi midogo 35,000 yenye thamani ya sh. 4,788,680,986 naomba kufanya marekebisho kwenye kitabu iliyoko katika Mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Mara, Pwani, Rukwa Iringa, Mwanza na Zanzibar kama inavyoonekana katika kiambatisho namba mbili (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi itaongeza jitihada zaidi kuhimiza na kushauri Asasi za Kiraia kuandaa miradi mingi zaidi ili kunufaika na fedha kutoka Mfuko wa Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Ofisi imeratibu maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo hufanyika tarehe 5 Juni ya kila mwaka. Mwaka 2014 maadhimisho hayo yatafanyika Kitaifa Mkoani Mwanza. Aidha, kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu Kimataifa inasema *Rise Your Voice not The Sea Level* ikiwa na maana kwamba, "ongeza sauti yako kutetea mazingira na siyo kuongeza kina cha bahari". Ujumbe huu unahimiza umuhimu wa kuhifadhi na kulinda rasilimali za mazingira zinazosababisha kuongezeka kwa kina cha bahari na kuleta maafa katika nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maktaba wa Montreal kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni umehusishwa kujenga uwezo wa mafundi mchundo hamsini na wakufunzi 70 wa Vyuo vya Ufundis Stadi VETA kuhusu teknolojia mbadala na rafiki kwa tabaka la ozone na katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Stockholm wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu, ulitekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa wataalam kumi na sita watakaohusika na ukusanyaji wa taarifa za kuingiza matumizi na uchakavu wa kemikali za awali na kemikali mpya zilizoongezwa kwenye mkataba. Katika mwaka wa fedha ujao 2014/2015 ripoti ya ukusanyaji takwimu za kemikali zinazozibitiwa na mkataba huu itakamilishwa na kufanya ukaguzi wa maeneo yaliyoharibiwa na kemikali hizo zenyе sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Usafirishaji wa Utupaji wa Taka za Sumu baina ya Nchi na Nchi na Mkataba Unaozuia Uingizaji wa Taka za Sumu Afrika ulifanyiwa kazi kwa kutengeneza filamu kuhusu shughuli za usimamizi wa taka sumu katika Jiji la Dar es Salaam hususan mafuta machafu, betri chakavu na vifaa vya umeme na elekroniki, Madawa ya kilimo na viuatirifu.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa pili ni kupunguza uharibifu wa ardhi katika miinuko ya Mkoa wa Kilimanjaro na mradi wa tatu ni ule wa kuhusisha masuala ya usimamizi endelevu wa misitu ya Miombo katika Mikoa ya Tanga na Katavi. Shughuli za miradi hii zinatekelezwa kama inavyoonekana katika ibara ya 88 hadi ya 92 ya kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ujao wa 2014/2015, Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na miradi inayotekelze wa chini ya mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usimamizi wa matumizi ya mifuko ya plastiki, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau imeandaa Rasimu ya Kanuni za Plastiki ya mwaka 2013. Rasimu ya Kanuni hii inaendana na viwango vya ubora vya mifuko ya plastiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopitishwa mwaka 2012. Rasimu hii itatoa fursa kwa kutumia baadhi ya bidhaa za plastiki kwa ajili ya shughuli muhimu katika viwanda vya aina mbalimbali kama vile sekta ya maziwa na usindikaji wa vyakula. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi itakamilisha Rasimu ya Kanuni na itaendelea kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nielekee kwenye Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambapo kazi kubwa inayofanywa ni uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Katika kipindi hiki Baraza lilifanya ukaguzi wa mazingira katika viwanda na mahoteli ambayo hayajafanya tathimini athari kwa mazingira na ukaguzi wa awali wa mazingira.

Katika Mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam, Mbeya, Tanga, Mtwara na Lindi kama inavyoonekana katika ukurasa wa 65 hadi 70 wa kitabu cha hotuba ya Bajeti. Pamoja na kazi hiyo, Baraza lilifanya tathimini ya athari kwa mazingira na usajili wa wataalam na makampuni ya kufanya tathimini ya athari kwa mazingira kama inavyoonekana kwenye ibara ya 107 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya kuhifadhi mazingira kwa umma kupitia Baraza la Hifadhi ya Mazingira imetolewa kwa Wakuu wa Idara na Maafisa Waandamizi 180 wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Singida, Ukerewe, Sengerema, Kwimba, Kilwa na Lindi. Hii inafanya jumla ya Wilaya zilizofikiwa na mafunzo hayo kufika 32 tangu mradi ulipoanzishwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza pia lilitoa elimu kwa wadau 80 ambaa ni Maafisa wa Polisi, Wanasheria wa Serikali za Mitaa, Mahakimu na Wadau wa Asasi Zisizo za Serikali katika Mikoa ya Mara, Mtwara na Arusha. Aidha, Baraza limepeleka nakala za video zilizoandaliwa katika Wilaya za Dodoma Vijiji, Iringa, Meatu, Magu na Bariadi, katika vituo vya Televesheni na Radio vilivyopo katika

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kanda za Kusini, Nyanda za Juu na Kanda za Ziwa kwa lengo la kuelimisha Jamii kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabia nchi na jinsi ya kuhimili. Baadhi ya makala hizo zimeanza kurushwa hewani kupitia kituo cha Iringa Municipal Television na Shirika la Taifa la Utangazaji (TBC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Iringa, Baraza limeandaa makala ya filamu inayoonesha athari zinazowakabili na harakati wanazozitumia wananchi katika kuhimili mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo ya Mto Ruaha itakayoanza kuoneshwa katika vituo vya televisheni, kuanzia mwaka wa fedha ujao. Kazi ya kutayarisha machapisho kwa ajili ya kutoa elimu imeelezwa katika ibara ya 112 na 113 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza limeboresha tovuti yake kwa kuweka taarifa mpya na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mazingira. Baraza pia limeendelea kusimamia tovuti ya Taifa ya mazingira iliyozinduliwa mwaka 2012 ikiwa ni mojawapo ya vyanzo vya upatikanaji wa taarifa za mazingira kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi wa *Oil for Development*, unaofadhiliwa na Serikali ya Norway, Baraza linashirikiana na Taasisi ya Mazingira ya Norway ili kuboresha mfumo uliopo wa taarifa za kijiografia. Hatua hii italiongezea Baraza uwezo wa kukusanya, kutunza na kusambaza taarifa za mazingira zikiwemo za utafutaji wa mafuta na gasi asilia pamoja na taarifa za uchimbaji wa gesi asilia unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka ujao wa fedha Baraza litaendelea kukusanya taarifa na kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira katika maeneo makubwa matano ambayo ni kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; masuala ya mazingira katika sekta mpya za gesi na uchimbaji wa madini ya urani; matumizi endelevu ya rasilimali za nchi; namna ya kudhibiti utupati ovyo wa taka na udhibiti wa ujenzi holela katika fukwe za mito, bahari, maziwa, mabonde na vyanzo vya maji.

Baraza litaendelea pia kusambaza makala za video katika vituo vya luninga na video vilivyopo katika kanda zingine ili kukuza uelewa wa jamii kuhusu athari na jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo la Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Juhudi za kutekeleza mpango wa ujenzi wa Ofisi ya Baraza katika eneo la Mikocheni, Mtaa wa Regency Migombani, ziliendelezwa kwa kununua kiwanja namba 28 kilichopakana na viwanja namba 29 na 30 vilivyopo katika eneo la Ofisi ya Baraza, ili kupata eneo la kutosha linalokidhi mahitaji ya ujenzi huo.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Michoro ya jengo hilo inaandaliwa na jitihada za kutafuta fedha zinafanywa tukiwa na matumaini kwamba ujenzi huo utaanza mwaka ujao wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza lilikadiria kukusanya tozo kiasi cha shilingi bilioni mia moja, milioni mia tano, lakini hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, kiasi cha shilingi milioni mia nane hamsini na sita zimekusanywa, sawa na asilimia 58 ya makadirio. Kutofikiwa malengo ya ukusanyaji kunatokana na uwezo mdogo wa Baraza kifedha na upungufu wa vitendea kazi, ufahamu mdogo kuhusu Kanuni za tozo za mwaka 2008 pamoja na Sheria ya Mazingira sura ya 191 kwa wamiliki wa viwanda na wawekezaji. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza litaendelea kutafuta vyanzo vya fedha na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limeanza utekelezaji wa kuhifadhi bonde la Kihansi pamoja na Lindi maji kwa kupitisha mpango kazi wa mradi. Mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika vipengele vikuu viwili, ambavyo ni kujenga uwezo wa kitaasisi na usimamizi wa bonde la Kihansi na kutunza viumbe ndwele vilivyopo katika bonde hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa masuala ya Muungano na usimamizi wa mazingira kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya ofisi; jamii kuwa na uelewa mdogo kuhusu masuala ya muungano na masuala ya mazingira; upungufu katika kuwepo na kupatikana kwa wakati takwimu sahihi za mazingira na mwitikio usioridhisha kwa Serikali za Mitaa, katika masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizo, ni kutafuta fedha za ndani na kutoka kwa wafadhili kwa njia ya kuandaa miradi ili kuiwezesha ofisi kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia radio, television, magazeti, machapisho, maadhimisho na maonyesho ya Kitaifa kuhusu masuala ya mazingira na Muungano; Kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa mafunzo na vifaa kwa waratibu wa mazingira wa sekta na maafisa mazingira wa Serikali za mitaa na kuendeleza kuhamasisha Serikali za mitaa kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ofisi pamoja na usimamizi wa Baraza la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira. Imefanyia kazi kwa uadilifu masuala ya mafunzo, kupanda vyeo, uboreshajji wa mazingira ya utendaji kazi, upimaji wa viwango vya utendaji kazi, maslahi na stahili za wafanyakazi na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

masuala ya afya za wafanyakazi kama inavyoonekana katika ukurasa wa 84 hadi 87 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye shukurani; naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliotusaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi. Napenda kuzitaja baadhi ya nchi na Mashirika na taasisi yafuatayo:-

Serikali ya Norway, Serikali ya Marekani, Shirika la mpango wa maendeleo Umoja wa Mataifa (UNDP), United Nation and Cultural Organization (UNESCO), Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea, Umoja wa Nchi za Ulaya, Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Mfuko wa Mazingira (GEF), Benki ya Dunia, International Development Agency (IDA), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), SADC RIP, World Life Conservation Society, World Life Fund, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Crop Life International, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Misaada la Kiufundi la Ujerumani (JZ), Asasi Zisizo za Kiserikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba washirika wa maendeleo waendelee kushirikiana nasi katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikisha zaidi katika vita dhidi ya umaskini, kuboresha maisha ya kila Mtanzania, kuhifadhi mazingira na kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Ili ofisi iweze kutekeleza malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

Fungu 26 - Makamu wa Rais, yaani private office, katika mwaka wa fedha 2014/2015, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya sh. 5,726,996,000/=, kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za mishahara sh. 879,540,000/= na fedha za matumizi mengineyo ambazo ni sh. 4,847,156,000/=.

Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais; katika mwaka wa fesha 2014/15, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe sh. 50,200,719,000/=, fedha za matumizi ya kawaida na sh. 6,562,746,000/= fedha za maendeleo.

Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha sh. 44,039,608,000/= fedha zitakazopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sh. 3,832,091,000/= fedha za ruzuku kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kinachosalia cha sh. 8,329,020,000/= ni fedha za matumizi ya kawaida za Idara na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kwa upande wa fedha za maendeleo zinajumuisha fedha za ndani ambazo ni sh. 4,500,000,000/= na fedha za nje ambazo ni sh. 2,062,746,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofii)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MWENYEKITI:** Hoja hiyo imeungwa mkono, nakushukuru Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala!

### **Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. FAKHARIA K. SHOMAR (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5), (9) na 117(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais inajumusha mafungu mawili ambayo ni: Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu - 31 Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2013/2014, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano mnamo tarehe 3 Mei, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa lbara ya 47(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Sheria ya Mabadiliko ya Kumi Na Moja ya Katiba Namba 34 kifungu cha 11 ya mwaka 1994, Ofisi ya Makamu wa Rais imekabidhiwa majukumu ya Kitaifa ya kuratibu mambo yote ya Muungano na Ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Ofisi hii inahusika na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira hapa nchini. Kwa mantiki hiyo ni ofisi muhimu kwa mustakabali wa Muungano wetu adhimu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 26 Aprili, 2014 nchi yetu iliadhimisha miaka hamsini ya Muungano wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na iliyokuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ulioanzishwa mnamo tarehe 26 Aprili, 1964. Muungano huu uliasisiwa na waasisi wa Taifa letu ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka hamsini ya Muungano, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa, ikiwemo kudumisha amani, utulivu na mshikamano mionganoni mwa Watanzania. Ni matumaini ya Kamati yangu na wananchi kwa ujumla kuwa Muungano huu utaendelea kudumu kwa miaka mingine hamsini au zaidi ijayo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni, mapendekezo na ushauri wa kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati yangu ilitoa ushauri, mapendekezo na maoni yenyehengi la kuimairisha na kuboresha utendaji kazi wa ofisi hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi na mwingine unaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwanza, elimu itolewe zaidi kwa wananchi kupitia vyombo vya habari kama redio, televisheni, majarida na machapisho mbalimbali kwa lengo la kuboresha na kuimarisha Muungano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa historia, maendeleo, changamoto pamoja na namna zinavyotatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetua elimu kwa kuanda makongamano nane (8) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Zanzibar, Mbeya na Iringa mwezi Septemba, Oktoba, Novemba na Desemba 2013 na Februari, 2014 kwa ajili hiyo.

Elimu hiyo iliwaluhusisha wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na baadhi ya viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Pili, Wabunge wanaotoka Zanzibar wapewe nafasi ya kushiriki katika kujadili fedha za miradi zinazotoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uongozi (Steering Committee) ya TASAF kwa Pemba na Unguja ina uwakilishi wa Wabunge kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao hushirikishwa kujadili miradi na masuala ya fedha za TASAF.

Tatu, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Tunguu Zanzibar likamilishwe mapema na upungufu katika ujenzi huo urekebishwe na Mkandarasi anayejenga jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa na Serikali kuwa ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano lilioko Zanzibar umefikia hatua za mwisho na upungufu uliojitekeza unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoikabili Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano inayoratibu masuala yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti; bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuwezesha kugharamia utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ni ndogo hivyo, kutokidhi mahitaji halisi ya uendeshaji wa majukumu ya Ofisi hii.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa mdogo kuhusu masuala ya Muungano; masuala ya Muungano yameainishwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka, 1977 pamoja na marekebisho yake. Kwa kiasi fulani masuala haya bado hayajaelewka vya kutosha mionganoni mwa wananchi, hivyo, kusababisha manung'uniko yasiyo ya lazima kuhusu Muungano. Endapo elimu ya kutosha itatolewa changamoto hii itapungua au kumalizika kabisa.

Fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutokufahamika mionganoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipeleka fedha katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya shughuli za kibajeti na kugharamia masuala mbalimbali ya maendeleo na kijamii. Hata hivyo, mchango huo haufahamiki mionganoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla, jambo linalofanya kuwepo kwa kauli potofu kuhusu Mchango wa Serikali ya Muungano kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa Jengo la ghorofa linalomilikiwa na mtu binafsi jirani na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar. Katika eneo ambapo Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais iliyopo Tunguu Zanzibar, kuna jengo la ghorofa la mtu binafsi karibu sana na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Jengo hilo ni refu kiasi cha kumwezesha mmiliki wa jengo hilo kuona shughuli zote zinazofanyika katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais jambo ambalo sio sahihi kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 26 na Fungu 31, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa uratibu mzuri inaoufanya katika masuala ya Muungano, hususan, katika kushughulikia hoja tisa (9) kati ya 13 za Muungano zilizowasilishwa katika vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jitihada hizo ni kubwa na zenye azma ya kumaliza changamoto ndogondogo zinazoukabili Muungano wetu ili kuhakikisha kuwa unadumu na mahusiano baina ya pande mbili za Muungano yanaimarika katika ustawi wa wananchi wetu na kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo, Kamati inaona kwamba bado iko haja ya kuongeza nguvu zaidi katika kushughulikia masuala ya Muungano kwa lengo la kuboresha Muungano wa nchi yetu. Hivyo basi, Kamati inashauri ifuatavyo:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwanza, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu na faida ambazo zinazotokana na Muungano kwa pande zote mbili ili kuwawezesha wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi mapana ya nchi yetu na kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Pili, kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa kuna fedha zinazopelekwa Zanzibar kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kusaidia shughuli mbalimbali za kibajeti, kiuchumi na kijamii, fedha ambazo hazifahamiki mionganii mwa wananchi, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais iweke utaratibu wa kutoa elimu na taarifa kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi kwa ujumla kuhusu namna na kiasi gani cha fedha Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaichangia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ili kuondoa dhana potofu inayoenezwaa kwa Wazanzibari kuwa hakuna mchango wowote unaotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Elimu hiyo itasaidia wananchi kuuthamini na kuuenzi Muungano wetu.

Mfano, katika Mwaka wa fedha 2013/214 kwa kipindi kinachoishia Machi, 2014, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepeleka fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama ifuatavyo:-

Moja, gawio la misaada na mikopo ya kibajeti (*General Budget Support - GBS*) Sh. 27,190,502.190.97 kati ya Sh. 32,627,535,000 zilizoidhinishwa na Bunge.

Pili, *Pay as you Earn (PAYE)* Sh. 15,750,000,000.

Tatu, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Sh.1, 243.925,860.

Nne, fedha za kugharamia maadhimisho ya miaka hamsini ya Mapinduzi ya Zanzibar Sh. 600,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *number three*, kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ndiye mratibu mkuu wa mambo ya Muungano na ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamati inashauri kwamba pale ambapo kuna fedha zozote zinazopelekwa Zanzibar kupitia Hazina au mamlaka yoyote taarifa kuhusu fedha hizo ziwasilishwe Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa ajili ya kumbukumbu na kuujulisha umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohakana na Serikali kujenga jengo la Ofisi ya Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar chini ya kiwango na kutumika fedha nyingi za wananchi, Kamati inashauri Serikali kuwa makini wakati wa uteuzi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

makandarasi ili kuhakikisha kuwa wanaopewa tenda za ujenzi wa ofisi nyeti kama ya Makamu wa Rais wanakuwa na uwezo, ujuzi na weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wakala wa Majengo ya Serikali nchini (TBA) iwe makini wakati wowote kukagua ili kuhakikisha kuwa majengo ya Serikali yanajengwa kwa ubora wa viwango stahiki. Pia TBA ihakikishe kwamba Serikali kwa mambo yote haikabidhi jengo lililojengwa chini ya kiwango ili kuhakikisha kuwa Serikali haipati hasara kwa kupoteza fedha nyingi katika kugharamia wakati majengo ya Serikali yanajengwa chini ya kiwango.

Kamati inashauri kwamba ujenzi wa jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar, ambao umebainika kuwa na upungufu mkubwa kama vile nyufa katika jengo la makazi, shutter za madirisha ya mbao kuchakaa, mfumo wa viyoyozi kutokufanya kazi, yarekebishwe ili kuondoa upungufu huo kabla ya kukabidhiwa. Aidha, samani za kutosha na bora kwa ajili ya jengo hili zinunuliwe ili ofisi hiyo iweze kutumika.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zifanye mazungumzo na mmiliki wa jengo lililo jirani na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo la kulinunua kwa kuimarisha usalama wa ofisi na makazi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa baadhi ya kero za Muungano kama vile suala la hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, mafuta na gesi, mgawanyo wa fedha za wafadhili na malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili wanapopeleka bidhaa zao Tanzania Bara zipo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa na Serikali zote mbili.

Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa Serikali yetu iko katika mchakato wa utungaji wa Katiba Mpya, Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu ni wajumbe wa Bunge hilo; ni vyema kuitia mchakato huo watakapofikia katika eneo hilo watafakari kwa kina namna ya kuzimaliza kero hizo kwa lengo la kuimarisha na kudumisha Muungano wetu.

Kamati inashauri kwamba, mapendeleko yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha mwaka 2006 kuhusu utaratibu wa mgawanyo wa fedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yatolewe uamuzi haraka ili kuondoa kero hii ya muda mrefu na utekelezaji wake uanze mara moja.

Kutokana na majukumu muhimu ya Ofisi ya Makamu wa Rais Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti na kutoa kwa wakati fedha zinazoidhinishwa ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ili waweze kutekeleza majukumu yao na kuleta tija katika ofisi na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati niatambua kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na mambo mengine kuratibu ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo, Kamati inashauri kazi hii iendelezwe kuitia vikao vya kisekta kila inapohitajika ili kuimarisha ushirikiano huo wa kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha na makadirio ya bajeti ya mwaka 2014/2015. Ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano inaomba fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015; kwa muhtasari kwa fungu 26 na 31kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba. Aidha, hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano; Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili makadirio na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa umesaidia kufanikisha kukamilishwa kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba wajumbe wote wa Kamati waingie katika hansard kama kawaida inavyokuwa. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashilillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kipekee. Nawashukuru ndugu Matamus Fungo na ndugu Maria mdulugu kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumzi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kama yalivyoainishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Kilimo anawatangazia Wabunge wote wanaotoka kwenye mikoa yote yenye zao la pamba, wakutane ofisini kwake Wizara ya Kilimo leo saa saba na nusu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira!

### **Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

#### **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai , afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5), (9) na 117 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais inajumisha mafungu mawili ambayo ni: Fungu 26 -Makamu wa Rais, na Fungu - 31 Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Samia S. Hassan (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano mnamo tarehe 3 Mei, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 47 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Sheria ya Mabadiliko ya kumi na moja ya Katiba Namba 34 kifungu cha 11 ya mwaka 1994, Ofisi ya Makamu wa Rais imekabidhiwa majukumu ya kitaifa ya kuratibu mambo yote ya Muungano na Ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Ofisi hii inahusika na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira hapa nchini. Kwa mantiki hiyo ni ofisi muhimu kwa mustakabali wa Muungano wetu adhimu na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 26 ,Aprili, 2014 nchi yetu iliadhimisha miaka hamsini ya Muungano wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na iliyokuwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar ulioanzishwa mnamo tarehe 26, Aprili, 1964. Muungano huu uliasisiwa na waasisi wa Taifa letu ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume.

**Mheshimiwa Spika**, katika miaka hamsini ya Muungano, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa, ikiwemo kudumisha amani, utulivu na mshikamano mionganoni mwa watanzania. Ni matumaini ya kamati yangu na wananchi kwa ujumla kuwa Muungano huu utaendelea kudumu kwa miaka mengine hamsini au zaidi ijayo.

## **2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI,MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati yangu ilitoa ushauri, mapendelekezo na maoni yenye lengo la kuimairisha na kuboresha utendaji kazi wa ofisi hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi na mwingine unaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

- i) **Elimu itolewe zaidi kwa wananchi kupitia vyombo vyaa habari kama radio, televisheni, majarida na machapisho mbalimbali kwa lengo la kuboresha na kuimairisha muungano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa historia, maendeleo, changamoto pamoja na namna zinavyotatuliwa.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetoa elimu kwa kuandaa makongamano nane (8) katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Zanzibar, Mbeya na Iringa mwezi Septemba, Oktoba, Novemba, na Desemba 2013 na Februari, 2014 kwa ajili hiyo. Elimu hiyo iliwasuhisha wanafunzi wa vyuo vyaa elimu ya juu na baadhi ya

viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

- ii) **Wabunge wanaotoka Zanzibar wapewe nafasi ya kushiriki katika kujadili fedha za miradi zinazotoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya uongozi (Steering Committee) ya TASAF kwa Pemba na Unguja ina uwakilishi wa Wabunge kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao hushirikishwa kujadili miradi na masuala ya fedha za TASAF.

- (iii) **Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Tunguu Zanzibar likamilishwe mapema na mapungufu katika ujenzi huo yarekebishwe na Mkandarasi anayejenga jengo hilo.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa na Serikali kuwa ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano lililoko Zanzibar umefikia hatua za mwisho na mapungufu yaliyojiteza yanafanyiwa kazi.

### **3.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano inayoratibu masuala yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

**Ufinyu wa bajeti:**

**Mheshimiwa Spika**, bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuwezesha kugharamia utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ni ndogo hivyo, kutokidhi mahitaji halisi ya uendeshaji wa majukumu ya Ofisi hii.

**Uelewa mdogo kuhusu masuala ya Muungano:**

**Mheshimiwa Spika**, masuala ya Muungano yameainishwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka, 1977 pamoja na marekebisho yake. Kwa kiasi fulani masuala haya bado hayajaeleweka vya kutosha mionganoni mwa wananchi hivyo, kusababisha manung'uniko yasiyo ya lazima kuhusu Muungano. Endapo

elimu ya kutosha itatolewa changamoto hii itapungua au kumalizika kabisa.

**Fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutokufamika mionganoni mwa Wajumbe wa baraza la wawakilishi Zanzibar, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Wananchi:**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipeleka fedha katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya shughuli za kibajeti na kugharamia masuala mbalimbali ya maendeleo na kijamii. Hata hivyo, mchango huo haufahamiki mionganoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi jambo linalofanya kuwepo kwa kauli potofu kuhusu Mchango wa Serikali ya Muungano kwa Zanzibar.

**Kuwepo kwa Jengo la ghorofa linalomilikiwa na mtu binafsi jirani na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar:**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo ambapo Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais iliyopo Tunguu Zanzibar kuna jengo la ghorofa la mtu binafsi karibu sana na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Jengo hilo ni refu kiasi cha kumwezesha mmiliki wa jengo hilo kuona shughuli zote zinazofanyika katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais jambo ambalo sio sahihi kiusalama.

#### **4.0 MAONI ,USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama yalivyowasilishwa kwa kila fungu, yafuatayo ni maoni na mapendekezo ya Kamati:

##### **4.1 MAKAMU WA RAIS NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Fungu 26 na Fungu**

**31**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa uratibu mzuri inaoufanya katika masuala ya Muungano, hususan, katika kushughulikia hoja 9 kati ya 13 za Muungano zilizowasilishwa katika vikao vya kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jitihada hizo ni kubwa na zenye azma ya kumaliza changamoto ndogondogo zinazoukabili Muungano wetu ili kuhakikisha kuwa unadumu na mahusiano baina ya pande mbili za Muungano yanaimarika katika ustawi wa Wananchi wetu na kwa faida ya vizazi vijayvo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada hizo, Kamati inaona kwamba bado iko haja ya kuongeza nguvu zaidi katika kushughulikia masuala ya Muungano kwa lengo la kuboresha Muungano wa Nchi yetu. Hivyo basi Kamati inashauri ifuatavyo:

- i) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu na faida ambazo zinazotokana na Muungano kwa pande zote mbili ili kuwawezesha wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi mapana ya nchi yetu na kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.
- ii) Kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa kuna fedha zinazopelekwa Zanzibar kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kusaidia shughuli mbalimbali za kibajeti, kiuchumi na kijamii, fedha ambazo hazifahamiki miongoni mwa wananchi, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais iweke utaratibu wa kutoa taarifa/elimu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wananchi kwa ujumla kuhusu namna na kiasi gani cha fedha Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaichangia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ili kuondoa dhana potofu inayoenezwa kwa Wazanzibar kuwa hakuna mchango wowote unaotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Elimu hiyo itasaidia wananchi kuthamini na kuuenzi muungano wetu.

Mfano katika Mwaka wa fedha 2013/214 kwa kipindi kinachoishia Machi, 2014, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepeleka fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama ifuatavyo:

- (a) Gawio la misaada na mikopo ya kibajeti ( General Budget Support-GBS) **Sh. 27,190,502.190.97** kati ya Sh. **32,627,535,000** zilizoidhinishwa na Bunge.
- (b) Pay as you Earn (PAYE)**Sh. 15,750,000,000.**
- (c) Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo **Sh.1,243.925,860.**
- (d) Fedha za kugharamia maadhimisho ya miaka hamsini ya Mapinduzi ya Zanzibar **Sh. 600,000,000**

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- iii) Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo mratibu Mkuu wa Mambo ya Muungano na ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kamati inashauri kwamba pale ambapo kuna fedha zozote zinazopelekwa Zanzibar kupitia Hazina au mamlaka yoyote, taarifa kuhusu fedha hizo ziwasilishwe Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano kwa ajili ya kumbukumbu na kuujulisha Umma wa Watanzania.
- iv) Kutokana na Serikali kujenga Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar chini ya kiwango na kutumia fedha nyingi za wananchi, Kamati inashauri Serikali kuwa makini wakati wa uteuzi wa Makandarasi ili kuhakikisha kuwa wanaopewa tenda za ujenzi wa Ofisi nyeti kama ya Makamu wa Rais wanakuwa na uwezo, ujuzi na weledi wa hali ya juu. Aidha, Wakala wa Majengo ya Serikali Nchini (TBA) iwe makini wakati wote kukagua ili kuhakikisha kuwa majengo ya Serikali yanajengwa kwa ubora na viwango stahiki. Pia TBA ihakikishe kwamba Serikali kwa namna yoyote ile haikabidhiwi jengo lililojengwa chini ya kiwango ili kuhakikisha kuwa Serikali haipati hasara kwa kupoteza fedha nyingi katika kugharamia ujenzi wakati majengo ya Serikali yanajengwa chini ya kiwango.
- v) Kamati inashauri kwamba ujenzi wa jengo la Ofisi na makazi ya Makamu Rais Zanzibar ambao umebainika kuwa na mapungufu makubwa kama vile nyufa katika jengo la makazi, shata za madirisha ya mbao kuchakaa, mfumo wa viyoyozi kutofanya kazi yarekebishwe ili kuondoa mapungufu hayo kabla ya kukabidhiwa. Aidha, samani za kutosha na bora kwa ajili ya jengo hilo zinunuliwe ili Ofisi hiyo ianze kutumika.
- vi) Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zifanye mazungumzo na mmiliki wa jengo lililo jirani na Ofisi ya makamu wa Rais kwa lengo la kulinunua kwa kuimarisha usalama wa ofisi na makazi hayo.
- vii) Pamoa na kuwa baadhi ya kero za Muungano kama vile suala la Hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, mafuta na gesi, mgawanyo wa fedha za wafadhli na malalamiko ya wafanyakishara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili wanapoleta bidhaa zao Tanzania Bara zipo katika hatua mbalimbili za kushughulikiwa na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali zote mbili, Kamati inashauri kuwa kwa kuwa Serikali yetu iko katika mchakato wa utungaji wa Katiba Mpya na Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu ni Wajumbe wa Bunge hilo, ni vyema kupitia mchakato huo watakapofikia katika eneo hilo watafakari kwa kina namna ya kuzimaliza kero zote kwa lengo la kuimarisha na kudumisha Muungano wetu.

- viii) Kamati inashauri kwamba mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha Mwaka 2006 kuhusu utaratibu wa mgawanyo wa fedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yatolewe uamuzi haraka ili kuondoa kero hii ya muda mrefu na utekelezaji wake uanze mara moja.
- ix) Kutokana na majukumu muhimu ya Ofisi ya makamu wa Rais, Kamati inaendelea kuishauri serikali kuongeza bajeti na kutoa kwa wakati fedha zinazoidhinishwa ili kumuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
- x) Serikali iendelee kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ili waweze kutekeleza majukumu yao na kuleta tija katika ofisi na Taifa kwa ujumla.
- xi) Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na mambo mengine kuratibu ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivyo, Kamati inashauri kazi hii iendelezwe kupitia vikao vya kisekta kila inapohitajika ili kuimarisha ushirikiano huu wa kihistoria.

## 5.0 MAOMBI YA FEDHA NA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano inaomba fedha kwa mwaka 2014/2015 kwa muhtasari kwa mafungu 26 na 31 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya kamati yangu. Aidha hatuna budikukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bungekwa kuliongoza Bunge letu utukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa. Napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Naibu Waziri Mhe. Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa ushirikiano mkubwa waliooutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

- (i) Mhe. William M.Ngeleja, Mb - Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Gosbert B. Blandes, Mb - M/ Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb - Mjumbe
- (iv) Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb - Mjumbe
- (v) Mhe. Nimrod Elirehemu Mkono, Mb - Mjumbe
- (vi) Mhe. Halima J. Mdee, Mb - Mjumbe
- (vii) Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb - Mjumbe
- (viii) Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb - Mjumbe
- (ix) Mhe. Ali Khamis Seif, Mb - Mjumbe
- (x) Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb - Mjumbe
- (xi) Mhe. Abdallah Sharia Ameir, Mb - Mjumbe
- (xii) Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb - Mjumbe
- (xiii) Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb - Mjumbe
- (xiv) Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
- (xv) Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb - Mjumbe
- (xvi) Mhe. Jason S. Rwekiza, Mb - Mjumbe
- (xvii) Mhe. Nyambari C.M. Nyangwine, M - Mjumbe
- (xviii) Mhe. Ramadhan Haji Saleh - Mjumbe
- (xix) Mhe. Zahra Ali Hamad - Mjumbe
- (xx) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Matamus Fungo na ndugu Maria Mdulugu, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kama yalivyowasilishwa na Mto Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe.William Mganga Ngeleja (Mb.)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA**

Mei, 2014

**Taarifa ya Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEIGR (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya na kuweza kusoma taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2013/2014, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kanuni ya 99(9), Toleo la mwaka 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Mazingira - Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, 2013 kifungu cha 6(8) na kifungu cha 7(1), kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na kuchambua bajeti ya ofisi hii, kuisimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 4 Mei, 2014 Kamati ilikutana katika ukumbi wa Benki Kuu, Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pamoja na wataalam wake na kupokea taarifa ya ofisi kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mwaka wa fedha 2013/2014 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua bajeti hiyo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipata fursa ya kujadili utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na malengo yanayoombwa fedha kwa mwaka 2014/2015.

Pili, muhtasari wa kazi zilizotekelawa na Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Tatu, utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili bajeti ya mwaka wa fedha wa 2013/2014 na mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji na ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa majadiliano ya bajeti ya mwaka 2013/2014. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2013/2014; Kamati ilitoa ushauri katika maeneo mbalimbali kwa Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati japokuwa kuna maeneo ambayo Serikali haijayatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya ofisi hii, hasa kwa Idara ya Mazingira na NEMC kwa miaka mitatu mfululizo; 2011/2012, 2012/2013 na 2013/2014, bado Serikali imeendelea kutenga fedha kidogo ambapo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya sh. 5,184,372,000 zilitengwa ikiwa ni pungufu kwa asilimia 3.5 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha wa 2012/2013 ambapo ofisi hii ilitengewa Sh. 5,372,218,000. Katika hali halisi fedha hizi hazitoshelezi mahitaji ya msingi katika kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango mingi inayopangwa na Serikali haiwezi kufanikiwa iwapo mazingira yatakuwa yameharibika. Mipango mizuri kama ya Kilimo Kwanza, umeme, inayotokana na maji haiwezi kufanikiwa kama mazingira hayako salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatenga fedha kidogo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambapo ni ya pili kwa umuhimu baada ya Ofisi ya Rais. Fedha kidogo zinazotengwa haziwiani na kazi za idara hii muhimu ya sekta yenye, lakini pia na uzito wa ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bajeti hiyo finyu, Serikali imeonesha uwezo mdogo katika kusimamia kanuni ya matumizi ya mifuko ya plastiki na kuhakikisha inatekelezwa kama ilivyo katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Ni dhahiri kwamba, mazingira yameendelea kuchafuliwa kwa kuzagaa ovyo kwa mifuko hii katika miji yetu ikiwa ni pamoja na maeneo ya fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutimiza ahadi yake ili kulinda mazingira na afya za wananchi kutokana na madhara yanayojitokeza. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia na kuyafanya kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ili kazi ya kutunza na kuhifadhi mazingira ifanikiwe kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2013/2014. Matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu 31 iliidhinishiwa Sh. 55,682,428,000 ambapo kati ya hizo mishahara ilikuwa Sh. 1,980,404,000 na Sh. 42,710,545,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kiasi hicho kinajumuisha Sh. 32,627,535,000/= kwa ajili ya mgao wa kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na fedha za Ruzuku za NEMC Sh. 3,164,303,000/=. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 ofisi ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya Sh. 54,827,487,289/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 98.5 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya Sh. 55,682,429,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, ziliidhinishwa jumla ya Sh. 12,971,883,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh. 3,700,000,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na Sh. 9,271,803,000/= zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 jumla ya Sh. 2,967,056,886/= tu, ambazo ni fedha za ndani zilikuwa zimetolewa, sawa asilimia 22 ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii kwa mara nyingine inadhihirisha kilio cha Kamati kuhusu Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kwani mpaka mwezi Machi, 2014, ikiwa ni miezi tisa toka mwaka wa fedha 2013/2014 uanze, hakuna fedha yoyote iliyotolewa kutoka kwa wadau wa maendeo. Utugemezi huu kwa wahisani unasababisha miradi mingi ya maendeleo kutotekelzeka.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kamati inaishauri Serikali kuacha kutegemea sana misaada kutoka nje na badala yake ianze kujenga uwezo wake wa ndani kwa kuwa imedhihirika kwamba, misaada ya wafadhili haina uhakika kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kukabiliwa na ufinyu wa bajeti, bado imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

Kwanza, kuendelea kutoa elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa umma kupitia warsha, maadhimisho, maonesho na njia nyinginezo.

Mbili, kuendelea kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira chini ya ufadhilli wa DANIDA na Canada CIDA. Kwa kipindi hiki ofisi imeweza kuandaa mwongozo wa kuendesha Mfuko wa Mazingira, mwongozo wa kusimamia fedha za Mfuko wa Mazingira na kuondoa utaratibu wa kuendesha Baraza la Usuluhishi la Mazingira.

Tatu, kuratibu na kutekeleza Mikataba minne ya Kimataifa ya mazingira ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Nne, kutekeleza Sheria ya usimamizi wa Mazingira, ambapo Baraza la NEMC kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi limeanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira.

Tano, kuendelea kuratibu, kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya mazingira kwa kufanya kaguzi katika viwanda na shughuli za uzalishaji zaidi ya sabini, na kubomoa ujenzi uliokiuika Sheria katika maeneo ya mikondo ya mito, Mikoko jijini Dar es Salam.

Sita, kuendelea kusajili Wataalam wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Uguzi wa Mazingira, na Kukagua Miradi ya Maendeleo ili kuhakikisha kuwa inatekeleza matakwa yaliyoainishwa kwenye hati ya TAM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (Changamoto), kama ilivyoolezwa hapo awali, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, ufinyu wa Bajeti unaendelea kuwa na changamoto kubwa inayosababisha kutotekelawa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa.

Aidha, Changamoto nyingine ambazo zimeendelea kuikabili Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ni pamoja na:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- Uelewa mdogo wa Jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa Mazingira;
- Kukosekana kwa Takwimu sahihi ya Mazingira, kwa wakati; na
- Mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa katika Hifadhi na utunzai wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuihiza Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kuweka, kusimamia na kutekelza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizi. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

- Kuendelea kutoa Elimu kwa Umma kwa kutumia fedha kidogo, wanayoipata katika Bajeti, lakini pia kwa fedha inayotokana na miradi mbalimbali ambayo huiandika;
- Kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoka mafunzo na vifaa kwa waratibu wa mazingira wa Sekta mbalimbali na Maafisa Mazingira wa Serikali za Mitaa; na
- Kuendela kuhamasisha Serikali za Mitaa, kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2014/2015, Kamati ilijulishwa kwamba Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi yamezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano. Mkakati wa Pili wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania (MKUKUTA II) na maoni na mapendekezo ya Bunge wakati wa kujadili, Mipango ya Bajeti ya Ofisi, ni kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Hivyo basi, fedha kiasi cha Sh. 62,763,465,000/= katika mwaka wa fedha 2014/2015, zinaombwa kwa ajili ya Fungu 31. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida Sh. 56,200,719,000/= na fedha za matumizi ya maendeleo Sh. 6,562,746,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha matumizi ya kawaida, kinajumlisha fedha za mgao wa asilimia 4.5 ya bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sh. 44,039,608,000/=. Hivyo Idara ya Mazingira imetengewa kiasi cha Sh. 6,091,039,000/= ambazo zinajuisha Sh. 3,832,091,000/= za fedha za ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingifra (NEMC).

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande fedha za maendeleo, jumla ya Sh. 6,562,746,000/= zimetengwa ambazo zinajumuisha fedha za ndani Sh. 500,000,000/= na fedha za Nje Shilingi Bilioni 2,062,746,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya bajeti Ofisi ya hii, na kupitia Kifungu kwa Kifungu, hivyo ninaliomba Bunge lako Tukufu, likubali, kujadili maombi hayo yenye jumla Sh. 55,682,428,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili kwa kina Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Rais (Mazingira), Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza japo kidogo Bajeti kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuyapa mazingira uzito unaostahili, kwa kuongeza Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), hasa kwa kuzinfatia kuwa mazingira ni Sekta mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira hasa katika Sekta ya Kilimo, Misitu, Mifugo, Nishati, Maji; inasikitisha koonaa kwamba Serikai yetu bado haijatoa kipaumbele katika suala la Mazingira. Ni ukweli usiofichika kwamba ili kuwa na maendeleo endelevu, lazima uhifadhi wa mazingira upewe kipaumbele. Hii itawezekana endapo tu Serikali itatambua umuhimu huu na kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi na mazingira.

Mfano, mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbali mbali za nchi, ni athari zinatotokana na uharibifu wa mazingira, na hivyo kuigharimu Serikali fedha nyingi kurekebisha miundombinu iliyoharibiwa.

Mheshimiwa Mweleyekiti, Kamati inapendekeza kwamba, kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Fungu 31, hujumuisha mgawo wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar, na kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa chini ya Fungu 31, ni pesa nyingi ukilinganisha na zinazobaki kwa ajili ya Idara ya Mazingira. Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu kuipatia Idara ya Mazingira na Baraza lake Fungu la pekee, ili kiasi hiki cha fedha zinazotengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira, ijulikane wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maoni ya Kamati hii, kwa Ofisi ya mwaka wa fedha 2013/2014, ilikuwa ni Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi na maendeleo kwa kuwa fedha za nje hazina uhakika wa kupatikana.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kamati inafarijika kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, ambapo kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015, Serikali imetenga fedha za ndani Sh. 4,500,000,000/= ikilinganishwa na Sh. 2,062,746,000/= fedha za nje. Hii ni dalili nzuri. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za ndani zaidi na za kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyo kusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa ya Idara ya Mazingira ni uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira, hasa Sheria ya Mazingira, Na. 20 ya mwaka 2004. Sheria hii inasema wazi kwamba itakuwa ni makosa kufanya shughuli zifuatazo, bila kupata kibali cha Waziri mwenye dhamana ya Mazingira:-

- Kujenga jengo au umbile lolote kwenye fukwe za bahari; ziwa, ukingo wa mito au bwawa;
- Kufukua au kutoboa fukwe na kingo za mito;
- Kuchepusha na kuzuia mito; na
- Kufanya shughuli za kudumu za kibinadamu, ujenzi wa nyumba ndani ya mita sitini kutoka baharini au kwenye kingo za mito ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha ulinzi wa mazingira na utunzaji wa bahari au kingo za mito. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kuhusu kuwepo kwa ujenzi usiofuata sheria katika maeneo ya fukwe na kingo za mito. Halili hii inasababishwa na wananchi aidha kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Mazingira, ama kukaidi Sheria hiyo kwa sababu ya rushwa. Ujenzi huu, hasa katika kingo za mito unathihiri mazingira ya asili ya mito ikiwa ni pamoja na kupindisha mikondo ya mito. Hali hii, ni ya hatari kwani, imekuwa ikisababisha mafuriko kwa upande ambao mito imeelekezwa na hivyo kuharibu mazingira. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013, Kamati ilitoa agizo hili ambalo halikutekelezwa. Kamati inataka Serikali, kubomoa nyumba zote zilizojengwa kinyume cha sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari. Ili kurudisha mito iliyodhihirika katika hali yake ya asili na kuondoa athari kubwa ya kimazingira, zinazoweza kutokea.

Kamati inataka kujua maendeleo ya zoezi la uchunguzi wa hati za nyumba zilizojengwa kinyume cha sheria. Aidha, pale ambapo ikibainika kwamba, waliojenga katika maeneo tuliyotaja kwa kupewa vibali, kama vile

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hati, kinyume cha sheria waliohusika na vigendo hivi kifisadi vyakutoa vibali, au hati wakomeshwe na kufikishwa katika vombo vyakheria. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni dhahiri kwamba wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faida zake, hususan wakati huu ambapo kuna changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabia nchi. Adhari mbalimbali zimeendelea kutokea kutokana na uharibifu wa mazingira. Vitendo vyakuharibu vyanzo vyakheria, ukatani hovyo wa miti na utupaji hovyo wa taka ni vitendo vilivyofanyika kwa kiasi kikubwa kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira mionganoni mwa wananchi . (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kwamba Serikali itengete fedha za kutosha ili kuiwezesha Idara ya Mazingira, kuendeleza Program ya Elimu kwa Umma itakayoleta mafanikio. Kamati inaishauri Serikali kutambua umuhimu wa elimu hii na kuongeza Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo Oktoba, 2006 Serikali ilitoa agizo la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji na matumizi ya mifuko ya plastics, yenye unene chini ya mikroni 30. Agizo hili lilitirudiwa tena mwezi Agosti, 2013. Aidha, Serikali iliahidi kuchukua hatua ya kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko laini ya plastic ili kulinda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kutekeleza agizo lake na kuimarissha Kanuni ya kudhbibti matumizi ya mifuko ya plastics mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo hili sugu la uchafuzi wa mazingira ambalo linatia aibu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo, ni pendekezo la Kamati kwamba Serikali isimamie usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji taka hovyo. Vile vile elimu ya utunzaji, usafi wa mazingira, iwekwe kwenye mitaala katika Shule za Msingi ili kuwajengea wanafunzi utamaduni wa kuwa na mazingira safi yaliyohifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali za Mitaa zimeendelea kuwa na mwitikio mdogo kwa hifadhi za utunzaji wa mazingira, Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kufuatilia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo za Hifadhi ya Misitu, Hifadhi ya Vyano Vya Maji, Tathmini ya Mazingira na Usafi wa Mazingira.

Kamati inazipongeza Halmashauri ziliozoanza kutunga na kutekeleza Sheria ndogo hizo na kutoa msisitizo kwa Halmashauri nyingine kuiga mfano huo. Halmashauri zilizotunga Sheria ndogo zinazohusu mazingira ni Manispaa ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Moshi, Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Wilaya Njombe, Babati, Singida Vijijini, Iramba, Bahi, Mbeya Vijijini na Mpanda.

Kamati inaishauri Serikali itafute namna mpya ya kuhimiza suala la usafi wa mazingira badala ya utaratibu uliozoleka kutenga siku moja kwa mwezi kwa ajili ya kufanya usafi wa Mazingira. Kuna haja ya kubadili mikakati ili tuwe na utamaduni wa kila siku au mara kwa mara, na kuwe na motisha kwa ajili ya Halmashauri, Manispaa, zitakazoshinda kwa utunzaji wa mazingira.

Kamati inapendekeza pia kuwe na utaratibu wa kutoa hati chafu, kwa Halmashauri au Manispaa zilizofanya vibaya katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgogoro wa kimamlaka katika baadhi ya Sekta na Idara za Mazingira. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo ambayo huhifadhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, kama vile maeneo ya hifadhi za misitu, fukwe na vyanzo vya maji. Hata hivyo, bado mamlaka nyingine za Halmashauri na Wizara kwa kutumia sheria zao zinaendelea kutoa vibali kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile ujenzi kando kando ya mito fukwe na bahari.

Ni rai ya Kamati kwamba kwa kuwa Mamlaka hizi zipo chini ya Serikali moja, zishirikiane kwa pamoja kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi inayoendelea kukua kwa kasi nchini. Kamati inashauri Serikali iweke mfumo wa mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, na Maofisa wa Mazingira wa Sekta na Halmashauri ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria.

Aidha, Maofisa Mazingira wa Sekta na Halmashauri, washirikishwe katika kutoa maamuzi ya mipango ya matumizi ya ardhi na maamuzi mbalimbali ya kisekta. Ofisi ya Makamu wa Rais, ishirikiane na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili utekelezaji wa miradi mbalimbali uweze kuzingatia masuala ya mazingira. Kamati inaiagiza Serikali, ifuatilie utekelezaji wa masharti yaliyotolewa kwa Mradi wa Dar es Salaam, Rapid Transport (DARTs), wakati walipopewa Hati ya tathimini ya Mazingira (TAM), kama yamezingatiwa.

Mheshiiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa suala la mabadiliko ya tabia nchi limeendelea kuleta athari nyingine ikiwa ni pamoja na ukame na mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini na duniani kote. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kukuza uweledi kuhusu tatizo hili na jinsi ya kukabiliana nalo kwa wananchi wote, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha upandaji wa miti na kuzuia kilimo kisichofuata utaratibu kwa miinuko kinachosababisha maporomoko ya ardhi na mmomonyoko wa udongo.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha, Kamati inashauri, Sera ya Mabadiliko ya Tabia nchi ianzishwe ili itoe mwongozo kwa Serikali, Taasisi na Mashirika mbalimbali kuhusu uhuishaji wa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi katika mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira ambacho tayari kimeanza kazi. Kamati inaamini kabisa kwamba ushirikiano wa Kitengo hiki na Baraza la NEMC, utafanikisha shughujli za Ukaguzi hasa kwa viwanda na hatimaye kukamata wahalifu wa mazingira. Kamati inashauri Kitengo cha Polisi, Mazingira, kiimarishwe na kiboreshwae zaidi ili wasiwe wanausbiri kuitwa, bali wajengewe uwezo wa kufanya ufuatiliaji wa masuala ya mazingira. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), na Naibu Waziri, Mhehsimiwa Ummy Mwalimu, Ndugu Sozi M. Saluta, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, ikiwa ni pamoja na Wataalam wote wa Ofisi hii na Baraza la Taifa la Hifadhi la NEMC, kwa ushiriano, ushauri na utaalam wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu...

**MWENYEKITI:** Acha kushukuru, maliza!

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR – (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majina ya Wajumbe yaingie moja kwa moja kwenye Hansard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusoma hayo, na kwa kuzingatia kwamba haja kubwa ya Kamati ni ufinyu wa Bajeti usiotosheleza utekelezaji wa malengo katika Idara ya Mazingira kwa miaka mitatu mfululizo; mwaka 2012/2013, 2014/2015, na kwa kuwa jambo hili sasa linashughulikiwa na Kamati ya kudumu ya Bajeti, naomba kuwasilisha. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**Maoni ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRAKUHUSU  
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS -MAZINGIRA KWA  
MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014; PAMOJANA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MATUMIZIYA OFISI HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9) Toleo la Mwaka 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira (**Fungu-31**), kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;

**1.2 Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge (2013) Kifungu namba 6(8) na 7 (1)kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kuchambua Bajeti ya Ofisi hii; kusimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 04/05/2014 Kamati ilikutana katika ukumbi wa Benki Kuu Dar ES Salaam na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) pamoja na wataalam wake, na kupokea Taarifa ya Ofisi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

**1.4 Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Bajeti hiyo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipata fursa ya kujadili:-

1.4.1 Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais( Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na malengo yanayoombewa fedha kwa Mwaka wa 2014/2015;

1.4.2 Muhtasari wa kazi zilizotekelawa na Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;

1.4.3 Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2013/2014; na

1.4.4 Mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI ULIOTOLEWA WAKATI WA MAJADILIANO YA BAJETI KWA MWAKA WA 2013/2014

**2.1 Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa 2013/2014, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo mbali mbali kwa Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

**2.2 Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati japokuwa kuna maeneo ambayo Serikali haijayatekeleleza ipasavyo kama inavyoainishwa hapa chini:-

- **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi hii hasa kwa Idara ya Mazingira na NEMC kwa miaka mitatu mfululizo (**2011/2012; 2012/2013 na 2013/14**), bado Serikali imeendelea kutenga fedha kidogo ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa **2013/2014** jumla ya shilingi **5,184,372,000/=** zilitengwa ikiwa ni pungufu kwa asilimia **3.5** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha wa **2012/2013** ambapo Ofisi hii ilitengewa Shilingi 5,372,218,000/=. Katika hali halisi fedha hizi hazitoshelezi mahitaji ya msingi katika kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Mipango mingi inayopangwa na Serikali haiwezi kufanikiwa iwapo mazingira yatakuwa yameharibika. Mipango mizuri kama ya Kilimo Kwanza, umeme unaotokana na maji n.k haiwezi kufanikiwa kama mazingira hayako salama.

- **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatenga pesa kidogo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni ya pili umuhimu baada ya Ofisi ya Rais. Fedha kidogo zinazotengwa haziwiani na Kazi za Idara hii, umuhimu wa sekta yenyelewe lakini pia na uzito wa Ofisi.

- **Mheshimiwa Spika**, kutokana na bajeti hiyo finyu, Serikali imeonesha uwezo mdogo katika kusimamia Kanuni ya matumizi ya mifuko ya plastiki na kuhakikisha inatekelezwa kama ilivyo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni dhahiri kwamba mazingira yameendelea kuchafuliwa kwa kuzagaa ovyo kwa mifuko hii katika miji yetu ikiwa ni pamoja na maeneo ya fukwe. Kamati inaishauri Serikali kutimiza ahadi yake ili kulinda mazingira na afya za wananchi kutokana na madhara yanayojitokeza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ili kazi ya kutunza na kuhifadhi mazingira ifanikiwe kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

### 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

### **3.1 MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Rais **Fungu 31** iliidhinishiwa Shilingi **55,682,428,000/=** ambapo kati ya hizo mishahara ilikuwa shilingi **1,980,404,000/=** na shilingi **42,710,545,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Aidha, kiasi hicho kinajumuisha shilingi **32,627,535,000/=** kwa ajili ya mgao wa kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na fedha za ruzuku za NEMC shilingi **3,164,303,000/=** Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Ofisi ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi **54,827,487,289/=** kwa ajili matumizi ya kawaida sawa na asilimia **98.5** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya shilingi **55,682,428,000/=**.

### **3.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ziliidhinishwa jumla ya Shilingi **12,971,883,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo; kati ya fedha hizo shilingi **3,700,000,000/=** zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi **9,271,803,000/=** zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 jumla ya Shilingi **2,867,056,886/=** tu ambazo ni fedha za ndani zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 22 ya bajeti ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii kwa mara nyine, inadhihirisha kilio cha Kamati kuhusu Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwani mpaka Mwezi Machi 2014, ikiwa ni miezi 9 toka mwaka wa fedha 2013/2014 uanze, hakuna fedha yoyote kutoka kwa wadau wa maendeleo imetolewa. Utetemezi huu kwa wahisani unasababisha miradi mingi ya maendeleo kutokutekelezeka. Kamati inaishauri Serikali kuacha kutegemea sana misaada toka nje na badala yake ianze kujenga uwezo wake wa ndani, kwa kuwa imedhihirika kwamba misaada ya wafadhili haina uhakika wa kupatikana kwa wakati.

## **4.0 MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

### **4.1 MAFANIKIO**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kukabiliwa na ufinyu wa bajeti, bado imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

4.1.1 Kuendelea kutoa elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa umma kuitia warsha; maadhisho; maonesho na njia nyinginezo;

4.1.2 Kuendelea kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira chini ya ufadhilli wa DANIDA na CANADA CIDA. Kwa kipindi hiki Ofisi imeweza kuandaa mwongozo wa kuendesha mfuko wa mazingira, mwongozo wa kusimamia fedha za mfuko wa mazingira na kuandaa utaratibu wa kuendesha Baraza la usuluhishi la Mazingira.

4.1.3 Kuratibu na kutekeleza Mikataba minne (4) ya Kimataifa ya Mazingira ikiwa ni pamoja na Mkataba wa mabadiliko ya Tabianchi.

4.1.4 Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ambapo Baraza (NEMC) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi limeanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira.

4.1.5 Kuendelea kuratibu, kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa kufanya kaguzi katika viwanda na shughuli za uzalishaji zaidi ya 70 na kubomoa ujenzi ulioukiuka Sheria katika maeneo ya mikondo ya mito na mikoko Jijini Dar es Salaam;

4.1.6 Kuendelea kusajili wataalam wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na ukaguzi wa Mazingira na kukagua miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa inatekeleza matakwa yalioanishwa kwenye hati za TAM.

## 4.2. CHANGAMOTO

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo awali, pamoja na mafanikio yaliyopatikana ufinyu wa bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa inayosababisha kutotekelawa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa. Aidha, changamoto nyingine ambazo zimeendelea kuikabili Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ni pamoja na:-

4.2.1 Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira;

4.2.2 Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati;

4.2.3 Mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa katika hifadhi na utunzaji wa mazingira.

**4.3 Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuihimiza Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuweka, kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

- kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia fedha kidogo wanayopata katika bajeti, lakini pia kwa fedha inayotokana na miradi mbalimbali ambayo huiandika;
- kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa mafunzo na vifaa kwa waratibu wa mazingira wa sekta mbalimbali na maafisa mazingira wa Serikali za Mitaa; na
- Kuendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo.

## **5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**5.1 Mheshimiwa Spika**, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2014/2015, Kamati ilijulishwa kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yamezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka 5, Mkakati wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), na maoni na mapendekezo ya Bunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa 2013/2014.

**5.2 Mheshimiwa Spika**, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vyta majukumu ya Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Hivyo basi, fedha kiasi cha shilingi **62,763,465,000/=** katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 zinaombwa kwa ajili ya Fungu **31**. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi **56,200,719,000/=** na fedha za matumizi ya maendeleo shilingi **6,562,746,000/=**.

**5.3 Mheshimiwa Spika**, kiasi cha matumizi ya kawaida kinajumuisha fedha za mgao wa asilimia **4.5** ya bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi **44,039,608,000/=** hivyo Idara ya Mazingira imetengewa kiasi cha shilingi **6,091,039,000/=** ambazo zinajumuisha shilingi **3,832,091,000/=** za fedha za ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

**5.4 Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya shilingi **6,562,746,000/=** zimetengwa ambazo zinajumuisha fedha za ndani shilingi **4,500,000,000/=** na fedha za nje shilingi **2,062,746,000/=**.

**5.5 Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii na kupitia Kifungu kwa Kifungu. Hivyo naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili maombi hayo yenye jumla ya shilingi 55,682,428,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuujadili kwa kina Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

**6.1 Mheshimiwa Spika**, awali ya yote Kamati inaipongeza Serikali kwa kuungeza japo kidogo bajeti kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira . Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuyapa Mazingira uzito unaostahili kwa kuungeza bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira hasa kwa kuzingatia kuwa mazingira ni sekta mtambuka.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira hasa katika sekta za kilimo, misitu, mifugo, nishati, maji n.k, inasikitisha kuona kwamba Serikali yetu bado hajatoa kipaumbele katika suala la mazingira. Ni ukweli usiofichika kwamba ili kuwa na maendeleo endelevu lazima uhifadhi wa mazingira upewe kipaumbele. Hii itawezekana endapo tu Serikali itatambua umuhimu huu na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira. Mfano mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali za nchi ni athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira na hivyo kuigharimu Serikali fedha nyingi kurekebisha miundombinu iliyoharibiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwamba, kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Fungu 31 hujumuisha mgao wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa chini ya **Fungu 31** ni pesa nyingi kulinganisha na zinazobaki kwa ajili ya Idara ya Mazingira, Serikali kuitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuipatia Idara ya Mazingira na Baraza lake Fungu la pekee ili kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira kijulikane wazi.

**6.2 Mheshimiwa Spika**, Moja ya maoni ya Kamati hii kwa Ofisi kwa Mwaka wa fedha **2013/2014**, ilikuwa ni Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kwa kuwa fedha za nje hazina uhakika wa kupatikana.

Kamati inafarrijika kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa ambapo, kwa Mwaka ujao wa fedha **2014/2015**, Serikali imetenga fedha za ndani Tsh. **4,500,000,000/=** ikilinganishwa na **2,062,746,000/=** fedha za nje. Hii ni dalili nzuri.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za ndani zaidi na za kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa;

**6.3 Mheshimiwa Spika**, Moja ya changamoto kubwa ya Idara ya Mazingira ni uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira hasa Sheria ya Mazingira namba 20 ya Mwaka 2004. Sheria hii inasema wazi kwamba itakuwa ni makosa kufanya shughuli zifuatazo bila kupata kibali cha Waziri mwenye dhamana ya mazingira:-

- Kujenga jengo au umbile lolote kwenye fukwe za bahari, ziwa, ukingo wa mto au bwawa;
- Kufukua/kutoboa fukwe na kingo za mito;
- Kuchepusha au kuzuia mito;

Kufanya shughuli za kudumu za kibanadamu(ujenzi wa nyumba)ndani ya mita 60 kutoka baharini au kwenye kingo za mito ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha ulinzi wa mazingira na utunzaji wa bahari au kingo za mito.

**Mheshimiwa Spika**, waheshimiwa wabunge ni mashahidi kuhusu kuwepo kwa ujenzi usiofuata Sheria katika maeneo ya fukwe na kingo za mito. Hali hii inasababishwa na wananchi aidha kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Mazingira ama kukaidi Sheria hiyo au kwa sababu rushwa. Ujenzi huu hasa katika kingo za mito unaathiri mazingira ya asili ya mito ikiwa ni pamoja na kupindisha mikondo ya mito. Hali hii ni ya hatari kwani imekuwa ikisababisha mafuriko kwa pande ambazo mito imeelekezwa na hivyo kuharibu mazingira;

**Mheshimiwa Spika**, mwaka jana Kamati ilitoa agizo hili ambalo halikutekelezwa. Kamati inaitaka Serikali kubomoa nyumba zote zilizojengwa kinyume cha Sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari ili kurudisha mito iliyothirika katika hali yake ya asili na kuondoa athari kubwa ya kimazingira zinazoweza kutokea; Kamati inataku kujua maendeleo ya zoezi la uchunguzi wa hati za nyumba zilizojengwa kinyume cha sheria.

Aidha, pale ambapo ikibainika kwamba waliojenga katika maeneo tuliyoyataja kwa kupewa vibali kama vile hati n.k kinyume cha Sheria, waliohusika na vitendo hivi vyta kifisadi vyta kutoa vibali au hati wakamatwe na kufikishwa katika vyombo vyta Sheria.

**6.4 Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, ni dhahiri kwamba wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faida zake hususan wakati huu ambapo kuna changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabia nchi.

Athari mbalimbali zimeendelea kutoea kutokana na uharibifu wa mazingira. Vitendo vya kuharibu vyanzo vya maji, ukataji ovyo wa misitu na utupaji ovyo wa taka ni vitendo vinavyofanyika kwa kiasi kikubwa kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira mionganoni mwa wananchi;

Kamati inaona kwamba, Serikali itenye fedha za kutosha ili kuiwezesha Idara ya Mazingira kuendesha programu ya elimu kwa umma itakayoleta mafanikio. Kamati inashauri Serikali kutambua umuhimu wa elimu hii na kuongeza bajeti hii;

**6.5 Mheshimiwa Spika**, Mnamo Oktoba 2006, Serikali ilitoa agizo la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni thelathini (30). Agizo hili lilitrudiwa tena mwezi Agosti 2013. Aidha Serikali iliahidi kuchukua hatua ya kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko laini ya plastiki ili kulinda mazingira. Hata hivyo, ni dhahiri kabisa agizo hilo halijatekelezeka kwani mazingira yetu yameendelea kuchafuliwa na mifuko hiyo hususan maeneo ya mijini na kwenye fukwe za bahari ya Hindi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza agizo lake na kuisimamia kanuni ya Kudhibiti Matumizi ya Mifuko ya Plastiki mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo hili sugu la uchafuzi wa mazingira ambalo linaitia aibu nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Sanjari na hilo, ni pendekazo la Kamati kwamba Serikali isimamie usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji taka ovyo. Vilevile elimu ya utunzaji/usafi wa mazingira iwekwe kwenye mitaala katika shule za misingi ili kuwajengea wanafunzi utamaduni wa kuwa na mazingira safi na yaliyohifadhiwa vizuri;

**6.6 Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali za Mitaa zimeendelea kuwa na mwitikio mdogo katika hifadhi na utunzaji wa Mazingira, Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Makamu wa Rais- mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI kufuatilia utungaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo za hifadhi ya misitu, hifadhi ya vyanzo vya maji, tathmini ya mazingira na usafi wa mazingira. Kamati inazipongeza Halmashauri zilizoanza kutunga na kutekeleza Sheria Ndogo hizo na kutoa msisitizo kwa Halmashauri nyingine kuiga mfano huo. Halmashauri zilizotunga Sheria Ndogo zinazohusu mazingira ni Manispaa ya Moshi, Jiji la Mwanza, Halmashauri za Wilaya ya Njombe, Babati, Singida Vijijini, Iramba, Bahi, Mbeya Vijijini na Mpanda; Kamati inaishauri Serikali itafute namna mpya ya kuhimiza suala la usafi wa Mazingira badala ya utaratibu uliozooleka wa kutenga siku moja kwa mwezi kwa ajili ya kufanya usafi wa Mazingira. Kuna haja ya kubadili mkakati ili tuwe na utamaduni wa kila siku au mara kwa mara na kuwe na motisha kwa ajili ya Halmashauri/Manispaa zitakazoshinda kwa

utunzaji Mazingira. Kamati inapendekeza pia kuwe na utaratibu wa kutoa hati chafu kwa Halmashauri au Manispaa zilizofanya vibaya katika utunzaji wa Mazingira.

**6.7 Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na mgongano wa kimamlaka katika baadhi ya sekta na Idara ya Mazingira. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo ambayo huhifadhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kama vile maeneo ya hifadhi za misitu, fukwe na vyanzo vya maji. Hata hivyo, bado mamlaka nyingine za Halmashauri na Wizara kwa kutumia Sheria zao zinaendelea kutoa vibali kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile ujenzi kandokando ya mito na fukwe za bahari. Ni rai ya Kamati kwamba kwa kuwa Mamlaka hizi zote zipo chini ya Serikali moja, zishirikiane kwa pamoja kuondoa migongano ya matumizi ya ardhi inayoendelea kukua kwa kasi nchini; Kamati inaishauri Serikali iweke mfumo wa mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na maafisa Mazingira wa sekta na Halmashauri ili kurahisisha utekelezaji wa sheria.

Aidha, Maafisa Mazingira wa sekta na Halmashauri washirikishwe katika kutoa maamuzi ya mipango ya matumizi ya Ardhi na maamuzi mbali mbali ya kisekta. Ofisi ya Makamu wa Rais ishirikiane na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili utekelezaji wa miradi mbali mbali uweze kuzingatia masuala ya Mazingira. Kamati inaiagiza Serikali ifuatilie utekelezaji wa masharti yaliyotolewa kwa mradi wa Dar ES Salaam Rapid Transport (DART) wakati walipopewa hati ya Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) kama yamezingatiwa.

**6.8 Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi limeendelea kuleta athari nyingi ikiwa ni pamoja na ukame na mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini na duniani kote. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kukuza weledi kuhusu tatizo hili na jinsi ya kukabiliana nalo kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha upandaji miti na kuzuia kilimo kisichofuata utaratibu katika miinuko kinachosababisha maporomoko ya ardhi na mmomonyoko wa udongo.

Aidha, Kamati inashauri Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ianzishwe ili itoe mwongozo kwa Serikali, Taasisi na mashirika mbalimbali kuhusu uhuishaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya maendeleo.

**6.9 Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha kitengo cha Polisi wa Mazingira ambacho tayari kimeanza kazi. Kamati inaamini kabisa kwamba ushirikiano wa kitengo hiki na Baraza (NEMC), utafanikisha shughuli za ukaguzi hasa wa viwanda na hatimaye kukamata wahalifu wa mazingira. Kamati inashauri kitengo cha Polisi

Mazingira kiimarishe na kiboreshe zaidi ili wasiwe wanasubiri kuitwa bali wajengewe uwezo waweze kufanya ufuatiliaji wa masuala ya Mazingira.

## 7.0 HITIMISHO

**7.1 Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Mhe. Dkt.Bilinit Mahenge, (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Naibu Waziri Mhe. Ummy Mwalimu; Ndugu Sazi M. Salula - Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wataalamu wote wa Ofisi hii na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa ushirikiano, ushauri na utaalamu wao ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

**7.2 Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa busara, ushirikiano na kujituma kwao bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti inayoombwaa na hivyo kufanikisha Taarifa hii. Naomba niwatambue kwa kuwataaja majina kama ifuatavyo:-

- |  |                |
|--|----------------|
| 1. Mhe. James Daudi Lembeli, Mb          | - Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Abdulkarim E.Hassan. Shah, Mb    | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Zakia Hamdani Meghji, Mb         | Mjumbe         |
| 4. Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi , Mb | "              |
| 5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb       | "              |
| Mary Machuche Mwanjelwa, Mb              | "              |
| 6. Mhe. Dkt.                             |                |
| 7. Mhe. Muhamad Amour Chomboh, Mb        | "              |
| 8. Mhe. Michael Lekule Laizer, Mb        | "              |
| 9. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb         | "              |
| 10. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb          | "              |
| 11. Mhe. Amina Andrew Clement, Mb        | "              |
| 12. Mhe. John John Mnyika, Mb            | "              |
| 13. Mhe. Salim Hassan Turky, Mb          | "              |
| 14. Mhe. Abuu Hamoud Jumaa, Mb           | "              |
| 15. Mhe. Kisyeri Werema Chambiri, Mb     | "              |
| 16. Mhe. Al-Shymaa John Kwegyr, Mb       | "              |
| 17. Mhe. Dkt Henry Daffa Shekifu, Mb     | "              |
| 18. Mhe. MwanaKhamis Kassim Said, Mb     | "              |
| 19. Mhe. Waride Bakar Jabu, Mb           | "              |
| 20. Mhe. Clara Diana Mwatuka,Mb          | "              |
| 21. Mhe. Haji Khatibu Kai,Mb             | "              |
| 22. Mhe.Benedict Ole Nangoro,Mb          | "              |

**7.1 Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge

Ndg. Charles Mloka, Katibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili akisaidiwa na Ndg. Lukindo Adrian Choholo kwa kuratibu shughuli za Kamati kwa ufasaha na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**4.4 Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi wa Makamu wa Rais- Mazingira kama ilivyowasilishwa.

**4.5 Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, na kwa kuzingatia kwamba hoja kubwa ya Kamati ni ufinyu wa bajeti usiotosheleza utekelezaji wa malengo katika Idara ya Mazingira kwa miaka mitatu mfululizo (2012/13-2014/15); na kwa kuwa jambo hili sasa linashughulikiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge Bajeti, naomba kuwasilisha.

James Daudi Lembeli, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI  
NA MAZINGIRA**

12 Mei, 2014

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Maana Mheshimiwa Lissu nakuona unatetemeka, unataka kuwahi tu kuja hapa. (Kicheko)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na ninaomba mniondoe hofu kwamba mitambo ya TBC leo itakuwa sawasawa ili isije ikawa kama siku fulani. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu mpango na Makadirio ya Mapato na Matumiizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za mwaka 2013.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Jamhuri ya Muungano Tanzania imefikisha umri wa nusu karne tangu ilipozaliwa tarehe 26 Aprili, 1964. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, katika hotuba yake ya tarehe 7 Mei, 2014, kuhusu Mapitio na Mwelekeo ya Wakazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2014/2015, miaka 50 kwa lugha yoyote ile, siyo kipindi kifupi.

Waziri Mkuu, alitumia takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, zinazoonyesha kwamba asilimia 90.6 ya Watanzania wote wamezaliwa ndani ya Muungano na nchi wanayoifahamu ni Jamhuri ya Muungao wa Tanzania. Kwa maneno ya Waziri Mkuu, sote tunawajibika kuwatendea haki watu hawa kwa kuulinda, kuuimarisha na kuudumisha Muungano wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa Watanzania wengine wengi na mimi pia nimezaliwa ndani ya Muungano. Ninaamini kwamba ukweli huu unawahuju pia Waheshimiwa Wabunge wengi waliomo ndani ya Bunge hili Tukufu na sisi pia tunaomba kutendewa haki kuhusu Muungano huu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, haki tunayoomba kutendewa ni moja tu, kuambiwa ukweli juu ya Muungano huu na historia yake, hali yake ya sasa na mwelekeo wake wa baadaye. Haki tunayoomba kuendewa ni kwa watawala kuacha propaganda na uongo juu ya Muungano na kutuambia ukweli wote juu ya Muungano huu. (Makofii)

Bob Marley aliyejikuwa Mwanamuziki mpigania uhuru wa watu weusi maarufu kutoka Jamaica, aliwahi kusema katika wimbo wake, “Get up, stand up; stand up for your rights.” Yaani amkeni, simaneni; simameni kwa haki zenu. Kwamba you can fool some people sometime but you can full all the people all the time. Yaani unaweza kuwadanganya baadhi ya watu kwa muda Fulani, lakini huwezi kuwadanganya watu wote kwa muda wote. (Makofii)

Baada ya nusu karne ya uongo na propaganda kuhusu Muungano huu, Watanzania wa kizazi hiki cha Muungano wanataka ukweli. Watanzania hawa hawataulinda wala kuuimarisha au kuudumisha Muungano huu endapo wataendelea kudanganywa au kufichwa ukweli juu ya mambo mengi yanayouhusu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kizazi cha Muungano tunahitaji kutendewa haki. Acheni propaganda na uongo kuhusu Muungano huu, ndipo muweze kutuambia tuulinde, tuuimarishie na tuudumishe. (Makofii)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sherehe za miaka 50 ya Muungano ni mahali pazuri pa kuanzia kudai ukweli juu ya Muungano huu. Mtu yeote anayetembea sasa katika Barabara ya Nyerere kuanzia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere hadi katikati ya Jiji la Dare es Salaam au barabara ya Ally Hassan Mwinyi kuanzia Morocco hadi katikati ya jiji, ataona kila mlingoti wa taa za barabarani umepambwa kwa picha za Waasisi rasmi wa Muungano, yaani Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume wakiwa katika matukio mbalimbali ya siku za mwanzo za Muungano.

Picha hizo za Waasisi hao pia zimepambwa karibu kila mahali katika barabara za katikati ya eneo kuu la kibashara la jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar, barabara zote kuu za Mji wa Zanzibar ikiwemo ile inayotoka Mji Mkongwe kuititia lkulu ya Zanziar hadi uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, hakuna picha hata moja ya Waasisi wa Muungano katika matukio yanayoonyeshwa kwenye picha zilizopo Dar es Salaam. Badala yake, barabara hizo zimepambwa kwa picha za Marais wa Zanzibar kutoka Mapinduzi ya mwaka 1964 hadi sasa. Ni ndani ya eneo la wageni maarufu pekee ndiyo kuna picha moja ya Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume. Hii ni katika wiki ambayo Muungano huu umeahimisha miaka 50 tangu kuzaliwa kwake.

Kwa jinsi ambavyo tangu mwaka huu uanze, Watanzania tumepigwa propaganda za kila aina juu ya Muungano na TBC na vyombo vingine vya habari vya Serikali na vya binafsi, kukosekana kwa dalili yoyote ya shehere za Muungano kwa upande wa Zanzibar wakati wa kilele cha sherehe hizo, kunatilia shaka juu ya uimara wa misingi ya Muungano wenye. Hii ndiyo kusema kwamba pengine kuna ukweli katika hitimisho la Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwamba Tanganyika ndiyo imevaa koti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pengine ndiyo maana Muungano huu haujawahi kuungwa mkono Zanzibar kwa kiasi ambacho wanaopenda kutuaminisha vinginevyo, wamekuwa wakidai. (Makofii)

Aidha, pengine ndiyo maana hata picha za kuchanganya udongo zinazoonyeshwa na TBC kila kukicha, zinamwonyesha Mwalimu Nyerere akichanganya udongo peke yake, wakati Sheikh Karume haonekani kabisa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine linalofikirisha sana kuhusu picha hizi za Sherehe za Miaka 50 ya Muungano zilizopamba Mitaa ya Dar es Salaam. Baadhi ya picha hizo zinawaonyesha watu wengine ambao wamefutwa kabisa katika historia rasmi wanayofundishwa watoto wetu mashulenii na vyuoni.

Kwa mfano, katika picha maarufu ya Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume wakisaini hati za makubaliano ya Muungano, wapo pia kwa upande wa Tanganyika, Oscar Kambona, Bhoke Munanka na Job Lusinde, wakati kwa upande wa Zanzibar wanaoonekana kwenye picha hiyo ni Abdallah Kassim Hanga, Abdulaziz Twalla na Ally Mwinyigogo. Aidha, kuna picha inayowaonyesha Mwalimu Nyerere, Sheikh Karume na Kassim Hanga wakitabasamu kwa furaha kubwa.

Katika kitabu chake "Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru," Zanzibar na Mapinduzi ya AFRABIA kilichochapishwa mwaka 2010 Harith Gasan ameonyesha jinsi ambavyo Oscar Kambona, Abdallah Kassim Hanga, Abdulaziz Twalla na Saleh Saadala Akida walitoa mchango mkubwa katika kufanikisha Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964 na baadaye kufanikisha Muungano wa Tanganyika na Tanganyika wa Aprili, 26 wa mwaka huo.

Katika kitabu chake "The Partnership; Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Miaka 30 ya Dhoruba," Rais wa pili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Alhaji Aboud Jumbe ameeleza kwamba ni Kambona, Bhoke Munanka na Job Lusinde ndio waliompelekea Sheikh Karume nakala za hati za makubaliano kabla ya hati hizo kusainiwa tarehe 22 Aprili, 1964.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kuu ambalo sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano tunataka lijibiwe kwa ukweli kabisa, ni Waasisi hawa wengine wa Muungano, akina Abdallah Kassim Hanga, Abdulaziz Twalla na Salehe Saadala Akida kwa upande wa Zanzibar; na Oscar Kambona, Bhoke Munanka na Job Lusinde kwa upande wa Tanganyika walipotelea wapi na kwa nini hawatajwi katika historia rasmi ya Muungano na Waasisi wake? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kassim Hanga alikuwa Waziri Mkuu na baadaye Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakati Twalla alikuwa Waziri wa Fedha wa Serikali hiyo na Salehe Saadala alikuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi. Kwa upande wa Tanganyika Oscar Kambona alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ulinzi wakati wa Mapinduzi ya Zanzibar na baadaye wakati wa kuzaliwa kwa Muungano Bhoke Munanka alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais mwenye dhamana ya masuala ya Usalama na Job Lusinde alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa.

Katika "Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru," Gasani ameonyesha jinsi ambavyo akina Hanga, Twalla, Saadala pamoja na Viongozi wengine waandamizi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama vile Othman Sharif, Mtungi Ussi na Jaha Ubwa waliuawa na kuzikwa katika handaki moja katika sehemu inayoitwa kama, nje kidogo ya Mji wa Zanzibar. Sisi wa kizazi cha Muungano tunataka kujua ukweli juu ya makosa waliyoyafanya Waasisi hawa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Muungano hadi wakauawa na kuzikwa katika kaburi au handaki moja. Tunataka kujua ukweli kama walifanya makosa, walishaktiwa katika Mahakama gani iliyowahukumu adhabu ya kifo? (Makofij)

Aidha, tunataka kuambiwa ukweli, kwa nini mchango wao katika kuzaliwa kwa Muungano umefichwa kwa muda wote wa nusu Karne ya Muungano huu? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Oscar Kambona, inafahamika kwamba katika miaka ya mwisho ya ukoloni na miaka ya mwanzo ya uhuru, Mwasisi huyu wa Muungano alikuwa mtu wa karibu sana na Mwalimu Nyerere. Mwalimu Nyerere ndiye alikuwa bestman wa Kambona wakati wa harusi yake iliyofanyika London mwaka 1960. Inafahamika hata hivyo kwamba mwaka 1967 Oscar Kambona alikosana na Mwalimu na akalazimika kukimbilia uhamisho nchini Uingereza alikoishi hadi aliporudi nyumbani wakati aliporudi nyumbani wakati wa kurudishwa tena kwa mfumo wa Vyama vingi vya Siasa mwaka 1992.

Tuliosoma miaka ya 1970 na 1980 tulifundishwa mashulenii na kuimbishwa nyimbo zilizotuaminisha kwamba Oscar Kambona alikuwa msaliti aliyetaka kuipondua Serikali yetu Tukufu. Hata hivyo, hatukuwahi kuambiwa kwamba aliwahi kushitakiwa katika Mahakama yoyote hapa nchini na kama ni hivyo kama alipatikana na hatia yoyote na kuadhibiwa na Mahakama. Tunachojuu ni kwamba aliporudi mwaka 1992 Mzee Kambona hakukamatwa wala kushitakiwa kwa kosa lolote lile.

Sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano huu, tunataka tutendewe haki kwa kuambiwa ukweli juu ya tuhuma za usaliti dhidi ya Mzee Oscar Kambona ambaye sasa anaandikiwa vitabu kuwa ni mmoja wa watu waliota mchango mkubwa katika kuzaliwa kwa Muungano huu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kutolewa kwa nyaraka za Muungano. Katika maoni yake wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka wa fedha 2012/2013 Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kwamba Serikali iweke wazi nyaraka mbalimbali zinazohusu historia ya Muungano wetu na mapito yake ili Watanzania waelewe masuala yote yaliyotokea yanayouhusu. Hii ni muhimu zaidi kwa kuzingatia ukweli kwamba, Mataifa ya Magharibi kama vile Marekani na Uingereza yalikwishatoa hadharani nyaraka za mashirika yao ya kijasusi pamoja na Balozi zao Tanzania zinazoonyesha jinsi ambavyo Serikali za Mataifa hayo zilihusika katika kuzaliwa kwa Muungano.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilifafanua kwamba kuanikwa kwa nyaraka zilizopo katika mamlaka mbalimbali za Serikali, kutasaidia kuthibitisha au kukanusha taarifa ambazo chanzo chake ni nyaraka za kidiplomasia na kijasusi za nchi hizo kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulitokana

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

na njama za kibeberu za kudhibiti ushawishi wa siasa za kimapunduzi za Chama cha Umma na Viongozi wake ndani ya Baraza la Mapinduzi.

Aidha, nyaraka hizo zitatoa mwanga juu ya kilichowasibu Viongozi Waandamizi wa Chama hicho ambacho bila uwepo wao kutambuliwa rasmi, historia ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Muungano inabaki pungufu.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisisitiza juu ya haja ya Taifa letu kuambiwa ukweli juu ya Muungano huu. Miaka karibu 50 ya Muungano ni umri wa kutosha kwa Taifa la Tanzania kuambiwa ukweli wote juu ya kuzaliwa kwake na mapito ambayo limepitia katika kipindi hicho. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilirudia wito wake huo wakati wa kuwasilisha maoni yake juu ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala juu ya nyaraka za Muungano huu ulichukua picha mpya wakati Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba walipohoji uwepo wa Hati ya Makubaliano ya Muungano na uhalali wa Muungano wenyewe wakati wa mjadala juu ya sura ya kwanza na ya sita ya Rasimu ya Katiba. Baada ya walio wachache wa Kamati namba nne kuonyesha ushahidi kwamba Serikali ya mapinduzi Zanzibar haijawahi kuwa na nakala ya hati hiyo na kwamba haijawahi kupelekwa na kusajiliwa katika Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa, Serikali hii ya CCM ililazimika kutoa kile ilichokiita Nakala ya Hati ya Makubaliano ya Muungano. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuhitaji kuzungumzia tofauti kubwa ya sahihi ya Sheikh Karume iliyopo kwenye hati hiyo na sahihi ya Sheikh Karume iliyopo katika Sheria mbalimbali alizosaini kama Rais wa Zanzibar na wakati mwingine kama Kaimu Rais wa Jamhuri ya Muungano. Cha muhimu ni kwamba mgogoro juu ya Hati ya Makubaliano ya Muungano unathibitisha ukweli kwamba matokeo ya utamaduni huu wa kufichaficha nyaraka muhimu za nchi, ni kwa wananchi kukosa imani na Serikali iliyoko madarakani kwa kuwa wananchi wanajenga hisia kwamba nyaraka hizo zinafichwa kwa sababu zina ushahidi wa maovu yaliyofanywa na Serikali hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zote hizi, kwa mara nyingine tena Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa nyaraka za Muungano huu hadharani ili Watanzania waweze kuelewa historia halisi ya Muungano badala ya kuendelea kulishwa propaganda na TBC na kwenye majukwaa ya kisiasa ya CCM na Serikali yake. Vinginevyo, chochote kitakachosemwa na TBC na watawala katika majukwaa yao ya kisiasa kuhusu Muungano huu, hakitaaminika tena na wananchi wa Tanzania. (Makofii)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu, Bunge lako Tukufu limeambiwa kwamba Muungano huu ni wa kipekee na wa kupigiwa mfano duniani kote. Aidha, ni kielelezo kamili cha umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa wananchi. Ni kweli kwamba Muungano huu ni wa kipekee kwa sababu haujawahi kuigwa na nchi nyingine zozote katika Afrika. Kama Muungano huu ungekuwa wa kupigiwa mfano duniani kote kama inavyodaiwa na Waziri Mkuu, basi kungekuwa na angalau nchi moja iliyoomba kuijunga na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Angalau kungekuwa na nchi zilizoiga mfano wa Muungano huu kwingineko Afrika na duniani kote. (Makof)

Kwa kuwa, hakuna hata nchi moja iliyowahi kuomba kuijunga nasi na kwa kuwa hakuna nchi nyingine zilizoiga mfano wa Muungano huu, pengine huu ni muda muafaka wa kuhoji ukweli wa kauli kwamba Muungano huu ni kielelezo cha umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa wananchi wa Tanganyika na Zanzibar. (Makof)

Mzee Puis Msekwa, Mwenyekiti Mstaafu wa CCM na Spika Amertus wa Bunge hili Tukufu aliwahi kusema katika mada yake, hali ya Muungano, kwa Semina iliyofanyika Tanga miaka 20 iliyopita kwamba Muundo wa sasa wa Muungano huu umepelekea wengi kuamini kwamba Muungano huu ni kiinimacho tu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu chini ya Muungano huu Zanzibar ilikabidhi sehemu muhimu ya mamlaka yake mahusiano ya nchi za nje, ulinzi na usalama, uraia, kodi na ushuru, sarafu, nguvu kuu za kuendeshea uchumi na mengineyo kwa Tanganyika na kasha Tanganyika ikajigeuza jina na kuijita Jamhuri ya Muungano.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Spika, Amartus Msekwa aliongeza kwamba kwa jinsi mambo yalivyo sasa, Zanzibar inaonekana kama vile ni invited guest, yaani mgeni mwalikwa katika Muungano huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rage, kaa kwanza! Hebu kaa!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Naye msomi mashuhuri wa kiafrika, Professor Ally A. Mazrui katika makala yake *Imperialism After the Empire, Lessons from Uganda and Tanzania* yaani Ubeberu baada ya himaya, funzo kutoka Uganda na Tanzania iliyochapishwa katika Gazeti la Kenya, the Sunday Nation la Mei 22, 1994, alisema:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

"Kwa sababu ya Muungano, Zanzibar imepoteza kila kitu chake muhimu, wakati Tanganyika imebadilika jina tu na kuwa Tanzania huku ikiwa na mamlaka zaidi, lakini ikibaki na Rais wake, nembo yake ya Taifa, Wimbo wake wa Taifa na hata Kiti chake katika Umoja wa Mataifa. Kama tunavyoonyesha katika maoni haya, gharama ya kuyapuuza maneno haya ya watu hawa wazito imekuwa kubwa kweli kweli hasa kwa Zanzibar. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misaada na mikopo ya kibajeti. Ushahidi wa nyaraka ambazo zimewasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu na Serikali hii ya CCM unaonyesha kwamba Muungano huu ni kielelezo cha unyonyaji na ukandamizaji mkubwa ambao nchi ndogo ya Zanzibar imefanyiwa na nchi kubwa ya Tanganyika. Ni mfano wa jinsi ambavyo nchi moja kubwa ya kiafrika inaweza kuigeuza nchi nyingine ndogo ya kiafrika kuwa Koloni lake. Kwa sababu maneno haya yanaweza kupotoshwa na wale ambao wamefaidika na uhusiano huu wa kikoloni kati ya Tanganyika na Zanziba, naomba kutoa ufanuzi kama ifuatavyo:- (Makofii)

Kwa miaka mingi Zanzibar imelalamika kwamba inapunjwa katika mgawanyo unaotokana na fedha zinazotolewa na nchi wafadhili na Taasisi za Kimataifa kwa Jamhuri ya Muungano. (Makofii)

Kwa sababu ya malalamiko hayo, mwaka jana, 2013 Kamati ya Kudumu ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala iliagiza Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili, ni vema ukaangaliwa upya kwa Serikali zote mbili, yaani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano. (Makofii)

Aidha, Kamati ilishauri kwamba Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu mwaka 2006 na kuwasilishwa tena mwaka 2010 kuhusu utaratibu wa mgawo wa fedha za Serikali zote mbili. Serikali hii ya CCM imejibu maagizo haya ya Kamati kama ifuatavyo:-

Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya pamoja ya Fedha. Aidha, kuhusu mgawanyo wa fedha zinazotoka kwa Wafadhili, upo utaratibu wa mgawanyo wake ambao kwa upande wa misaada na mikopo ya kibajeti isiyokuwa na masharti maalum, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hupata gawio la 4.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii ya Serikali ya CCM ni ya uongo. Katika maelezo yake mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) aliitaarifu Kamati kwamba kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hadi kufikia mwezi Machi 2014 Serikali ya Mapinduzi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Zanzibar ilipata gawio la misaada ya kibajeti la Shilingi bilioni 27.190 kati ya Shilingi bilioni 32.627 zilizoidhinishwa na Bunge hili. Hii ndiyo kusema kwamba kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kama gawio la misaada na mikopo ya kibajeti kwa Zanzibar, ni 83% ndizo zilizolipwa hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hili siyo tatizo, kwani kwa mwelekeo wa takwimu hizi hadi kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha gawio lililoidhinishwa na Bunge lako Tukufu linaweza kuwa limelipwa lote. Tatizo kubwa na la msingi ni kwamba gawio lililoidhinishwa na Bunge hili Tukufu siyo gawio halali kwa Zanzibar. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Fedha, akiwasilisha mapendekezo ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2014/2015 kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano tarehe 30 Aprili, 2014 mapato halisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo nafuu ya nje, ilikuwa Shilingi bilioni 1,163 au Shilingi trilioni 1.163 kwa mwaka jana wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Zanzibar ingepatiwa 4.5% ya mapato hayo kama inavyotakiwa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Serikali hii ya CCM, basi kwa mwaka 2013 peke yake gawio halali la Zanzibar la misaada na mikopo ya kibajeti lingekuwa Shilingi bilioni 52.335. Badala ya kupatiwa Shilingi bilioni 52.335 ambazo ni fedha zake halali, Zanzibar iliidhinishiwa Shilingi bilioni 32.627 au 52% ya fedha zake halali.

Fedha hizo ni sawa na 2.8% ya fedha zote za misaada na mikopo ya kibajeti kwa Jamhuri ya Muungano. Fedha zilizobaki, yaani Shilingi trilioni 1.130 au 97.2% ya fedha zote za misaada ya kibajeti, zimetumika na zitatumika Tanganyika. Kwa ushahidi huu nyaraka za Serikali ya CCM, kwa sababu ya Muungano huu, kwa mwaka 2013 peke yake Zanzibar imeibiwa Shilingi bilioni 25.145 au 48% ya fedha zake halali za gawio la misaada na mikopo ya kibajeti. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapendekezo yaliyoletwa kwenye Bunge lako Tukufu na Serikali hii ya CCM, Zanzibar itaibiwa fedha nyingi zaidi kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa mwaka huu wa fedha, fedha zitakazokwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinajumuisha Shilingi bilioni 21.639 mgawo wa misaada ya kibajeti. Kwa upande mwagine, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Fedha, misaada na mikopo ya kibajeti kwa mwaka huu wa fedha itakuwa Shilingi bilioni 992.170. Hii ina maana kwamba kwa mwaka huu wa Fedha Zanzibar itapata 2.18% tu ya fedha za misaada na mikopo ya kibajeti. Hii inaonyesha pia kwamba kwa mwaka huu, fedha za misaada na mikopo ya kibajeti ambazo zitabaki na kutumika Tanganyika, ni shilingi bilioni 970.531 au 97.82% ya fedha hizo.

Kwa Serikali hii ya CCM, kama Serikali hii ya CCM ingehesimu utaratibu wake wa 4.5% ya fedha hizo kwa Zanzibar, gawio halali la Zanzibar kutokana na fedha za misaada na mikopo ya kibajeti kwa mwaka ujao wa fedha lingekuwa Shilingi bilioni 44.647. Kwa maana hiyo, Serikali hii ya CCM inapendekeza kuilipa Zanzibar asilimia 48.47 ya fedha zake halali. Endapo Bunge lako Tukufu litapitisha mapendelekezo kama haya kama inavyoombwa na Serikali hii ya CCM Zanzibar itaibiwa Shilingi bilioni 23 au 51.53% ya fedha zake halali kwa mwaka wake wa fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ieleze Bunge lako Tukufu na iwaeleze Watanzania na hasa Wazanzibari, kwanini fedha halali za Zanzibar kutokana na misaada na mikopo ya kibajeti inayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano hazijalipwa kwa mwaka jana wa fedha? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako Tukufu na iwaeleze Watanzania na hasa Wazanzibari kwanini inapendekeza kuipatia Zanzibar pungufu ya fedha zake halali kama gawio la misaada na mikopo ya kibajeti kwa mwaka huu wa fedha? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilete mbele ya Bunge lako Tukufu takwimu za fedha zote zilizopokelewa na Serikali kama misaada na mikopo ya kibajeti kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita na sehemu ya fedha hizo zilizolipwa kwa Zanzibar kama gawio lake katika kipindi hicho. Takwimu hizi ni muhimu ili Watanzania na hasa Wazanzibari waweze kufahamu kama Zanzibar imekuwa ikipata sehemu yake halali ya mapato ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ya Bunge hili itakayochunguza mgawanyo wa mapato yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti kati ya Tanganyika na Zanzibar ili kupata ukweli juu ya uhalali wa malipo hayo kwa Zanzibar. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekliti, lingine ni misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti. Misaada na mikopo ya kibajeti siyo eneo pekee ambapo Zanzibar inanyonywa na Tanganyika kwa sababu ya Muungano huu. Ukweli ni kwamba hali ni mbaya zaidi kuhusiana na fedha za misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti. Hapa pia takwimu za Serikali hii ya CCM zinatisha na kusikitisha, hivyo kwa mfano kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2013/2014 fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha misaada na mikopo ya basket fund na misaada na mikopo ya miradi zilikuwa Shilingi trilioni 2.692 au Shilingi bilioni 2,692. Fedha hizi zote zilitumika kwa ajili ya miradi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya maendeleo ya Tanganyika. Hapa, Zanzibar haikupata kitu chochote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri wa Fedha yanaonesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/2015 misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti kutoka nje inatazamiwa kuwa Shilingi bilioni 2019.43, au Shilingi trilioni 2.019. Hizi zote ni fedha zitakazotumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika. Hapa pia, Zanzibar haitapata kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa Bunge lako Tukufu kukumbuka kwamba, kwa sababu ya Muungano huu Zanzibar imenyang'anywa mamlaka ya kuomba mikopo au misaada kutoka nje bila kwanza kupata kibali cha Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano ambayo kiuhalisia ni Wizara ya Fedha ya Tanganyika. (Makofii)

Sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano tunataka kujua unyonyaji na wizi huu wa fedha za Wazanzibari utakomeshwa lini? Aidha, sisi tulio kizazi cha Muungano huu tunataka kuambiwa kama mgawanyo wa aina hii wa mapato yanayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano ndiyo kielelezo cha umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa wananchi wa Tanganyika na Zanzibar, ulioletwa na Muungano huu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwamba Zanzibar haipati stahili yake ya mapato yanayopatikana kwa jina la Jamhuri ya Muungano kutoka vyanzo vya nje bali, pia fedha zinazopatikana kutokana na mambo ya Muungano zinatumika kwa mambo yasiyo ya Muungano ya Tanganyika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matokeo ya mjadala wa Katiba wa mwaka 1983/1984 uliopelekea kuchafuka kwa hali ya hewa ya kiasasa Zanzibar na kung'olewa madarakani kwa Alhaji Aboud Jumbe ni kuingizwa kwa Sura ya Saba inayohusu masharti kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. (Makofii)

Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1984, Ibara mpya ya 133 ya Katiba iliweka masharti kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti ya pamoja ya fedha ambapo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka 30 tangu kupitishwa kwa mabadiliko ya Tano ya Katiba, masuala ya Tume ya Pamoja ya Fedha na Akaunti ya Pamoja ya Fedha yamekuwa mojawapo ya kile kinachoitwa kero za Muungano

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambazo ufumbuzi wake umeshindikana. Kwa mfano, licha ya Katiba kuelekeza kuundwa kwa Tume ya Pamoja ya Fedha, Sheria ya Kuunda Tume hiyo ilipitishwa miaka 12 baadaye (1996). Baada ya hapo, Tume yenye wewe iliundwa rasmi mwaka 2003 miaka saba baada ya kutungwa Sheria na miaka 19 tangu Katiba iweke masharti ya kuundwa Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha, leo ni mwaka wa 30 tangu Katiba kuelekeza akaunti hiyo kufunguliwa na bado hajafunguliwa. Kutokana na kushindikana kufunguliwa huko kwa miaka yote hii, bajeti ya Muungano ndiyo bajeti ya Tanganyika kinyume na maelekezo ya Katiba. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 Tume ya Pamoja ya Fedha iliajiri Watalaam waelekezi kutoka Kampuni ya Kimataifa ya Uhasibu ya Price Water House Coopers kuangalia suala la gharama na mgawanyo wa fedha za Muungano. Taarifa ya uchambuzi ya Price Water House Coopers ilitolewa kama mapendekezo ya Tume kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano ya mwezi Agosti, 2006. Taarifa ya Tume ya Pamoja ya Fedha inaonesha hali ya kusikitisha kuhusu mapato na matumizi ya fedha za Muungano hasa kwa upande wa Tanganyika. Ili kupata picha kamili ya hali halisi ilivyo, tunaomba kunukuu sehemu ya taarifa hiyo.

"Uchambuzi unaonesha kuwa mapato yanayotokana na vyanzo vya Muungano yanakidhi matakwa ya Muungano na kuwa na ziada ya kutosha. Takwimu zinaonesha kuwa kiasi kidogo cha mapato hayo kimekuwa kinagharamia matumizi ya Muungano. Uchambuzi unaonesha vilevile kuwa, kiasi kikubwa cha ziada ya mapato ya Muungano kimekuwa kinatumika kugharamia mambo yasiyo ya Muungano."

Takwimu za utafiti za Price Water House Coopers zinaonesha kwamba, kwa mwaka wa fedha 2003/2004 pekee, matumizi halisi kwa vifungu vya Muungano yalikuwa Shilingi bilioni 537 ambayo ni 20% tu ya bajeti yote ya Serikali ya Muungano kwa mwaka huo. Mapato halisi ya vyanzo vya mapato vinavyotokana na mambo ya Muungano kwa mwaka huo yalikuwa Shilingi bilioni 1,030. Kwa maana nyingine, mapato na matumizi ya fedha zinazotokana na vyanzo vya mambo ya Muungano yaliacha ziada ya Shilingi billioni 493 kwa mwaka huo mmoja. Ziada hii nje ya mapato yaliyotokana na misaada na mikopo kutoka nje na ilitumika kwa shughuli za maendeleo za Tanganyika zisizo za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Tanganyika imekuwa inafaidika sana na utaratibu huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo kiuhalisia ni Serikali ya Tanganyika iliyovaa joho la Muungano, imekataa kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha kwamba uwepo utaratibu

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

utakaowezesha kutenganisha mapato na matumizi ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Miaka nane tangu mapendekezo hayo yatolewe mwaka 2006, Serikali zetu mbili kwa maneno ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine kubwa ya Muungano huu na ambayo ina umri sawa na Muungano wenyewe inahusu hisa za Zanzibar zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki kabla ya Bodi hiyo kuvunjwa mwaka 1965 na Benki Kuu ya Tanzania kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile fedha za Zanzibar katika Bodi ya Sarafu zilichukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano baada ya masuala ya fedha, sarafu na Benki Kuu kufanywa kuwa mambo ya Muungano mwaka 1965, sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano tuna haki ya kuambiwa ukweli kwanini Serikali hii ya CCM imeshindwa kurudisha fedha hizo kwa Wazanzibari kwa takribani miaka 50 tangu fedha hizo zinyakuliwe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo ndiyo Serikali ya Tanganyika? Tunahitaji kuelezwaa Serikali hii ya CCM inahitaji muda wa miaka mingapi mingine ili iweze kurudisha fedha za watu na kuwaepusha Watanganyika na laana ya wizi wa fedha za Wanzanzibari! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au Wazanzibari wenyewe katika umoja wao, wana haki ya kutumia njia yoyote ile watakayoona inafaa, ikiwemo kufungua kesi za madai katika Mahakama za ndani au za Kimataifa kudai fedha zake zote halali ambazo zimeibiwa na Tanganyika kwa kutumia kivuli cha Muungano katika kipindi chote cha miaka 50 ya Muungano huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya nusu karne ya Muungano wa aina hii, wananchi wa Tanganyika na hasa Wazanzibar hawako tayari kuendelea na utaratibu huu wa kiunyonyaji na kikandamizaji. Wananchi wanataka mabadiliko ya msingi ya Muundo wa Muungano na uendeshaji wake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Lissu. Ahsante sana. Yaliyobaki yanaingizwa kwenye Hansard yakiwa kama kumbukumbu sahihi za taarifa yako. Nakushukuru sana. (Makofi)

**Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuhusu  
Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama  
ilivyowasilishwa Mezani**

**MAONI YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO), MHESHIMIWA TUNDU A.M. LISSU (MB.) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)  
KWA MWAKA 2014/2015**

(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)

## **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka huu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefikisha umri wa nusu karne tangu ilipozaliwa tarehe 26 Aprili, 1964. Kama anavyosema Waziri Mkuu Mh. Mizengo Pinda katika hotuba yake ya tarehe 7 Mei, 2014 ‘Kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2014/2015’: “Miaka 50 kwa lugha yoyote ile siyo kipindi kifupi.” Waziri Mkuu ametumia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 zinazoonyesha kwamba asilimia 90.6 ya Watanzania wote “wamezaliwa ndani ya Muungano na nchi wanayoifahamu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.” Kwa maneno ya Waziri Mkuu, “sote tunawajibika kuwatendea haki watu hawa kwa kuulinda, kuuimarisha na kuudumisha Muungano wetu.”

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyo kwa Watanzania wengine wengi, na mimi pia nimezaliwa ndani ya Muungano. Ninaamini kwamba ukweli huu unawahu pia waheshimiwa wabunge wengi walimo ndani ya Bunge hili tukufu. Na sisi pia tunaomba kutendewa haki kuhusu Muungano huu. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, haki tunayoomba kutendewa ni moja tu: kuambiwa ukweli juu ya Muungano huu na historia yake, hali yake ya sasa na mwelekeo wake wa baadaye. Haki tunayoomba kutendewa ni kwa watawala kuacha propaganda na uongo juu ya Muungano na kutuambia ukweli wote juu ya Muungano huu.

Bob Marley, aliyejewa mwanamuziki mpigania uhuru wa watu weusi maarufu kutoka Jamaica, aliwahi kusema katika wimbo wake ‘Get Up, Stand UP, Stand Up For Your Rights’ ('Amkeni, Simameni, Simameni kwa Haki Zenu') kwamba: “You can fool some people some time, but you cannot fool all the people all the time”, yaani, unaweza kuwadanganya baadhi ya watu kwa muda fulani, lakini huwezi kuwadanganya watu wote kwa muda wote! Baada ya nusu karne ya uongo na propaganda kuhusu Muungano huu, Watanzania wa kizazi hiki cha Muungano wanataka ukweli.

Na Watanzania hawa hawataulinda, wala kuuimarisha au kuudumisha Muungano huu endapo wataendelea kudanganywa au kufichwa ukweli juu ya mambo mengi yanayouhusu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, sisi kizazi cha

Muungano tunahitaji kutendewa haki: acheni propaganda na uongo kuhusu Muungano huu ndipo muweze kutuambia tuulinde, tuuimarishe na tuudumishe!

### **SHEREHE ZA MUUNGANO NA ‘WAASISI’ WA MUUNGANO**

**Mheshimiwa Spika**, Sherehe za Miaka 50 ya Muungano ni mahali pazuri pa kuanzia kudai ukweli juu ya Muungano huu. Mtu ye yote anayetembea sasa katika Barabara ya Nyerere kuanzia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere hadi katikati ya jiji la Dar es Salaam; au Barabara ya Ali Hassan Mwinyi kuanzia Morocco hadi katikati ya jiji, ataona kila mlingoti wa taa za barabarani umepambwa kwa picha za Waasisi rasmi wa Muungano, yaani Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, wakiwa katika matukio mbali mbali ya siku za mwanzo za Muungano. Picha hizo za Waasisi hao pia zimepambwa karibu kila mahali katika barabara za katikati ya Eneo Kuu la Kibiashara (CBD) la Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar, barabara zote kuu za Mji wa Zanzibar, ikiwamo ile inayotoka Mji Mkongwe kupitia Ikulu ya Zanzibar hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, hakuna picha hata moja ya Waasisi wa Muungano katika matukio yanayoonyeshwa kwenye picha zilizoko Dar es Salaam. Badala yake, barabara hizo zimepambwa kwa picha za Marais wa Zanzibar toka Mapinduzi ya mwaka 1964 hadi wa sasa. Ni ndani ya eneo la wageni maarufu (VIP) pekee ndio kuna picha moja ya Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume. Hii ni katika wiki ambayo Muungano huu umeadhimisha miaka hamsini tangu kuzaliwa kwake!

Kwa jinsi ambavyo tangu mwaka huu uanze Watanzania tumepigwa propaganda za kila aina juu ya Muungano na TBC na vyombo vingine vya habari vya serikali na vya binafsi, kukosekana kwa dalili yoyote ya sherehe za Muungano kwa upande wa Zanzibar wakati wa kilele cha sherehe hizo kunatilia shaka juu ya uimara wa misingi ya Muungano wenyewe. Hii ndio kusema kwamba pengine kuna ukweli katika hitimisho la Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwamba Tanganyika ndiyo imevaa koti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na pengine ndio maana Muungano huu haujawahi kuungwa mkono Zanzibar kwa kiasi ambacho wanaopenda kutuaminisha vinginevyo wamekuwa wakidai. Aidha, pengine ndio maana hata picha za kuchanganya udongo zinazoonyeshwa na TBC kila kukicha zinamwonyesha Mwalimu Nyerere akichanganya udongo peke yake, wakati Sheikh Karume haonekani kabisa!

**Mheshimiwa Spika**, Kuna jambo lingine linalofikirisha sana kuhusu picha hizi za Sherehe za Miaka Hamsini ya Muungano zilizopamba mitaa ya Dar es Salaam. Baadhi ya picha hizo zinawaonyesha watu wengine ambao wamefutwa kabisa katika historia rasmi wanayofundishwa watoto wetu mashulenii na vyuoni. Hivyo, kwa mfano, katika picha maarufu ya Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume

wakisaini Hati za Makubaliano ya Muungano wapo pia, kwa upande wa Tanganyika, Oscar Kambona, Bhoke Munanka na Job Lusinde, wakati kwa upande wa Zanzibar wanaoonekana kwenye picha hiyo ni Abdallah Kassim Hanga, Abdulaziz Twala na Ali Mwinyigogo. Aidha, kuna picha inayowaonyesha Mwalimu Nyerere, Sheikh Karume na Kassim Hanga wakitabasamu kwa furaha kubwa.

Katika kitabu chake *Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru! Zanzibar na Mapinduzi ya Afrabia* kilichochapishwa mwaka 2010, Harith Ghassany ameonyesha jinsi ambavyo Oscar Kambona, Abdallah Kassim Hanga, Abdulaziz Twala na Saleh Saadalla Akida walitoa mchango mkubwa katika kufanikisha Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964, na baadaye kufanikisha Muungano na Tanganyika wa Aprili 26 ya mwaka huo. Katika kitabu chake *The Partnership: Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Miaka 30 ya Dhoruba*, Rais wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Alhaj Aboud Jumbe ameeleza kwamba ni Kambona, Bhoke Munanka na Job Lusinde ndio waliompelekea Sheikh Karume nakala za Hati ya Makubaliano ya Muungano kabla ya Hati hizo kusainiwa tarehe 22 Aprili, 1964.

**Mheshimiwa Spika,** Swali kuu ambalo sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano tunataka ijibiwe kwa ukweli kabisa ni ‘waasisi’ hawa wengine wa Muungano, akina Abdallah Kassim Hanga, Abdulaziz Twala na Saleh Saadalla Akida kwa upande wa Zanzibar; na Oscar Kambona, Bhoke Munanka na Job Lusinde kwa upande wa Tanganyika walipotelea wapi na kwanini hawatajwi katika historia rasmi ya Muungano na waasisi wake? Kassim Hanga alikuwa Waziri Mkuu na baadaye Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; wakati Twala alikuwa Waziri wa Fedha wa Serikali hiyo na Saleh Saadalla alikuwa mjurid wa Baraza la Mapinduzi. Kwa upande wa Tanganyika, Oscar Kambona alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ulinzi wakati wa Mapinduzi ya Zanzibar na baadaye wakati wa kuzaliwa kwa Muungano; Bhoke Munanka alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais mwenye dhamana ya masuala ya usalama, na Job Lusinde alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa.

Katika *Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru!*, Ghassany ameonyesha jinsi ambavyo akina Hanga, Twala na Saadalla pamoja na viongozi wengine waandamizi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama vile Othman Shariff, Mdungi Ussi na Jaha Ubwa waliuawa na kuzikwa katika handaki moja katika sehemu inayoitwa Kama, nje kidogo ya mji wa Zanzibar. Sisi wa kizazi cha Muungano tunataka kujua ukweli juu ya makosa waliyoyafanya hawa waasisi wa Muungano hadi wakauawa na kuzikwa katika kaburi au handaki moja. Tunataka kujua ukweli kama walifanya makosa walishtakiwa katika mahakama gani iliyowahukumu adhabu ya kifo. Aidha, tunataka kuambiwa ukweli kwanini mchango wao katika kuzaliwa kwa Muungano umefichwa kwa muda wote wa nusu karne ya Muungano huu.

Kuhusu Oscar Kambona, inafahamika kwamba katika miaka ya mwisho ya ukoloni na miaka ya mwanzo ya uhuru, 'mwasisi' huyu wa Muungano alikuwa mtu wa karibu sana wa Mwalimu Nyerere. Mwalimu Nyerere ndiye alikuwa 'Best Man' wa Kambona wakati wa harusi yake iliyofanyika London, Uingereza mwaka 1960. Inafahamika, hata hivyo, kwamba mwaka 1967 Oscar Kambona alikosana na Mwalimu Nyerere na akalazimika kukimbilia uhamishoni nchini Uingereza alikoishi hadi aliporudi nyumbani wakati wa kurudishwa tena kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992.

Tuliosoma miaka ya sabini na ya themanini tulifundishwa mashulenii na kuimbishwa nyimbo zilizotuaminisha kwamba Oscar Kambona alikuwa msaliti aliyetaka kuipindua Serikali yetu tukufu. Hata hivyo, hatukuwahi kuambiwa kama alishtakiwa katika mahakama yoyote ya hapa nchini na, kama ni hivyo, kama alipatikana na hatia yoyote na kuadhibiwa na mahakama. Tunachojua ni kwamba aliporudi nyumbani mwaka 1992, Mzee Kambona hakukamatwa wala kushtakiwa kwa kosa lolote lile. Sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano huu tunataka tutendewe haki kwa kuambiwa ukweli juu ya tuhuma za usaliti dhidi ya Mzee Oscar Kambona ambaye sasa anaandikiwa vitabu kuwa ni mmoja wa watu waliota mchango mkubwa katika kuzaliwa kwa Muungano huu.

### KUTOLEWA KWA NYARAKA ZA MUUNGANO

**Mheshimiwa Spika**, Katika maoni yake wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka wa fedha 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kwamba Serikali iweke wazi "nyaraka mbali mbali zinazohusu historia ya Muungano wetu na 'mapito' yake ili Watanzania waelewe masuala yote yaliyotokea yanayouhusu. Hii ni muhimu zaidi kwa kuzingatia ukweli kwamba mataifa ya magharibi kama vile Marekani na Uingereza yalikwishatoa hadharani nyaraka za mashirika yao ya kijasusi pamoja na balozi zao za Tanzania zinazoonyesha jinsi ambavyo serikali za mataifa hayo zilihusika katika kuzaliwa kwa Muungano."

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilifafanua kwamba "kuanikwa kwa nyaraka zilizoko katika mamlaka mbali mbali za Serikali kutasaidia kuthibitisha au kukanusha taarifa ambazo chanzo chake ni nyaraka za kidiplomasia na kijasusi za nchi hizo kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ultokana na njama za kibeberu za kudhibiti ushawishi wa siasa za kimapinduzi za Chama cha Umma na viongozi wake ndani ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar la wakati huo. Aidha, nyaraka hizo zitatoa mwanga juu ya kilichowasibu viongozi waandamizi wa chama hicho ambaa bila uwepo wao kutambuliwa rasmi, historia ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Muungano inabaki pungufu."

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisisitiza juu ya haja ya taifa letu kuambiwa ukweli juu ya Muungano huu: "... Miaka karibu hamsini ya Muungano

ni umri wa kutosha kwa taifa la Tanzania kuambiwa ukweli wote juu ya kuzaliwa kwake na mapito ambayo *limepitia katika kipindi hicho.*" Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilirudia wito wake huo wakati wa kuwasilisha maoni yake juu ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka jana.

**Mheshimiwa Spika**, Mjadala juu ya nyaraka za Muungano huu ulichukua picha mpya wakati wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba walipohoji uwepo wa Hati ya Makubaliano ya Muungano na uhalali wa Muungano wenyewe wakati wa mjadala juu ya Sura ya Kwanza na ya Sita ya Rasimu ya Katiba. Baada ya wajumbe walio wachache wa Kamati Namba Nne kuonyesha ushahidi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijawahi kuwa na nakala ya Hati hiyo, na kwamba haijawahi kupelekwa na kusajiliwa katika Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa, Serikali hii ya CCM ililazimika kutoa kile ilichokiita nakala ya Hati ya Makubaliano ya Muungano.

Hatuhitaji kuzungumzia tofauti kubwa ya sahihi ya Sheikh Karume iliyoko kwenye Hati hiyo na sahihi ya Sheikh Karume iliyoko katika Sheria mbali mbali alizosaini kama Rais wa Zanzibar na wakati mwingine kama kaimu Rais wa Jamhuri ya Muungano. Cha muhimu ni kwamba mgogoro juu ya Hati ya Makubaliano ya Muungano unathibitisha ukweli kwamba matokeo ya utamaduni huu wa kufichaficha nyaraka muhimu za nchi ni kwa wananchi kukosa imani na serikali iliyoko madarakani, kwa kuwa wananchi wanajenga hisia kwamba nyaraka hizo zinachifwa kwa sababu zina ushahidi wa maovu yaliyofanywa na serikali hiyo.

Kwa sababu hizi zote, kwa mara nyingine tena, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa nyaraka za Muungano huu hadharani ili Watanzania waweze kuelewa historia halisi ya Muungano badala kuendelea kulishwa propaganda na TBC na kwenye majukwaa ya kisiasa ya CCM na Serikali yake! Vinginevyo, chochote kitakachosemwa na TBC na watawala katika majukwa yao ya kisiasa kuhusu Muungano huu hakitaaminika tena na wananchi wa Tanzania.

### **KIELELEZO CHA UMOJA NA MSHIKAMANO AU UNYONYAJI WA KIKOLONI?**

**Mheshimiwa Spika**, Katika hotuba ya Waziri Mkuu Bunge lako tukufu limeambiwa kwamba "Muungano huu ni wa kipekee na wa kupigiwa mfano duniani kote. Aidha, ni kielelezo kamili cha umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa wananchi...." Ni kweli kwamba Muungano huu ni wa kipekee kwa sababu haujawahi kuigwa na nchi nyingine zozote katika Afrika. Na kama Muungano huu ungekuwa wa 'kupigiwa mfano duniani kote', kama inavyodaiwa na Waziri Mkuu, basi kungekuwa na angalau nchi moja iliyoomba kuijunga katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Angalau kungekuwa na nchi zilizoiga mfano wa Muungano huu kwagineko Afrika na duniani kote.

Kwa kuwa hakuna nchi hata moja iliyowahi kuomba kujunga nasi, na kwa kuwa hakuna nchi nyingine zilizoiga mfano wa Muungano huu, pengine huu ni muda muafaka wa kuhoji ukweli wa kauli kwamba Muungano huu '*ni kielelezo cha umoja, mshikamano na upendo miiongoni mwa wananchi*' wa Tanganyika na Zanzibar. Mzee Pius Msekwa, Mwenyekiti Mstaafu wa CCM na Spika Emeritus wa Bunge hili tukufu, aliwahi kusema katika mada yake *Hali ya Muungano* kwa semina iliyofanyika Tanga miaka 20 iliyopita kwamba, muundo wa sasa wa Muungano huu umepelekea wengi kuamini kwamba Muungano huu ni kiini macho tu.

Hii ni kwa sababu, chini ya Muungano huu, Zanzibar ilikabidhi sehemu muhimu ya mamlaka yake (mahusiano ya nchi za nje, ulinzi na usalama, uraia, kodi na ushuru, sarafu, nguvu kuu za kuendeshea uchumi na mengineyo) kwa Tanganyika; na kisha Tanganyika ikajigeuza jina na kuijita Jamhuri ya Muungano. Spika Emeritus Msekwa aliongeza kwamba kwa jinsi mambo yalivyo sasa, Zanzibar inaonekana kama vile ni '*invited guest*' (mgeni mwalikwa) katika Muungano huu.

Naye msomi mashuhuri wa Kiafrika, Profesa Ali A. Mazrui katika makala yake '*Imperialism after the Empire: Lessons from Uganda and Tanzania*', yaani '*Ubeberu Baada ya Himaya: Funzo Kutoka Uganda na Tanzania*', iliyochapishwa katika gazeti la Kenya, *The Sunday Nation*, la Mei 22, 1994, alisema kwa sababu ya Muungano, Zanzibar imepoteza kila kitu chake muhimu, wakati Tanganyika imebadilika jina tu na kuwa Tanzania, huku ikiwa na mamlaka zaidi lakini ikibaki na Rais wake, nembo yake ya Taifa, wimbo wake wa Taifa na hata kiti chake katika Umoja wa Mataifa. Kama tunavyoonyesha katika Maoni haya, gharama ya kuyapuuza maneno haya ya watu hawa wazito imekuwa kubwa kweli kweli, hasa kwa Zanzibar.

## MISAADA NA MIKOPO YA KIBAJETI

**Mheshimiwa Spika**, Ushahidi wa nyaraka ambazo zimevasilishwa kwenye Bunge lako tukufu na Serikali hii ya CCM unaonyesha kwamba Muungano huu ni kielelezo cha unyonyaji na ukandamizaji mkubwa ambao nchi ndogo ya Zanzibar imefanyiwa na nchi kubwa ya Tanganyika. Ni mfano wa jinsi ambavyo nchi moja kubwa ya Kiafrika inaweza kuigeuza nchi nyingine ndogo ya Kiafrika kuwa koloni lake. Kwa sababu maneno haya yanaweza kupotoshwa na wale ambao wamefaidika na uhusiano huu wa kikoloni kati ya Tanganyika na Zanzibar naomba kutoa ufanuzi kama ifuatavyo.

Kwa miaka mingi Zanzibar imelalamika kwamba inapunjwa katika mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotolewa na nchi wafadhili na taasisi za kimataifa kwa Jamhuri ya Muungano. Kwa sababu ya malalamiko hayo,

mwaka jana Kamati ya Kudumu ya Bunge lako tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala iliiagiza Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba: "Utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili ni vyema ukaangaliwa upya kwa Serikali zote mbili yaani SMZ na SMT." Aidha, Kamati ilishauri kwamba "Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu mwaka 2006 na kuwasilishwa tena mwaka 2010 kuhusu utaratibu wa mgao wa fedha za Serikali zote mbili."

Serikali hii ya CCM imejibu maagizo haya ya Kamati kama ifuatavyo: "Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, kuhusu mgawanyo wa fedha zinazotoka kwa wafadhili, upo utaratibu wa mgawanyo wake ambapo, kwa upande wa misaada na mikopo ya kibajeti isiyokuwa na masharti maalum, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ... hupata gawio la asilimia 4.5."

**Mheshimiwa Spika**, Kauli hii ya Serikali ni ya uongo. Katika maelezo yake mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, aliitaarifu Kamati kwamba "Kwa mwaka wa fedha 2013/14, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 SMZ imepata Gawio la Misaada ya Kibajeti (General Budget Support – GBS) shilingi 27,190,502,190.97/= kati ya shilingi 32,627,535,000/= zilizoidhinishwa na Bunge." Hii ndio kusema kwamba kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu kama gawio la misaada na mikopo ya kibajeti kwa Zanzibar, ni asilimia 83 ndizo zilizolipwa hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, hili sio tatizo, kwani kwa mwelekeo wa takwimu hizi, hadi kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha, gawio lililoidhinishwa na Bunge lako tukufu linaweza kuwa limelipwa lote. Tatizo kubwa na la msingi ni kwamba gawio lililoidhinishwa na Bunge hili tukufu sio gawio halali kwa Zanzibar. Hii kwa sababu, kwa mujibu wa Maelezo ya Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (MB.) Akiwasilisha Mapendekezo ya Mfumo wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/15 kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya tarehe 30 Aprili, 2014, mapato halisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo nafuu ya nje ilikuwa shilingi bilioni 1,163 au trilioni 1.163.

Kama Zanzibar ingepatiwa asilimia 4.5 ya mapato hayo, kama inavyotakiwa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Serikali hii ya CCM, basi kwa mwaka jana peke yake, gawio halali la Zanzibar la misaada na mikopo ya kibajeti lingekuwa shilingi bilioni 52.335. Badala ya kupatiwa shilingi bilioni 52.335 ambazo ni fedha zake halali, Zanzibar iliidhinishiwa shilingi bilioni 32.627 au asilimia 52 ya fedha zake halali. Fedha hizo ni sawa na asilimia 2.8 ya fedha zote za misaada na mikopo ya kibajeti kwa Jamhuri ya Muungano. Fedha zilizobaki, yaani shilingi trilioni 1.130 au asilimia 97.2 ya fedha zote za misaada ya kibajeti

zimetumika na zitatumika Tanganyika. Kwa ushahidi huu wa nyaraka za Serikali hii ya CCM, kwa sababu ya Muungano huu, kwa mwaka jana peke yake Zanzibar iliibiwa shilingi bilioni 25.145 au asilimia 48 ya fedha zake halali za gawio la misaada na mikopo ya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mapendekezo yaliyoletwa kwenye Bunge lako tukufu na Serikali hii ya CCM, Zanzibar itaibiwa fedha nyingi zaidi kwa mwaka huu wa fedha 2014/15. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa mwaka huu wa fedha, “fedha zitakazokwenda SMZ zinajumuisha shilingi 21,639,608,000.00 mgao wa misaada ya kibajeti....” Kwa upande mwingine, kwa mujibu wa Maelizo ya Waziri wa Fedha, ‘misaada na mikopo ya kibajeti’ kwa mwaka huu wa fedha itakuwa shilingi bilioni 992.170. Hii ina maana kwamba kwa mwaka huu wa fedha, Zanzibar itapata asilimia 2.18 tu ya fedha za misaada na mikopo ya kibajeti. Hii inaonyesha pia kwamba, kwa mwaka huu, fedha za misaada na mikopo ya kibajeti ambazo zitabaki na kutumika Tanganyika ni shilingi bilioni 970.531 au asilimia 97.82 ya fedha hizo.

Kama Serikali hii ya CCM ingeheshimu utaratibu wake wa asilimia 4.5 ya fedha hizo kwa Zanzibar, gawio halali la Zanzibar kutokana na fedha za misaada na mikopo ya kibajeti kwa mwaka ujao wa fedha lingekuwa shilingi bilioni 44.647! Kwa maana hiyo, Serikali hii ya CCM inapendekeza kuilipa Zanzibar asilimia 48.47 ya fedha zake halali. Endapo Bunge lako tukufu litapitisha mapendekezo haya kama inavyoombwa na Serikali hii ya CCM, Zanzibar itaibiwa shilingi bilioni 23 au asilimia 51.53 ya fedha zake halali kwa mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako tukufu na iwaeleze Watanzania, na hasa Wazanzibari, kwa nini fedha halali za Zanzibar kutokana na misaada na mikopo ya kibajeti inayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano hazijalipwa kwa mwaka jana wa fedha. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako tukufu na iwaeleze Watanzania, na hasa Wazanzibari, kwa nini inapendekeza kuipatia Zanzibar pungufu ya fedha zake halali kama gawio la misaada na mikopo ya kibajeti kwa mwaka huu wa fedha.

Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilete mbele ya Bunge lako tukufu takwimu za fedha zote zilizopokelewa na Serikali kama misaada na mikopo ya kibajeti kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita na sehemu ya fedha hizo zilizolipwa kwa Zanzibar kama gawio lake katika kipindi hicho. Takwimu hizo ni muhimu ili Watanzania, na hasa Wazanzibari, waweze kufahamu kama Zanzibar imekuwa ikipata sehemu yake halali ya mapato ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti. Mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge lako tukufu kuunda Kamati Teule ya Bunge hili itakayochunguza mgawanyo wa mapato

yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti kati ya Tanganyika na Zanzibar ili kupata ukweli juu ya uhalali wa malipo ya mapato hayo kwa Zanzibar.

## MISAADA NA MIKOPO ISIYOKUWA YA KIBAJETI

**Mheshimiwa Spika,** Misaada na mikopo ya kibajeti sio eneo pekee ambapo Zanzibar inanyonywa na Tanganyika kwa sababu ya Muungano huu. Ukweli ni kwamba hali ni mbaya zaidi kuhusiana na fedha za misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti. Hapa pia takwimu za Serikali hii ya CCM zinatisha na kusikitisha. Hivyo, kwa mfano, kwa mujibu wa Maelezo ya Waziri wa Fedha, kwa mwaka wa fedha 2013/14 fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha misaada na mikopo ya Basket Fund na misaada na mikopo ya miradi zilikuwa shilingi trilioni 2.692 au bilioni 2,692. Fedha hizi zote zilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika. Hapa Zanzibar haikupata kitu chochote!

Maelezo ya Waziri wa Fedha yanaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/15, misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti kutoka nje inatazamiwa kuwa shilingi bilioni 2,019.43 au trilioni 2.019. Hizi zote ni fedha zitakazotumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika. Hapa pia Zanzibar haitapata kitu chochote. Ni muhimu kwa Bunge lako tukufu kukumbuka kwamba, kwa sababu ya Muungano huu, Zanzibar imenyang'anywa mamlaka ya kuomba mikopo au misaada kutoka nje bila kwanza kupata kibali cha Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano, aka Wizara ya Fedha ya Tanganyika. Sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano tunataka kujua unyonyaji na wizi huu wa fedha za Wazanzibari utakomeshwa lini. Aidha, sisi tulio kizazi cha Muungano huu tunataka kuambiwa kama mgawanyo wa aina hii wa mapato yanayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano ndio kielelezo cha umoja, mshikamano na upendo mionganoni mwa wananchi wa Tanganyika na Zanzibar ulioletwa na Muungano huu.

**Mheshimiwa Spika,** Sio tu kwamba Zanzibar haipati stahili yake ya mapato yanayopatikana kwa jina la Jamhuri ya Muungano kutoka vyanzo vya nje, bali pia fedha zinazopatikana kutokana na mambo ya Muungano zinatumika kwa mambo yasiyo ya Muungano ya Tanganyika. Moja ya matokeo ya mjadala wa katiba wa mwaka 1983/84 uliopelekea 'kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa Zanzibar' na kung'olewa madarakani kwa Alhaj Aboud Jumbe ni kuingizwa kwa Sura ya Saba inayohusu 'Masharti Kuhusu Fedha za Jamhuri ya Muungano' katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1984, ibara mpya ya 133 ya Katiba iliweka masharti kwamba "Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza 'Akaunti ya Pamoja ya Fedha ... ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na

Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha ... kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano."

Aidha, ibara ya 134 iliweka masharti ya kuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenyeye majukumu ya "kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo." Majukumu mengine ya Tume hiyo ni "kuchunguza ... mfumo wa shughuli za fedha kwa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili."

**Mheshimiwa Spika**, Kwa miaka thelathini tangu kupitishwa kwa Mabadiliko ya Tano ya Katiba, masuala ya Tume ya Pamoja ya Fedha na Akaunti ya Pamoja ya Fedha yamekuwa mojawapo ya kile kinachoitwa 'Kero za Muungano' ambayo ufumbuzi wake umeshindikana. Kwa mfano, licha ya Katiba kuelekeza kuundwa kwa Tume ya Pamoja ya Fedha, sheria ya kuunda Tume hiyo, yaani Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, ilipitishwa miaka kumi na mbili baadaye, yaani mwaka 1996.

Baada ya hapo Tume yenye we iliundwa rasmi mwaka 2003, yaani miaka saba baada ya kutungwa kwa sheria na miaka 19 tokea Katiba iweke masharti ya kuundwa kwa Tume hiyo. Kwa upande wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha, leo ni mwaka wa thelathini tangu Katiba kuelekeza Akaunti hiyo kufunguliwa na bado hajafunguliwa. Kutoana na kushindikana kufunguliwa huko, kwa miaka yote hii, bajeti ya Muungano imekuwa ndio bajeti ya Tanganyika, kinyume na maelekezo ya Katiba.

Mwaka 2006 Tume ya Pamoja ya Fedha iliajiri wataalamu waelekezi kutoka kampuni kimataifa ya uhasibu ya PriceWaterhouseCoopers kuangalia suala la gharama na mgawanyo wa fedha za Muungano. Wataalamu hao walifanya uchambuzi halisi wa mambo yapi ni ya Muungano na yapi ni ya Tanganyika na yapi ni ya Zanzibar na gharama za uendeshaji wa kila moja. Baada ya orodha kupatikana, watafiti hao walitafuta matumizi halisi ya bajeti ya vifungu hivyo kwa muda wa kiasi cha miaka 10 iliyopita.

Watafiti wa PriceWaterhouseCoopers walikwenda mbali zaidi ya hapo na kukusanya mapato yote kwa kila kifungu cha mambo ya Muungano halisi. Mwishowe, wakalinganisha iwapo mapato hayo yanakidhi matumizi ya Muungano au yana upungufu. Taarifa ya uchambuzi wa PriceWaterhouseCoopers ilitolewa kama Mapendekezo ya Tume Kuhusu Vigezo vya Kugawana Mapato na Kuchangia Gharama za Muungano ya mwezi Agosti 2006.

Taarifa ya Tume ya Pamoja ya Fedha inaonyesha hali ya kusikitisha kuhusu mapato na matumizi ya fedha za Muungano, hasa kwa upande wa Tanganyika. Ili kupata picha kamili ya hali halisi ilivyo, tunaomba kunukuu sehemu ya Taarifa hiyo in extenso, kwenye ukurasa wake wa 18: "Uchambuzi unaonyesha kuwa mapato yanayotokana na vyanzo vya Muungano yanakidhi matumizi ya Muungano na kuwa na ziada ya kutosha. Takwimu zinaonyesha kuwa kiasi kidogo cha mapato hayo kimekuwa kinagharimia matumizi ya Muungano. Kwa mfano, uwiano huu ulikuwa ni (shilingi bilioni 360.679 kati ya (shilingi bilioni 1,030.513) sawa na asilimia 35 mwaka 1999/2000, (shilingi bilioni 468.450) kati ya (shilingi bilioni 1,801.733) sawa na asilimia 26 mwaka 2002/03, na (shilingi bilioni 636.078) kati ya (shilingi bilioni 2,271.710) sawa na asilimia 28 mwaka 2003/04.

"Uchambuzi unaonyesha kuwa kiasi kikubwa cha ziada ya mapato ya Muungano kimekuwa kinatumika kugharimia mambo yasiyo ya Muungano. Viwango hivi kwa mwaka 1999/2000 vilikuwa ni (shilingi bilioni 39.822) sawa na asilimia 5.9 kwa (Serikali ya Mapinduzi Zanzibar) na (bilioni 631.714) sawa na asilimia 94.1 kwa Tanzania Bara. Viwango hivi vilibadilika kwa kiasi kikubwa kwa mwaka wa fedha 2003/04 ambapo kwa (Serikali ya Mapinduzi Zanzibar) kilishuka hadi (shilingi bilioni 37.053) sawa na asilimia 2.3, na (shilingi bilioni 1,588.494) sawa na asilimia 97.7 kwa (Serikali ya Muungano wa Tanzania)."

Takwimu za utafiti wa PriceWaterhouseCoopers zinaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2003/2004 pekee, matumizi halisi kwa vifungu vya Muungano yalikuwa shilingi bilioni 537.258 ambayo ni asilimia 20 tu ya bajeti yote ya Serikali ya Muungano kwa mwaka huo. Mapato halisi ya vyanzo vya mapato vinavyotokana na mambo ya Muungano kwa mwaka huo yalikuwa ni shilingi bilioni 1,030.826, au takriban shilingi trilioni 1.030. Kwa maana nyingine, mapato na matumizi ya fedha zinazotokana na vyanzo vya mambo ya Muungano yaliacha ziada ya shilingi bilioni 493.567 kwa mwaka huo mmoja. Ziada hii ni nje ya mapato yaliyotokana na misaada na mikopo kutoka nje, na ilitumika kwa shughuli za maendeleo za Tanganyika zisizo za Muungano.

Kwa sababu Tanganyika imekuwa inafaidika sana na utaratibu huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano - ambayo kiuhalisia ni Serikali ya Tanganyika iliyovaa joho la Muungano – imekataa kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha kwamba uwekwe utaratibu utakaowezesha kutenganisha mapato na matumizi ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Miaka nane tangu mapendekezo hayo yatolewe mwaka 2006, "Serikali zetu mbili", kwa maneno ya Mh. Samia Suluhu Hassan, "bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha."

**Mheshimiwa Spika**, Kero nyingine kubwa ya Muungano huu na ambayo ina umri karibu sawa na Muungano wenyewe inahusu hisa za Zanzibar zilizokuwa

katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki kabla ya Bodi hiyo kuvunjwa mwaka 1965 na Benki Kuu ya Tanzania kuanzishwa. Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri Suluhu Hassan, hisa za Zanzibar katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ni mojawapo ya “kero zilizobaki katika orodha ya mambo ya kutafutiwa ufumbuzi....” Kufuatana na maelezo hayo, “masuala ya Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa faida ya Benki Kuu yapo katika ngazi ya Mawaziri wa Fedha wa (Serikali ya Jamhuri ya Muungano) na (Serikali ya Mapinduzi Zanzibar) kwa hatua za majadiliano.”

Alipohojija juu ya hisa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwezi Januari 2013, Waziri huyo huyo aliiambia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba: “*Katika Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 14 Januari 2013 imeelezwa kwamba Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ wamepatiwa nyaraka maalum zenyenye taarifa za siri na wamekubaliana kujadili suala hili mwezi Februari, 2013 baada ya kuzipitia nyaraka hizo.*” Kwa vile bado mawaziri wanajadiliana, kama tulivyosema mwaka jana, “*sio tu kwamba Wazanzibari hawajui ni kiasi gani cha fedha zao zilichukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kufuatia kuvunjwa kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, bali pia hawana uhakika watazirudishiwa lini!*”

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vile fedha za Zanzibar katika Bodi ya Sarafu zilichukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano baada ya masuala ya fedha, sarafu na Benki Kuu kufanya kuwa mambo ya Muungano mwaka 1965, sisi tuliozaliwa ndani ya Muungano tuna haki ya kuambiwa ukweli kwanini Serikali hii ya CCM imeshindwa kurudisha fedha hizo kwa Wazanzibari kwa takriban miaka hamsini tangu fedha hizo zinyakuliwe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano aka Serikali ya Tanganyika? Tunahitaji kuelezwaa Serikali hii ya CCM inahitaji muda wa miaka mingapi mingine ili iweze kurudisha fedha za watu na kuwaepusha Watanganyika na laana ya wizi wa fedha za Wazanzibari?

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au Wazanzibari wenyewe katika umoja wao, wana haki ya kutumia njia yoyote ile watakayoona inafaa, ikiwamo kufungua kesi za madai katika mahakama za ndani au mahakama za kimataifa, kudai fedha zake zote halali ambazo zimeilibiwa na Tanganyika kwa kutumia kivuli cha Muungano katika kipindi chote cha miaka hamsini ya Muungano huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vyovypote vile, takwimu hizi zinaonyesha kwamba, kwa sababu ya Muungano huu, uhusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar ni uhusiano wa kinyonyaji. Kwa sababu hiyo, huu ni uhusiano wa kikoloni. Ni uhusiano kati ya ‘himaya’ ya Tanganyika na ‘koloni’ lake la Zanzibar. Himaya za kikoloni huwa zinadhibiti masuala yote ya ulinzi na usalama, mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa, uraia, kodi, fedha, sarafu na benki kuu ya makoloni yao. Na himaya

za kikoloni huwa zinatumia nguvu na udhibiti wao wa masuala haya kuyanyonya makoloni yao kiuchumi, kuyadidimiza kijamii na kuyatawala kisiasa. Hivi ndivyo ambavyo imekuwa kwa mahuasiano kati ya Tanganyika na Zanzibar tangu kuzaliwa kwa Muungano huu tarehe 26 Aprili, 1964.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 20 Aprili, 1968, Mwalimu Nyerere alisema yafuatayo wakati akihojiwa na gazeti la *The Observer* la London, Uingereza: “*If the mass of the people of Zanzibar should, without external manipulation, and for some reason of their own, decide that the Union was prejudicial to their existence, I could not bomb them into submission.... The Union would have ceased to exist when the consent of its constituent members was withdrawn.*” Yaani, “endapo umma wa wananchi wa Zanzibar wataamua, bila kurubuniwa kutoka nje na kwa sababu zao wenyewe, kwamba Muungano unaathiri kuendelea kuwepo kwao, sitaweza kuwalazimisha kwa kuwapiga mabomu.... Muungano hautaendelea kuwepo pale ridhaa ya washirika wake itakapoondelewa.”

Miaka 45 baada ya kauli hiyo ya Mwalimu Nyerere, Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alisema yafuatayo katika Maoni aliyojatoa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba tarehe 13 Januari, 2013: “*Mfumo (wa Muungano) uliopo sasa hauinufaishi Zanzibar na hivyo haukulbaliki kwa Wazanzibari. Koti la Muungano kama *lilivyo* sasa *linabana* sana. Wakati umefika tushone koti jipya kwa mujibu wa mahitaji ya zama hizi.*

Nalo Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika maoni yake kwa Tume ya tarehe 5 Februari, 2013, limetaka ‘kuwa na Muungano wa dhati’, yaani “... Muungano wa kweli, hata kama ni kwa maeneo machache, kwa dhati ya wanasiwa na Watanzania kwa ujumla.” Kwa mujibu wa Baraza hilo, Muungano ‘wa dhati’ na ‘wa kweli’ ni ule ambaa kuna “... Mamlaka ya Zanzibar huru na Mamlaka ya Tanganyika huru ndani ya Muungano, (na) Mamlaka ya Muungano iwekwe wazi – maeneo yake, uwezo au nguvu zake, na utendaji wake. Mambo yote hayo yawekwe wazi na mipaka yake.”

Aidha, Baraza la Wawakilishi limependekeza kwamba “rasilmali za Muungano ziwe ni milki ya pande mbili za Muungano; na rasilmali hizo ndio zitumike katika uendeshaji wa Mamlaka za Muungano. Ugawaji wa rasilmali ufanywe kwa uwiyano maalum utakaokubaliwa kwa pamoja na pande mbili za Muungano.”

Hata kama baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar baadaye waliyakana maneno yao haya walipofika mbele ya wakubwa wao wa Tanganyika wakati wa vikao vya Bunge Maalum hapa Dodoma, haya sio maneno ya kupuza hata kidogo kwa sababu yanathibitisha kwamba hata wale Watanzania wachache, kama wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ambaa wamefaidika kwa kupata nafasi za uongozi kwa sababu ya Muungano, hawauni Muungano huu kama kielelezwa cha umoja, mshikamano

na upendo wao. Kuyapuuza maneno haya ni kujenga misingi imara na hakika ya Muungano huu kuvunjika.

### NCHI MOJA AU NCHI MBILI?

**Mheshimiwa Spika**, Kuna propaganda na uongo mwingine juu ya Muungano huu ambayo imeenezwala sana katika kipindi hiki cha nusu karne ya uhai wake. Propaganda hii inahusu kile kilichozaaliwa na Hati ya Makubaliano ya Muungano, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Baada ya jina la Jamhuri hiyo kubadilishwa kuwa Tanzania tarehe 28 Oktoba, 1964, ilizaliwa dhana kwamba Makubaliano ya Muungano yaliua nchi za Tanganyika na Zanzibar na kuanzisha 'nchi moja' ya Tanzania. Dhana hii imetumika, katika miaka hamsini ya Muungano huu, kuhalalisha ukiukwaji wa matakwa ya Makubaliano ya Muungano kwa kutumia dhana nyingine ya 'kuimarisha Muungano.' Dhana hizi mbili ndio msingi wa nyongeza zote za mambo ya Muungano, na ndio sababu kubwa ya kuporomoka kwa uhuru na mamlaka ya Zanzibar katika kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Dhana kwamba Hati ya Makubaliano ya Muungano iliua nchi mbili na kuzaa nchi moja ya Tanzania ni dhana potofu na isiyokuwa na msingi wowote katika Hati yenye. Kwanza, Hati ya Makubaliano ya Muungano ilitamka wazi kwamba sheria zilizokuwepo Tanganyika na Zanzibar kabla ya Muungano zitaendelea kutumika 'katika nchi zao' hadi hapo zitakaporekebishwa ili kutilia nguvu Muungano na Hati za Muungano; au sheria mpya zitakapotungwa na mamlaka husika au kutolewa kwa amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya utekelezaji wa Mambo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Pili, vifungu mbali mbali vya Katiba zilizofuatia Makubaliano ya Muungano ziliweka wazi kwamba Tanganyika na Zanzibar hazikuuawa na Makubaliano ya Muungano. Hivyo basi, hata baada ya mabadiliko ya jina kwenda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba na sheria mbali mbali ziliendelea kutumia jina la Tanganyika na Zanzibar. Kwa mfano, Sheria ya Kuongeza Muda wa Kuitisha Bunge la Katiba, 1965, iliyosainiwa na Rais Nyerere tarehe 24 Machi, 1965, inataja, katika vifungu vyote vitatu, 'Sheria za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.'

Aidha, Sheria ya Kutangaza Katiba ya Muda ya Tanzania ya tarehe 11 Julai, 1965, ilitangaza kwamba 'Tanzania ni Jamhuri Huru ya Muungano'; kwamba eneo lake ni "... eneo lote la Tanganyika na Zanzibar ..." na kwamba chama kimoja cha siasa "... kwa Tanganyika kitakuwa Tanganyika African National Union (TANU)...." Kwa wakati wote wa uhai wake, Katiba ya Muda haikuwahi kutamka kuwa Tanzania ni nchi moja. Badala yake, ibara ya 27(1) ya Katiba

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hiyo iliyokuwa inahusu sifa za kuchaguliwa kuwa mbunge ilitamka wazi kwamba: "**Raia ye yote wa Tanganyika** ambaye amefikisha umri wa miaka ishirini na moja na ni mwanachama (wa TANU) atakuwa na sifa ya kuchaguliwa kuwa mbunge wa jimbo...."

Kwa upande wake, licha ya kuanza kutumia jina la Tanzania Bara na Tanzania Visiwani kwa mara ya kwanza, Toleo la Kwanza la Katiba ya sasa ya Muungano lilitamka kwamba Tanzania ni 'Jamhuri ya Muungano.' Hapa pia hapakuwa na tamko la 'nchi moja.'

**Mheshimiwa Spika**, Maneno ya ibara ya 1 ya Katiba ya sasa ya Muungano kwamba "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano" yaliingia katika kamusi ya kikatiba na kisiasa ya nchi hii kufuatia 'kuchafuka kwa hali ya kisiasa ya Zanzibar' na kung'olewa madarakani kwa Rais Aboud Jumbe. Kufuatia hali hiyo, Katiba ya Jamhuri ya Muungano ilifanyiwa marekebisho makubwa ambayo, pamoja na mengine, yalitangaza kuwa "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano." Kwa sababu ya upinzani mkubwa wa Wazanzibari, Marekebisho hayo ya Katiba yaliondoa pia maneno 'Tanzania Visiwani' na kuweka 'Tanzania Zanzibar' badala yake. Maneno 'Tanzania Bara' yalibaki kama yalivyowekwa mwaka 1977.

Kwa maana hiyo, dhana ya Tanzania kama nchi moja haijatokana na Makubaliano ya Muungano bali ilitokana na siasa za Muungano, yaani mvutano kati ya viongozi wa Tanganyika wakiwa wamevalia joho la Jamhuri ya Muungano na viongozi wa Zanzibar waliotaka uhuru zaidi kwa nchi yao. Pili, dhana hiyo haina umri mkubwa sana kuliko inavyodhaniwa, kwani iliingia kwenye Katiba mwaka 1984, miaka thelathini iliyopita, na miaka ishirini baada ya Muungano.

## MUUNGANO USIO WA USAWA

**Mheshimiwa Spika**, Tangu mwanzo Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haukuwa Muungano wa usawa. Huu ni Muungano ulioipa Tanganyika – ikiwa imevalia koti la Jamhuri ya Muungano - mamlaka ya kuingilia uhuru na mamlaka ya Zanzibar. Hii inathibitishwa na Hati ya Makubaliano ya Muungano yenye. Kwanza, kwa kutamka kwamba katika kipindi cha mpito "Katiba ya Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Katiba ya Tanganyika...", ni wazi kwamba Mshirika wa Muungano aliyekuwa na nguvu katika Muungano huu ni Tanganyika.

**Pili**, kwa kuweka orodha ya mambo 11 ya Muungano, ni wazi kwamba Zanzibar ilinyang'anya mamlaka juu ya masuala hayo na mamlaka hayo yalihamishiwa kwa Tanganyika ikiwa imevaa koti la Jamhuri ya Muungano. Kwa maana hiyo, Zanzibar ilinyang'anya mamlaka yake juu ya masuala ya nchi za nje, ulinzi, polisi, mamlaka ya hali ya hatari, uraia, uhamiaji, biashara ya nje na mikopo na masuala mbali mbali ya kodi. Hati ya Makubaliano ya Muungano yenyewe inasema wazi kwamba "Bunge na Serikali (ya Jamhuri ya Muungano) litakuwa na mamlaka kamili kwenye mambo hayo kwa Jamhuri ya Muungano na, kwa nyongeza, mamlaka kamili kwa ajili ya mambo mengine yote ya na kwa ajili ya Tanganyika."

**Tatu**, kwa kutangaza kwamba rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano atakuwa Mwalimu Nyerere na Makamu wa kwanza wa Rais atakuwa Sheikh Abeid Karume; na kwa kutangaza kwamba Makamu wa Kwanza wa Rais atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano katika utekelezaji wa majukumu yake ya kiutendaji kuhusu Zanzibar, ni wazi kwamba Hati ya Makubaliano ya Muungano ilithibitisha nafasi ya chini (subordinate position) ya Zanzibar katika Muungano.

**Nne**, kwa kuzifanya alama za utaifa (national emblems) za Tanganyika kuwa ndio alama za taifa za Jamhuri ya Muungano, kuna-emphasize superior position ya Tanganyika ndani ya Muungano na subaltern position ya Zanzibar katika Muungano huu. Ukweli huo huo unahusu masuala ya kuzifanya taasisi na watumishi wa Serikali ya Tanganyika kuwa ndio taasisi na watumishi wa Jamhuri ya Muungano.

**Tano**, hata kwa kuangalia watu ambao wamewahi kupata fursa ya kuongoza Jamhuri ya Muungano, ni wazi kwamba Watanganyika ndio wamekuwa mabwana na Wazanzibari wamefanywa watwana katika masuala ya haki za kiutawala. Hivyo, kwa mfano, katika kipindi cha miaka hamsini ya Muungano huu, ni Mzanzibari mmoja tu ndiye aliyepata fursa ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa miaka kumi kati ya miaka hamsini hiyo.

Kwa utaratibu huo huo, tokea mwaka 1964, Zanzibar haijawahi kutoa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mkuu wa Jeshi la Polisi au Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Zote hizi ni taasisi za Muungano. Aidha, Zanzibar imewahi kutoa Waziri Mkuu mmoja tu, tena kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu, na Jaji Mkuu mmoja tu katika kipindi hicho cha nusu karne ya Muungano huu. Vile vile, katika Diplomatic Corps, kwa sasa kuna Wazanzibari wawili tu ambao ni mabalozi wa Tanzania nchi za nje kati ya mabalozi 32 wanaowakilisha Tanzania nchi za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Hata Bunge lako tukufu lina rekodi mbaya katika masuala haya. Hivyo, kwa mfano, katika miaka yote ya Muungano, hakuna Mzanzibari

ambaye amewahi kushikilia nafasi ya Spika au Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Aidha, licha ya Kanuni za Bunge lako tukufu kuruhusu kufanyika kwa vikao vya Kamati zake za Kudumu nje ya Dodoma, yaani Dar es Salaam na/au Zanzibar; na licha ya Kanuni kuruhusu Mikutano ya Bunge kufanyika nje ya Dodoma ikiwa 'itaelekezwa vinginevyo', hakuna Kamati hata moja ya Bunge hili tukufu ambayo imewahi kufanya vikao vyake Zanzibar na haijawahi kutokea Bunge hili likaelekezwa kufanya Mikutano yake nje ya Tanganyika!

## KURA YA MAONI JUU YA MUUNGANO

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya nusu karne ya Muungano wa aina hii, wananchi wa Tanganyika na, hasa wa, Zanzibar hawako tayari kuendelea na utaratibu huu wa kinyonyaji na kikandamizaji. Wananchi wanataka mabadiliko ya msingi ya muundo wa Muungano na uendeshaji wake. Wananchi wanataka kusikilizwa juu ya Muungano. Wananchi wanataka kufanya maamuzi kuhusu kama wanataka kuendelea na Muungano na, kama jibu ni ndiyo, muundo wa Muungano huo.

Wakati wa mjadala wa Sura ya Kwanza na ya Sita ya Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum, Kamati nydingi zilishindwa kufanya maamuzi kwa sababu ya kukosa uungwaji mkono wa theluthi mbili ya wajumbe wote wa Kamati kutoka Tanganyika na idadi hiyo hiyo ya wajumbe kutoka Zanzibar. Kama hali ni hiyo katika Bunge Maalum licha ya Bunge hilo kujazwa wajumbe wengi wa CCM kutoka kundi la 201, hali ni mbaya zaidi nje ya Bunge Maalum na nje ya Bunge lako tukufu. Nje ya mabunge haya, watu wengi, hasa Wazanzibari ambao ndio wamekuwa waathirika wakubwa wa Muungano huu katika nusu karne ya maisha yake, wananchi wengi hawataki tayari kuendelea na Muungano huu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mazingira haya, namna muafaka ya kutoka katika *constitutional impasse* inayokuja mbele yetu, ni kuwaliza wananchi wa Tanganyika na Zanzibar – kwa kutumia kura ya maoni - kama bado wanataka kuendelea na Muungano huu. Na kama jibu lao litakuwa ni ndiyo, basi wananchi waamue, katika kura hiyo, ni muundo gani wa Muungano wanautaka. Miaka hamsini ya watawala kuamua masuala haya muhimu peke yao inatosha. Huu ni wakati muafaka kwa wananchi kufanya maamuzi haya makubwa kwa maisha yao na kwa nchi zao mbili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka wabunge wa Bunge lako tukufu wawe kwenye upande sahihi wa historia, yaani upande wa wananchi katika jambo hili.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuhitimisha maoni haya, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wakuu wa vyama vyetu vitatu vinavyounda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kufanya maamuzi ya kuendeleza ushirikiano ulioanzia ndani ya Bunge Maalum, kwenye Bunge lako tukufu. Wananchi wetu wanataka mabadiliko ya msingi ya utawala wa nchi zetu mbili na usimamizi wa rasilmali zake. Kama ilivyokuwa kwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ndani ya Bunge Maalum, ndivyo wananchi wanavyotutazamia kuendesha shughuli zetu ndani ya Bunge hili tukufu. Historia itatuhukumu vikali endapo tutashindwa kukamata fursa hii ya kihistoria katika nchi zetu mbili.

Baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha.

---

Tundu Antiphas Mughwai Lissu  
MSEMAJI & WAZIRI KIVULI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)  
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Bungeni Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara (*Assignment of Ministerial Responsibilities Notice*) la Mwezi Januari, 2011 Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yameidhinishwa kama ifuatavyo:-

- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira; na
- Kufuatilia na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*National Environment Management Council - NEMC*).

Aidha, kutatua changamoto zinazohusiana na utaratibu na uharibifu wa mazingira ili kuhakikisha matumizi endeleo ya raslimali na maliasili.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliunda Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1977 na sera ilibaini matatizo makuu sita ya kimazingira yaliyomo nchini ambayo ni kama ifuatavyo:-

Uharibifu wa ardhi, kutopatikana kwa maji safi na salama kwa wakazi wa Mijini na Vijiji, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa makazi ya wanyama na baianuai, uhabirifu wa makazi na viumbe wa majini na ukataji wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini matatizo hayo, yakawekwa malengo ya sera ili kukabiliana na madhara hayo.

Moja, ni kuhakikisha udumishaji, usalama na matumizi sawa ya raslimali kwa msingi wa sasa na vizazi vijavyo bila kuharibu mazingira au kuhatarisha afya na usalama. (Makofii)

Pili, kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambayo ndiyo mfumo wa uhai wetu.

Tatu, kuhifadhi na kuendeleza urithi wetu na ule uliotengenezwa na binadamu ikiwa ni pamoja na maisha ya viumbe wa aina mbalimbali na wa kipekee nchini Tanzania.

Nne, kung'amua na kufahamu mahusiano muhimu kati ya mazingira na maendeleo na kuhimiza ushirikiano wa mtu binafsi na jamii katika kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndiyo msingi mkuu katika utunzaji wa mazingira na pia ndiyo msingi mkuu katika kuchangia mabadiliko ya tabianchi. Hivyo basi, matumizi mabaya ya ardhi ni kupelekea uharibifu wa mazingira na hivyo kuzidisha au kuharakisha mabadiliko ya tabianchi.

Ni ukweli kwamba kama ardhi imeharibika maana yake ni kwamba hakuna mmea utakaopandwa na kuota bila kutumia mbolea na hapa hoja ni: Je, wananchi wetu wanao uwezo kiasi gani kuendelea kununua mbolea za viwandani kwa ajili ya kuotosha miti ambayo mpaka kufikia muda wa kuvunwa ni takribani miaka saba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi makubwa na ya muda mrefu yasiyoratibiwa vyema ya mbolea za chumvi chumvi za viwandani, ni sababu tosha inayochangia uharibifu wa ardhi. Hivi sasa Nyanda za Juu Kusini, kilimo cha aina yoyote hakiwezi kufanyika bila ya kutumia mbolea za viwandani. Kambi Rasmi ya Upinzani inaanini kabisa kuwa tuna wataalam wengi na wazuri wa udongo na pia wataalam wa mazingira na tatizo hili siyo kwamba limetokea leo, bali ni la siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kama Sera ya Mazingira ya mwaka 1977 inavyosema, kuwa wao ndiyo wasimamizi wa sheria ya uhifadhi wa mazingira ya mwaka 2004: Je, ni ushauri gani wamekwishakuutoa kwa Taasisi au Wizara husika juu ya kupunguza au kusitisha matumizi ya mbolea za chumvi chumvi viwandani kwa wakulima hasa wa Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahoji hili kwa sababu Sheria ya Mazingira ndiyo Sheria iliyo juu ya sheria nyingine zote linapotokea suala la uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tayari imeathirika kwa uwepo wa mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na ukame wa muda mrefu unaojirudia rudia unaoambatana na athari kubwa katika kilimo, usafirishaji, nishati, biashara na sekta mbalimbali za uchumi kwa jamii. Hivi sasa zaidi ya 70% za majanga yote ya asili katika Tanzania yanahusika na mabadiliko ya tabianchi ukiwemo ukame na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majanga hayo, kilimo katika maeneo husika kinadorora au kusimama, mifugo mingi na wanyama wa porini wanakufa kwa kukosa chakula na maji na wakati mwingine kusombwa na mikondo ya maji yaliyofurika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viashiria vya uwepo wa mabadiliko ya tabianchi katika nchi yetu ni pamoja na vifo vya mifugo vilivyokithiri kutokana na ukame hasa maeneo ya Kaskazini mwa Tanzania kama vile Monduli na Longido. Wastani wa mvua kwa mwaka umepungua kwa 25%, utokeaji wa mafuriko unaosababishwa na ongezeko la mvua zisizotabirika katika maeneo makame yasiyo na mimea na hivyo maji kutiririka kwa kasi zaidi na kusababisha madhara maeneo yanapoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la joto duniani linasababisha ongezeko hatari na utokeaji wa magonjwa mapya kwa mamilioni ya watu hasa yale yanayoenezwa na vimelea na bakteria kwa maeneo ambayo asili hayakuwepo. Tafiti mbalimbali zinazohusu mwelekeo wa joto wa muda mrefu katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa zinaonesha ongezeko la joto katika maji ya kina kirefu kati ya nyuzi za centigrade 0.2 mpaka 0.7 kuanzia miaka ya 1,900. Hii ni taarifa ya Serikali ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa asili tulizoea watu kuhama na kuwa wakimbizi kutokana na mapigano ya vita, lakini kwa sasa wahamiaji wengi wanatokana na mabadiliko ya tabiachi na kwa lugha inayoelezeka ni

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

environmental refugees. Hili limekuwa tatizo sana kwani kutokana na kuhama maeneo yao ya asili kwa ajili ya ukweli kwamba maeneo hayo hayawezi tena kuwezesha kuishi kwao na hivyo inawalazimu kuhamia maeneo mengine ili kuendelea na maisha yao. Hili limetokea sana kwa wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaalam mabadiliko ya tabianchi yamechangiwa na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali katika uso wa dunia hasa zile zinazofanywa na binadamu. Shughuli hizi baadhi zikiwa za kimaendeleo na zisizo za kimaendeleo zimechangia kuzalisha hewa chafu (green house gases) ambazo huchangia katika ongezeko la joto duniani (global warming).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi ni kwamba shughuli zote ambazo zimeongeza hewa ya ukaa angani ndizo chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabianachi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya shughuli hizo kwa uchache ni kama vile ongezeko la viwanda hasa katika nchi za Ulaya na Asia, ukataji miti na uchomaji misitu, uzalishaji na utupaji taka hovyo, ufugaji usiozingatia idadi ya mifugo hasa mbuzi, ng'ombe, kondoo na wanyama wengine wanaoharibu mazingira kwa kuangamiza mimea, uchimbaji wa madini, matumizi mabaya ya mashine, mitambo na magari yaliyochoka yanayozalisha hewa ya ukaa, utumiaji wa vyombo chakavu kama majokofu, TVs, computers na vitu vingine vinavyoongeza shughuli za kivita sehemu mbalimbali duniani huchangia kuzalisha hewa chafu kama kulipua mabomu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushahidi mwingi sana kuthibitisha uwepo wa mabadiliko ya tabianchi. Miiongoni mwa ushahidi huo ni kuwepo kwa hali mbaya ya hewa kama vile ukame, mvua isiyotabirika, mafuriko, mkondo wa joto kali na kuongezeka kwa vimbunga, ongezeko la joto, magonjwa ambayo hapo mwanzo hayakuwepo, kuongezeka kwa kasi ya kuyeyuka kwa barafu na kubadilika kwa uoto na maumbile asilia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na Watanzania wa maeneo mbalimbali ni wahanga wa mabadiliko ya tabianchi kwa ushahidi uliotolewa hapo awali. Mkakati wa Taifa wa Mabadilko ya Tabianchi Mpango Kazi wake bado haujaonesha tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba madhara ya mabadiliko ya tabianchi yanaathiri kila mwananchi katika nchi yetu, hili limepelekea uwepo wa maslahi binafsi yanayokinanza Kimataifa na hivyo suala hilo kuwa gumu kufikia maridhiano katika historia ya dunia. Masuala na mabadiliko ya tabianchi yanashughulikiwa kwa kuzingatia sayansi na ujuzi wa masuala ya asili na ya hali ya hewa. Kwa sasa siasa za Kimataifa zimetokea kutunza au kulinda maslahi ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Taifa na itikadi na vinakuwa juu ya sababu nyingine zote za kuongoza maamuzi ikiwemo hata ile ya sayansi na utalaam unavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya bajeti 2014/2015, na hapa nisemee sehemu ya nne; Mojawapo ya malengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mazingira mwaka huu wa fedha ni hifadhi na usimamizi wa mazingira, kuandaa, kuanzidha Idara, sehemu ya Mabadiliko ya Tabianchi.

Kutokana na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi hapa kwetu, kila mtu anaona bila hata ya kuambiwa na kwa masikitiko makubwa kwamba hata Idara rasmi ya Wizara hii haipo, bali watendaji wake wamekuwa wanakwenda kuhudhuria Mikutano na Makongamano ya Kimataifa tu. Hoja ni kwamba: Je, ni kwa vipi ujuzi wao katika makongamano ya nje na ndani umekuwa ukisaidia nchi yetu kukabiliana na matatizo yanayoletwa na mabadiliko ya tabianchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba bila ya kuwepo kwa Idara ambayo iko chini ya mtu maalum, basi uwajibikaji hauwezi kupimwa. Kwa hili la mabadiliko ya tabianchi, swalii ni nani anayehitajika kuwajibika? Je, ni Wizara nzima ambayo ni Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira)? Kufanya hivyo ni kutoitendea haki Ofisi hiyo. Inatainakiwa iwe na Idara na Kurugenzi tofauti za kiutendaji kulingana na upana wa Sekta ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) katika mradi Na. 5006 – *Mainstreaming Environment and Climate Change Adaptation in the Implementation of National Policies and Development Plans*, zimetengwa jumla ya Sh. 800,825,000/=. Wizara haina Idara inayoshughulikia mambo ya mabadiliko ya tabianchi.

Pili, ukiangalia matumizi yaliyowekwa kwa ajili ya fedha hizo, zaidi ya 8% ni vikao tu na kuandaa mfumo wa kitaasisi katika usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hakuna mfumo wa kitaasisi kama Serikali ilivyokiri katika randama ya mabadiliko ya tabianchi, ni tatizo ambalo liko nje ya mipaka ya Tanzania. Hivyo basi, bila ya kuwa na mfumo wa kiutendaji unaoeleweka, fedha nyingi zinaendelea kuletwa na wahisani. Kama mwaka huu zinaingia Sh. 720,825,000/= na fedha hizo zitatumika kuilinda nchi yetu na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Namba, ambao namba yake haionekani, chini ya kichwa “*Climate Change Adaptation Programmes*, Sh. 1,892,777,000/=,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa mujibu wa randama inaonyesha kwamba kiasi cha Sh. 2,893,755,000/= zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kulikuwa na makosa ya kiuchapaji au ndivyo ilivyokusudiwa kwa ongezeko la bilioni moja! Kwa kuwa mradi wenyewe unaoombewa fedha hizi haionyezi ni mradi namba ngapi, na katika kuhakiki tarakimu ni dhahiri kuwa siyo makosa ya kiuandishi, bali kuna jambo ambalo Kambi Rasmi inahitaji ufanuzi wa utofauti wa fedha hizo za mradi tajwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera inatoa suluhisho la ushirikishwaji wa wananchi katika ngazi zote katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Wakati huo huo, sera ikijenga mazingira ya wananchi kunufaika na fursa zilizomo katika mabadiliko ya tabianchi katika ngazi zao zote za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya CCM haina Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi, ni dhahiri kwamba hakuna suluhisho lolote zaidi ya matumizi yasiyo na tija ya fedha za walipa kodi kuhusiana na tatizo hili la mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), inaonesha kwamba japokuwa Ofisi hiyo imetengewa fedha kidogo kwa kulinganisha na majukumu hasa ya kulinda na kuhifadhi mazingira katika dhana pana, Ofisi hii imetenga jumla ya Shilingi milioni 126.32 kwa ajili ya mafunzo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya watumishi wake kwa Idara mbalimbali kwenye Wizara hiyo. Ni ukweli ulio wazi kwamba kuna wahitimu wengi sana wenye sifa mitaani na kuna wanafunzi wengi sana ambao wanakosa mikopo na hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida tu, ni kwa vipi Serikali inaweza kutumia kiasi kikubwa cha fedha kusomesha watu ambaو tayari wanafanya kazi, wanao uwezo wa kujilipia masomo yao na mbaya zaidi wanaendelea kulipwa stahili zao kama watumishi? Kambi Rasmi ya Upinzani inalionna hili kuwa ni njia mojawapo ya kuwanyima fursa wale wote wanaohitaji zaidi msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge za tarehe 19 Aprili, 2013 ni kwamba takriban zaidi ya tani milioni moja ya mkaa hutumiwa kwa mwaka hapa nchini, Dar es Salaam pekee ikitumia zaidi ya asilimia 50 ya mkaa wote unaozalishwa, maana yake, magunia zaidi ya 28,000 yenye kilo 60 mpaka 80 huingizwa Dar es salaam kila siku. Hii ina maana kuwa Dar es Salaam pekee huingiza wastani wa zaidi ya magunia milioni 10.2 kwa mwaka. Kiasi hiki kinaifanya Tanzania kushika nafasi ya nne na kuwa mionganoni mwa nchi 10 duniani zinazoongoza kuzalisha mkaa kwa wingi kuliko nchi zote na Tanzania

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

inazalisha kiasi cha 3% ya mkaa duniani. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa Tanzania inatumia zaidi ya tani 2,650 za mkaa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzalisha tani moja ya mkaa kwa njia ya jadi kama inavyofanyika hapa nchini, zaidi ya tani 10 mpaka 12 za miti au kuni, huhitajika. Hii ina maana kuzalisha magunia 15 huhitaji tani 10 hadi 12 za miti. Hapa inahitajika hekari 846 za miti kila siku kuvunwa. Kwa ajili hiyo, takwimu zinaonyesha kuwa matumizi ya mkaa tangu miaka ya 1960 yamekuwa yakiongezeka kila siku. Itambulike kuwa eneo la misitu Tanzania ni kilometra za mraaba 343,326 sawa na asilimia 38.9 ya ardhii yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetubidi kunukuu maneno haya kwa sababu kubwa kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo yenyeye mamlaka na jukumu la msingi na kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa salama. Kwa uvunaji wa miti na uchomaji wa mkaa kiasi hicho, hoja hapa ni kwamba ni kwa jinsi gani tunaweza kuepukana na jangwa kwa miaka ijayo? Kama takwimu za matumizi ya mkaa kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee yako hivi: Je kwa Mikoa mingine nchini takwimu zikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni ukweli kuwa matumizi ya mkaa na kuni kwa maeneo ya vijiji ni makubwa, lakini siyo kama ambavyo mkaa unatumika mijini. Kwa mwaka 2013 ukweli ni kwamba Serikali haikutoa mwelekeo tunakwendaje mbele katika kuhakikisha matumizi ya mkaa kwa mijini yanapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tumejaliwa kuwa na gesi. Lakini kwa masikitiko makubwa makampuni yanayoingiza gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani ndiyo yanazidi kuongezeka. Jambo hili linatoa hisia kwamba Sekta ya Gesi ya Kupikia ndiyo sababisho la kwanza kuzuia gesi yetu ya asili isichakatwe kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji: Je, Ofisi hii ya Makamu wa Rais inachukua hatua gani katika mchakato huu za kuhakikisha matumizi ya mkaa yanapungua na uharakishaji wa matumizi ya gesi asilia kwa matumizi ya majumbani yanafanikiwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba bila kuwepo matumizi mbadala ya mkaa ambayo ni gesi, achilia mbali umeme ambaa bei yake haiwezekaniki kwa Mtanzania wa kawaida, vinginevyo suala la kukata miti haliepukiki kutokana na kutokuwa na mbadala wa uhakika kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu ujenzi holela mijini. Miradi yote hapa nchini kabla ya kuanza utekelezaji wake ni lazima kwanza ifanyiwe tathmini (*environmental impact assessment*) na kupata cheti cha kuwezesha uendelee kama ulivyokuwa umepangwa. Jambo la kushangaza ni kwamba miradi ambayo inamiliikiwa na Serikali imekuwa haipati Cheti cha Tathmini na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hivyo imekuwa ikileta usumbufu mkubwa sana kwa watumiaji na hivyo kuwa kero kwa Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii inatokana na ukweli kwamba Ofisi ya Kampuni inayojenga miundombinu ya mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam, Strabag, imepewa hati na Serikali kumiliki eneo hilo la Jangwani na hivyo tayari wamejenga Ofisi zao za kudumu. Mbali na kuhoji utolewaji wa hati hiyo kwa kampuni hiyo: Je, tathmini ya mazingira imefanyika? Kwani eneo hilo miaka yote linakumbwa na mafuriko; kitendo cha kujenga hapo ni kurudisha maji kwenye maeneo jirani na kuzidisha maafa. Aidha, kama kampuni hiyo imepewa hati ya kumiliki, kwa nini waliokuwa wamejenga eneo hilo walihamishwa na kupelekwa nje ya Mji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya tatizo kubwa mjini ni ujenzi holela wa makazi na viwanda, jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa hasa kwa kipindi hiki ambacho dunia imekabiliwa na tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi. Jiji la Dar es Salaam lina mabonde ambayo ndiyo njia kuu ya maji kutoka nchi kavu kuelekea baharini. Hivyo basi, ujenzi holela unazuia mkondo wa maji ni matatizo makuwa sana kwa majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote ambaao wamefanya hivyo ni watu ambaao wana hadhi katika jamii. Hapa nimtaje Mheshimiwa Mbunge, Mchungaji Getrude Rwakatare, amelalamikiwa sana kwani amezuia Mto Mdumbwi kwa kuziba mkondo wa maji na hivyo kusababisha mafuriko na daraja kuvunjika na kuleta madhara makubwa kwa wakazi wa eneo hilo.

Aidha, kuna mtu mwingine anayeendelea na ujenzi anayeitwa Mzamir Katunzi; amejenga na anaendelea na ujenzi katikati ya Mto na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa. Je, Serikali iko wapi? Au iko likizo? Serikali itoe kauli kutokana na ukiukaji huu wa sheria unaofanywa kwa makusudi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji kama Serikali ipo likizo kutokana na ukweli kwamba watumishi wa NEMC wametishiwa maisha kwa kupigwa wakiwa kazini, hakuna hatua zozote zimechukuliwa kwa wahusika. Tunaitaka Serikali kutoa maelezo kuhusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwendelezo huo huo wa uchafizi wa mazingira, malalamio ni makubwa kwa viwanda na makampuni ya madini kutokufuata sheria zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira. Mojawapo ya viwanda vinavyoharibu mazingira ni kiwanda cha 21<sup>st</sup> Century kilichopo Mkoani Morogoro, kinatiririsha maji machafu kwenye Mto Ngerengere, mto ambaao unaungana na Mto Ruvu ambaao ndiyo chanzo kikuu cha maji yanayotumiwa na wakazi wa Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na taka hizo zenye sumu kuingia katika chanzo cha maji yanayotumiwa na wakazi wengi, pia kiwanda hicho kinakadiriwa kwa siku kutumia kuni tani 50 kwa ajili ya uendeshaji wake. Hii ni teknolojia iliyopitwa na wakati. Kuni hizo au magogo hayo ni kutoka kwenye miti ya asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kiwanda hicho cha *21<sup>st</sup> Century*, kuna kampuni ya Barrick inayochimba dhahabu katika migodi ya Nyamongo, Tarime. Hadi sasa maji taka yenye sumu yanafiririka katika Mto Tigite na hakuna hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa kampuni ya Barrick kwani uchafuzi bado uko pale pale. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu zilizopo ni kwamba Bunge la Tisa lilikwishaunda Kamati Ndogo kwa ajili ya kuchunguza tatizo hilo, lakini kwa masikitiko makubwa taarifa yake haijawahi kuletwaha hapa Bungeni ili Bunge zima liijadili na kutoa maazimio. Huu kwa njia mojawapo unaweza kuwa ni uzembe au mwendelezo wa Bunge letu wa kutokutaka kujadili taarifa za Kamati zinazoundwa kuangalia matatizo yanayoikabili jamii. Kwa mfano, Kamati iliyochunguza wananchi kuchomewa nyumba zao kule Loliondo, Kamati iliyochunguza uchafuzi wa maji yanayoingia Mto Mara, taarifa zake zote hazijajadiliwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza NEMC iko wapi? Uwajibikaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais uko wapi? Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ambayo inasema kuwa makampuni yanayojihusisha na uchimbaji wa madini pindi wanapomaliza shughuli zao, ni lazima warudishie ardhi katika hali iliyokuwa kabla ya kuanza uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya Resolute iliyokuwa inafanya shughuli zake Wilaya ya Nzega na kampuni ya Barrick Gold Mine iliyokuwa inamiliki mgodi wa Tulawaka uliokuwa Wilaya ya Biharamulo imemaliza kazi na kuiuzia mgodi huo STAMICO, lakini haikutimiza kazi yake ya kuhakikisha mazingira yanarejeshwa katika hali yake ya uhalisia. Kambi Rasmi inaona kuwa huo mzigo ni mkubwa na umerudishwa kwa wananchi kupitia kampuni ya STAMICO japokuwa kampuni hiyo bado ni changa. Je, Serikali inatoa kauli gani katika ulaghai huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ndicho chombo kikuu chenye dhamana ya kuhakikisha Sheria ya Mazingira inafuatwa kwa ukamilifu wake, lakini kwa bahati mbaya ni kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya kutimiza majukumu yake ni kidogo sana kiasi kwamba Baraza linashindwa kufanya kazi muhimu ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, randama ya Wizara ya Wizara inaonyesha kuwa bajeti ya ruzuku kwa Baraza kwa mwaka 2013/2014 ilikuwa Shilingi bilioni 1.96. Kwa mwaka huu fedha ya ruzuku ya Baraza imetengwa Shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Aidha, Baraza linakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo kukosa ofisi inayojitosheleza kwa shughuli zote ikiwemo maabara na vitendea kazi kama inavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali katika kukabiliana na matatizo ya wakosaji, wavunjaji wa Sheria ya Mazingira kujificha katika Mahakama. Kuwepo na kitengo cha Mahakama kinachohusika na mazingira (*Environmental Appeal Tribunal*) ambacho kitashughulika kuwachukulia hatua wale wote ambao kwa makusudi wanakiuka Sheria ya Mazingira au wanakaidi amri halali ya Baraza. Aidha, katika kupambana na ujenzi holela, ni muhimu kila Ofisi ya Mipango Miji NEMC ihusishwe ili mtalaam wa mazingira atoe ushauri wake. Kwa njia hii matatizo yanayojitekeza sasa kwa kiasi kikubwa yatapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizikwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Mezani**

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHE MCH  
ISRAEL NATSE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA OFISI  
YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA KWA  
MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013)

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara (Assignment of Ministerial Responsibilities Notice), la mwezi Januari, Mwaka 2011, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yameainishwa kwa ifuatavyo:- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira, Kufuatilia na kuratibu Shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environment Management Council-NEMC).

Aidha, kutatua changamoto zinazohusiana na uharibifu wa Mazingira ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali na maliasili.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliunda Sera ya Taifa ya Mazingira mwaka 1997, sera ilibaini matatizo makuu sita ya kimazingira yaliyopo nchini ambayo ni:

1. Uharibifu wa ardhi;
2. Kutokopatikana kwa maji safi na salama kwa wakazi wa mijini na vijiji
3. Uchafuzi wa Mazingira
4. Upotevu wa Makazi ya Wanyamapori na bioanuai;
5. Uharibifu wa makazi na viumbe wa majini; na
6. Ukataji wa misitu.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kubaini matatizo hayo yakawekwa malengo ya sera ili kukabiliana na madhara hayo:

1. Kuhakikisha, udumishajji, usalama na matumizi sawa ya raslimali kwa msingi wa sasa na vizazi vijavyo bila ya kuharibu mazingira au kuhatarisha afya na usalama,
2. Kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambayo ndiyo mfumo wa uhai wetu,
3. Kuhifadhi na kuendeleza urithi wetu na ule uliotengenezwa na binadamu, ikiwa ni pamoja na maisha ya viumbe wa aina mbalimbali na wa kipekee nchini Tanzania;
4. Kung'amua na kufahamu mahusiano muhimu kati ya mazingira na maendeleo na kuhimiza ushirikiano wa mtu binafsi na jamii katika kuhifadhi mazingira.

## **UHARIBIFU WA ARDHI**

**Mheshimiwa Spika**, Ardhi ndio msingi mkuu katika utunzaji wa mazingira na pia ndio msingi mkuu katika kuchangia mabadiliko ya tabia nchi. Hivyo basi matumizi mabaya ya ardhi ni kupelekea uharibifu wa mazingira na hivyo kuzidisha au kuharakisha mabadiliko ya Tabia nchi.

Ni ukweli kwamba kama ardhi imeharibika maana yake ni kwamba hakuna mmea utakaopandwa na kuota bila ya kutumia mbolea, na hapa hoja ni je

wananchi wetu wanauwezo kiasi gani kuendelea kununua mbolea za viwandani kwa ajili ya kuotesha miti ambayo mpaka ni kuivuna inachukua muda wa kuanzia miaka saba?

**Mheshimiwa Spika**, Matumizi makubwa ya muda mrefu na yasiyoratibiwa vyema ya mbolea za chumvi chumvi za viwandani ni sababu tosha inayochangia uharibifu wa ardhi. Hivi sasa nyanda za juu kusini kilimo cha aina yoyote hakiwezi kufanyika bila ya kutumia mbolea za viwandani.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa tuna wataalam wengi na wazuri wa udongo na pia wataalam wa mazingira, na tatizo hili sio kwamba limetokea leo bali ni la siku nyingi.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kama sera ya Mazingira ya mwaka 1997 inavyosema kuwa wao ndio wasimamizi wa sheria ya uhifadhi wa mazingira ya mwaka 2004. Je, ni ushauri gani wamekwisha utoa kwa taasisi au wizara husika juu ya kupunguza au kusitisha matumizi ya mbolea za chumvi chumvi za viwandani kwa wakulima hasa wa mikoa ya Iringa, Njombe, Songea, Mbeya, Rukwa na Katavi?

**Mheshimiwa Spika**, Tunahoji hilo kwa sababu sheria ya Mazingira ndiyo sheria iliyokuwa juu ya sheria zingine zote linapotokea suala la kuhifadhi mazingira.

## 1. MABADILIKO YA TABIANCHI

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania tayari imeathirika kwa uwepo wa mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo pamoja na ukame wa muda mrefu unaojirudia rudia ambao unaambatana na athari kubwa katika kilimo, usafirishaji, nishati, biashara na sekta mbalimbali za uchumi kwa jamii. Hivi sasa zaidi ya asilimia 70 ya majanga yote ya asili katika Tanzania yanahusika na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame na mafuriko.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa majanga hayo, kilimo katika maeneo husika kinadorora au kusimama, mifugo mingi na wanyama wa porini wanakuwa kwa kukosa chakula na maji, na wakati mwingine kusombwa na mkondo wa maji yaliyofurika.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya viashiria vya uwepo wa mabadiliko ya tabianchi katika nchi yetu ni pamoja na vifo vya mifugo vilivyokithiri kutokana na ukame, hasa maeneo ya kaskazini mwa Tanzania kama vile Monduli na Longido. Wastani wa mvua kwa mwaka umepungua kwa asilimia 25. Utokeaji wa mafuriko unaosababishwa na ongezeko la mvua zisizotabirika katika maeneo makame yasiyo na mimea na hivyo maji kutiririka kwa kasi zaidi na kusababisha madhara maeneo yanapoelekeaa.

**Mheshimiwa Spika**, Ongezeko la joto duniani linasababisha ongezeko hatari na utokeaji wa magonjwa mapya kwa mamilioni ya watu, hasa yale yanayoenezwa na vimelea na bacteria kwa maeneo ambayo kwa asili hayakuwepo. Tafiti mbalimbali zinazohusu mwelekeo wa joto wa muda mrefu katika ziwa Viktoria,Tanganyika na Nyasa zinaonesha ongezeko la joto katika maji ya kina kirefu kati ya nyuzi za sentigredi 0.2 mpaka 0.7 kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1900(Taarifa za Serikali ya mwaka 2009).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa asili tulizoea watu kuhama au kuwa wakimbizi kutokana na mapigano ya vita, lakini kwa sasa wahamiaji wengi wanatokana na mabadiliko ya tabianchi na kwa lugha iliyozoleka ni “**environmental refugees**”. Hili limekuwa tatizo sana kwani kutokana na watu kuhama maeneo yao ya asili kwa ajili ya ukweli kwamba maeneo hayo hayawezi tena kuwezesha kuishi kwao na hivyo inawalazimu kuhamia maeneo mengine ili kuendelea na maisha yao. Hili limetokea sana kwa wafugaji na wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, Kiutalaam, mabadidiko ya tabianchi yamechangiwa na Kuongezeka kwa shughuli mbalimbali katika uso wa dunia, hasa zile zinazofanywa na binadamu. Shughuli hizo baadhi zikiwa za kimaendeleo na zisizo za kimaendeleo zimechangia kuzalisha hewa chafu (green house gases) ambazo huchangia katika ongezeko la joto duniani (global warming). Kwa ufupi ni kwamba shughuli zote ambazo zinaongeza hewa ukaa angani ndio chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya shughuli hizo kwa uchache ni kama vile ongezeko la viwanda hasa katika nchi za ulaya na Asia, ukataji miti na uchomaji misitu, uzalishaji na utupaji wa taka ovyo, ufugaji usiozingatia idadi ya mifugo hasa ng'ombe, mbuzi , kondoo na wanyama wengine wanaoharibu mazingira kwa kuangamiza mimea, uchimbaji madini, matumizi mabaya ya mashine/mitambo na magari yaliyochoka yanayozalisha hewa ya ukaa, utumiaji wa vyombo chakavu kama majokofu, computer, Tv na vitu vingine na ongezeko la shughuli za kivita sehemu mbalimbali duniani ambazo huchangia kuzalisha hewa chafu kwa kulipua mabomu.

**Mheshimiwa Spika**, Kuna ushahidi mwingi sana kuthibitisha uwepo wa “mabadiliko ya tabia nchi”. Mionganini wa ushahidi huo ni kuwepo kwa hali mbaya ya hewa, kama vile: ukame, mvua isiyotabirika, mafuriko, mkondo wa joto kali na kuongezeka kwa vimbunga, ongezeko la joto, magonjwa ambayo hapo mwanzo hayakuwepo katika baadhi ya maeneo, kuongezeka kwa kasi ya kuyeyuka kwa barafu na kubadilika kwa uoto na maumbile asilia duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania na watanzania wa maeneo mbalimbali ni wahanga wa Mabadiliko ya Tabia nchi, kwa ushahidi uliotolewa hapo awali.

Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango kazi wake bado haujawa na tija kwa taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba madhara ya mabadiliko ya tabianchi yanaathiri kila mwananchi katika kila nchi, hili limepelekea uwepo wa maslahi binafsi yanayokinzana kimataifa na hivyo suala hilo kuwa gumu kufikia maridhiano katika historia ya dunia. Masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanashughulikiwa kwa kuzingatia sayansi na ujuzi wa masuala ya asili na hali ya hewa. Kwa sasa siasa za kimataifa wakati mwininge maslahi binafsi ya taifa na itikadi yake vinakuwa juu ya sababu zingine zozote za kuongoza maamuzi ikiwemo hata ile ya sayansi na utaalaum unavyotaka<sup>1</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/14 na makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15, sehemu ya iv, mojawapo ya malengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa mwaka huu wa fedha katika Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, ni kuunda/kuanzisha Idara/sehemu ya Mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya Tabianchi hapa kwetu, kila mtu anaona bila ya hata kuambiwa. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba hata Idara rasmi katika Wizara hii haikuwepo, bali watendaji wamekuwa wanakwenda kuhudhuria mikutano na makongamano ya kimataifa tu.

---

<sup>1</sup> Sera ya CHADEMA mabadiliko ya Tabianchi-toleo la kwanza 2013

Hoja ni je ni kwa vipi ujuzi na uzoefu wao katika makongamano ya nje na ndani umekuwa ukiisaidia nchi yetu kukabiliana na matatizo yaletwayo na mabadiliko ya Tabianchi?

**Mheshimiwa Spika**, Ni dhahiri kwamba bila ya kuwepo kwa idara ambayo ipo chini ya mtu maalum basi uwajibikaji hauwezi kupimwa, na kwa hili la Mabadiliko ya Tabianchi, swali ni nani anahitajika kuwajibika? Je Wizara nzima ambayo ni Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira? Kufanya hivyo ni kuto-itendea haki kwani Ofisi hiyo inatakiwa iwe na Idara na Kurugenzi tafauti za kiutendaji kulingana na upana wa sekta ya mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira katika Mradi Na. 5306-(Mainstreaming Environment and Climate Change Adaptation in the Implementation of National Policies and Development Plans) zimetengwa shilingi 800,825,000.00. Wizara haina idara inayoshughulika na mambo ya Mabadiliko ya Tabianchi, pili ukiangalia matumzi yaliyowekwa kwa ajili ya fedha

hizo zaidi ya asilimia 8 ni vikao tu, na kuandaa mfumo wa kitaasisi katika usimamizi wa mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa hakuna mfumo wa kitaasisi kama Serikali inavyokiri katika Randama na mabadiliko ya Tabianchi ni tatizo ambalo liko nje ya mipaka ya Tanzania. Hivyo basi bila ya kuwa na mfumo wa kiutendaji unaoeleweka fedha nyingi zinaendelea kuletwa na wahisani, kama mwaka huu zinaingia shilingi 720,825,000.00 na fedha hizo hazitatumika kuilinda nchi yetu na madhara yanayotokana na mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi namba(....)?: **Climate Change Adaptation Programmes Sh. 1,892,755,000.00**. Kwa mujibu wa Randama inaonyesha kwamba kiasi cha shilingi **2,893,755,000.00** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, sijui kulikuwa na makosa ya kiuchapaji au ndio ilivyokusudiwa kwa ongezeko la shilingi **bilioni 1**.

Kwa kuwa mradi wenyewe unaoombewa fedha hizo haioneshi ni mradi namba ngapi, na katika kuhakiki tarakimu ni dhahiri kuwa si makosa ya kiuandishi bali kuna jambo ambalo Kambi Rasmi inahitaji ufanuzi wa utofauti wa fedha hizo za mradi tajwa wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Sera inatoa suluhisho la ushirikishwaji wa wananchi katika ngazi zote katika kupambana na mabadiliko ya Tabianchi, wakati huohuo Sera ikijenga mazingira ya wananchi kunufaika na fursa zilizomo katika mabadiliko ya tabianchi katika ngazi zao zote za jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Serikali ya CCM haina Sera kwa ajili ya Mabadiliko ya Tabianchi, ni dhahiri kwamba hakuna suluhisho lolote zaidi ya matumizi yasiyo na tija ya fedha za walipa kodi, kuhusiana na tatizo hili la mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kufanya uchambuzi wa bajeti ya ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, inaonyesha kwamba japokuwa ofisi hiyo imetengewa fedha kidogo kwa kulinganisha na majukumu hasa ya kulinda na kiuhifadhi mazingira katika dhana pana.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii imetenga jumla ya shilini milioni 126.32 kwa ajili ya mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya watumishi wake kwa idara mbalimbali kwenye Wizara hiyo. Ni ukweli uliowazi kwamba kuna wahitimu wengi sana wenye sifa mitaani na kuna wanafunzi wengi sana ambaa wanakosa mikopo na hawana kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa hali ya kawaida tu, ni kwa vipi Serikali inaweza kutumia kiasi kikubwa cha fedha kusomesha watu ambao tayari wanakazi na wanauwezo wa kulipia masomo yao? na mbaya zaidi wanaendelea kulipwa stahili zao kama watumishi. Kambi Rasmi ya Upinzani inalionna hili kuwa ni njia mojawapo ya kuwanyima fursa wale wote wanaohitaji zaidi msaada wa Serikali.

## 2. TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa rasmi za Bunge za tarehe 19 April 2013 ni kwamba "Takribani zaidi ya tani milioni moja ya mkaa hutumiwa kwa mwaka hapa nchini huku Dar es Salaam pekee ikitumia zaidi ya asilimia 50% ya mkaa wote unaozalishwa na kutumika hapa nchini. Magunia zaidi ya elfu ishirini na nane (28,000) yenye kilo kati ya 60 hadi 80 huingizwa Dar es Salaam kila siku. Hii ina maana kuwa, Dar es Salaam pekee huingiza wastani wa zaidi ya magunia milioni 10.2 kwa mwaka. Kiasi hiki kinaifanya Tanzania kushika nafasi ya nne na kuwa mionganoni mwa nchi kumi duniani zinazoongoza kuzalisha mkaa kwa wingi kuliko nchi zote ambapo Tanzania pekee inazalisha asilimia 3% ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa Tanzania hutumia zaidi ya tani 2,650 za mkaa kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuzalisha tani moja ya mkaa kwa njia ya jadi kama inavyofanyika hapa nchini, zaidi ya tani 10 hadi 12 za miti au kuni huhitajika. Hii ina maana kuwa kuzalisha magunia 15 huhitajika tani 10 hadi 12 za miti au kuni hivyo kuhitaji ekari 846 za miti kila siku ili kuvunwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya mkaa kwa watumiaji. Takwimu zinaonyesha kuwa matumizi ya mkaa tangu mwaka 1960 yamekuwa yakiongezeka kila siku. Itambulike kuwa eneo la misitu Tanzania ni kilomita za mraba **344,326** sawa na asilimia 38.9% ya ardhi yote".

**Mheshimiwa Spika**, Imetubidi kunukuu maneno hayo kwa sababu kubwa kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais ndio yenye mamlaka na jukumu la msingi la kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa salama. Kwa uvunaji wa miti na uchomaji wa mkaa kiasi hicho, hoja hapa ni kwa jinsi gani tunaweza kuepukana na jangwa kwa miaka ijayo kama takwimu za matumizi ya mkaa kwa mkoa mmoja wa Dar es Salaam yako hivyo, je na kwa mikoa mingine zaidi ya Dar es Salaam takwimu zikoje?

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, ni ukweli kuwa matumizi ya mkaa na kuni kwa maeneo ya vijiji ni makubwa lakini si kama ambavyo mkaa unatumika mijini. Na kwa mwaka jana ukweli ni kwamba Serikali haikutoa mwelekeo tunakwendaje mbele katika kuhakikisha matumizi ya mkaa kwa mijini yanapungua.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sasa tumejaaliwa kuwa na gesi, lakini kwa masikitiko makubwa makampuni yanayoingiza gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani

ndiyo yanazidi kuongezeka. Jambo hili linatoa hisia kwamba sekta hii ya gesi ya kupikia ndio sababisho la kwanza kuzuia gesi yetu ya asili isichakatwe kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Kambi Rasmi ya Upinzani ina hoji, Je Ofisi hii ya Makumu wa Rais inachukua hatua gani katika mchakato huu wa kuhakikisha matumizi ya mkaa yanapungua na uharakishaji wa matumizi ya gesi asilia kwa matumizi ya majumbani unafanikiwa haraka?

**Mheshimiwa Spika,** Ni dhahiri kwamba bila ya kuwepo matumizi mbadala ya mkaa ambayo ni gesi, achilia mbali umeme ambao bei yake haiwezekaniki kwa mtanzania wa kawaida. Vinginevyo suala la kukata miti haliepukiki kutokana na kutokuwepo kwa mbadala wa uhakika kwa watanzania.

### 3. UJENZI HOLELA MIJINI

**Mheshimiwa Spika,** Miradi yote hapa nchini kabla ya kuanza utekelezaji wake ni lazima kwanza ufanyiwe tathmini (Environmental Impact Assessment-EIA) na kupata cheti cha kuuwezesha uendelee kama ulivyokuwa umepangwa. Jambo la kushangaza ni kwamba miradi ambayo inamiliwi na Serikali imekuwa haipati cheti cha Tathmini na hivyo imekuwa ikileta usumbufu mkubwa sana kwa watumiaji na hivyo kuwa kero kwa Serikali yenye.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja hii inatokana na ukweli kwamba, Ofisi ya Kampuni inayojenga miundombinu ya mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam (Strabag) imepewa Hati na Serikali ya kumiliki eneo hilo la Jangwani na hivyo tayari wamejenga ofisi zao za Kudumu. Mbali na kuhoji utolewaji wa hati kwa Kampuni hiyo, je tathmini ya mazingira imefanyika? kwani eneo hilo miaka yote linakumbwa na mafuriko. Kitendo cha kujenga hapo ni kurudisha maji kwa maeneo jirani na kuzidisha maafa. Aidha, kama Kampuni hiyo imepewa hati miliki ni kwanini waliokuwa wamejenga eneo hilo walihamishwa na kupelekwa nje ya mji?

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya tatizo kubwa mijini ni ujenzi holela wa makazi na viwanda, jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa hasa kwa kipindi hiki ambacho Dunia imekabiliwa na tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi. Jiji la Dar es Salaam lina mabonde ambayo ndiyo njia kuu ya maji kutoka nchi kavu kuelekea baharini, hivyo basi ujenzi holela unazuia mkondo wa maji ni matatizo makubwa sana kwa majirani.

**Mheshimiwa Spika,** Wale wote ambao wamefanya hivyo ni watu ambao wanahadhi katika jamii, Mhe Mbunge Getrude Rwakatare amelalamikiwa sana kwani amezuia mto Ndumbwi kwa kuziba mkondo wa maji na hivyo kusababisha mafuriko na daraja kuvunjika na kuleta madhara makubwa kwa wakazi wa eneo jirani na hilo. Aidha, kuna mtu mwagine anayeitwa Mzamili Katunzi, amejenga na anaendelea na ujenzi katikati ya mto na hakuna hatua

zozote zinazochukuliwa. Je Serikali iko wapi? Au iko likizo? Serikali itoe kauli kutokana na ukiukwaji huu wa sheria unaofanywa kwa makusudi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ina hoji kama Serikali iko likizo kutokana na ukweli kwamba watumishi wa NEMC wametishiwa maisha kwa kupigwa wakiwa kazini, lakini hakuna hatua zozote zimechuliwa kwa wahusika. Tunaitaka Serikali kutoa maelezo kuhusiana na suala hili.

#### 4. UCHAFUZI WA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwendelezo huo huo wa uchafuzi wa mazingira, malalamiko ni makubwa kwa viwanda, na makampuni ya madini kutokufuata sheria zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira. Mojawapo ya kiwanda kinachoharibu mazingira ni kiwanda cha 21-Century kilichopo mkoani Morogoro- kinatiririsha maji machafu kwenye mto Ngerengere mto ambao unaungana na mto Ruvu ambao ndio chanzo kikuu cha maji yanayotumiwa na wakazi wa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Mbali ya taka hizo zenye sumu kuingia katika chanzo cha maji yanayotumiwa na wakazi wengi, pia kiwanda hicho inakadirwa kwa siku kutumia kuni tani 50 kwa ajili ya uendeshaji wake. Hii ni teknolojia iliyopitwa na wakati. Kuni hizo au magogo hayo ni kutoka kwenye miti ya asili.

**Mheshimiwa Spika**, Mbali na Kiwanda hicho cha 21-Century kuna Kampuni ya Barrick inayochimba dhahabu katika mgodi wa Nyamongo-Tarime, hadi sasa bado maji taka yenye sumu yana tiririka katika mto Tigite na hakuna hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa kampuni ya Barrick kwani uchafuzi bado uko pale pale.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kumbukumbu zilizopo ni kwamba Bunge la Tisa lilikwisha unda kamati ndogo kwa ajili ya kuchunguza tatizo hilo, lakini kwa masikitiko makubwa taarifa yake haijawahi kuletwa hapa Bungeni ili Bunge zima liijadili na kutoa maazimio. Huu kwa njia mojawapo unaweza kuwa ni uzembe au muendelezo wa Bunge letu kwa kutokutaka kujadili taarifa za kamati ndogo zinazopoundwa kuangalia matatizo yanayozikabili jamii- (**Kwa mfano: Uchunguzi Loliondo-Wananchi kuchomewa nyumba na Tarime- uchafuzi wa maji yanayoingia mto Mara**).

Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza kwa hili NEMC iko wapi? Uwajibikaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais uko wapi?

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi na Mazingira ya mwaka 2004, inasema kuwa makampuni yanayojihusisha na uchimbaji wa madini, pindi wanapomaliza shughuli zao ni lazima warudishie ardhi katika hali ilivyokuwa kabla ya kuanza uchimbaji.

**Mheshimiwa Spika**, Makampuni ya Lesolute iliyokuwa inafanya shughuli zake Wilaya ya Nzenga na Kampuni ya Barick Gold Mine iliyokuwa inamiliki mgodi wa Tulawaka uliokuwa Wilaya ya Bihamalo imemaliza kazi na kuiuzia mgodi huo STAMICO lakini haikutimiza kazi yake ya kuhakikisha mazingira yanarejshwa katika hali yake ya uhalisia. Kambi Rasmi ya Upinzani inalionna kuwa mzigo mkubwa umerudishwa kwa Wananchi kupitia kampuni ya STAMICO japokuwa kampuni hiyo bado ni change. Je Serikali inatoa kauli gani kwa ulaghai huo?

## 5. BARAZA LA USIMAMIZI WA MAZINGIRA-NEMC

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la usimamizi wa mazingira ndicho chombo kikuu chenye dhamana ya kuhakikisha sheria ya mazingira inafuatwa kwa ukamilifu wake, lakini kwa bahati mbaya ni kwamba fedha inayotengewa kwa ajili ya kutimiza majukumu yake ni kidogo sana kiasi kwamba Baraza linashindwa kufanya kazi muhimu ya ufuatiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, Randama ya Wizara inaonyesha kuwa Bajeti ya ruzuku kwa Baraza kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilikuwa shilingi bilioni 1.96, kwa mwaka huu wa fedha ruzuku kwa Baraza zimetengwa shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Aidha, Baraza linakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo kukosa ofisi inayojitosheleza kwa shughuli zote ikiwemo maabara na vitendea kazi kama inavyohitajika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inaitaka Serikali katika kukabiliana na matatizo ya wakosaji/ wavyunjaji wa sheria ya Mazingira kujificha katika mahakama, kuwepo na Kitengo cha Mahakama kinachohusika na Mazingira (Environmental Appeal Tribunal) ambacho kitakuwa kinahusika kuwachukulia hatua wale wote ambao kwa makusudi wanakiuka sheria ya mazingira/au wanaokaida amri halali ya Baraza.

Aidha, katika kupambana na ujenzi holela ni muhimu kila ofisi ya Mipango miji NEMC ihusishwe ili mtaalam wa Mazingira atoe ushauri wake, kwa njia hii matatizo yanayojitokeza sasa kwa kiasi kikubwa tutayapunguza.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
**Mch. Israel Y.Natse (Mb)**  
**Msemaji Mkuu Kambi Rasmi ya Upinzani-**  
**Ofisi ya Makamu wa Rais,Mazingira.**  
**12.05.2014**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji wa CPA - Tawi la Tanzania kuwa kutakuwa na kikao leo saa saba mchana katika ukumbi namba 227 jengo la utawala. Mheshimiwa Ndugulile!

### **HOJA BINAFSI YA MBUNGE**

### **UGONJWA WA DENGUE FEVER**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa hoja kuhusiana na ugonjwa wa dengue fever uliyopo nchini kwa sasa. Nafanya hivyo kwa kupitia kanuni ya 28(8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ugonjwa wa dengue fever umeingia na kusambaa sasa hivi hapa nchini, ugonjwa huu unasababishwa na mbu aina ya Aedes. Ugonjwa huu unafanana sana kwa dalili na ugonjwa wa Malaria na dalili zake ni pamoja na kuwa na homa, maumivu ya kichwa, maumivu ya viungo, kutokwa kwa vipele mwilini na hata kutokwa damu katika sehemu mbalimbali za mwili maana ya dengue hemorrhagic fever.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Dar es salaam na baadhi ya Mikoa mingine imeathirika sana na ugonjwa huu wa dengue fever. Kuna taarifa mbalimbali kwenye vyombo vyta habari na mitaani kuhusiana na wananchi wengi kuambukizwa ugonjwa huu na baadhi kupoteza maisha.

Kwa kuwa ugonjwa huu wa dengue fever bado unaendelea kushika kasi na kusambaa nchini; kwa kuwa ufahamu wa ugonjwa huu bado ni mdogo kwenye jamii, ni vema wananchi wakapewa taarifa sahihi za ugonjwa huu na hatua za kuchukua pindi wanapohisi wana dalili za ugonjwa huu.

Vile vile kuna umuhimu wa wahudumu wa afya kuelewa dalili za ugonjwa na njia za kimatibabu ambazo wanaweza kuzitoa kwa mgonjwa pamoja na kuwa ugonjwa huu hauna tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na sintofahamu ambayo imeanza kuleta hofu kwa wananchi, naomba uiagize Serikali kuleta hapa Bungeni taarifa ambayo itakuwa na mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuwaeleza kwa kina Wabunge na wananchi kwa ujumla chanzo cha ugonjwa huu na dalili zake na jinsi unavyosambazwa.

Pili, jinsi ya kujikinga na ugonjwa huu.

Tatu, idadi ya wananchi ambao wameathirika na ugonjwa huu na wale ambao wamepoteza maisha.

Nne, Mikoa ambayo imeathirika na ugonjwa huu; na

Tano, hatua zinazochukuliwa na Serikali kuelimisha jamii pamoja na hatua nyingine ambazo Serikali inachukua katika kudhibiti ugonjwa huu wa dengue fever.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ugonjwa huu upo Dar es Salaam na kwa taarifa za vyombo vya habari watu wameanza kufariki na Mganga wa Hospitali ya Temeke amefariki. (Makofii)

Naomba Serikali watupatie majibu haraka sana ni namna gani tiba zake na udhibiti wa ugonjwa huu ili wananchi wawe na imani, kutopoteza maisha yao.

Baada ya maneno haya machache, watakaochangia leo jioni...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo Mheshimiwa!

**MWENYKITI:** Tunaanza na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia)

**MWENYEKITI:** Tukae. Mchangiaji wetu wa mwanzo ni Mheshimiwa Mohammed Mnyaa.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mchango wangu kwa masikitiko makubwa sana kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ameweza kutumia 86% ya muda wake kuzungumzia mazingira, akatumia 14% kuzungumzia masuala ya Muungano kama kwamba jambo hili ni dogo wakati ni jambo kubwa mno na unyeti wake tunaujua lakini akazungumzia Muungano kuanzia ukurasa wa 6 19 tu. Hili ni jambo ambalo linanisikitisha kwa matatizo yaliyoko katika Muungano lakini akaweza kutumia 14% ya hotuba yake kwa masuala ya Muungano akatumika 86% kwa masuala ya mazingira pekee. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kweli Muungano wetu umeshatimiza miaka 50 na kuna 90.6% ya watu waliozaliwa wakati Muungano huu uko tayari kwa mujibu wa maneno ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, hilo bado halizuii katika Muungano wa dhuluma na katika Muungano wa namna hii, wa upande mmoja tu kuwa sisi tunyamaze kuwa miaka 50 ndiyo mingi kwa hiyo tena tunyamaze dhuluma za miaka yote hiyo. Kwanza miaka 50 ni kidogo sana ukilinganisha na miungano mingine duniani kwa mfano pale Uingereza tu wana miaka 300, ina miaka hiyo 50 inaingia mara sita na bado watu wa Scotland wanatetea Muungano ule na umeleta matatizo na wanapiga kura mwezi Septemba na wana miaka zaidi ya miaka tatu seuze miaka 50. Kwa hiyo, hatuwezi konyamaza kimya kwa kuona dhuluma hizi zinaendelea kwa Muungano wa upande mmoja tu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, katika kipindi cha muda mrefu, Wazanzibar wengi tuliamini kwamba Watanganyika ndiyo wanaotuletea matatizo na kudhulumu katika Muungano huu kumbe sivyo, ni baadhi tu ya kikundi *powerful*, hiki kikundi kina nguvu cha watu wa CCM walioko madarakani, walioko Serikali ndiyo ambao wanaleta dhuluma na matatizo katika Muungano huu. Baada ya kuona maoni ya Tume ya Jaji Warioba kumbe Watanganyika walio wengi wanataka haki itendeke na hawapendelei Muungano huu ambao una dhuluma wanataka Muungano wa haki. Kwa hiyo, watusamehe wale wenzetu mwanzo tuliofikiria na wao wameungana kumbe ni kikundi kidogo lakini *powerful*. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi hiki baadhi yao walithubutu kufanya uchochezi mkubwa Makanisani na mpaka leo wameachiwa wanadunda na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na ni uchochezi mkubwa sana uliofanywa Makanisani na walionesha dhahiri siri ilijoificha imefichuka kwamba wao kumbe nia ni kuidhibiti Zanzibar katika hali tofauti. Sababu walizozitoa ni kwamba Zanzibar ina eneo kubwa la bahari haiwezi kujilinda, siyo sahihi kwa sababu linalolinda toka hapo Muungano ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

siyo Wazanzibar peke yao. Kkwa hiyo, ni uchochezi mkubwa walioufanya na mpaka leo watu hawa wanaachwa. Katika nchi zenyе utawala bora uchochezi kama ule usingeachiwa na watu hawa tayari wangkuwa wamechukuliwa hatua za kijiuzulu. Jambo hili linasikitisha sana lakini ndiyo hali halisi na ndiyo katika mionganoni mwa kikundi kidogo cha walio na nguvu ndani ya CCM wenye roho mbaya wanaoendelea kutukandamiza Wazanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu yetu hapa wa Kambi ya Upinzani alizungumzia maeneo mengi ambayo Zanzibar inadhulumiwa kwa hali ya juu. Alizungumzia mambo ya *budget support*, alizungumzia mambo ya misaada mingine lakini kwa kweli ile ni sehemu ndogo tu ya dhuluma inazofanyiwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani asiyejua kwamba kuna mashirika ya Muungano tena mengi lakini mashirika haya yote hayana muundo wa Muungano kiuongozi na kiutawala. Tunapohoji unaambiwa kuna Board Member mmoja, kuna Board Member wawili, Board Member siyo kuwa jambo la pamoja liendeshwe upande mmoja, kuwa Mjumbe wa Bodii kuwa tena ndiyo Zanzibar imeshirikishwa. Mashirika hayo yako mengi, yako Mashirika kama TICRA, Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Vyuo Vikuu - TCU na kadhalika wala hauna haja ya kutafuta sehemu nyingi sana. Yote hayo kwa kiasi kikubwa Wazanzibar hawashirikishwi na hata mapato yake Zanzibar Government haipati. Kwa hiyo, nimkumbushe Ndugu yangu Tundu Lissu siyo kwamba ni mambo ya *budget support* tu na Mashirika mengi sana. Baadhi ya mashirika yamebinafsishwa na wakachukua fedha na Zanzibar haikupata chochote, yako mengi tu yakiwemo hayo ya NBC. Kwa hiyo, dhuluma hizi tunazofanyiwa haziko katika mambo ya misaada tu wala *budget support* tu dhuluma hizi ziko katika mambo mengi sana ambayo mpaka leo Zanzibar hawafaidiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Kamati ya Uchumi, Biashara na Viwanda tulipokuwa Bagamoyo alikuwepo Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, mimi nikamuuliza swali dogo tu, nikamuuliza hebu tuambie Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu hili deni la Taifa linalokua ambapo sehemu kubwa inatumika upande...

*(Hapa kengele illilia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Ya kwanza hiyo?

**MWENYEKITI:** Ya pili. Nakushukuru sana. Sasa ni Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nasema elimu ndiyo inatakiwa itolewe kwa sababu hawa wenzetu kama ingekuwa elimu imetoka kwa Wawakilishi, Wabunge, jamii inayotuzunguka kuhusu Muungano ukoje hawa wenzetu wasinge kuwa na porojo wanayoizungumza kwa sababu hii yote wanawafanya wananchi huko nje hawajui nini kinachoendelea kwa sababu misaada inayoletwa SMZ haitolewi kwa kutangazwa inatoka Serikali kwa Serikali. Sasa wananchi wanakuwa hawajui inayojua ni Serikali, sasa wenzetu wanapata mwanya, mara utasikia SMZ inanyonya, mara utasikia SMT inavaa koti la SMZ maneno kama haya ni porojo tupu ukweli housemwi. Mimi sishangai mpinzani kusema hivyo kwa sababu azungumze nini na yeye yuko katika kupinga lazima atasema hivyo. Hata hivyo, ndugu zangu Watanzania haya mnayoyasikia ni kusherehesha tu lakini ukweli atakapokuja Waziri wa Muungano atawaelezeni na hilo ndilo la kupokea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina mifano mifupi tu wakati nilipokuwa ninazungumza kwenye Kamati nilisema tumepiga kelele Pay As You Earn inakwenda upande mmoja, tumeletewa na safari hii tumepata bilioni 15.7, tena Mungu atupe nini na tutaendelea kupata. Haya tumekuja katika gawio la misaada na mikopo ya kibajeti 27.1 bilioni tumepata, hatusemi hayo! Tukija Mfuko wa Wabunge, tunapewa kule kwetu zinatoka na huku tunapata, tumepata 1.8, hatuzungumzi hayo. Nyingine ni hii 4.5, 4.5 tumeambiwa itarekebishwa, la kuzungumzwa tuongezwe siyo kusema hatupewi, tunanyonywa, tunanyanyaswa, hilo siyo la kuzungumza wakati tuko pamoja hapahapa, ni kukaa na kuzungumza tu na mazungumzo yanakubalika mahali popote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuwa nataka kuzungumza kuhusu habari nyingine ya uratibu wa vikao. Uratibu wa vikao vya SMZ na SMT ambayo ndiyo inayozungumziwa kwamba kero zinakaa huko, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Waziri jinsi hali ilivyo kwa sababu kuna vikao vya juu vya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu, kuna vikao vya Mawaziri; SMT na SMZ, kuna vikao vya watendaji; Makatibu Wakuu na Watendaji wao. Sasa hapa ndipo panapotakiwa patiliwe mkazo kwa sababu hawa ndiyo watakaoibua kero za Muungano na hawa watakaoibua kero za Muungano ndiyo zinaweza kupanda juu zikaamuliwa. Kukiwa hakuna ratiba, mimi ningemuomba Mheshimiwa Waziri atayariske ratiba ya mwaka mzima kwa watendaji wetu ili Wizara ambayo haitakaa na Wizara mwensiwe basi kuwe na adhabu, Wizara ile inapewa kwa nini haikukaa. Kama wamekaa hawakutimia wawajibishwe kwa nini Waziri fulani alikuwa hayupo au Katibu Mkuu alikuwa hayupo. Kama kutafanyika kitu hicho kidogo kitaweza kuibua kuonekana haya mambo yanatendeka. Kwa sababu vikao vinakaa lakini havifiki mwisho na

vikao vinakaa watendaji hawatimii matokeo yake vikao vinadorora na wenzetu wanapata mwanya wa kusema wanayoyataka wakapandikiza chuki katika Muungano wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kidogo ninataka kuzungumzia jengo la Mheshimiwa Makamu wa Rais Tunguu. Jengo hilo ukipita nje ni zuri sana, linavutia na limejengeka. Tatizo liliokuwepo ukiingia ndani siyo kwamba halipendezi baadhi ya *finishing* zake siyo nzuri. Kwanza, ukiingia lango kuu tu tumepita na gari tunaambiwa aah, msiweke gari maana vioo vyake hapo hafifu vitaharibika. Nyumba ya kiongozi, kuna watu atataka kuwaalika, magari ya kila aina yataingia unasema usiweke gari hapo vioo hafifu maana yake ni nini? Sasa hili ni lazima lirekebishwe na likae sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija tatizo lingine kuna geti ambapo ukitoka ofisini kwenda nyumbani kwa Makamu, ni geti la mbao na Zanzibar mvua ndiyo rasharasha yake, jua ndiyo haiba yake. Sasa ikiwa geti ni la mbao ambalo ndilo limewekwa pale ndiyo *main road* ya kuingia huku na kutoka huku, dhamana yake ni ajali, lile linapata mvua, lile linapata jua na matokeo yake hasara itatokea. Namwomba Waziri waliangalie lile geti na waliondoe waweke geti ambalo lina umadhubuti na lenye hadhi na nyumbani kwa Makamu wa Rais.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na ajiandae Mheshimiwa Akunaay.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, sina budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kuniwezesha jioni hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu kizuri kama Muungano. Muungano ndiyo wenye kuleta nguvu za kiuchumi lakini Muungano ndiyo wenye kuleta sauti ya umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mjadala ambayo imepita katika Bunge la Katiba na ukiangalia mijadala ambayo imepita katika Bunge hili, inaonesha wazi kwamba Muungano tulio nao hauwafai Wazanzibar, Muungano tulio nao hauwafai Watanzania. Muungano ambao sehemu moja ya nchi inakandamizwa, inadhulumiwa huo siyo Muungano. Kwa maana hiyo,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wazanzibar sasa tuko macho, tuko macho kupambana na hali yoyote ya dhuluma dhidi ya Zanzibar. Kwa hili hatuna mchezo kuhakikisha kwamba Zanzibar inapata haki zake kwa mujibu wa Sheria. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia maelezo ambayo Kambi ya Upinzani tumeyatoa, kuna malalamiko kwamba kuna fedha ambazo ni bilioni 27.190. Fedha hizi ni zile za makusanyo ya mapato katika magawio kutokana na fedha zilizopitishwa kwenye Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia fedha ambazo zimetajwa hapa na Mheshimiwa Waziri lakini zinatofautiana pia na fedha ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha anasema mikopo na misaada kutoka nje ni jumla ya trilioni 1.163 ambapo Zanzibar ingestahili kupata bilioni 52. Kwa hiyo, ile bilioni 32.627 siyo sahihi. Mheshimiwa Waziri wa Muungano nataka ajibu hili swali, hali ikoje? Kwa nini kauli yako wewe mwenyewe inapingana na kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna misaada ya fedha, Waziri wa Fedha katika kipindi kilichopita alipanga bajeti ya bilioni 992.170. Wakati wa majumuisho utagundua kwamba Zanzibar mwaka jana ilipata 2.8% lakini Bara ilipata 97.2%. Tofauti ni ipi mwaka huu? Zanzibar imepata 2.18% na Bara imepangiwa 97.82%, hii ni tofauti ya 0.62 kwa Bara imeongezeka na imepungua kwa Zanzibar. Tunataka Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini kuna punguzo hili kwa Zanzibar na kwa Bara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie haki za kiutawala kwa Muungano. Haki za kiutawala kwa Muungano hazijafanya haki hata kidogo. Ukiangalia tokea mapinduzi ya mwaka 1964 hadi leo ni miaka 50 lakini Zanzibar imepata kuliongoza Taifa hili kwa muda wa miaka kumi tu. Ukiangalia hata Bunge lako, Maspika wote ambao wote wapo, Manaibu Spika ambao wote wapo, hakuna Spika mmoja kutoka Zanzibar, huu ni Muungano wa aina gani? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taasisi muhimu kwa mfano Wizara ya Mambo ya Nje, hakuna hata Mzanzibar mmoja ambaye amekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walikuwa wakiongea)

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Tunazungumza kuhusu Kamati ambapo chini ya Kanuni 117 inatakiwa Kamati zote zifanye kazi aidha Dodoma, Dar es Salaam au Zanzibar, ni lini Kamati zako zilifanya kazi Zanzibar? Hakuna hata siku moja tokea kuasiwiwa kwa Bunge hili.

Huo siyo Muungano sahihi kabisa, unawadhulumu Wazanzibar na kuwakandamiza Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija suala la Taasisi ya Kijeshi, hii ni Wizara ya Muungano, ni Mzanzibar gani aliwahi kuwa Mkuu wa Majeshi, hakuna hata siku moja. Ukienda IGP, hakuna hata siku moja IGP kutoka Zanzibar. Haya si masuala ya Muungano, haiwezekani hata siku moja kwa miaka 50 ya Muungano taasisi muhimu kama hizi hakuna hata Mzanzibar mmoja ambaye ameingia. Ukienda BOT hakuna hata siku moja Mzanzibari ameshikilia pale nafasi ya BOT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maelezo haya...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Akunaay!

**MHE. MUSTAFA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha nisimame mbele ya Bunge hili nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninaendeleza mjadala juu ya Muungano. Kwa kuwa imeonekana kwamba Muungano huu una matatizo tangu mwaka 1991, 1993, 1994, 1998 mpaka sasa hivi. Baadhi ya wachangiaji wamesimama wanasema kuna tatizo na wengine wanasema hakuna matatizo na sehemu nydingi zimeonesha kwamba kuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuondoa matatizo haya, haiwezekani Waziri asimame hapa akajibu kwa nusu saa aeleze kwamba matatizo haya yatatatuliwa namna gani. Mimi nashauri kwamba imefika sasa wakati wa Bunge hili kuishauri Serikali kwamba ilette Muswada kwa certificate of urgency kwamba iitishwe kura ya maoni kwa Watanzania na Wazanzibari, je, Muungano unahitajika na kama unahitajika ni wa aina ipi, ni Serikali moja, mbili au tatu? Kama tutangojea Katiba mpya, Katiba mpya italeta matatizo makubwa. Nimeona mahali Kamati ya Mabadiliko ya Sheria inaomba bilioni 20. Bora hiso pesa zikatumika kwa kazi nydingine hayo Mabadiliko ya Katiba yakasimama ili tutatue hili tatizo kwa kura ya maoni yaani direct vote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie juu ya Sheria ya Mazingira. Imeonekana kwamba sheria hii imevunjwa sana na anayevunja sheria hii ni Serikali yenyeche hasa Watendaji wa Halmashauri au Manispaa hasa sehemu ya ardhi. Watu wengi na tena maghorofa mengi yamejengwa kando ya mito mjini na wananchi wanalima bustani kandokando ya mito hasa katika sehemu ya Mbulu ndio wanaofuatwa. Sasa tunashauri kwamba usimamizi ya NEMC hausaidii, NEMC iangaliwe upya ili wananchi waweze kutumikiwa sawasawa. Inaelekea inatumika rushwa kubwa katika kusimamia sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mji wa Arusha kuna hoteli kubwa zimejengwa mtoni lakini mwananchi wa kawaida akienda kulima bustani kidogo kandokando mwa mito ambayo hata haileti erosion yoyote yeye anakamatwa, hii si haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hiyohiyo mazingira yanaangaliwa kwamba katika kukata miti kwa ajili ya kuni au mkaa wanatumika Polisi. Sasa wakati wanapojenga hao wenyewe kujenga maghorofa mpaka 20 ama 23 hawa Polisi wako wapi? Inakuwaje mtu anauza mkaa au anachukua mkaa wake wa kutumia nyumbani kama gunia moja ama mbili anakimbizwa na bunduki na hao wengine wanaachwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashangaa kuona kwamba madini yanachimbwa hamna kibali chochote, Idara ya Madini na Mazingira hawana mawasiliano yoyote, wananchi wanadhirika kwa zebaki, wanyama wao nao pia wanadhirika na zebaki kwa sababu machimbo yanafanyika kwenye maeneo ambapo kuna maji wanayotumia kwa ajili ya kunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Serikali isimamie mazingira hayo hasa kipindi hiki ambacho gesi na mafuta imegundulika hapa Tanzania na kuna machimbo mengi ya aina hiyo na kuna kemikali nyingi zinatumika. Kama suala hili halitaangaliwa wananchi wengi watakufa, imefika mahali uranium inachimbwa sasa na hatujatayarisha mazingara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie sehemu ya matumizi ya mkaa. Mkaa na kuni ni nishati yetu lakini sasa unapokatazwa na nishati mbadala ilitegemewa kuwa ni umeme, umeme haupatikani, ilikuwa inategemewa labda ni solar au gesi, lakini bei ya vitu hivi ni ghali na wananchi wengi hawawezi kuvipata. Ama Serikali ipunguze bei katika eneo hilo na pili iongeze hela katika kuleta umeme kwa wananchi kwa kupitia REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba nizungumzie sasa juu ya mabadiliko ya hali ya nchi. Watabiri wetu wa hali ya hewa wametupunja sana kwa sababu sehemu nyingi zimekumbwa na mafuriko, hawakuwa wamejitayarisha, sehemu nyingi kulikuwa na kiangazi cha muda mrefu, sasa wananchi wamekosa mazao yao badala ya kufidiwa pesa wanaletewa chakula cha njaa kama kwamba hawa watu walikuwa ni wavivu kumbe watu walipatwa na majanga. Tunashauri Serikali sasa iweke mpango wa watu hawa kufidiwa kwa sababu mazao mengine sehemu nyingine watu hutumia kama chakula na sehemu nyingine wanatumia kama cash crop.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nimezungumzia matatizo ya Muungano kuhusu ile Joint Finance Committee...

(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sereweji ajiandae Mheshimiwa Masele.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Bismillah Rahman Rahim!* Namshukuru Mwenyezi Mungu kunifikisha leo hapa ili kuendelea na hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe pamoja na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia hotuba hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie huwa nashangazwa sana kwa sababu Kambi ya Upinzani kila wanapokaa hawayatoi mazuri na nashangazwa sana hasa na Wazanzibar hawayajui mazuri. Hakuna Mzanzibar hata mmoja katika Kambi ya Upinzani anayeshukuru jambo kubwa saba ulimwenguni na jambo hili ndilo linalotuletea maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo gani basi? Ni umeme. Leo kila mmoja anasema kwamba Muungano hauna maana wakati umeme Zanzibar tunaupata Tanganyika, nasema kama wanavyosema. Kama si Tanganyika tungeshindwa kuchukua ma-generator kutoka Uingereza wala kokote, hayo hawayasemi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hawajaitaja BoT, jengo kubwa lililojengwa pale. Lingine hawajasema wale vijana wetu wanaondoka Zanzibar kwenda JKT, wanlishwa, wanavishwa, wanapewa mazoezi, hawayasemi! Kila wakikaa hapa wanalaumu tu, mnalaumu nini? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashangazwa sana Kambi ya Upinzani leo wamesema hivi kwamba wanaihurumia sana Zanzibar lakini 2013, 2014 Kambi ya Upinzani kwenye bajeti hii walisema kwamba Zanzibar ni Mkoa, Zanzibar inanyonya Tanzania Bara, Zanzibar wana bendera yao, leo Mheshimiwa Tundu Lissu kageuka anasema Tanganyika ndio inayowanyonya Zanzibar, anasema Tanganyika haitoi chochote. Yuleyle kabadilisha usemi leo, sasa tumsikilize nani?

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa wewe ni msomi, wewe ni Mwanasheria ambaye hutakiwi kusema uwongo kama hivyo. Wakati mwingine

sisi hutaka tuchangie tusijibu hoja lakini inabidi tujibu hoja hasa zile zinazopotosha wananchi wetu. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Yes!

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Nakuja kwenye sherehe ya Muungano. Sherehe hii ya Muungano uzinduzi ulifanyika Zanzibar kilele chake kikafanyika Dar-es-Salaam. Maana ya kilele ni kwamba mambo yote yanapelekwa kunakofanyika kilele.

**MBUNGE FULANI:** Naam!

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Viongozi wote wa Zanzibar wamekuja pale, viongozi wa Mikoa wamekwenda Dar-es-Salaam, viongozi wa nje wamepitia Nyerere Airport kuja kwenye kiwanja, sasa Zanzibar tupambe tunampambia nani? Kwa hiyo, mkisema hapa msipotoshe wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Sheikh Karume alisema hivi, mimi nitafariki waangalieni sana wasomi sio wote basi tunakuangalia sana. Kwenye Jeshi la Polisi, kwenye Jeshi la Ulinzi watu kama hawa mara kasema hivi ama vile, huwa tunawaita wa hivyohivyo na wewe sasa tutakuita wa hivyohivyo. (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine akasema kwamba Muungano huu kama utakwenda hivi, hatuulindi, hatuudumishi, wewe tunajua hulindi Muungano, hudumishi Muungano lakini wenyewe wapo hapa na majumbani kwetu na Majimboni kwetu, tutaulinda, tutauimarisha kama kawaida, potelea mbali! (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Mpe vidonge vyake.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri kuanzia sasa lolote ambalo litafanyika la Jamhuri ya Muungano ambalo linalopelekwa Zanzibar litangazwe na tena litangazwe humuhumu na hasa Kambi ya Upinzani wafahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nililogundua leo yeye kuiponda Tanganyika au Tanzania Bara na kuipendelea Zanzibar anawakosa wale Mawaziri wapya Kivuli na ndio maana akasema hivyo. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine akasema kwamba Afrika nzima hawajafanya Muungano kama huu, Afrika wamefanya Muungano, Senegal na Gambia walifanya Muungano lakini wakashindwa halafu Nyasaland na North Rhodesia wakafanya Muungano wakashindwa, sisi leo tumefika miaka 50 tuna Muungano bado tunalalamika? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niliingia kwenye boti ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili, ahsante.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Huvisa, ajiandae Mheshimiwa Masele!

**MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu kwa kunipa wadhifa wa Uwaziri kwa miaka mitatu nikishughulikia mazingira. Pia nimpe shukrani zangu za dhati Mheshimiwa Samia pamoja na Katibu Mkuu Mheshimiwa Salula kwa kunipa ushirikiano wa pekee na wafanyakazi wote wa ofisi ya Makamu wa Rais, bado nipo na nyie na nipo tayari kushirikiana na nanyi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niunge mkono hoja hii lakini pia Bunge hili linitambue kama ni mtaalam wa kidunia wa mazingira na haya ninayoyasema ninasema kwa uhakika mkubwa kwamba bila mazingira hakuna maendeleo, bajeti yote tunayoifanya ni kazi bure. Naomba sana, Serikali, Waziri wa Fedha uzingatie bajeti ya Mazingira. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano wa nchi moja Afghanistan. Miaka ya nyuma ilikuwa tajiri sana ikapuuzia mazingira sasa hivi ni maskini sana. Hakuna maendeleo endelevu bila mazingira. Naomba sana huu mchezo wa kuchezea bajeti ya Mazingira kuweka kiduchu, ninaomba tujirekebishe, tuongeze bajeti ya Idara ya Mazingira. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea na mchezo huu, tusitegemee chochote, ila tutegemee mafuriko makubwa, barabara zote kusombwa, nyumba kubomoka, vifo zaidi, maradhi kama Dengue haya yatakuwa mengi sana, mapambano kati ya wakulima na wafugaji yataendelea kwa sababu malisho hayatakuwepo, sehemu za kilimo hazitakuwepo, visiwa vitazama sana,

majanga kama njaa kubwa na mambo makubwa kama hayo, hayo ndiyo tutegemee. Ripoti ya mwaka jana ya Wataalam, Wanasyansi wa Kidunia iliyotolewa kwenye Mkutano Mkuu wa Climate Change wa 19, ilisema kwamba tumebakiza miaka 30 na kama hatutajirekebisha kwa muda wa miaka 30, majanga yatakayotokea hatutaweza kuyabadilisha. Kwa hiyo, tutegemee haya mafuriko ya sasa hivi ni rasharasha yatakuja makubwa zaidi, kwa hiyo, hakuna maendeleo kwenye mazingira mabovu. Kwa hiyo, Waziri wa Fedha, naomba mpandishe ceiling ya mazingira ili tuweze kuishi otherwise tungojee maafa makubwa na majanga makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalotaka kuzungumzia ni hifadhi ya mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa. Bajeti ya mwaka jana ilizungumzia kwamba kuna fedha zimetengwa na bonde hili muda wowote, matatizo ya mpaka yakiisha mradi huu unaweza ukatekelezwa. Sasa naomba Waziri unapokuja kujibu hoja, uniambie ni lini mradi huu wa kuhifadhi bonde la Ziwa Nyasa utaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni la usafi. Kwa kweli ni kitu cha fedheha kuona miji yetu mi michafu. Suala la usafi ni tabia. Mimi naomba Wabunge tushirikiane tuhakikishe miji yetu ni misafi lakini Waziri naomba uweke msisitizo na kuweka mpango mzuri wa kuhakikisha Halmashauri kwa sababu suala la utekelezaji wa usafi wa mazingira lipo chini ya TAMISEMI basi ninaomba TAMISEMI ingawa hawajasema sana katika bajeti yao lakini ninaomba sana suala hili tulizingatia na miji yetu iwe misafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ni upandaji wa miti. Mimi nashangaa kila mwaka bajeti ya ofisi ya Makamu wa Rais inasema miti iliyopandwa katika kila Mkoa lakini ukienda kwenye Mikoa, msitu huu tangu mwaka 2006 hauonekani popote, ni jambo la kushangaza. Mimi naomba tuweke mkakati mashuhuri wa kuhakikisha hii miti inapandwa lakini tukague huo msitu uko wapi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa zaidi ambalo mwenzangu mmoja ameligusia ni suala la zebaki (*mercury*). Mwaka jana nilienda kwenye mkutano Japan, mercury ina athari kubwa kwa sababu niliwaona wananchi wa Japan walioathirika na mercury inayoitwa Minamata, ile sehemu ni Minamata lakini ugonjwa huu sasa unaitwa Minamata disease. Ni ugonjwa wa ajabu amba unabadilisha ubongo, watu wanakuwa na utindio wa ubongo, mifupa inakunjika, ni kitu cha ajabu, wale mavu ni wengi, nilisikitika nikasema Tanzania tutakuwa na wale mavu wangapi? Kwa hiyo, mimi naomba wataalam wa NEMC muanze kupima nywele za watu kwenye sehemu zenye migodi ya dhahabu tuone mercury imeingia kichwani kiasi gani na tuangalie chemical mbadala ambayo haina athari kubwa. (Makofij)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni msitu wa Kazimzumbwi. Msitu ule uliwekwa kwa makusudi kunyonya hewa ukaa ya Dar-es-Salaam, Mkoa wa Pwani na maeneo mengine. Cha kushangaza ule msitu umeshaingiliwa na hili linajulikana kabisa na Wizara ya Ardhi ilitoa kibali cha kuingilia ule msitu. Tatizo hili limeshazungumzwa na amri ilishatolewa watu wale waondolewe lakini wale watu sijui wanalindwa vipi bado wapo pale. Kijiji chao wameweka kabisa kibao kinaitwa Kijiji cha Nsanza na wamepandisha na bendera...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Huvisa. Sasa tunakuomba basi wewe ni Mtaalam kama mercury utapima kwa watu wenye nywele na wasiokuwa na nywele watafutie namna. Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Maida ajiandae! (Kicheko)

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu baadhi ya hoja zilizotolewa na wawasilishaji hasa kutoka upande wa Upinzani hasa walipokuwa wakizungumzia rehabilitation...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Jamani tunaomba uvumilivu. Vumilieni wenzenu walivumilia asubuhi.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendeshaji wa migodi zipo sheria ambazo zinasimamia uendeshaji wa migodi lakini pia kuna sera ambayo inaongoza Wizara katika kuendesha na kusimamia shughuli za migodi. Katika eneo hili la mazingira hasa migodi inapofika mwisho na kufungwa, sheria ipo wazi kwamba inaundwa Kamati ambayo inasimamia kwa kushirikiana na Halmashauruuuri utaratibu wa kufunga mgodi ambayo inaitwa *Mining Closure Committee* ambayo Mwenyekiti wake ni *Chief Inspector of Mining* ambacho ni kitengo kipo katika Wizara kwa ajili ya ukaguzi wa kila siku wa shughuli za migodi ambazo zinaendelea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa Mgodi wa Tulawaka ambapo kuna hoja ilitolewa, Mgodi huu haujafungwa na fedha ambazo ziliikuwa zimetengwa kwa ajili ya rehabilitation zipo zaidi ya dola za Marekani milioni 19 zimelipwa kwa STAMICO ambaye ndiye amechukua jukumu la kusimamia ufungaji wa mgodi huo pale atakapomaliza kuchimba dhahabu iliyobakia. Wastani wa dhahabu ambayo ipo Tulawaka ni zaidi ya wakii laki moja ambayo inaweza kuchimbwa kwa miaka isiyopungua mitano. Hivyo, STAMICO

itaendeleza mgodi ule kwa kuchimba na itakapokamilisha fedha zile zilizotengwa kwa ajili ya *rehabilitation* ambazo ni dola milioni 19 zilizolipwa na Barrick zitafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgodi wa *Resolute Nzega*, mgodi ule umeshafungwa na umekabidhiwa Chuo cha Madini cha Dodoma ili kuendeleza ufundishaji wa vijana wetu. Kazi ya *rehabilitation* inaendelea na hivi tunavyoongea mimi nimetembelea pale, mashimo yale yaliyokuwa yamechimbwa tayari wameshafanya recap, wamechukua udongo ule uliokuwa umewekwa pemberi wamefukia na wahaendelea kufukia mpaka mwezi wa kumi na mbili mwaka huu watakapotukabidhi. Zoezi hilo linasimamiwa vizuri na Kamati hii na Serikali inakagua mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *North Mara* kulikuwa na kelele muda mrefu. NEMC imefanya uchunguzi na ikathibitisha kwamba kero zile zilizokuwa zinazungumzwa zote zimedhibitiwa kitalaam na hivi sasa kila kitu kinasimamiwa kwa utalaam chini ya NEMC, wanakagua mara kwa mara na hatujapokea ripoti mpya inayoonesha kwamba kuna uvujaji wa kemikali kwenye mto Mara. Endapo tutapata taarifa nyingine mpya, mimi nimetoka juzi kule na nimeongea na Halmashauri hawakukiri kwenye kikao kile kama kuna uvujaji wa kemikali mto Mara. Serikali iko makini na tunakagua kila siku kama itatokea hivyo tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba hakuna athari za kimazingira zinatokea kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya nishati mbadala, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini tunao mpango ambao tumeshauanza baina yetu Serikali ya Tanzania na Algeria ambao wana uzoefu wa muda mrefu wa kutengeneza mitungi ya gesi ya kupikia na tayari Kamati ile ambayo iliundwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini inafanya kazi, wanafanya feasibility study na watakapokamilisha tutaanza rasmi mradi wa kutengeneza mitungi ya kupikia ambayo itakuwa ni suluhu kwa misitu yetu, itakuwa ni suluhu kwa wananchi wetu ambapo mitungi ile itaweza kutoa gesi kwa bei nafuu kuliko gesi hii ambayo tunapokea kutoka nje. Kazi hiyo inafanyika, inaendelea chini ya Wizara ya Nishati na Madini na muda siyo mrefu watakamilisha ripoti hiyo na kuanza utekelezaji wa kufunga viwanda ambavyo vitazalisha mitungi ya gesi ya kupikia. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye gesi asilia hasa kule baharini, tuna miradi mikubwa sana ya gesi ambayo inahitaji ulinzi wa pamoja baina yetu na Zanzibar. Nasisitiza kwamba bado Muungano wetu ni muhimu kwa ulinzi wa miradi yetu ambayo ipo baharini. Tanzania Bara na Tanzania Visiwani kwa pamoja tunapaswa kushirikiana kuhakikisha kwamba tunaimarisha ulinzi katika bahari kuu ili miradi hii mikubwa ambayo nchi yetu imewekeza iweze kuwa katika hali ya usalama. Katika Muungano wetu naona watu wanaongelea tu

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

nani anapata nini, nani anapata nini. Mheshimiwa Sereweji ameongea vizuri sana hapa, mimi Wizara ya Nishati na Madini, Zanzibar kuna deni la umeme la zaidi ya bilioni 30 lakini kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na tunafanya kazi kwa kushirikiana kwa maana ya *win win*, tunaendelea kulipana polepole na TANESCO haijaweza kukata umeme Zanzibar lakini tungkuwa tunahesabu kila kitu Bara na Visiwani ni nani anapata zaidi, nina hakika hapa tusingweza kukaa kuzungumzia Muungano. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge Muungano wetu huu tuutizame kwa maslahi mapana zaidi ya nchi yetu lakini tukiutizama kwa jambo moja tu kwamba wewe unapata nini na mimi ninapata nini, ukiangalia Zanzibar inategemea sehemu kubwa Tanganyika na Tanganyika inategemea sehemu kubwa Zanzibar hasa kwenye masuala ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu aliyejikuwa anazungumzia kwamba Tanzania haijawahi kutoa Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Diria alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Maida Hamad.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu katika kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushirikiane katika kuipitisha bajeti hii ili ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwanza kwa kupunguza angalau kidogo utegemezi katika bajeti hii. Mara nyingi tumekuwa tukisema Tanzania tumekuwa na utegemezi mkubwa wa bajeti kutoka nje lakini mara hii angalau. Ukiangalia ofisi hii imepunguza kwa kiwango angalau kidogo utegemezi, ukiangalia fedha za ndani ni nyingi zaidi kuliko zile za nje. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hapa Mheshimiwa Tundu Lissu Kaka yangu anaturudisha kwenye Bunge Maalum la Katiba. Mheshimiwa Tundu Lissu, Waheshimiwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, upande wa Tanzania Bara na upande wa Zanzibar, msiyumbishwe, wala msipotoshwe.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Muungano huu siyo kiini macho, Muungano huu ni sahihi, Muungano huu ni halali na uliwekwa sahihi na viongozi wetu wawili na picha zipo, mikutano ipo, hivyo tusipotoshe wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote katika pande hizi za Muungano tunafahamu kwamba kuna changamoto lakini wenzetu mlitoka tutazitatuaje changamoto. Kwenye Bunge Maalum la Katiba mlitoka, kuna kifungu 109 mpaka 112 ambayo ni Tume ya SMT na SMZ zikae pamoja, chombo hiki tukiunde Kikatiba ili tuweze kutatua changamoto hizi, mmetoka! Mnakwenda kutunga Katiba kwenye mikutano ya hadhara Kibanda Maiti sijui Pemba wapi, jamani tukae kwenye Bunge la Katiba tutunge Katiba. Wananchi hawana shida na muundo, muundo wanaukubali, wanauridhia lakini changamoto zilizopo zinawakwaza. Tukae pamoja kwenye Bunge la Katiba tutunge Katiba na kuondoa changamoto zilizopo. Wenzetu wasipotoshe wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nathubutu kusema kwamba Muungano huu ni halali. Katika hatua mbalimbali za kuangalia historia ya Muungano huu kwanza kuweka saini makubaliano ya Muungano mwaka 1964, kupitishwa rasmi katika Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi, Hati ya Makubaliano ya Muungano ilipitishwa rasmi Karimjee, kuchanganya udogo amesema Mzee Abeid Aman Karume hakuwepo, angalieni nyuma alikuwepo, picha ipo angalieni vizuri. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walioshiriki katika kuchanganya udongo ule kwanza ni mwananchi kutoka Zanzibar na mwananchi kutoka Tanzania Bara na wale waliokamata chungu ni Tanzania Bara na Zanzibar. Baada ya kuchanganywa udongo ule kulifanywa sherehe rasmi ambapo mgeni rasmi alikuwa Mwalimu Nyerere na Mzee Abeid Karume siku hiyohiyo. Walikuwa ni wageni rasmi na kuhudhuriwa na wananchi mbalimbali kutoka pande zote za Muungano. Muungano huu siyo sahihi kweli? Hapana! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eti Muungano huu haujulikani kimataifa, hivi sisi ni nchi gani? Kwa sababu kimataifa tunajulikana kama *The United Republic of Tanzania*, kwa hiyo ni nchi gani tupeni jina basi, msipotoshe wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, nimesema mwanzo na sasa hivi naendelea kusema, kama ikiwa kuna madeni, kama ikiwa kuna malimbikizo, kama ikiwa kuna kitu gani Tume ile tukiunda kwa mujibu wa Katiba ambayo ndiyo iko kwenye Rasimu sasa hivi, tukiunda ndipo tutakapojuwa madeni ni kiasi gani, kilichopo ni kiasi gani lakini leo eti tunakuja kusema madeni uko nje, utatuaje? Halafu anasimama mtu anasema hapa tuanzishe sheria, Katiba hatujaimaliza tuje kwenye sheria? Katiba hatujaimaliza tuje kwenye sheria, hatukubali, hatukubali, hatubali. (Makofi)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waride ajiandae Mheshimiwa Chomboh.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya na uzima lakini pia napenda kuunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza nchi yangu ya Tanzania kwa kuweza kutimiza miaka hamsini ya Muungano. Muungano ulioleta amani, Muungano ulioleta utulivu, Muungano ulioleta mshikamano na Muungano wetu ndiyo Utanzania wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza Balozi wa Zanzibar, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Ndugu yangu Tundu Lissu jinsi gani alivyokuwa anauteea Muungano kwa kuukandamiza, alivyokuwa anauteea Muungano kwa kuupinga lakini tunamjua yeye ni mpinga mapinduzi na mpinga Muungano pamoja na hao anaowawakilisha huko Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema sasa hivi anawapenda Wazanzibar lakini mengi yameshasemwa. Mimi nilikuwa nataka kusema nimekuja kuchangia bajeti kwa sababu haya yote aliyokuwa anayasema alikuwa kama santuri mbovu, kwa sababu alikwishayasema wakati akichangia Bunge la Katiba ndiyo yale yale kabadilisha huku na huku. Kwa hivyo, kama mnaijua santuri mbovu ndivyo alivyokuwa Mheshimiwa Tundu Lissu leo asubuhi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza ofisi ya Makamu wa Rais kwa kumaliza yale mambo tuliyokuwa tunayaita mambo ya kushughulikia kero za Muungano, isipokuwa kuna dosari ambazo zimejitokeza za utekelezaji. Tunaomba zile taasisi zinazohusika hasa katika mambo ya fedha, zile dosari ambazo zinajitokeza waweze kuzitatua ili hizi zinazoitwa kero za Muungano ziweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Muungano amalizie lile jengo la Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa sababu sasa hivi Makamu wa Rais anafanya kazi ikulu. Naomba amalizie lile jengo lake analogjenga pale ili aweze kufanya kazi zake kwa umakini hata wao wenywewe Mawaziri, watendaji wake wote aweze kuwaita pale aweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kuunga mkono Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu jengo la Zanzibar. Mimi mwenywewe nilikuwa shahidi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

nimekwenda katika jengo lile, jengo limejengwa ukiliona kwa nje ni zuri sana linavutia, lakini kwa ndani lina nyufa kubwa linaonekana kabisa limejengwa chini ya kiwango, hata mbao zilizotumika sijui ni za rangi ya brown au nyeusi, hatujui hata yule mkandarasi alitumia mbao za aina gani. Tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri umuite mkandarasi na msahauri wake, walirejee lile jengo kwa kulifanya marekebisho kwa pesa zao wenyewe. Tunaamini wamepewa pesa nydingi za kujenga jengo lile. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana uingilie ujenzi wa jengo la tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kule Zanzibar tunaita Marine Science. Jengo lile kwa kweli ni la Muungano wenzetu wa Dar es Salaam wameamua kutujengea tawi kule Zanzibar, kila siku katika bajeti ya Wizara ya Elimu tunaambiwa zinaingizwa pesa lakini hawapewi wala haliendelezwi. Kama Waziri wa Muungano, tunaomba uingilie katika jengo lile liweze kujengwa na kumalizika. Wale wenzetu Wahadhiri, wanafunzi na Watafiti wanafanya kazi katika mazingira magumu. Wapo pale bandarini Zanzibar, boti, wavuvi, wachukuzi wote wanasababisha kelele katika taasisi yao wanashindwa kufanya kazi vizuri. Inaonekana Wizara ya Elimu ya Juu labda imeshindwa nakuomba Waziri ile ni ya Muungano ingilia waweze na wao kumaliza lile jengo lao waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie kwa kuwapongeza sana TBC kwa kuweza kuelimisha na kurusha vipindi vyao vizuri wakati wa kuadhimisha miaka hamsini. Kwa kweli wamefanya kazi ya kijasiri, tunawapongeza. Wasiowapongeza tunawajua ndiyo kawaida yao hawawezi kupongeza kitu kizuri wakati walikuwa wanaona na kila mwananchi ameelewa nini kilichofanyika katika Muungano kwa miaka hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba pia Waziri wa Mazingira na ye ye afanye jitihada kama alivyofanya Waziri mwenzake aende Zanzibar akaonane na wenziwe waweze kujenga mahusiano na maelewano ya pamoja ili tuweze kudumisha mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Chomboh subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba ya kesho imebadilika kutakuwa na Wizara ya Ulinzi badala ya Wizara iliyopangwa na Wizara ya Ulinzi itakwisha saa moja na saa moja Wizara ya Maliasili watasoma taarifa yao na itajadiliwa kesho kutwa. Mheshimiwa Chomboh.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania utanzania wetu ni Muungano wetu, tuulinde, tuuimarishe na tuudumishe. Ni jambo la kawaida hata katika familia, ikitokea familia ina utajiri au ina maendeleo mazuri ambayo yamejengwa na wazazi au wazee waliopita, kutokea katika familia ile mmojawapo au wawili wakawa wakorofi sana wakataka pia kusambaratisha familia ile lakini kwa busara za wengine hujitahidi pia kulinda maslahi ya familia ile na mambo yakaenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanatokea katika Muungano wetu, Muungano wetu umeundwa na Wazee wetu, tumeurithi na watu wengine ambao walikuwa hawathamini kitu cha kurithi, wanafika hata kumtukana hata Mzee wake aliyemzaa. Tuliyaona hapa wakatukana Waasisi wa Muungano wetu hawakujali wala hawakubali waliona kwamba *bullshit*. Hicho ni kitu cha kawaida na wala mimi simshangai Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu hicho ni kitu ambacho yeye kwa bahati mbaya sana watu kama yeye wakipata wimbo fulani na ukiganda ndani ya kichwa chake basi atakuwa anauimba uleule tu. Akitaka kula wimbo huohuo, kila kitu wimbo huohuo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nyimbo ya Muungano hakuianza leo, aliianza toka alivyoingia Bungeni hapa, mara anageuza kule anageuza huku na atakwenda nayo mpaka mwaka kesho, atatukana, atausimanga Muungano, atausimanga Zanzibar na atasimanga Mapinduzi ya Zanzibar. Mara nyigi huwa anakuja na kutaka kueleza watu waliokufa lakini haijatokea hata siku moja akaeleza kilichomuua Karume, hata siku moja! Karume aliuwawa na wapinga Mapinduzi kama yeye na wenzake. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu kwa sababu Muungano huu bila ya Mapinduzi ya Zanzibar kusingekuwa na Muungano. Karume ndiyo Muasisi wa Mapinduzi yale lakini hajasimama hata siku moja akaeleza kilichomfanya Karume akafa, Mwanamapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hii sistaajabu, huyu mtu ni maumbile Mwenyezi Mungu aliyomjalia, kitu kaganda nacho kichwani hakitoki lakini mtu mwenye mwelekeo mzuri, lakini kuna ndugu zangu hawa nao, akisema maneno haya huwa wanashangilia sijui nao kama ni Lusu kama yeye, tuwaeleweje na wanajua maana ya Lusu ni nini lakini nao hushangilia, niwaeleweje ndugu zangu? Nataka kuwaambia ndugu zangu achene michepuko, sisi tuliwaamini ninyi kama ni wenzetu ndiyo maana tukaweka

Serikali ya Umoja wa Kitaifa, achene michepuko, rudini njia kuu, sisi ninyi ndio wenzetu. (Makofi)

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walismama wakitaka mwongozo wa Spika*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chomboh, subiri nitakuongezea dakika zako.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Lissu anatoa taarifa ya Kambi ya Upinzani kulikuwa na miongozo mingi sana nilizua, nilizua ili Mheshimiwa Lissu aseme yale aliyokuwa nayo na ya Kambi ya Upinzani.

**MBUNGE FULANI:** Hakutukana lakini.

**MWENYEKITI:** Kama hakuyasema hapa...

(*Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Wewe kaa chini mimi nikisimama! (Makofi)

Ili ajibiwe, kama asipoyasema hapa akiyasema nje kutakuwa hakuna majibu. Sasa vumilieni kama kuna matusi mimi ndiye nitakayeja siyo nyie. (Makofi)

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba dakika zangu uzilinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri ndugu zangu acheni michepuko, rudini njia kuu, ninyi sisi ni wenzetu, waliwasema sana hao kama mnakumbuka wakawatukana sana kwa sababu tuliungana na ninyi ndugu zetu kuweka maslahi ya Zanzibar, leo ninyi imekuwaje? Mmelaghaiwa kidogo mmechepuka, achaneni nao, michepuko siyo dili, njooni kwetu, rudini tukae tuzungumze maslahi ya Zanzibar na Muungano wetu wa Tanzania, achene michepuko sio deal, hao wanachokitaka ni kutugombanisha. Huyu Tundu Lissu kila siku ya Mungu kazi yake ni kutugombanisha. Wazanzibar, Wazanzibar na ni leo kajivika kilemba cha ukoka, kilemba cha ukoka kazi yake ni kubeba mzigo wa kuni tu, hamna lolote. (Makofi)

Ndugu zangu nakuambieni sana achaneni na hawa watu, sisi ndiyo wenzenu na sisi ndiyo tunaojijua, nakuambieni sisi ndiyo wenzenu, piga ua sisi ndiyo wenzenu na hapa tumekuja zetu ngomani, ngoma ikivunjika watakuja kushangilia, acheni michepuko, rudini njia kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makof)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walikuwa wakiongea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane. Sasa namwita Mheshimiwa Mwigulu. (Makof)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa uliyonipa. Nianze tu kwa kusema kwamba mimi nimesimama kuweka kumbukumbu sawa. Ni kwamba fedha ambazo Zanzibar wanastahili kupata miaka yote wamekuwa wakipata kama inavyostahili. Kinachowachanganya watu ni kimoja na nilishasema mara nydingi sana jambo kama hulijui ni vema sana ukaulizia ili ulijue. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinapokuja fedha za misaada kwanza wafadhili huwa wanatoa commitment, huwa wanaahidi, wanapoahidi tunaweza tukatenga hesabu ya 4.5 kutokana na ahadi lakini fedha watakazozipata zitatokana na fedha tutakazozipata. Kwa hiyo, utaratibu ni huo tu. Sasa kama hivi ambavyo ilikuwa inasomwa hapa kwamba ilitakiwa ipatikane bilioni 32 na hazikupatikana, fedha ambayo ilishapatikana tumetafuta uwiano wa 4.5 ya fedha tulizozipata ndiyo tukazipeleka Zanzibar. Mimi nadhani ni vizuri sana kuwa na utaratibu wa kuwapa Wabunge takwimu hizi ili wawe wanazijua kwa sababu wanawapotosha sana wananchi ambao hawana muda wa kupata takwimu za aina hii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mambo mengine pia niwashauri ndugu zangu wa Zanzibar kuweni na muda basi wa kuuliza hata kwa viongozi wenu, msiwe mnakuja kusemea hapa mambo yote. Mambo mengine yanawahusu nyie wenye. Mna Ofisi yenu ya Wizara ya Fedha kulekule, mambo yanayohusu uchumi ulizeni mjue kuliko kuja kupandikiza chuki hapa. Gharama ya kupandikiza chuki hizi ni kubwa mno. (Makof)

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niwaambie tu kwamba haya anayoyasema leo Lissu mnaweza mkadhania anawapenda kumbe hizi ni jitihada baada ya kuona chuki aliyokuwa anaipandikiza Tanzania Bara haijaweza kuwa na mashiko akaamua ahamie kwenu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Lissu alisema kero za Muungano si mali binafsi ya Wazanzibar. Nasoma Hansard ukurasa wa 113,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

alisema kero za Muungano si mali binafsi ya Wazanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pekee na anasema hata Watanganyika wanakerwa na ubaguzi unaendeshwa dhidi yao na Wanzibar huyuhuyu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anasema Watanzania Bara hawahawa ndiyo wanawanyanya wale kule kwamba ndiyo wanawanyonya. Amesema Wazanzibar wamependelewa huyuhuyu. Kwa kweli wakati mwininge huwa naona aibu kweli kwamba na Lissu naye katokea Singida kulekule nilikotokea. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii anakuja mtu yuleyule anasema Zanzibar imeibiwa kwa kipindi chote hiki na anasema huu ni ukoloni uliofanywa, unajua hata sisi kama Serikali nadhani tumezidi upole, mambo ya mtu anaweza akakosa adabu kwa mtu mwininge likavumilika lakini mtu anapokosa adabu dhidi ya Taifa lake, ni ukosefu wa adabu wa hali ya juu kabisakabisa. Hivi sasa leo hii ndugu yangu huyu anayesema Watanzania Bara wamewa-colonize Wazanzibar, wamewanyonya Wazanzibar, sasa limetokea la kutokea Wazanzibar wakabaki kule wewe Lissu utakwenda kule? Haya ni mambo ya ajabu kabisakabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwaombe Watanzania tusije tukaingia kwenye uchochezi wa aina hii. Kila jambo linaenda kwa hesabu zake. Sasa unaongelea tu kwamba Zanzibar inadai, Zanzibar inadai, hivi takwimu hizo kwanza wewe umezitoa wapi? Hivi unajua kwenye mchango wa kuanzisha Benki Kuu Tanzania Bara imechangia kiasi gani na Zanzibar imechangia kiasi gani? Hivi unajua Uwanja wa Ndege ule pale unaojengwa wa Zanzibar fedha za mikopo zilizokopwa kwa kofia ya Muungano na zinalipwa kwa kofia ya Muungano unajua ni kiasi gani? (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Sema!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):** Msiwe mnaropoka kwenye vitu ambavyo hamna taarifa zake, hili Taifa linatuhusu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Watanzania changamoto mara zote Taifa linapokuwa hai zinakuwepo palepale ndiyo maana tunahangaika kuzishughulikia. Mnahangaika na mambo yaliyopita, wenzenu tuliyi na dhamana tuliona tumeshapata fursa ya kutengeneza Katiba tuweze kuwa na jawabu la kudumu kwenye jambo hili. Tulishasema hivyo kwamba kama ni mkopo, kama ni misaada kila nchi ina GDP yake. Kwa hiyo, kila mmoja atapiga hesabu ana kiwango gani anachoweza kukopa, atakopa na atalipa deni. Wenzetu walipoona tunaanza kujadili mambo ya wananchi kwa sababu hawana hoja za wananchi wakatoka nje. Leo mnakuja kwa kisirisiri tena

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuturudisha kwenye mambo mengine ambayo sisi tulishapita. Hili si jambo la msingi.

Nyie wenzetu wa Zanzibar, mimi niwaambieni jambo la Muungano mnatakiwa muelewe vizuri sana tena sijui niseme Kiingereza, *you cannot eat the whole cake and have it*. Hauwezi ukawa na mamlaka kamili na ukawa na Muungano, hayaendi pamoja. Mnakuja hapa mnaongea halafu tukitangaza Bunge linakuja hapa mnakuja kwa furaha, sasa Mnyaa unakuja kufanya nini hapa? Kuna mambo mengine yasikitisha sana. (Makofii)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walikuwa wakiongea)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):** Nawaombeni nimalizie.

**MWENYEKITI:** Order please, order.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):** Nawaombeni nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba iliyotolewa na Waziri na Waziri atajibu, ina mambo ya msingi inayofafanua lakini ina mipango mizuri ambayo itasaidia kuondokana na mambo haya ambayo yamedumu kwa muda mrefu, ndiyo jambo la msingi lakini ukija unafanya jithada za kuwagombanisha Watanzania Bara unaona hizo hazishiki kasi, unahamia kwa Wazanzibar, mimi niwaambieni mnarudishiwa mpira na mnachotaka kufanya kwa kushangilia mnafunga kwenye nyavi zenu, muda ambapo mtashtukia yeye Lissu atakuwa Singida huku kule kwenu nyie mtabaki wenyewe. Ni vyema tukakaa mezani kwa fursa ambazo zinatolewa tukajadili mambo haya kwa sababu haya mnayoyasema nyie ni mambo ambayo hata hamjapata uhakika wake.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walikuwa wakiongea)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Sasa namwita mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Saada Mkuya, Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa naunga mkono hoja ambayo imewasilishwa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tu kwa kuendeleza nataka kutoa ufanuzi wa taarifa hii ambayo imetolewa hapa na naweza kukiri kwamba kuna mambo mengi sana yamechanganya bila kujua ukweli wake hasa ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna eneo ambalo Mheshimiwa Tundu Lissu aki-recall maelezo yangu ambayo nilikuwa nimeyatoa kupendekeza mfumo wa mapato na matumizi wa Serikali kwa mwaka 2014/2015 kwa Wabunge tarehe 30 Aprili. Alini-quote nikisema kwamba mapato halisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo nafuu ya nje, ilikuwa ni shilingi trilioni 1.16 Zanzibar yeye anavyoona ingepata asilimia 4.5 ya mapato hayo. Vilevile ana-quote kuhusiana na issue ya misaada na mikopo ya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka kuweka sawa. Misaada na mikopo nafuu ya nje (*concession loans*) ni tofauti na misaada na mikopo ya kibajeti. Hizi ni concept mbili tofauti.

**MBUNGE FULANI:** Hajui.

**WAZIRI WA FEDHA:** Sasa ukija kwenye misaada na mikopo nafuu (*concession loans*) na siyo misaada ni *concession loans*, Zanzibar inaweza ku-access yenye. Juzi tumesikia Waziri wa Fedha akitangaza bajeti ya bilioni 750 na *almost* asilimia 50 inatokana na vyanzo hivi ya nje, ni kwamba mle ndani mna misaada lakini vilevile mna mikopo ambayo Zanzibar imepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Sheria, Zanzibar inaweza ika-access misaada asilimia 100, misaada ile ambayo inakwenda kwenye projects na upande wa mikopo kinachotakiwa tu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kufanya ufanuzi kwenye Kamati yetu ya madeni ambayo Zanzibar pia kuna member wake pale akiwemo Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tunakuwepo wote pale, tunachanganua na once ikishakuwa cleared, the whole amount ambayo Zanzibar ilikuwa ikihitaji inapelekewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ni concept ya *concession loans* na haiingii kwenye asilimia 4.5, hapana! Kuna miradi chungu nzima ambayo imepitia utaratibu huo, mwenzangu Naibu Waziri ameshaeleza. EXIM Bank imepitia utaratibu huo, miradi ya barabara imepitia utaratibu huo lakini kwa upande wa grant kwa pamoja tulifanya miradi ya MCC ambapo barabara tano za Pemba tumefungua juzi pamoja na *underline cable* ambayo imetoka Dar es Saalam kwenda Zanzibar zote tumepitia utaratibu huo. Kwa hiyo, kwa upande wa misaada Zanzibar inaweza ika-access lakini kwa upande wa mikopo tunafanya kazi sote kwa pamoja. (Makofii)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Hapa TV za ukumbini ziligoma kuonesha picha)

**MBUNGE FULANI:** Angekuwa Tundu Lissu tungenesimama, endelea.  
(Kicheko)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye General Budget Support, upande wa General Budget Support kinachokwenda asilimia 4.5 kwa Zanzibar ni ile earmarked GBS yaani hizi concept kweli nadhani ushauri umetolewa Mheshimiwa Fakharia na wengine, tukae labda tuelezane kuliko kuwa tunatoa taarifa ambazo hazikufanyiwa uchunguzi. Kinachokwenda Zanzibar kwenye General Budget Support ni an earmarked grant yaani ni misaada ambayo haiko kisekta lakini vilevile an earmarked loans na mikopo ambayo haijamaanishwa kwenye kisekta yaani general tu inakwenda 4.5. Kuna sehemu mbili ambazo Zanzibar bado haziendi hadi leo, ni fedha ambazo zinatokana na European Union za road na mkopo ambao unatokana na sekta ya maji kutoka Japan lakini zote zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachogomba hapa pengine na ndiyo maana tunaweka basis ya taarifa zetu ni kwamba commitment ni tofauti na disbursement. Commitment akija donor akisema mimi mwaka huu natoa trilioni 1, haimaanishi ile ndiyo 4.5 ndiyo itakwenda Zanzibar. Mpaka leo hivi tunavyozungumza kuna baadhi ya donors hawajatoa pesa zao. Kuna wengine watatoa mwakani Julai. Kwa hiyo, ikiwa portion ya Zanzibar tunahakikisha kwamba tunaisimamia, tunaipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sielewi kwa nini inachukuliwa hivi kijumla jumla lakini pengine ni katika tu utaratibu mzima wa kisiasa kupotosha taarifa lakini taarifa zipo na tunazismamia. Ukweli wenyewe upo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukisema deni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maana yake ni pamoja na mikopo iliyochukuliwa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuna miradi chungu mzima pale. Kuna miradi ambayo tunadaiwa African Development Bank.

**MBUNGE FULANI:** Figure!

**WAZIRI WA FEDHA:** Figure ninazo siyo lazima, nikianza kuzitaja hapa mwezi mzima tunaweza kumaliza lakini mimi ndiye ninayedhamini. Zanzibar hawalipi, hakuna deni ambalo mpaka sasa Zanzibar imelipa. Hiyo ukiambiwa 27 trillion au deni la external ambalo linafikia around 24 trillion ni pamoja na mikopo ambayo imechukuliwa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Leo deni lile ambalo tunajenga airport kutokana na mkopo wa EXIM Bank amount yote imekwenda Zanzibar.

(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu maeneo mengi yamekumbwa na mafuriko. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani mafuriko ni mabaya sana na kusababisha watu wengi kupoteza mazao, mifugo, mali na hata nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba mvua za mwaka huu ni nyingi kuliko kawaida, lakini kuna sababu kubwa mbili ambazo zimefanya hali iwe mbaya zaidi. Sababu hizo ni ukataji holela wa miti lakini pili ni uchimbaji holela wa mchanga kwenye mito na vijito hivyo kuondoa kinga ya asili ya mito. Ukataji holela wa miti kwa ajili ya mkaa unaoendelea bila kizuizi chochote kiasi kwamba watu wanaendelea bila woga na kuacha nchi bila ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzuia hili lisiendelee ni lazima Serikali ifanye yafuatayo:-

(1) Kuwapatia watu nishati mbadala ya kupikia mijini na vijijini. Bei ya umeme ni kubwa sana kiasi watu wengi hawamudu (hata mijini) kutumia umeme kwa kupikia.

(2) Kuwe na mkakati na elimu ya kutosha na hata motisha kwa mtu kuruhusiwa kakata miti. Miti kama miarubaini inaota na kukua kwa haraka lakini pia inaota karibu kila mahali. Serikali ihamashe upandaji miti iwe ni siku moja kila mwezi ili kuongeza kwa kasi kubwa idadi ya miti. Zoezi hili lifanyike mijini na vijijini.

(3) Sheria za kuhifadhi miti irejewe upya ili hatua kali zichukuliwe kwa watu wanaokata miti hovyo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa mchanga imekuwa biashara kubwa sana hasa maeneo jirani na mijini kwa sababu ndiyo sehemu zenye ujenzi mwingi. Hata hivyo, sasa hivi machimbo mengi watu wamevamia kwenye mito na vijito sehemu wala hazijaandikishwa kwa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi viongozi tunapita Dumila lakini hakuna mtu anayesimama kuhoji ni kwa nini mchanga unachimbwa hapo. Daraja la

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Lugalo, daraja la Mlalakuwa, daraja karibu na mzunguko wa "White Sand", Vikawe kwenye mto Mpiji ambao unakwenda mpaka daraja la Mpiji. Matokeo yake aidha uchimbaji huo umebadilisha njia ya maji/mto hiyo lakini pia imeacha mito hiyo bila ya kinga yake ya kawaida, lakini pia imefanya udongo kuwa laini na hivyo kusombwa na maji kwa urahisi. Huu mchanga unaochimbwa kiholela unashuhudiwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Waheshimiwa Madiwani na pia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine pamoja na wachimbaji wa mkono, watu wamepeleka vyombo/machine za kuchimbia mchanga. Watu hao ni waharibifu lakini ni wabinafsi wasiojali maisha ya mtu mwingine au watoto wetu wa baadaye. Serikali imelala kabisa wakati hayo yakitendeka. Serikali ilete Muswada/Sheria Bungeni ili adhabu kwa wanaothibitika wachukuliwe hatua kali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itoe elimu ya kutosha kuhusu utunzaji wa mazingira.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nashauri mfumo unaofaa ni mfumo wa Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Tume ya Pamoja ya Fedha ni chombo muhimu sana na kina utalaam wa hali ya juu kuhusu masuala ya Muungano. Hivyo, nashauri chombo hiki kiendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini formula ya ku-share mapato ya Muungano itajulikana na formula hiyo inayotumika kwa sasa ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais itaanza lini kufanya kazi (Tunguu)? Wizara ya Muungano inapaswa kubuni kuongeza miradi ya maendeleo ili kuimarisha masuala ya Muungano (*joint projects*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mazingira katika Halmashauri zote nchini yaimarishwe. Katika taarifa za upandaji miti kitaifa mwaka 2012/2013, Mkoa wa Njombe haujaonesha taarifa ya upandaji miti katika Halmashauri ya Wilaya ya Wangingombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inapaswa kuweka mikakati ya kilimo cha Vinyungu ili kulinda vyanzo vya maji kama mto Ruaha and the little Ruaha. Somo la utunzaji wa mazingira linapaswa kufundishwa shulenii pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inapaswa kujua matumizi ya kuni nchini na kutafuta mbadala wa matumizi ya kuni. Kwa sasa Wizara ina mpango gani wa kupunguza ukataji miti ya kuni nchini?

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kwamba mazingira ni sekta mtambuka na ni muhimu sana kwa uhai wa wanadamu na viumbi vyote, namwomba Mheshimiwa Waziri/Serikali kutembelea Bonde la Eyasi – hasa uharibifu wa mazingira unaofanywa kwa makusudi na viongozi waandamizi wa CCM jambo ambalo ni hatari sana kwa maisha ya watu na viumbi vyote vinavyoishi katika bonde hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusikia toka Serikalini ni lini hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wote waliohusika na uharibifu huo? Hii ni baada ya juhudzi za Mkuu wa Wilaya ya Karatu kugonga mwamba. Chondechonde, Serikali iokoe Eyasi. Kinyume chake wananchi wamechoka na wachache wasiofuata sheria na kama Serikali haiwezi watuambie wananchi la kufanya.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira nchini bado sheria zilizowekwa hazifuatwi na hivyo kufanya mazingira mabovu kuchukua nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Pamoja na elimu kutolewa bado usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa uharibifu wa mazingira ni mkubwa. Mfano Serikali imeshindwa kuzuia uchimbaji holela wa mchanga wa ujenzi mbalimbali katika miji mfano Wilaya ya Mpanda, Kata ya Kawajense mitaa ya mji wa Kazima. Serikali imeshindwa kuzuia uchimbaji holela huo unaoharibu sura ya mji wa Mpanda kwa mashimo ambayo ni hatari kwa usalama na watoto vilevile kufukiwa kwa vifusi vya mashimo hayo. Sijui Serikali inachukuliaje hilo kwa kupiga marufuku uchimbaji holela wa mchanga katikati ya miji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna utupaji hovyo wa uchafu unaotolewa hospitali na kupelekwa kwenye madampo ya mji kama mabomba na sirinji za sindano za hospitali, pamba na gozi zilizotibu vidonda hospitalini na kusababisha watoto wanaozunguka majalalani kushika vitu kama hivyo. Naiomba Serikali iruhusu vitu kama hivyo kuchomwa moto kabisa ili watoto wazururaji majalalani wasiumie ni hatari pia kwa mazingira ya miji, haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke sheria kali kwa kuzuia uchomaji wa mkaa holela kwani sasa hivi kila pori zuri tayari wachoma mkaa wanavamia na kuchoma mkaa mpaka hata miti midogo ambayo bado inakua. Serikali basi itoe elimu kwa wachoma mkaa na kutenga maeneo ya kukata miti ya kuchoma makaa na siyo kama ilivyo sasa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tena Serikali iboreshe mazingira kwa kujenga barabara zenyе ubora na madaraja pia kwa uwiano wenyе ubora na imara ili kukabiliana na mvua kali zinazonyesha sasa na kuharibu miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa awamu ya tatu ya TASAF, ni kweli inasaidia kupunguza umaskini katika kaya maskini Tanzania Bara na Zanzibar. Hata hivyo, nashauri Serikali kupitia TASAF inapotoa mradi kwa kaya maskini ijaribu kurudi kukagua maendeleo na mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati ya UKIMWI ilifanya ziara katika Halmashauri ya Bagamoyo Kijiji cha Vigwaza, ilitembelea kaya maskini na kukagua miradi iliyotolewa na TASAF kwa wazee ambayo ni mradi wa ufugaji bata na kuku. Kamati iligundua kuwa tangu mradi uanzishwe, Bwana Mifugo hajawahi kuzungukia kuwapa ushauri wa namna ya ufugaji, huduma ya dawa, chanjo kwa kuku hawapati na hivyo kuku walikuwa wamekufa kwa kupata ugonjwa wa mdondo na fedha wanayopata kila mwezi Sh.7000/= ni ndogo. Ushauri wangu, naomba Serikali isimamie viongozi watembelee na kuona miradi inakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii kwa ufupi sana. Napenda kuchangia kuhusu uchafuzi wa mazingira na athari kwa afya za binadamu na mimea ikiwemo viumbe vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nitajikita katika Mgodi wa North Mara. Itakumbukwa katika Hansard za shughuli za Bunge kwa nyakati tofauti nimezungumzia juu ya mgodi wa Barrick kuendesha shughuli za uchimbaji bila kuwahamisha wananchi pamoja na shule. Shughuli ambazo zinapelekea wananchi wanaoishi maeneo yale kuathirika. Mfano mmojawapo ni shule ya Msingi Ngabisena ambayo Serikali pamoja na mgodi walihidi kuihamisha tangu 2012 hadi sasa. Watoto wale sio tu wanaathirika na vumbi linalotokana na vumbi la kifusi kinachomegwa kwenye pits baada ya kuchambua dhahabu bali huathirika pia na kelele za operation za mgodi kama vile baruti, magari makubwa, moshi na vinginevyo. Vilevile purukushani za Polisi na wananchi ambaeo hupelekea mirindimo ya risasi na mabomu ambapo mwaka juzi ziliweza kuwazuru watoto wa Chakechea ambapo waling'olewa meno, kutobolewa jicho. Swali hili nilimuuliza (swali la papo kwa papo) Waziri Mkuu akasema taarifa amezipata na kukiri kulifanyia kazi ikiwemo kuwahamisha/kuhamisha shule hiyo. Kimazingira uelewa wa watoto unapunguzwa si tu na kelele bali pia upofu utokanao na vumbi, kikohozi, uziwi na kadhalika. Naomba majibu ni kwa nini hii shule haijahamishwa hadi leo na mgodi unaendelea ku-operate. Mheshimiwa Huviza aliyekuwa Waziri wa Mazingira alikiri kutembelea eneo husika na kuahidi shule kuhamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni athari kwa wananchi kwenye makazi yao kwani vifusi hivi humwagwa kwenye makazi, hadi kwenye nyumba za hawa wananchi na vimeshasababisha vifo vya watoto na hata kijana. Je, Wizara inaruhusu vipi mgodi kuendesha shughuli bila kwanza kuwahamisha wakazi wote. Eneo hili lipo katika kijiji cha Nyakungano eneo la Kipimio na sehemu zingine za operation ambapo kuna nyumba za mama Metusera, Mzee Majwi, hii sio haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mashimo yanabaki, baada ya machimbo hayafukiwi wala kuzungushia uzio kitu ambacho hupelekea magonjwa na vifo kwa watoto kuzama na kufa. Aidha, kuna dawa zinapulizwa wakati wa alfajiri ambazo nimehoji inasemekana kuwadhuru wananchi wanaoishi ndani ya mgodi hasa eneo la utawala, *main camps* yao. Wananchi wanahoji zile dawa ni aina gani na hupulizwa kwa kusudio gani? Naomba majibu yanayojitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwepo na miundombinu imara ya mifereji hasa kwenye majiji. Majengo mengi yanajengwa hovyo hovyo na hasa majengo makubwa bila kuzingatia mfumo wa majitaka, hii ina-pollute miji na kuleta madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kelele za magari mabovu na *air pollution* kwenye magari na vyombo vingine vya moto ni athari kubwa zinazohitaji utatuzi wa haraka sana.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kulinda na kuhifadhi mazingira, Serikali itoe suluhisho la nishati mbadala kwa matumizi ya majumbani. Tukio la hivi karibuni Wilaya ya Nzega si la kibinadamu hata kidogo kutumia Jeshi la Polisi na silaha kupambana na wauza mkaa, ni lazima tujue nishati rahisi inayopatikana badala ya mkaa. Vinginevyo binadamu ili aishi anahitaji moto ataendelea kutafuta moto kwa namna yoyote ile ili aishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu, Wilaya ya Mpanda ina misitu mingi iliyohifadhiwa, tunanufaika na *carbon credit*, kama ndiyo ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa kujua suluhisho la wafugaji katika nchi hii ili kunusuru mazingira na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kufahamu jitihada zilizochukuliwa katika kulinda, kuhifadhi na kuendeleza uwepo wa Ziwa Rukwa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambalo linakauka kwa kasi kutokana na uharibifu wa mazingira na mapendekezo ya kunusuru Ziwa hili na uwepo wake.

**MHE. KOMBO HAMISI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja hii, ni vyema ikazingatiwa kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ni kiini kinachohusu pande mbili za Muungano. Hata hivyo, Wizara hii haikupewa nafasi stahiki katika uchangiwaji wake, kwani walioomba kuchangia Hotuba hii ni wengi lakini nafasi hazikutolewa kwa lengo lile na nia ileile ya kuzuia matatizo yanayowakabili Washirika wa Muungano huu yasisikike kwa Wananchi, kwani Wananchi wa pande zote mbili wakielewa hawatokubaliana na matakwa ya watawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayoukabili Muungano wa Tanganyika na Zanzibar si tu kwamba, yanachefua nafsi za Watanganyika na Zanzibar, bali umechukua nafasi kubwa ya kufanya Zanzibar kama si Nchi Washirika wa Muungano huu bali umeifanya Zanzibar kama koloni lake na siyo Mshirika wa Muungano. Kwa mfano:-

Kwanza, mfumo wa kupatikana na kwa Rais wa Zanzibar, Wazanzibari hawana maamuzi ya kuchagua Rais wao bila ya kutolewa maamuzi na Tanganyika.

Pili, kauli iliyotolewa na Waziri Mkuu juu ya Kauli aliyoitumia kusema kuwa Zanzibar si nchi ni uthibitisho tosha wa kuonesha kuwa Zanzibar ni Koloni la Watanganyika.

Tatu, kutofunguliwa kwa Akaunti ya Pamoja ya Mfuko wa Muungano ni kielelezo na uthibitisho tosha kwamba, Zanzibar ni Koloni la Watanganyika.

Nne, Kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Salmin Awadhi kwamba, Sera ya CCM ni Serikali Mbili kuelekea Moja, ni uthibitisho tosha kwamba, Tanganyika imekalia Zanzibar kama Koloni lake.

Tano, kauli ya kejeli na kebehi iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangalla katika Mkutano wa Bunge Maalum kusema kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni *Local Government* na hakutokea Kiongozi yeyote kukemea kauli hiyo, ni uthibitisho tosha kwamba Zanzibar ni Koloni la Tanganyika.

Sita, kauli iliyotolewa kanisani Machi, 2014 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu wa Bunge), akimwakilisha Waziri Mkuu kwamba, asilimia 95 ya Wazanzibari ni Waislam, tukiwaachia wataunda Serikali ya Kiislam; nani kamwambia hilo? Aliendelea kusema pia hawawezi kuiachia Zanzibar hata siku moja na endapo Mfumo wa Serikali Tatu utapita, Jeshi litachukua

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

madaraka, ni uthibitisho tosha kwamba Zanzibar ni Koloni la Tanganyika. Kauli ya udini ni kauli ya kuwafanya Watanganyika amba ni jamii ya Wakristu wawachukie Waislam siyo tu Wazanzibari lakini hata Watanganyika (Waislam walioko Tanganyika).

Saba, kauli iliyotolewa na Rais wa Jamhuri wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete wakati akihutubia Bunge Maalum juu ya kupinga Rasimu ambayo aliiweka saini yeye mwenyewe na kuthubutu kusema katika uhai wake Serikali Tatu haiwezekani na ikitokea Jeshi litachukua Serikali; ni kwa nini basi Tume ya Jaji Warioba ilitumia zaidi ya bilioni sabini wakati Serikali ilikuwa haikubaliani na maoni hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kuzuia Wajumbe wasipate nafasi ya kuchangia Wizara hii inayohusiana na mambo ya Muungano ni nia ileile ya kuwafumba macho Wazanzibari na Watanganyika wasijue kiini macho kinachoendelea ndani ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaosema na wanaodai kwamba, wanaotaka Serikali Tatu wana uchu wa madaraka, wanaodai mwendelezo wa Serikali Mbili wana uchu zaidi wa kulinda matakwa yao, waendelee kukaa madarakani, si uumini bali ni kulinda masilahi yao tu. Hivyo, hila na ghiliba wanazozitumia kuwalisha Wazanzibari na Watanganyika kwa muda wa miaka hamsini kwa masilahi yao sasa iwe basi na uchache wao kwa kuwatumia jamaa na ndugu zenu ambao wameshatoa kauli kwamba, wao wana asili ya Tanganyika na hao ndiyo ambao wana nafasi za Uongozi Zanzibar na kwa fursa hizo walizonazo ndiyo wanafanya kila njama na kila hila kila kuifuta Zanzibar katika Ramani ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna hila na njama ya kufuta baadhi ya Majimbo hasa Kiswani Pemba kwa nia na madhumuni ya kutafuta theluthi mbili ya Wajumbe wa BLW na Bunge kuwa na urahisi wa kuibadili Katiba ya Zanzibar na kufikia malengo ya kuibadili katiba ya Jamhuri ya Muungano ili malengo ya Watanganyika yakamilike dhidi ya Wazanzibari. Wazanzibari tulio Wanjanibari na ambao hatukuingizwa Zanzibar kwa malengo ya Watanganyika, mbinu zote na ghiliba zote kama alivyoshindwa Mwalimu J.K. Nyerere kufikia malengo yake dhidi ya Zanzibar na Wazanzibari, na mwingine yeyote hatofikia malengo; *Ishaallah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema, Tanganyika umefikia wakati sasa ivue koti la Muungano kwa masilahi ya Zanzibar na Wazanzibari kama hawataki hivyo, tugawanye mbao tubaki na ujirani mwema kama kabla ya kiini macho cha Muungano, uliobatizwa jina la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kumbe ni ile ile Tanganyika.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, mambo ya msingi ambayo ni kero katika Muungano huu bado yanafichwa. Hivi karibuni aliyekuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi 1964, alinukuliwa akisema Zanzibar haikuridhia Muungano huu bali kulitumika hila na ghiliba katika kuitawala Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea mwaka 1964 hadi leo 2014, hatujaelezwa ni Balozi ngapi ambazo zimewahi na zinaendelea kukaliwa na Wazanzibari na ni kigezo gani kilichotumika katika kupewa nafasi hizo. Vilevile Tanganyika ina Mabalozi wangapi na je, hicho ni kigezo cha uwepo wa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar? Kuna wafanyakazi wangapi kutoka Zanzibar ambaa wako katika Balozi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar inaidai Serikali ya Jamhuri fedha ambazo kama italipwa, itachukua miaka kumi na saba katika bajeti zake kuilipa Zanzibar. Hata hivyo, kwa kuwa Tanganyika imeikalia Zanzibar kama Koloni lake, haina wasiwasi wowote juu ya madai hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wazanzibari tumeshachoka na Muungano huu ambaa ni Jahanam kwa Wazanzibari na hauna faida wala tija, isipokuwa Ubunge tunaopata Wazanzibari. Kila Mbunge mmoja anaathiri maisha ya Wazanzibari 27,500. Kwa mantiki hii, hili haliwezekani, ni wakati wa kuufikiria upya Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize ndani ya kipindi cha miaka hamsini Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilikuwa haielewi kwamba inawatendea uovu Wazanzibari kuwakosesha fursa za kiuchumi kwa kuzuia kutumia fursa ya kutaka kufanya maombi ya misaada nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaodai kwamba, Wabunge wa NCCR na CUF sasa wameungana na CHADEMA kuna uovu gani walioufanya CHADEMA kwa NCCR na CUF kuliko mauaji yaliyofanywa na CCM katika Unguja na Pemba 1992 na 2001 na tumekubali kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na ambayo hadi sasa haiwaridhishi. Mwisho, namalizia kwa kusema, mdharau mwiba mguu huota tende, CCM mnatudharau Wazanzibari.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Bajeti ya Ofisi ya Makamu Rais (Mazingira), kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekua hakuna elimu kabisa kwa Wananchi juu ya kuweka mazingira safi. Mfano, wakati wa safari mbalimbali, abiria hasa wa barabarani wamekuwa na tabia ya kutupa taka hovyo hovyo njiani bila kujali wanaathiri mazingira na Wananchi wanaoishi eneo husika kwa kutupa taka hizo. Naomba Wizara yako iandae mkakati maalum wa kuielisha jamii juu ya utunzaji mazingira na hata kuweka matangazo katika vyombo vyaa usafiri vyaa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

abiria na hata katika vituo vya kusafiria. Hii itakuwa inakumbusha Wananchi juu ya kuweka mazingira safi na hatimaye itajenga tabia ya kuweka mazingira safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni tabia sugu katika nchi hii kwa baadhi ya watu kuendeleza ujenzi holela katika maeneo yanayozunguka maji, yaani Bahari, Mito, Maziwa na kadhalika. Wanaofanya hivyo wengi ni watu wenye uwezo mkubwa kifedha, which means ni rushwa zaidi inatumika katika kukiuka sheria hii ya kutokujenga umbali wa mita 60 kutoka katika vyanzo vya maji. Hili lipo zaidi katika Mkoa wa Arusha; kwa mfano, Hoteli ya Naura Spring Arusha, imejengwa ndani ya mto kabisa. Ujenzi ulipoanza walismamishwa kwa muda, lakini baada ya muda ujenzi ukaendelea na sasa ni Hoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hatua kali zichukuliwe kwa wote wanaokiuka sheria hii bila kujali ni nani anakaidi sheria hii, kwa sababu wanaopata shida ni Wananchi amba wamekuwa wakitegemea maji au viumbe vilivyo katika maji kufanikisha mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguliaji wa maji taka wakati mvua zinaponyesha limekuwa tatizo sugu na limekuwa likiangaliwa bila kukemewa. Hii hali inaumiza sana sana kwa kuwa uchafu huo umekuwa ukienda na kuzagaa katika mazingira ya Wananchi wanaoumia zaidi ni watoto wadogo amba hawaelewi tofauti ya uchafu, kwa sababu wana tabia ya kuokota kila kitu wanachokiona mbele yao na kuweka mdomoni. Napendekeza hatua kali zichukuliwe na hili litafanikiwa zaidi kama Halmashauri zetu zitashirikishwa kwa kina, kwa sababu mambo haya yanafanyika katika mitaa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwakilisha.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitoe shukrani zangu kwa kuniwezesha nami kutoa mchango wangu wa maandishi kwenye Hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayepinga kwamba Muungano ni jambo jema, isipokuwa cha msingi na cha kuzingatia ni vipi Muungano huo unaendeshwa kwa pande mbili zilizoungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri yapo malalamiko mengi ya upande mmoja kati ya pande hizo mbili zilizoungana. Ni kweli kwamba, Muungano wetu huu umefikia umri wa nusu karne (miaka 50).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikie wakati sasa wa kuzimaliza kero za Muungano wetu ambazo ndiyo msingi wa malalamiko ya upande mmoja amba ni upande wa Zanzibar.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, vikao vimekuwa vikifanyika na kutoa maamuzi ya kero hizo, lakini kwa bahati mbaya maamuzi hayo ambayo yanakuwa yakifanyika yamekuwa yakibakia kwenye maandishi tu. Kubakia kwenye maandishi kwa maamuzi hayo bila ya kufanyika au kuonekana kwa vitendo, hakusaidii kitu isipokuwa kunaendeleza manung'uniko ya jambo ambalo tayari limefikiwa maamuzi bila ya usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati umefika ambapo Taifa letu limo katika kutunga Katiba mpya, kero za Muungano pamoja na manung'uniko ya kila siku ya upande wa Zanzibar yapate suluhi na sasa tuimbe wimbo mmoja wa maendeleo badala ya kuimba wimbo wa kero za Muungano, jambo ambalo ikiwa ipo nia njema linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwenye Hotuba yake, kampeni ya upandaji miti milioni 1.5 kwa mwaka kwa kila Halmashauri ya Wilaya, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014. Vilevile amesema Ofisi yake imepokea taarifa za Mikoa 20 kuhusu miti iliyopandwa na kumea Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kwa uwazi kati ya Halmashauri na Mikoa 20 alioitaja ni Halmashauri gani na Mikoa gani ya Zanzibar iliyohusika na zoezi hilo la upandaji wa miti? Naomba aitaje na kama hakuna Halmashauri yoyote au Mkoa wowote, nitamtaka aeleze sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku Wizara imekuwa ikizungumzia suala hili bila mafanikio. Naomba niseme kuhusu suala la udhibiti wa mifuko ya plastiki kwa Tanzania Bara limeshindikana. Nasema hivyo kwa sababu nina uzoefu wa suala hili kule Zanzibar. Suala hili lilijitokeza kule Zanzibar na lilidhibitiwa. Suala hili la udhibiti wa mifuko ya plastiki yalijitokeza malalamiko mengi, lakini kwa sababu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikusudia kuondoa jambo hili liliwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa Zanzibar hakuna kiwanda, kampuni au maduka ambayo unaweza kuona mifuko ya plastiki inauzwa. Cha kusikitisha, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara hii kwa upande wa Tanzania Bara hadi leo inazungumzia jambo hili bila mafanikio na cha ajabu viwo viwanda, makampuni na hata maduka yanauzu mifuko hii. Vipi leo na kila siku Wizara imekuwa ikiimba wimbo wa kudhibiti mifuko wakati hakuna nia njema na jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Wizara isiige mfano kutoka Zanzibar? Nafahamu hali halisi ilivyo Zanzibar kuhusu jambo hili kwa nini Wizara au Serikali isichukue maamuzi magumu juu ya jambo hili?

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamwomba Mheshimiwa Waziri aniambie Serikali ina masilahi gani na biashara ya mifuko ya plastiki?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi kwenye fukwe za bahari limekuwa ni tatizo kubwa hasa katika Jiji letu la Dar es Salaam, pamoja na wenye kujenga nyumba hizo siamini hawajui sheria sababu wengi ni vigogo. Pamekuwepo na malalamiko mengi, lakini mpaka leo hii hakuna hatua zilizochukuliwa kwa nyumba hizo zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fukwe nyingi hazitunzwi, kwa mfano, Coco Beach kuna nguzo zilizojengwa ili kuzuia magari kuengeshwa huku ikiwa ni pamoja na kuuzia vyakula kule na kutupa uchafu. Baadhi ya nguzo zile zimeng'olewa, magari yameegeshwa. Serikali ina mikakati gani na Ukanda huo wa Bahari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi vijiji, kwa mfano, Moshi, Mto Rau, wakulima wamekuwa wakifanya shughuli za kilimo kando kando ya mito na kusababisha mmomonyoko; ni jukumu la Serikali kuwapa Wananchi hawa elimu na madhara yake. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha wale wote waliojenga kwenye fukwe ndani ya mita 60, wanabomoa nyumba zote. Bila kufanya hivyo, watu wengine wataendelea kujenga na mazingira yatazidi kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu karibu zote Duniani kwa sasa mifuko ya plastiki hairuhusiwi kwa sababu wanaharibu mazingira kwa uchafu, inaharibu ardhi, ikichomwa ni sumu na mifugo ikimeza mifuko hiyo hufariki. Kama Zanzibar wameweza kupiga marufuku mifuko ya plastiki wanashindwaje Tanganyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itoe Waraka wa kuvigiza viwanda vyote vyenye kutengeneza mifuko ya plastiki wabadilishe mashine hizo na watengeneze mifuko ya karatasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji letu la Dar es Salaam limekithiri kwa uchafu wa mazingira, baadhi ya magari yanayozoa taka ngumu badala ya kutunza mazingira ndiyo yanayochangia kuharibu mazingira. Magari haya yapo wazi, yanadondosha uchafu njiani na kupelekea baadhi ya sehemu kutoa harufu mbaya. Baadhi ya mifereji ya maji machafu ipo wazi na hata kufanya mifereji ile jalala. Njia za kupeleka taka ngumu ni mbovu kupelekea magari kushindwa kupeleka taka ngumu na taka nyingi kurundikana ovyo mijini, ambako ndiyo kioo cha nchi yetu; hii ni aibu!

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha Jiji letu linakuwa safi kama ilivyo Manispaa ya Moshi chini ya Uongozi wa CHADEMA inavyofanya vizuri na kuwa mahali pa Halmashauri nyingine kuja kujifunzia?

**MHE. DKT. HAJI HUSSEIN MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa RAMSA katika bonde la Mto Kilombero limekuwa kubwa sana kuliko matumizi yake ambayo yamelenga kulinda Mto Kilombero na ardhi oevu. kutoptaka na ukubwa huo, kumesababisha migongano ya mara kwa mara baina ya wananchi wa vijiji jirani na uongozi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marejeo ya Sheria ya Wanyamapori (2009) Serikali ilipewa kazi ya kurejea upya mipaka ya mradi huo wa RAMSA (Kilombero) lakini hadi leo kazi hiyo haijatekelezwa. Ili kuondoa unyanyasaji unaofanywa kwa wananchi ambao wapo kihalali katika baadhi ya vijiji, nashauri mipaka hiyo irekebishwe haraka kama ilivyoelekezwa na Bunge katika mapitio/marekebisheso ya Sheria ya Wanyamapori (2009).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na maoni ya Kamati ya Bunge (Ardhi, Maliasili na Mazingira) kutekeleza uzuiji wa utengenezaji na matumizi ya mifuko ya plastic ya kubebaa bidhaa (mifuko ya rambo) ili kupunguza hali mbaya ya kuzagaa kwa taka ngumu katika maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SAID ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kulinda na kuhifadhi mazingira, Serikali itoe suluhisho la nishati mbadala kwa matumizi ya majumbani. Tukio la hivi karibuni Wilaya ya Nzega siyo la kibinadamu hata kidogo! Kutumia Jeshi la Polisi na silaha kupambana na wauza mkaa, ni lazima tujue nishati rahisi inayopatikana badala ya mkaa. Vinginevyo, binadamu ili aishi anahitaji moto, ateendelea kutafuta moto kwa namna yoyote ile ili aishi.

Ningependa kufahamu, Wilaya ya Mpanda ina misitu mingi iliyohifadhiwa, tunanufaika na Carbon Credit kama ndiyo ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa kujua suluhisho la wafugaji katika nchi hii ili kunusuru mazingira na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jitihada zilizochukuliwa katika kulinda kuhifadhi na kuendeleza uwepo wa Ziwa Rukwa ambalo linakauka kwa kasi kutoptaka na uharibifu wa mazingira na mapendekezo ya kunusuru Ziwa hili na uwepo wake.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono na kuupongeza Muungano wetu wenye muundo wa Serikali mbili ambao sasa umefikia miaka 50 ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu wenye muundo wa Serikali mbili umetuletea umoja, ushirikiano, amani, ulinzi na usikivu katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muungano wowote ule lazima changamoto zitakuwepo. Kwa hiyo, changamoto (ker) za Muungano wetu zisiwe ndiyo sababu ya kuuvunja Muungano wetu uliodumu kwa kipindi cha miaka 50 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, mbali na kutafuta kero za Muungano zilizotambuliwa, lakini bado kero zipo. Kwa hiyo, suluhisho lake ni kufuta kero zote za Muungano ili kuwafanya wananchi wake waishi katika nchi ya Tanzania bila bugudha na uwoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isiwapo nafasi hata kidogo wapinga Muungano huu na kuwatisha wananchi. Ni vyema kutatua kero zote ili wakose na la kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu uhifadhi wa Mazingira. Napenda kuiomba Serikali ihamasishe zaidi juu ya uhifadhi wa mazingira na kuwawekea sheria kali kwa wale wanaokiuka sheria na kanuni za kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu umefikia miaka 50 tokea ulipoanzishwa. Katika miaka 50 hiyo, Muungano wenyewe umekabiliwa na kero nyingi kwa tafsiri ya malalamiko, manung'uniko na upungufu ulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejaribu kutatua baadhi ya kero lakini zipo nyingi hazijatatuliwa na baadhi ya kero nyingine zinasababishwa na muundo wenyewe wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kero za Muungano zinazosababishwa na muundo wa Muungano ni Tanganyika kuva koti la Tanzania, utungaji wa sheria zinazohusiana na mambo ya Muungano kwa wingi wa kura ukililia maanani Wabunge wa Zanzibar ni wachache na pia utaratibu wa Wabunge

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Zanzibar kuchangia mambo yasiyo ya Muungano wakati sisi ni Wabunge wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanganyika kuvaat koti la Muungano hufanya zile fursa za nchi (*Sovereign State*) zote kuchukuliwa na kufaidika kwa Tanganyika. Mawasiliano baina ya nchi kwa nchi ambayo ni rasmi, yanafanywa na Tanzania lakini Tanganyika imo humo humo. Ni dhahiri kero hiyo haitaendelea kama muundo wa Muungano utaendelea hivyo ulivyo. Vinginevyo, Serikali naomba iniarifu, vipi Zanzibar itakuwa na hadhi sawa Kimataifa pamoja na Tanganyika ikiwa mshirika mwenzake wa Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa kawaada, sheria zinazohusiana na utungaji wa sheria za kuyatawala au kuyaendesha mambo ya Muungano inakuwa kwa wingi wa kura (*simple majority*), kura ya theluthi tatu (2/3) inatumika kwa kuongeza au kupunguza mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina Wabunge 358. Wabunge wa Zanzibar ni 77 na Wabunge kutoka Tanzania Bara (Tanganyika) ni 281. Ni dhahiri Muswada wowote wa sheria kwa mgao wa Wabunge aina hiyo unaweza kupitishwa kwa kura za Tanzania Bara (Tanganyika) hata kama Wabunge wa Zanzibar hawakubaliani na sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muundo huu wa Muungano, kero hiyo haitaondoka. Nashauri kero hiyo iangaliwe kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RAMADHAN HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa afya njema ili nami niweze kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu juu ya kero za Muungano. Mimi binafsi sioni kuwa Muungano una kero, kwani kuna baadhi ya michango inayotoka Tanzania Bara, ambayo inaenda Zanzibar, haijawekwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha ambazo zinatoka kwenye Wizara hii zipatazo Shilingi bilioni 44 wananchi Wazanzibar pamoja na Wawakilishi wa Zanzibar hawafahamu kuhusu fedha hizo; jambo ambalo limekuwa likipigiwa kelele na watu wengi kwa kutokujua ukweli. Fedha hizi kama zitawekwa wazi na watu wakajua, basi hata hizo kelele zinazopigwa kuhusu kero za Muungano zingekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri aende Zanzibar kukutana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuwafahamisha juu ya fedha hizo na ni namna gani Serikali ya Muungano inachangia fedha kwenye Serikali ya Zanzibar, kwani hilo ndilo suluhisho kubwa la kero za Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na watendaji wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu huu niliutoa pia kwa Waziri Mkuu (Maafa) lakini napenda wadau wote waupate ili tuufanyie kazi kwa pamoja. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, kuna athari nyingi ambazo zinaendelea kutokea na kusababisha madhara ya kiuchumi, kiafya, njaa na kadhalika; kwa mfano, mvua nyingi zinazonyesha na kusababisha mafuriko ya mara kwa mara yanayoharibu makazi ya watu, miundombinu ikiwemo barabara na madaraja, kusababisha vifo vya watu na mifugo. Mara kwa mara, maeneo mengi likiwemo Jiji la Dar es Salaam na Mikoa kama Morogoro, Mara, Mbeya na kadhalika, yamekumbwa na mafuriko. Mafuriko hayo kwa kiasi kikubwa yanatasababishwa na maji yanayoletwa na mito ambayo "Catchment Areas" zake ziko mbali ya maeneo yanayoathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la kudumu ni kuanzisha na kujenga mabwawa makubwa ya kudhibiti mafuriko na kumwagilia mashamba (*Irrigation and Flood Control Dams*). Mabwawa hayo yakijengwa, yanaweza kutumika kwa mambo mengi yafuatayo:-

- (i) Umwagiliaji wa mashamba ya mazao ya chakula;
- (ii) Umwagiliaji wa malisho ya mifugo;
- (iii) Matumizi ya maji ya binadamu na mifugo; na
- (iv) Kuzalisha umeme (*hydropower*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo na faida za ujenzi wa mabwawa makubwa:-

- (i) Kujitosheleza kwa chakula, hivyo kuimarisha usalama wa chakula na nchi;

(ii) Kutoa maji ya kumwagilia malisho ya maji ya mifugo, hivyo kuchangia kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji;

(iii) Kupunguza mafuriko na athari zake kama uhalifu wa makazi na miundombinu;

(iv) Kupunguza uharibifu wa mali za watu;

(v) Kuokoa gharama za kuwahudumia waathirika kwa kuwapa chakula na matibabu, kuwahamisha na kuwatunza katika makambi ya muda; na

(vi) Ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mabwawa makubwa unapaswa kubuniwa kama miradi ya pamoja ikizingatiwa kwamba sekta zinazohusika ni nyingi na manufaa yake ni mtambuka. Aidha, miradi hiyo ikijengwa itawezesha Serikali kukinga madhara yanayotokana na mafuriko badala ya kutumia gharama kubwa kushughulikia hasara zinazotokana na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa pia mchango huu kwa Sekta za Maji, Mifugo na Uvuvi; Waziri Mkuu (maafa) na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kupongeza na kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. NYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais huyakasimu kwa Makamu wa Rais anapokuwa katika majukumu mengine, inao wajibu katika kuhusu masuala mawili muhimu: Muungano na Mazingira.

Hivyo, Ofisi hii inapaswa kutoa Uongozi kwa Taifa wakati huu ambao mchakato wa Katiba umekwama. Ukiendelea kukwama kwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba katika wakati ambapo tayari kuna pande mbili za misimamo iliyojipenyeza katika taasisi muhimu kufuatia Rasimu iliyowakilishwa katika Bunge Maalum iliyotokana na wananchi ni kuweka mustakabali wa Muungano wenyewe mashakani.

Hali ya sasa na ya siku za usoni ni ile aliyowahi kuieleza Mwalimu Nyerere kuwa ni nyufa. Hivyo zisipozibwa kwa majadiliano na maridhiano huku maoni ya wananchi yakiheshimiwa na matakwa ya Umma kuzingatiwa, Ofisi ya Rais itakuwa haijatekeleza vizuri majukumu yake ya kumshauri Rais katika masuala ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais kuiangalia Dar es Salaam siyo katika suala la usafi wa kutokutupa takataka ovyo tu, bali sura pana na jicho kali la kimazingira. Hii itawezesha kuyapa kipaumbele masuala yote yenye athari kwenye mazingira ikiwemo udhaifu katika Mipango Miji, athari za mabadiliko ya tabia-nchi ikiwemo ongezeko kubwa la mafuriko, magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, dengue na kadhalika, uchafuzi wa Mito toka viwandani na kadhalika, kwa kasi yake ya ongezeko la watu juu ya idadi kubwa ya sasa, Jiji la Dar es Salaam lisiporekebishwa na mfumo wake kufanyiwa mabadiliko makubwa, ni bomu la wakati.

Katika kuanza kuelekeza wajibu huo, naomba Idara ya Mazingira na NEMC kwa pamoja tukubaliane tufanye ziara Ubungo mpaka kubaini maeneo ya uharibifu, Mabibo na kwingleko. Aidha, muunge mkono kushawishi TAMISEMI juu ya hoja ya kuwa na dampo lingine Goba (Kivindu) au Kwembe. Mazingira ni maisha, hivyo uharibifu wake ni tishio kwa uhai. Hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Idara zake na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lililo chini yake ni vyombo muhimu vya kuwezesha mazingira safi, salama na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Ofisi hii inapaswa kuongezewa fedha katika mafungu yale yote mawili, fungu la 26 na 31 katika majukumu yanayohusu Mazingira. Kiasi hicho kielekezwe katika kazi za kusimamia sheria ya Mazingira (CMA) ya mwaka 2004 ikiwemo kupitia NEMC. Natambua kwamba Makamu wa Rais amewahi kufanya ziara Dar es Salaam kuhusu usafi wa mazingira. Hata hivyo, nitoe mwito...

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme machache kwenye Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Nianze na suala la Mazingira. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Katika hotuba yetu ya mwaka 2013 tulitoa agizo kwa Serikali kuhusu mifuko ya *plastic* ambayo Serikali ilisema imetoa muda wa kutumika kwa mifuko hiyo, lakini cha kushangaza mifuko hiyo bado inaendelea kuagizwa nchini na mingine inatengenezwa katika viwanda vya hapa nchini.

Mazingira ya nchi yetu yanazidi kuchafuka cha kushangaza Serikali inasema kuna ugumu wa utambuzi wa unene wa mifuko hiyo. Hivi mpaka kufikia uamuzi wa kupiga marufuku mifuko hiyo, Serikali ili kuwa haijajipanga kupitia wataalamu wake kuhusu suala hilo? Naomba Serikali itoe majibu yenye kuleta matumaini kwa sababu tatizo hili ni kubwa sana katika nchi. Kama majibu hayatakuwa na dhamira ya kweli, suala hili la mifuko ya *plastic* litaendelea kuwa kero katika nchi yetu.

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni wale watu waliojenga kwenye fukwe za bahari bila kufuata taratibu. Kamati yetu ilitembelea maeneo hayo na kujionea hali halisi ilivyo katika maeneo hayo, na Kamati ilitoa maelekezo kwa Wizara kwa wale waliovunja sheria, hatua za kubomolewa nyumba zao ufanyike. Lakini cha kushangaza watu hao wamekimbilia Mahakamani huku wakijua kabisa wamevunja sheria, wengine ni viongozi wakubwa wanaotunga sheria, lakini wao wanakuwa wa kwanza kuvunja sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotembelea maeneo hayo, ziko nyumba ambazo zilibomolewa; waliobomolewa wanadai nyumba zao zilibomolewa kwa sababu wao ni wanyonge na hawana fedha za kuhonga. Ili kuondoa dhana hiyo, ni vizuri suala hili likafanyiwa kazi ili wananchi waone haki inatendeka kwa wote bila kujali ana uwezo gani. Tabia ya wavunja sheria kukimbilia Mahakamani kuzuia kazi zisifanyike ni kosa kubwa. Tunaomba Serikali ifuatilie suala hili maana imekuwa ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache niliyoyaandika, naomba Serikali ifanyie kazi masuala hayo. Nashukuru kupata nafasi hii kuchangia, ila liko jambo moja muhimu sana. Kama tunataka Wizara hii iweze kufanya kazi zake vizuri ni lazima bajeti yake iongezeke maana Wizara hii ina kazi kubwa sana ya kuelimisha wananchi kuhusu suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**AMINA A. CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwasuala la mazingira ni muhimu sana, kulitokea elimu ya kutosha kwa wananchi wote ili wapate uelewa wa kutosha kwenye mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004 ipewe kipaumbele cha kutosha kwa kutoelewa elimu ili wananchi wote wafike na mambo yote yanayohusu kuhusiana na utunzaji wa mazingira, naiomba Serikali iandae vipeperushi pamoja na vyombo vyatuhabari vitumike kwa kuwaelimisha wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya plastic bado ni tatizo. Naiomba Wizara ichukue hatua za haraka kuitekeleza kanuni ya kuzuia mifuko ya plastic ili na kule Zanzibar isiweze kupelekwa kinyemela kwa sababu wale wenzetu Wazanzibari wako juu katika kutokomeza suala la matumizi ya mifuko ya plastic.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi kutowapa vibali vya ujenzi kwa wale wote wanaojenga katika maeneo hatarishi kama kwenvye vyanzo vya maji, wanaofukia maeneo ya mito na bahari na njia zinazopita maji. Wanapoachiwa watu kufanya mambo kama hayo ndio sababu kubwa ya mafuriko pamoja na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Niipongeze Serikali kwa kujitahidi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Muungano na historia yake kwa kutoa vipeperushi, vitabu mbalimbali na kufanya makongamano. Elimu hii iendelee kutolewa ili kuweka wazi masuala yote yanayohusu Muungano na utekelezaji wake wananchi walio wengi hasa wale waliozaliwa baada ya mwaka 1964 hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana na historia ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete kukubali kuanzisha mchakato wa uanzishajji mpya kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba katika hatua ya kutimiza miaka 50 ya Muungano huu, imesaidia sana wananchi kujua Muungano ni nini na historia yake imeanzia wapi na tumefaidika nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali sasa kuendelea na kazi hiyo ya kutoa elimu kwa umma ili wananchi kuweza kujua hasara zake na faida zake na kuendelea kudumisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali hatua iliyofikia ya mchakato wa utungaji wa Katiba mpya isisite kuendeleza mchakato huu na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kwamba maoni ya wananchi yapo mengi ndani ya rasimu ya Katiba na tunalo jukumu kubwa kuyazingatia na kuyafanya kazi kwa maendeleo ya Taifa na wananchi walio wengi hawakuwa na tatizo na muundo wa Muungano ila changamoto zilizopo ndizo zilizokwamisha kuimarisha na kuleta maendeleo yao nchini. Hivyo basi, Bunge limalize kazi yake vizuri, baadaye wananchi wanayo haki ya kuyaangalia maoni kama yamepuuzwa au yametupiliwa mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba mionganini mwa mambo ya Muungano ni masuala ya ulinzi na usalama wa Taifa letu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika utekelezaji wa suala hili, kiajira imekuwa ikijitahidi kuchukua vijana nchini toka katika pande zote za Muungano ili kuendelea kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili kwa upande mmoja kule Zanzibar limekuwa na utofauti katika miaka ya hivi karibuni kwa kufanya uchakachuaaji wa hali ya juu kwa kuangalia hali za watu na kusababisha rushwa iliyokithiri kuchukuliwa kwa vijana hao hata kama hawakukamilisha vigezo vinavyohitajika na kuwakatisha tamaa wale vijana wasio na uwezo ambao tayari wameshapata mafunzo ya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana ili hali hii isijirudie tena, ni vyema ajira hizi zikasimamiwa na jeshi lenyewe katika maeneo yote nchini, kwani wao nadio wanaojua nani amepata mafunzo ya kutosha na viwango vinavyohitajika, kwani katika vikosi vyetu nchini vya kujitolea vinao vijana wengi waliomaliza mafunzo kuliko nafasi hizi kupelekwa Wilayani na Mikoani. Vijana wazoefu ambao kipato chao ni cha chini hawapati nafasi hizi kwa kutumia utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni sikuvi, tuendelee kudumisha Muungano wetu kwa maendeleo ya wananchi na vizazi vijavyo kwa maslahi ya Taifa letu.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira; vyanzo vya maji vinaharibiwa kutokana na kutolewa kwa vibali vya uchimbaji wa madini. Kule Muheza kuna eneo linaitwa Ubembe Kwemhosi kuna mradi wa maji wa Benki ya Dunia, wameingia wachimbaji wanaharibu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba NEMC waende kufanya ukaguzi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pole kwa Serikali na kwa jamii zilizoathirika na mafuriko. Pamoja na jitihada zote ambazo Serikali inafanya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na naomba kuongezea ushauri wangu katika maeneo yafuatayo:-

(1) Mamlaka husika ifanye tathimini ya mito ilijojaa mchanga na kuondoa mchanga huo kama ilivyofanya katika mto baadhi ya maeneo ya Mbezi Dar es Salaam. Hatua hii itawezesha kiasi kikubwa cha maji kupita mtoni baada ya kusambaa na kuharibu barabara zetu na pengine kusababisha mafuriko katika makazi ya watu.

(2) Katika ule mto maeneo ya mamlaka kuna miti ya Luceana ambayo imeota katika kingo za mto. Miti hii ina mchango mkubwa wa kuzuia mmomonyoko wa kingo za mto pia mchanga usiingie mtoni. Kama aina hii ya miti haikaushi maji ni ushauri wangu mbegu hizi zisambazwe katika mito mingi nchini ambayo riverine vegetation imeharibika kutokana na shughuli za kiuchumi.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(3) Kingo za barabara zinazopakana na madaraja ziimarishwe kwa kujengea mawe na saruji ili kuzuia athari za mafuriko.

(4) Ujenzi wa shule uwe wa viwango (kenchi na paa ziwe imara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa ushauri katika maeneo mengine kama ifuatavyo:-

(1) Madampo yaliyozagaa katikati ya makazi ya watu hapa nchini yahamishwe, (kwa mfano, maeneo ya Mdenga – Mtwara, Kijitonyama na Temeke, Dar na Kirumba Mwanza).

(2) Elimu kuhusu biashara ya hewa ukaa itolewe kwa wananchi ili kuhimiza wananchi kutunza mazingira kibiashara.

(3) TANESCO Mtwara ipate fedha ya biashara ya hewa ukaa kutokana na matumizi ya umeme wa gesi badala ya diesel.

(4) Wizara ijiandae kufanya tathimini ya kupungua kwa matumizi ya Solid fuel kama utekelezaji wa malengo ya millennia, lengo namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kutatua kero za Muungano, lakini jitihada zaidi zinatakiwa ili hizi ziishe na tubakie na Serikali mbili. Masuala ya mazingira yaingizwe katika Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabia nchi yanaendelea kuleta madhara nchini Tanzania. Mikoa ya Kaskazini imekuwa affected sana na mabadiliko haya na ukame umeikumba sana Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Kwa bahati mbaya sijaona juhudhi za kutosha za Serikali kulikabili tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za ukataji miti, uchomaji wa mkaa unaendelea kwa kasi kubwa bila udhibiti. Mkaa mwingu unauzwa na hasa Dar es Salaam inaelekea kama vile Maafisa Misitu wa Wilaya hawako kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine nchini yameathirika na mabadiliko ya tabia nchi, kiasi cha kusababaisha maporomoko ya udongo

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(katika Wilaya ya Same, watu 24 walikufa) maeneo kama Same yapo mengi nchini na mtu yejote atatarajia angalau Serikali itoe elimu kwa wananchi ili kujihami na maporomoko ya udongo na kupusha madhara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuhusu kupanda miti, kuhusu kutumia nishati mbadala badala ya kuchoma mkaa, ni muhimu sana. Kupatikana na kwa gesi iwe ni chachu ya kupunguza mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye hima ku-supply gas ya kutosha mjini Dar es Salaam ili wakazi wa Dar es Salaam wapikie gesi, uchomaji mkaa upungue na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo imekuwa chanzo cha kuvuruga vyanzo vya maji nchi hii. Mabonde yote muhimu na mito mikubwa kama Malagarasi, Rufiji, Ruvuma, Kilombero, yamejaa mifugo tofauti hapo nyuma ufuutiliaji wa sheria (*implementation*) umekuwa hafifu sana, ndio maana mifugo inasambaa, mifugo nchi yote. Muhimu mifugo hii idhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUPH HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii adhim kumshukuru Allah Subhanah Wataala kwa neema ya uhai na uzima. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu naelezea kwenye chenji ya Rada. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika mambo ishirini na mbili (22) ya Muungano pamoja na Ulinzi na Usalama na Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo utakuta mambo mawili muhimu yanayohusu mambo ya Rada yamo katika Muungano nayo ni ulinzi na usalama na usafiri wa anga. Mimi binafsi nimekuwa nikijuliza Rada hii ambayo ulifanywa ujisadi mkubwa ni Rada ya aina gani ya Taasisi gani hata kufikia kuwa si ya Muungano na Zanzibar isipate gawio la chenji ya Rada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi mikubwa ya Muungano wetu ni udugu wa nchi mbili hizi pamoja na ujirani wa karibu wa nchi mbili hizi. Muungano wetu ni Muungano wa mfano duniani, ni Muungano wa muda mrefu duniani, Ni Muungano imara kuliko yote na ni Muungano wa kupigiwa mfano. Haya yote sina pingamizi na wala sibishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo sahihi na fasaha kuhusu Rada hii, inahusika na Taasisi gani au kama ya mtu binafsi kwa ajili ya fenicha

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

nyumbani kwake, basi iwekwe wazi mimi nijue. Ikiwa Rada hii ni ya Ulinzi na Usalama, bado ni Muungano, hivyo Zanzibar wanahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ulinzi Zanzibar inawajibika katika shughuli mbalimbali za ulinzi na usalama ndani na nje ya nchi. Wapo askari waliopigana vita vya kumng'oa Idd Amini Dada wa Uganada, wako waliopata vilema na wapo waliopoteza maisha, lakini pia katika matukio ya hivi karibuni Sudani na Kongo wamo askari kutoka Zanzibar wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba udugu wetu uwe udugu wa kweli, udugu wa kufaana wakati wa amani na wakati usiokuwa wa amani, udugu wetu usiwe wa kufanana bali uwe wa kufaana. Naomba busara itumike ili haki itendeke, Zanzibar wapewe chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za Muungano kuna dalili kubwa Serikali yenye we haifahamu ni ngapi ambazo zimepatiwa ufumbuzi na ngapi ambazo hazijapatiwa ufumbuzi na ngapi ambazo hazijapatiwa ufumbuzi. Hii inatokana na maelezo aliyotoa Waziri wa Mambo ya Muungano wakati akiomba nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba. Alisema kero zote za Muungano zimepatiwa ufumbuzi isipokuwa mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho cha Bunge Maalum la Katiba, Rais wa Jamhuri ya Muungano kuzungumzia kero za Muungano akifungua Bunge la Katiba yeye akasema zimebakia kero nne kutekelezwa. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa viongozi wakuu wa nchi hii ambao wana dhamana kubwa wanatofautiana, nina wasiwasi hata utekelezaji wake.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Kamati huko Bagamoyo, ambapo Kamati ya Uchumi, Biashara na Viwanda, nilimuuliza Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha kuhusu ongezeko la deni la Taifa pamoja na Devaluation ya shilingi ya Tanzania, Zanzibar inafidiwa vipi wakati haya yote yanayosababishwa na upande mmoja tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Naibu Katibu Mkuu ni kwamba, Zanzibar inakopa kupitia Jamhuri ya Muungano na hawalipi madeni yao ambapo Jamhuri ya Muungano ndio inayolipa deni la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa jibu hilo Naibu Katibu Mkuu aliliona sahihi ndiyo njia ya kufidia Zanzibar, basi wakati sasa umefikia ikipatikana Katiba mpya au laa basi hesabu zifanywe za miaka 50 kwa Mashirika yote ya Muungano ambapo Zanzibar haijapata faida au mgawo wowote, basi hesabu zifungwe ili fedha ya mkopo iliyolipiwa Zanzibar na fedha yote Zanzibar ilistahili ilipwe kutoka Mashirika ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu, fedha yote ya Muungano iliyopelekwa kwa makampuni binafsi ya Tanganyika kwa njia ya uwekezaji au kwa njia ya mtaji wa kuanzisha mabenki au miradi mingine upande wa Tanganyika, basi na Zanzibar imo 11.02% yake ikiwa ni shares zake katika BOT na hata kama hawatambui 11.02% basi hivyo 5% wanayotaka bado Zanzibar ina fedha yake iliyoingia katika Taasisi zote zisizo za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa haja hii ni kwamba hakuna ukokotoaji ni kwamba hakuna ukokotoaji uliofanywa kabla ya fedha hizi hazijagawiwa kwa pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi inatumia fedha zote kwa ajili ya mazingira ya upande mmoja tu wa Muungano. Angalia kiambatisho Namba Moja (Na. 1) na kiambatisho Namba Mbili (Na. 2) lipi lilofanyika Zanzibar?

Kisiwa Panza mazingira yameharibika kiasi cha Bahari kufukua makaburi ya kale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukanda wa Kusini Unguja kuanzia Makunduchi, Jambiani Paje, Bwejuu, Uroa, Pwani Mchangani na kadhalika, mazingira yameharibika sana kiasi cha mita mbili mpaka tatu za ardhi inaliwa na bahari. Kwa nini tunataja hii fedha fulani itapelekwa Zanzibar lakini hakuna kitu?

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhifadhi mazingira kutokana na ukataji miti na uchomaji mikaa, wananchi waelimishwe kupitia redio kwani wengi wana uwezo wa kumiliki redio. Waelimishwe madhara na hasara yatokanayo na ukataji miti na pia waelimishwe kutumia *alternative energy* (nishati mbadala) kama vile biogas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biogas haipatikani kutoka kinyesi cha wanyama tu, wataalam wanasesma hata kinyesi cha binadamu kinatumika kupata biogas. Wananchi waelimishwe matumizi ya biogas ili kuепusha nchi yetu na ukame unaoweza kusababishwa na ukataji miti uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi utekelezwe ipasavyo. Taarifa itolewe kupitia vyombo vya habari ili wananchi wapate uelewa kuhusu mkataba huo ili waweze kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira hayo.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majengo mengi yaliyojengwa kando kando ya ufukwe wa Bahari ya Hindi, hii ni kinyume cha sheria. Serikali ichukue sheria na kuzibomoa nyumba hizo kwani nyingi zimejengwa kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri uk. 58 inaelezea utekelezaji wa Mkataba kuhusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu wa Basel na Mkataba wa Bamako. Aidha napendekeza pamoja na kuandaa filamu kuhusu shughuli za usimamizi wa taka sumu katika Jiji la Dar es Salaam hususan mafuta machafu, betri chakavu na vifaa vya umeme na elektroniki ili kuwaelimisha wananchi, vipindi vifupi vya dakika tano tano viandalisiwe na kurushwa katika media zetu zikiwemo redio ili wengi zaidi waelimike. Fedha ya kutosha katika kipengele cha elimu kwa umma, itengwe ili kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuelimisha umma kuhusu Muungano, napenda kuipongeza Serikali kwa kuandaa utaratibu huo, lakini hata hivyo ninashauri uongezwe mkakati zaidi wa kuelimisha wananchi kupitia vyombo vya habari (Tv, redio, magazeti, vipeperushi, mitandao) na utaratibu uwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano, pia naipongeza Serikali kwa kufanya vikao vya pamoja vya kushughulikia masuala hayo. Ninachoomba Serikali zetu mbili zitilie mkazo na kutekeleza kwa vitendo kwa yale mambo yanayoamuliwa katika vikao hivyo muhimu kwani wananchi wanasi kia vikao vinafanyika lakini hakuna utekelezaji.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna masikitiko ya muda mrefu kuhusu kutokamilika vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano, kwa mfano; Usajili wa vyombo vya moto, mgawanyo wa faida ya Benki Kuu, kodi kwa wafanyabiashara n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini na mwaka gani mambo haya yataweza kukamilishwa ili kuepukana na kero hizi za muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ziko fedha ambazo Zanzibar inapatiwa kwa kila wakati husika ambazo zinatoka sehemu ya Jamhuri ya Muungano, hivyo itakuwa ni vizuri kuwekwa bayana fedha hizo na viongozi kuwajulisha Wabunge kwa kila awamu.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo fedha za TASAF ambazo zinawafikia wananchi wa Zanzibar pia iko haja fedha hizi kujulishwa Wabunge na Waziri mhusika ili Wabunge waweze kufuatilia kuona shehia husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira lina umuhimu sana na ni suala la kuchukuliwa hatua za hali ya juu ili kuweza kutunza mazingira. Lakini suala la ukataji miti kwa ajili ya mkaa ni suala la kazi za siku zote vijijini na suala la kazi ambayo wanawahudumia kwa ajili ya kipato chao vijijini ili kuweza hata kusomeshea watoto wao. Je Serikali imeweza kufanya mambo gani mbadala kwa hawa wananchi wenyewe kujishughulisha na shughuli hizi ili kuendeshea maisha yao ya kila siku?

**MHE. GOODLUCK J. OLE – MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Nawapongeza Mawaziri wote Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na watendaji wa ofisi hiyo na taasisi zake kwa jitihada wanazofanya kusimamia utekelezaji wa sera na sheria zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikakati ya kukabiliana na maafa ya kimazingira: Tanzania imekuwa ikikakibiliwa na maafa yatokanayo na ama ukame au mafuriko kila mwaka. Miaka ambayo tumejaliwa kupata mvua basi mafuriko hayaepukiki. Mafuriko yatokanayo na mvua siyo ajali isiyoepukika. Tatizo la Taifa letu ni kukosa mkakati wa kuzuia maafa na badala yake tumewekeza fedha nyingi katika mkakati wa kupambana na maafa. Nashauri yafuatayo yafanyike ili kuepuka maafa yatokanayo na ukame pamoja na mafuriko:-

Serikali iandae mpango mkakati na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakati yatakayokinga maji ya mvua na kuyahifadhi kwa ajili ya:- Matumizi ya binadamu, mifugo, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa samaki na kuzuia mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika meneo ya Dar Es Salaam (mabwawa yajengwe Kisarawe na Pugu); Kibaha/Bagamoyo (mabwawa yajengwe Kidunda); Rufiji (bwawa lijengwe Stieglers Gorge); Mto wa Mbu (bwawa lijengwe kwenye catchment zinazounda Mto Kirurumo); Arumeru (bwawa lijengwe Thembi ya Simba na Bwawani) pamoja na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lishirikiane na Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa mkakati utakaowezesha maafisa Ardhi, Ugani wa Kilimo na misitu kupata nguvu za kisheria kuzuia matumizi mabaya ya ardhi ikiwemo ujenzi holela na kilimo kisichozingatia kanuni za kilimo bora ili kuzuia uhalibifu wa mazingira ambao

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

husababisha mmomonyoko wa udongo na hivyo ardhi kupoteza rutuba za kushindwa kuzalisha mazao ya kutosha. Aidha kufanya hivyo kutazuia udongo mwingi kuingia kwenye mito, maziwa na bahari na kusababisha kina cha bahari kupanda na hivyo kuchangia mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya biotechnology katika Kilimo: Kwa muda mrefu, tasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo na Tume ya Sayansi na Teknolojia zimekuwa zikiomba kibali cha kufanya utafiti wa teknolojia mpya kwa madhumuni ya kukuza/kugundua mbegu mpya (GMO) ili kuboresha mazao kwa kupata mimea yenye kustahimili magonjwa na yenye kutoa mavuno mengi zaidi. Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira imekuwa kikwazo katika jithada za kurekebisha kanuni ili kuruhusu walau utafiti kuanza nchini. Gharama ya ung'ang'anizi huo kwa Taifa imekuwa kubwa sana. Sisi sote ni Watanzania na tumekuwa tukisafiri kwenda nchi mbalimbali duniani ambapo vyakula tulavyo, nguo tunazonunua huko baadhi ni matokeo ya matumizi ya teknolojia hiyo. Hatujadurika lakini pengine kwa sababu ya kuamua kubisha, bado tunaendelea kubishana, muda hautungoji, jirani zetu wanaendelea na utafiti na hatimaye tutakuwa soko lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa utafiti wa GMO uruhusiwe ili tujue namna ya kuepuka mbegu isiyofaa kuingia nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na narudia kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utunzaji wa mazingira ni suala muhimu sana kwa maendeleo yetu na uhai. Sababu ya uhalifu wa mazingira na ufanyaji wa shughuli za binadamu kama kilimo kisichozingatia mwelekeo wa miinuko, uchomaji wa petroli, dizeli, utumiaji kuni, uchomaji wa misitu, viwanda, majumba, uendeshaji magari, vinavyoongeza gesi ya ukaa hewani. Kuongezeka kwa hewa ya ukaa kumesababisha ongezeko la joto duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la joto duniani linasababisha mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha athari kubwa kama: Mafuriko zaidi, upemo mkali, ukame, njaa, theluji ya Mlima Kilimanjaro na kuibuka kwa magonjwa mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi inabidi kufanya yafuatayo:- Kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira na juu ya mabadiliko ya tabia nchi, kuendelea kuhamasisha na kuwawezesha wananchi kupanda miti na miti ya asili, kuhakikisha kitengo cha

hali ya hewa kimewezeshwa na kina vifaa na teknolojia ya kutosha kuweza kubashiri hali ya hewa (ijayo), kitengo cha maafa kupewa fedha za kutosha ili waweze kurekebisha uhalibifu wa barabara, reli, nyumba, mashamba yanayoharibiwa na mvua/mafuriko, wananchi kutumia nishati jadidifu (renewable energy) badala ya kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua; Kuna utaratibu gani ulioandaliwa na Wizara ili wananchi waache kutumia kuni na mkaa na ili watumie nishati jadidifu? Nijuavyo mimi Tanzania hatuna sera ya nishati jadidifu. Serikali ina mpango gani wa kuiandaa na kuitumia hapa nchini ili ichangie kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa? *NAMP (The National Adaptation and Mitigation Programme)* je, inatekelezwa? Ni kitu gani kimetekelvezwa hadi sasa? Kwa kiasi gani Wizara inanufaika na *climate change green funds*?

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niongelee suala la mabadiliko ya tabianchi, na uharibifu unaofanywa na ukataji miti ovyo kutokana na shughuli za kibinadamu za kilimo, ufugaji na ukataji miti kwa ajili ya mazao ya misitu, kama mbao, kuni, mkaa na magogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa misitu kutokana na shughuli nilizotitaja, umekuwa ni mkubwa sana. Kilimo cha kuhamahama, kinasababisha ukataji wa misitu mikubwa mara kwa mara na hivyo kutengeneza jangwa maeneo ambayo yalikuwa yana misitu mikubwa iliyokuwa inaleta uhifadhi wa ardhi na vyanzo vya maji. Bado Serikali ina kazi kubwa, ya kuwaelimisha wananchi, hasa Wilaya ya Liwale, kuacha kutumia kilimo cha kuhamahama, kutoka eneo moja hadi nyingine. Na hili litawezekana tu iwapo Serikali itaendelea kuhimiza kilimo cha kisasa cha kutumia mbolea na mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa mbao, miti, uchomaji wa mkaa ni moja ya sababu inayosababisha mabadiliko ya tabia nchi. Serikali ni vyema iongoze juhudini kubwa katika kupambana na vita hii ya ukataji miti holela kwa ajili ya mazao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji watengewe maeneo maalumu ili kuzuia uharibifu na mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano: Malalamiko yote yanayohusu Muungano yaliyobakia yaongelewe na yamalizwe ili kuufanya Muungano huu kubaki na kuwa imara zaidi. Yale mambo yote yanayogusa Muungano yafuatwe; ajira, mgawanyo wa fedha, miradi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kutoa elimu ya kuhifadhi mazingira kwa umma, itolewe Wilaya ya Liwale, uharibifu wa mazingira na misitu ni mkubwa mno ni vyema ukomeshwe.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima napenda kutoa mchango wangu kuhusu Wizara hii ya Muungano na Mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Muungano wetu umetimiza umri wa miaka 50. Katika kipindi hiki cha uhai Muungano huu tumeptitia katika misukosuko mingi iliyotishia uhai wa Muungano. Jambo hili msingi wake mkuu ni malalamiko ya kila upande wa Muungano huo, mfano malalamiko mengi yanayotokea upande wa Zanzibar yanahusu mgawanyo wa mapato na uhuru wa Zanzibar kujiamulia mambo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika suala la mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya nje kuendelea kuigawia Zanzibar 4.5% ni jambo ambalo linafaa kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiki, pia suala la ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna mambo kadhaa ambayo Serikali ya Muungano imewakilisha katika Jumuiya hiyo kwa kivuli cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kosa kubwa ni kwamba Serikali ya Muungano imeshindwa kuiwakilisha Zanzibar kwa ukamilifu katika mambo ambayo siyo ya Muungano hivyo kuifanya Zanzibar kukosa uwakilishi katika Jumuiya hiyo hali inayopelekea Zanzibar kupoteza fursa adhimu katika masuala kadhaa. Mfano, Wizara ya Kilimo na Chakula ni Wizara isiyo ya Muungano, Wizara ya Biashara na Viwanda siyo ya Muungano na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hebu tujiulize linapokuja suala la Kilimo katika Jumuiya hiyo msemaji wake ni nani? Linapokuja suala la utalii mtetezi wa Zanzibar ni nani? Suala la Biashara Afrika Mashariki msemaji wake ni nani. Hili ni tatizo na kasoro kubwa isiyovumilika katika Muungano huo. Hivyo naomba majibu kwa Serikali kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika Afrika ya Mashariki kwa masuala ambayo siyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Jumuiya ya OIC, tunakumbuka Zanzibar iliwahi kujeunga katika Jumuiya ya Kiislam OIC kwa malengo zaidi ya kiuchumi na siyo vinginevyo. Kwa bahati mbaya sana ilitafsiriwa isivyo na kusababisha mtafaruku mkubwa katika Muungano, hali iliyopelekea kulazimishwa Zanzibar kujitoa katika Jumuiya hiyo kwa shingo upande na kuinyima fursa Zanzibar kujikwamua kiuchumi. Hata hivyo Serikali ya Muungano iliweka ahadi mahsusii ya kwamba kujitoa kwa Zanzibar OIC kutaenda sambamba na Jamhuri ya Muungano kujeunga na Jumuiya hiyo kwa malengo yale yale ya kunufaika kiuchumi. Jambo la kusikitisha ni kwamba mpaka leo hii takriban miaka zaidi ya 15 sasa hakuna chochote kinachofanyika wala jitihada zinazoonekana kuchukuliwa kushughulikia jambo hili muhimu. Je ni mpango gani wa Serikali uliopo katika kutekeleza ahadi yake hiyo? Je, iwapo suala hili kwa Jamhuri ya Muungano lina ukakasi, itakuwa tayari sasa kuiruhusu Zanzibar ijiunge na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jumuiya hiyo? Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu suala hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magari kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam: Kwa muda mrefu kumekuwa na usumbufu wa watanzania kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam kwa aidha matembezi au shughuli zao binafsi pale wanapotaka kuingia na magari yao kwa matembezi binafsi, jambo hili ni la muda mrefu na linaleta balaa kubwa. Hivi inakuwaje raia wa nchi jirani, mfano Zambia, Congo, Kenya, Burundi, wamewekewa, utaratibu mzuri wa kueleweka pale wanapoingia nchini na magari yao, iwe tatizo kwa wananchi wa nchi yao wenyewe liwe ni jambo zito linaloshindwa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kwamba kila Mtanzania leo hii ni mhanga wa deni la Taifa wastani wa zaidi ya dola mia tano kwa kila raia wa nchi hii, lakini raia huyo huyo wa upande mmoja wa Muungano anawekewa vikwazo visivyo na msingi anaposafiri na chombo chake kwenda upande wa pili wa Muungano. Kinachoshangaza zaidi ni pale Mtanzania wa Zanzibar anavyokumbana na vikwazo hiyo. Nimeshuhudia raia jirani akiiringia nchini bila vikwazo, kama utaratibu tu wa kulipia *foreign permit* isiyozidi dola 30 na kuvinjari katika nchi na usafiri wake. Ni vyema jambo hili lipatiwe ufumbuzi wa haraka ili tuondolewe na kuona fahari kuita ni kero ya Muungano, suala hili nipatiwe jibu linavyoshugulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Balozi za Tanzania nje ya nchi: Kumekuwa na malalamiko makubwa upande wa Zanzibar kuhusu uteuzi wa Mabalozi na wafanyakazi wa Balozi zetu nje ya nchi. Ni kweli kwamba katika Balozi zetu zaidi 50 duniani ni Balozi tatu tu ndizo zinawakilishwa na Wazanzibar, jambo ambalo halileti taswira nzuri ya uwakilishi wa Jamhuri yetu. Halikadhalika wafanyakazi na Wambata wa Balozi hizo, hivyo naomba tuelezwe vigezo gani vinatumika katika jambo hili linalofanya Zanzibar kupata nafasi 3 kama ilivyo sasa, pia ili kuondoa malalamiko haya, napendekeza angalau nafasi 15 ipewe Zanzibar.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu mazingira. Uchafuzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali hususan Jiji la Dar es Salaam umekuwa kikwazo cha maendeleo na hivyo ni vyema jitihada za makusudi zichukuliwe ili kunusuru majanga mbalimbali ya maradhi na uchafuzi wa mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo mbalimbali vya maji kama mito na maziwa vimeendelea kuchafuliwa na mabaki ya viwandani. Lakini pia mifugo mingi imekuwa ikutumia vyanzo vya maji ambavyo ni binadamu wanatumia hivyo kuhatarisha usalama wa Watanzania. Ni vyema Serikali itenye maeneo ya kunyweshea maji wanyama.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu wa kipekee, ni vyema sasa Wizara ichukue hatua za makusudi ili angalau Halmashauri zote nchini ziwe na sheria ndogo za mazingira ili kusaidia Halmashauri za mji na majiji ziweze kuwa na control ya shughuli za utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani.

**MWENYEKITI:** Waziri Mtoa hoja dakika thelathini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama na kutetea hoja ya Wizara katika Ofisi ya Makamu wa Rais toka nimeteuliwa, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunithea na kuniamini na mimi namuahidi yeye na Wabunge wenzangu kwamba sitawaangusha. Aidha, nawaomba wananchi wa Makete tuendelee kushirikiana ili kujiletea maendeleo yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuongea humu ndani na wale ambao wametuletea kwa maandishi. Tumepokea hoja zote, tutaziandika na kuzifafanua kwa ufanuzi mzuri. Tutatengeneza bango kitita ili muweze kuzisoma kwa undani na kwa uzuri zaidi. Kwa sababu muda uliopo hapa hauwezi kutosha kuweza kufafanua hoja zote na kama walivyosema wengine hoja ya mazingira ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kufafanua suala hili la matumizi ya mifuko ya plastic. Ni kweli inaonekana kama vile Serikali haijafanya kazi, kama vile Serikali haijatii maagizo ya Wabunge lakini ni vizuri tukaliangalia kwamba kwa mara ya kwanza agizo la kutumia mifuko ya plastic lilitolewa mwaka 2006 na wakati ule agizo hili liliagiza kutumia mifuko isiyo chini ya maikroni 30. Kwa wakati huu ninapoongea Kanuni zilizopo, ipo Kanuni ambayo inaruhusu mifuko inayozidi maikroni 30 na kwenda juu. Toka hapo hakuna Kanuni ambayo imepitishwa ambayo ingeweza ku-burn ile mifuko moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuruhusu kwamba mifuko ya plastic itumike kuanzia maikroni 30 kwenda juu yalilenga kwamba ile mifuko itakayozalishwa na vile viwanda vinavyohusika basi iwe ni mifuko ambayo inaweza ikarejeshwa, inaweza ikawa recycled kwa ajili ya matumizi tena na hivi ingeondoa matatizo ya kuzagaazagaa mitaani. Hilo halikutokea lakini tunaona vilevile plastic zikaendelea kuzagaa kwa sababu ya matatizo ambayo tumeyaainisha kwenye taarifa yetu, tatizo mojawapo ikiwa ni kwamba tumekuwa hatuna utaalam wa kujua zile maikroni ni kiasi gani, bidhaa kama hizi

zimekuwa zinaingia kwa milango ya nyuma na tuna viwanda ambavyo havijasaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado Serikali haijakata tamaa. Mwaka 2012, Serikali ilitoa tangazo hapa Bungeni kwamba ili sasa tuweze kuondoa matumizi ya mifuko ya *plastic* ambayo iko chini ya maikroni 30 basi tuongeze kiwango na kwamba sasa tutaruhusu matumizi ya maikroni 100. Bado *plastic* zinazagaa na bado maagizo haya yamekuwa vigumu kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe wa kweli, ni lazima tuangalie tulikotoka na tunakokwenda kwamba Serikali juhudzi zake zipo zinaonekana lakini matokeo yake ni kidogo. Sasa kwa nini? Kwanza, suala hili linahusisha wadau wengi. Unapoongelea mifuko ya *plastic* unaongelea viwanda vinavyozalisha mifugo ya *plastic* ambavyo ni Sera yetu wenyele iliruhusu viwanda hivyo viweze kuanzishwa na vinazidi siyo chini ya 20. Unaongelea TRA, unaongelea *Tanzania Investment Centre* na unaongelea ajira za vijana walioko kwenye zile sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la muhimu hapa la kulifanya la kwanza ni kuhakikisha kwamba ili kuondoa mifuko hii ya *plastic* katika uzalishaji wake lazima tukae na hawa wadau ambao nimewatamka. Kwa hiyo, siyo kwamba Serikali imekataa kutekeleza maagizo ya Bunge, tutafanya mambo mawili. Jambo la kwanza tutaendelea kutekeleza maagizo ambayo Serikali imeyatoa na ili kutekeleza maagizo ya kufikia maikroni 100 ni lazima zitengenezwe Kanuni. Kanuni zimeshaandaliwa na zipo katika hatua za mwisho ya kukamilishwa ili zianze kutumika. Tutazisimamia ili kuona kwamba maikroni 100 na zaidi ndiyo zinaweza zikatumika na hasa zile ambazo zinaweza zikawa *recycled* kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba hata ukiruhusu maikroni 100 bado zitatumika na zitarudi tena kwenye uchafu. Kwa hiyo, nadhani tatizo kubwa hapa ni namna gani tuweke mikakati ya kusimamia *solid waste management*. Kwa hiyo, tunadhani mkakati wa pili ambao tutauleta na tumeusema kwenye Kamati kwamba tukae na wadau, wadau wanaozalisha, tukae na wadau mbalimbali ili tuone ni namna gani sasa wakati Serikali inasimamia ku-phase out uzalishaji wa hizi *plastic* zisiwepo lakini kwa sasa hivi tuone ni namna gani hizi *plastic* zinaweza zikakukusanywa na zinaweza zikawa *recycled*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote ni mashahidi, *plastic* hizi zilikuwa zinazagaa sana lakini leo hii ni fedha, zinakusanywa, zimetoa ajira kwa vijana na kwa kweli sasa hivi huwezi kuzipata. Tunaamini kwamba tukiwa na mkakati kama huo hata *plastic* za mifuko hii zinaweza kukusanywa na zikatoa ajira, tukikaa na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hawa ambao wanazizalisha. Huu ni mkakati wa muda kuondoa huu uchafu uliopo wakati tunahakikisha kwamba tuna-phase out uzalishaji moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imechangiwa sana na Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira, Mheshimiwa aliyechangia hapa Mheshimiwa Kwegyir. Suala hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana kuhusu mifuko ya plastic na vilevile Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka niliongelee ambalo ni la *general* ni kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Kila aliyesimama hapa ameongelea matatizo ya mafuriko, matatizo ya uharibifu wa miundombinu, matatizo mbalimbali yanayotokana na uharibifu wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya kudumu ya mifumo ya hali ya hewa na uso wa dunia. Mabadiliko haya yanatokana na ongezeko la gesi joto ambazo zinasababishwa na shughuli za binadamu za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kwamba, sisi kama Afrika siyo ambao tunesababisha kwa kiasi kikubwa hizi gesi joto ambazo ziko kwenye anga. Sehemu kubwa imesababishwa na nchi zilizoendelea ambazo ndiyo zinazalisha hizi gesi joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea gesi joto kwa ufahamu zaidi Waheshimiwa Wabunge, tunaongelea gesi za hewa ukaa ambazo ni carbondioxide, tunaongelea zile gesi ambazo zinazalishwa kwa viumbwe ambavyo vimeoza ambayo ni *methan*, tunaongelea gesi ambazo zinatokana na mbolea za viwandani na tunaongelea gesi ambazo zinatokana na viwanda vyenyewe. Kwa hiyo, kazi kubwa ni namna gani tutazipunguza gesi hizi ambazo ndiyo zinasababisha ongezeko la joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinafanya kazi namna gani? Gesi hizi zimetanda kwenye anga, zinatengeneza aina kama *blanket* kiasi kwamba miale ya jua inapokwenda kwenye ardhi na inapokuwa inakuwa-absorbed na vitu vingine iko ile ambayo inarudi kwenye anga, lakini inazuwa na lile *blanket* la hizi gesi joto na hivyo kurudi tena ardhini na kuongeza joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa za wanasayansi, IPCC (*Inter-Governmental Panel on Climate Change*) mpaka sasa hivi joto limeongezeka kwa 0.85 Centigrade Degrees na wanasema kwamba, ikifika kwenye nyuzi degree 2 basi hali itakuwa mbaya zaidi. Kwa hiyo, tunatakiwa tufanye kazi ya kuhakikisha kwamba, hatufiki huko kwenye 2, ili kuweza kuzuia haya matatizo ambayo yanatokea sasa hivi.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafanya nini katika Serikali yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ili kukabiliana na matatizo haya ya tabianchi la kwanza, tunayo Sheria ya Mazingira ambayo ilitengenezwa mwaka 2004 na sheria hii imeeleza waziwazi vitu gani vya kufanywa. Lakini vilevile mwaka 2004 Serikali yetu ilitoa Mwongozo wa Kuwekeza katika Miradi ya Upunguzaji wa Gesi Joto, huo Mwongozo upo; lakini vilevile mwaka 2007 tuliandaa program ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi (NAPA) na ipo na wadau wengi wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile mwaka 2009 Kitabu cha Kukuza Uelewa kwa Miradi ya Upunguzaji wa Gesi Joto kiliandaliwa. Mwaka 2010 tunao mkakati ambao unafanya tathmini ya teknolojia zinazohitajika nchini kwa kushughulikia mabadiliko ya tabianchi. Lakini tunao mkakati ambao uliandaliwa mwaka 2012 ambao unaonesha kila sera ni namna gani inaweza ikashughulikia mabadiliko ya tabianchi katika eneo husika, iwe ni kwenye maji, iwe ni kwenye kilimo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ambayo Serikali yetu imefanya katika kuhakikisha kwamba tunahimili mabadiliko ya tabianchi au kuyakabili. Tunayo miradi ya ujenzi wa kuta pale Zanzibar, tunajenga ukuta Dar-es-Salaam, tunajenga ukuta Pangani na miradi mingine. Lakini vilevile tumekuwa tunatoa miradi mbalimbali inatangazwa kuitia grant ndogondogo ambayo wananchi, makampuni mbalimbali yanatengeneza miradi ya ubunifu ya majiko banifu na mingine mbalimbali ambayo inaelekea kuondoa umasikini kwa wananchi wetu, ili wasivune misitu kwa ajili ya kutengeneza mkaa waweze kujipatia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema athari za mabadiliko ya tabianchi ni kubwa, ni nyingi. Athari ziko kwenye afya, ziko kwenye kilimo, ziko kwenye uchumi, ziko kwenye miundombinu ambayo inaharibika na maeneo mengi zinatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nihitmishe kwa kusema kwamba, hivi sasa mabadiliko ya tabianchi ndiyo sasa tatizo linaloleta changamoto kubwa sana duniani hasa katika ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii ya maendeleo endelevu, hasa katika nchi zinazoendelea hususan Bara la Afrika. Suala la mabadiliko ya tabianchi linahusu maisha ya wananchi, uchumi, mazingira, usalama wa nchi na biashara ya kimataifa na kimataifa. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi kuzidi kuwa kubwa, iko haja ya nchi zinazoendelea kujipanga zaidi kukabiliana na tatizo hili, ili kupunguza athari zake katika nyanja zote za mazingira, uchumi, siasa na utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali yetu inajijunga na nchi nyingine za kimataifa katika kujadili namna gani gesi hizi ziweze kupunguzwa, kwa hiyo, hiyo

ni njia mojawapo. Na sisi kwa sababu hatuzalishi sana hizi gesi-joto, msimamo wetu katika nchi za Kimataifa tunasema kwamba, nchi za kimataifa zitoe fedha kwa ajili ya kuweza kukabili mabadiliko ya tabianchi katika nchi zinazoendelea, lakini vilevile kwa ajili ya miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Haya yanaendelea na tutakua tunaendelea kutoa taarifa, lipi ambalo limefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka niwaombe Wabunge wenzangu, kwenye suala la *plastick* kwamba, tumekuwa tunasema tutumie mifuko ya vikapu, mifuko ya majani na nashauri, sisi ni Viongozi, tuanze sisi kwamba, unapokwenda pale *Mlimani City, Shoppers Plaza*, basi uende na mfuko wako, ili ku-discourage matumizi ya *plastic* kwenye yale maduka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la ubomoaji wa nyumba zilizojengwa kinyume cha sheria katika maeneo ya ufukwe wa bahari, maziwa na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya 2004 inazuia shughuli za kibinadamu kufanyika katika kingo za mito, bahari na vyanzo vya maji chini ya mita 60. Lengo ni kulinda maeneo kwa ajili ya matumizi sahihi na uhifadhi wa mazingira katika maeneo hayo. Hata hivyo, kuna wimbi kubwa la ukiukaji wa matakwa ya Sheria ya Mazingira mionganoni mwa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na hali hiyo, Baraza limechukua hatua mbalimbali kwa nyakati tofauti dhidi ya wananchi waliokiuka Sheria ya kujenga katika fukwe za bahari na mikondo ya mito kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 Baraza kwa kushirikiana na wadau wengine Wizara ya Maliasili na Utalii, Manispaa ya Kinondoni na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa pamoja walibomoa nyumba zilizojengwa kinyume cha sheria Wilayani Kinondoni katika eneo la Mbezi, Kilongawima. Katika Zoezi hilo jumla ya nyumba 27 na kuta 8 zilibomolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika zoezi hilo pia ubomoaji ulifanyika kwa waliovamia maeneo ya Mto Mbezi kwa kubomoa ujenzi uliokuwa unafanyika ndani ya mto huo na kurejesha mkondo wake ili kuruhusu maji ya mvua kuingia Bahari ya Hindi bila kikwazo kingine. Tatu, hatua dhidi ya nyumba tatu zilizojengwa kwenye kingo za Mto Midumbwi zilichukuliwa kwa kuvunja nyumba mbili kati ya tatu zilizojengwa kinyume cha sheria kwenye kingo za mto huo. Nyumba kwenye Kiwanja Na. 2009 na Kiwanja Na. 609 zilibomolewa isipokuwa nyumba moja iliyojengwa kwenye Kiwanja Na. 2019 na 2020 inayojulikana kama ya Mchungaji Rawakatare haikubomolewa kutohana na mmiliki wa nyumba hiyo kufungua kesi Mahakamani na kuweka zuwio (*injunction*) dhidi ya Baraza.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kesi Mahakamani: Kesi ya msingi ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni na katika kesi hii Mahakama ilitupilia mbali maombi ya mlalamikaji; kwa lugha nyingine, Baraza lilishinda kesi hii katika ngazi hiyo ya Mahakama. Mlalamikaji alifungua kesi nyingine Mahakama Kuu ya Tanzania – Kitengo cha Ardhi, tarehe 24/04/2012; kesi hii imekuwa ikiendelea na itasikilizwa tena tarehe 25 mwezi wa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tatizo siyo Baraza kutofanya kazi, ni kwamba, nchi yetu inaheshimu utawala wa sheria na kwa hiyo, lazima mhimili huu tuuachie ufanye maamuzi yake. Aidha, Baraza ni Mjumbe wa Kamati ambayo aliiunda Mheshimiwa Waziri wa Mkuu, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayohakiki maeneo ya ufukwe kwenye Mikoa yote nchini, ili kujiridhisha na uhalali wa ujenzi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili limeanza katika Mkoa wa Dar-es-Salaam na nyumba na kuta 496 zimebainika kujengwa kwenye maeneo yenye utata wa kisheria. Baada ya zoezi hili kukamilika Baraza litachukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya wamiliki wa nyumba hizi, Baraza litachukua hatua za kisheria baada ya sheria hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Baraza linafanya kazi yake vizuri, lakini lazima liheshimu utawala wa Sheria pale inapobidi na pale ambapo inatakiwa, basi wanafanya kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo limeduwa raised na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ni kuhusu kiwanda cha 21<sup>st</sup> Century kuendelea kutumia magogo na viwanda vingine. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba nimefanya ziara mwenyewe juzi, kile kiwanda sasa hakitumii tena magogo, kinatumia makaa ya mawe. Tatizo liliopo sasa pale ni kwamba, ile mitambo, yale ma-boiler, yalikuwa yametengenezwa kwa ajili ya kutumia magogo kwa hiyo, wanapoweka makaa bado kuna vumbi linatoka ambalo linaathiri maeneo ya wananchi. Tumeagiza lifanyiwe kazi na wanabadilisha ma-boiler mapya ambayo yatakuja kabla ya mwezi wa 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nitumie nafasi hii kukiagiza kiwanda cha A to Z ambacho kimepewa maagizo mara kwa mara na watu wangu wa NEMC na bado hawajatekeleza, wanaendelea kutumia magogo. Tutakifuata na tutahakikisha kwamba, hii kazi haifanyiki tena. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uniruhusu nipitie baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, moja moja, kulingana na muda utakavyoruhusu. Ya kwanza ni Mheshimiwa Huviza, kwanza nimshukuru sana kwa mchango wake

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambao ni mzuri na uzoefu wake ambao amekuwa akiendelea kutupatia na tunashukuru sana kwa ushirikiano wake. Ametaka kujua je, ni lini mradi wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa utaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni kwamba, project idea form imeshaandaliwa na kukubaliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), *Global Environmental Facility*. Kinachofuata ni andiko la mradi ambao ukishapitishwa na GEF utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu una jumla ya Dola 1,500,000/. Na utafaidisha Mikoa ya Njombe, Mikoa ya Mbeya kwa maana ya Rungwe, Mkoa wa Ruvuma na Wilaya nyingine zinazohusika zilizo kandokando ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Natse, ameniomba tutembelee Bonde la Eyasi kwa ajili ya kwenda kukagua uharibifu ambao ulifanyika kule; namuahidi kwamba, tutafika na tutaangalia hali halisi na kutoa maelekezo kulingana na inavyotakiwa. Lakini nimuahidi kuwa maombi yake mengi yale ya kitaalamu tutayaandika, ili yaweze kupata ufanuzi ambao ni wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ametaka kufahamu kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ndiyo wasimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004. Je, ni ushauri gani ultolewa kwa Taasisi au Wizara husika kuhusu kupunguza au kusitisha matumizi ya mbolea ya viwandani, hasa kwa Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008, ofisi iliandaa mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya Bahari Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito, Mabwawa, ambapo ilielekeza kubainishwa maeneo yaliyoathiriwa na mbolea na dawa, kuimarisha matumizi sahihi na kuhamasisha matumizi ya mbolea asili. Mkakati huu unatekelezwa na wadau mbalimbali ikiwemo *TAMISEMI* na Wizara inayohusika na masuala ya Kilimo. Ofisi itawasiliana na Wizara husika, ili kupata taarifa za uharibifu wa ardhi utokanao na matumizi ya mbolea katika maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alitaka pia kujua wataalamu wa mazingira wamekuwa wakihudumia mikutano na makongamano ya kimataifa yanayohusu mabadiliko ya tabianchi. Je, ni kwa vipi ujuzi na uzoefu wao katika makongamano hayo umekuwa ukisaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, makongamano ni muhimu sana. Kuhudhuria kwao katika makongamano hayo ndiyo imesababisha sisi tunapata mgawo wa fedha wa kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyo kwenye randama, ikiwemo miradi ya *Mainstreaming, Environment and Climate Change*, ambayo ina Dola

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

milioni 732. Miradi miwili ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Ukanda wa Pwani yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 8.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi Chana; Ofisi inapaswa kujua matumizi ya kuni nchini je, kwa sasa Ofisi ina mpango gani wa kupunguza ukataji wa miti ya kuni nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji wa Miti inahimiza kila Halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka na kutenga maeneo ya mashamba ya miti kwa ajili ya kuni. Uhamasishaji wa matumizi ya nishati mbadala kama vile upepo na jua unaendelea kuhamasishwa. Na kama alivyoeleza Mheshimiwa Masele, namshukuru sana kwa ufanuzi wake, kupitia Wizara ya Nishati na Madini, Serikali inatekeleza mradi wa kufikisha nishati nafuu kwa wananchi ikiwa ni pamoja na zile za nishati mbadala. Aidha, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vya nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rebecca Michael; elimu kwa umma juu ya mkataba wa Nairobi. Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri unazingatiwa. Hata hivyo, elimu inatolewa kupitia utekelezaji wa mradi wa sekta ya mikakati ya Kitaifa, kama vile mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari ukanda wa pwani, maziwa na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zarina Shamte; hili nimeshalijibu.

Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye; ushauri kwa utafiti wa GMO uruhusiwe na marekebisho ya Kanuni yafanyike, kuruhusu kuanza kwa utafiti wa GMO nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili Serikali imeshaanza kulifanyia kazi. Na kwa kuanzia Serikali imeona ni vizuri ianze kwenye kuruhusu masuala ya utafiti na utafiti ule tu ambao unahu mazao ambayo binadamu hayatumii, ikiwemo mazao ya pamba. Na baada ya hapo itaendelea kutoa taratibu mbalimbali ili kusimamia zoezi zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, kwa niaba ya Kamati; kwamba Miradi ya Serikali haifanyi tathmini ya athari ya mazingira; kama inafanya je, DART ilifanya TAM au tathmini ya afya na mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 miradi yote, ikiwemo miradi ya Serikali, inatakiwa kufanya tathmini ya afya na mazingira, kupata hati ya mazingira ikiambatana na masharti ya utekelezaji. Baadhi ya miradi ya Serikali iliyofanya TAM ni kama ifuatavyo:- Miradi yote ya barabara kuu (*Trunk Roads*), miradi ya umeme, miradi ya kilimo. Sasa kwa mradi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

huu wa DART (mabasi yaendayo kasi) Dar-es-Salaam, pale Jangwani EIA ilifanyika na wale walipewa masharti ya kutimiza ili waweze kuendelea. Na Wataalamu wangu wa NEMC wametembelea wakagundua kwamba, yale masharti yamekiukwa na wameshawaandikia waweze kurekebisha. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, wakirekebisha wasiwasi huu ambao wanao Wabunge, hautakuwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Mnyika; kumekuwa na suala la wananchi kutupa taka hovyo njiani wakiwa katika vyombo vya usafiri. Serikali iandae Mkakati maalum wa kuelimisha umma juu ya utunzaji wa mazingira na pia kuweka matatangazo katika vituo vya mabasi na ndani ya vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza liliendesa kampeni ya kuelimisha madereva wa mabasi, makondakta na uongozi wa Kituo cha Mabasi cha Ubungo juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwa kutupata taka hovyo barabarani na ndani ya vyombo vya usafiri; elimu hii itatolewa katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko; uchafuzi wa mazingira na athari kwa afya za binadamu na mimea ikiwemo viumbe vingine, hususan kuhusiana na mgodi wa North Mara. Anauliza kwa nini, shule ya Nyabigena na wananchi wanaozunguka mgodi huo hawajahamishwa kutoka eneo hilo na kulipa fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa mambo yaliyokubalika kimsingi katika majadiliano ya pamoja kati ya uongozi wa Wilaya ya Tarime, uongozi wa Mgodi na NEMC ni kimsingi shule hizo kuhamishiwa maeneo mengine. Kwa hiyo, tutafuatilia kuona kwamba, ni kwa nini hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, naomba nisigongewe kengele ya pili. Tutaandaa Bango Kitita kwa kila hoja ambayo imetolewa na wabunge, ili waweze kupata ufanuzi wake kwa ndani. Na niendelee kuwashukuru sana kwa ushauri ambao wameutoa, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Asante. Mtoa Hoja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango, nasaha na ushauri walioutoa. Hoja yetu imechangiwa na Waheshimiwa 34 kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 16 kwa kuzungumza.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea labda niseme kwamba nilichowasilisha hapa ni utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 na maombi ya fedha ya mwaka 2014/2015. Sikuwasilisha mjadala unaohusu Muungano au Katiba ya nchi. Kwa hiyo yaliyofukuka, yaliyochimbuka inaonesha kwamba ni ile theory ya mjamzito anapoamua kula udongo au mkaa ni kwa sababu ana upungufu wa madini yanayopatikana kule na mwili unamtuma afanye hivyo. Kwa hiyo yaliyoibuka hapa inaonesha wazi kwamba Waheshimiwa Wabunge wana hamu ya mjadala wa aina hii. Sasa mwezi wa nane Waheshimiwa hauko mbali, naomba wote tuwepo huko ili tuendelee na mjadala huu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze sasa na hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Katika hoja hizo mengi ni ushauri, lakini mambo matatu makubwa tumetakiwa kuyafanya kazi. La kwanza ni kuongeza jitihada katika kuelimisha umma wa Watanzania pamoja na wanasiisa kuhusu mambo ya Muungano, hadhi yake, hali ilivyo sasa, changamoto zilizopo na hali ya baadae. Na hili pia limezungumziwa na Kambi ya Upinzani pia kwamba kuna haja ya kufanya hivyo. Lakini lingine ambalo tumetakiwa kulifanya kazi ni kurudi na kusimamia vyema ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar ambao kwa sasa hivi ujenzi ule umeonesha kuna hitilafu, kwa hiyo tumetakiwa kuzisimamia na kuhakikisha mkandarasi anazirekebisha na sisi tutafanya hivyo na tumeanza kufanya hivyo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine ni kusimamia usalama wa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ipo Zanzibar; kwamba nyuma ya ofisi hii kuna majengo mengine yanajengwa ambayo hayajakaa vizuri na usalama wa Ofisi ile.

Mheshimikwa Mwenyekiti, lakini yaliyobakia mengine kutoka Kamati ni maoni na ushauri na niseme tu kwamba tunayachukua na tutayafanya kazi. Baadhi ya maoni au baadhi ya ushauri tayari hata sisi tumeona na tumeanza kuyawekea bajeti yake ili tuweze kuyatekeleza. Kwa mfano, suala la kununua samani kwa ajili ya jengo jipya la Ofisi ya Makamu wa Rais pale Luthuli; lakini pia ya Zanzibar tayari kwenye bajeti yetu tumetenga milioni 400 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba tufanye mazungumzo; hili nimeshalijibu mazungumzo na mmiliki wa jengo lilipo pale kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Tumeanza mazungumzo sisi pamoja na Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati kule Zanzibar ili kuona uhalali wa yule aliyejenga na kama ana kibali na vipi tunaweza tukazungumza naye na tukaelewana ili kuhakikisha usalama wa pale.

Mheshuimiwa Mwenyekiki, lakini pia tumeshauriwa kutumia fursa ya utungaji wa Katiba mpya kuondosha kero zinazoukabili Muungano wetu sasa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hivi na tunasema kwamba fursa hiyo tutaitumia na wote kwa pamoja tuifanye kazi hiyo ili tuweze kuweka mambo mazuri katika Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie katika maoni na ushauri wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Lakini niseme kwamba yale yote ambayo yalihitaji majawabu na hasa yanayohusu mambo ya fedha, kiasi cha fedha kinachoingia Tanzania, mgawo wa Zanzibar, aina gani ya mgawo Zanzibar wanapata. Niwashukuru sana Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha kwa kutoa majawabu haya. Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mengine yaliyozungumzwa ni yale yale niliyosema kwamba yameletwa, yamezungumzwa, lakini si mahali pake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Zanzibar kuna msanii anaitwa Ali Kuniki. Ali Kuniki huchukua fulana ile *pull neck* anaivaa juu chini, chini juu ile mikono yeye ndiyo anatia miguu na katikati kukawa kuna tundu anatembea nayo. Lakini ili ikae inabidi atafute kamba afunge na ile fulani ifanye marinda ili iweze kukaa vizuri. Sasa nimetaa mfano huu kwamba Ali Kuniki anafanya vile ili kuvutia kuongeza hamasa kwenye usanii wake, lakini pia anatumia kile kifaa alichopewa visivyo. Sasa niseme tu kwamba haya mengine yote yaliyoandikwa kwenye Kambi ya Upinzani ni hiyo fulana ya Ali Kuniki kwamba yameletwa sipo lakini pia ni kutia bashasha katika usanii wa yale ambayo yalitakwa kuelezwaa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja aidha kwa maandishi au kwa kusema, na nianze na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari ambaye yeye aliunga mkono tu kwamba kero za Muungano zitatuliwe ili wananchi waishi kwa amani. Kama alivyoona ni kwamba tumejitahidi kufanya kazi hiyo. Lakini Mheshimiwa Ali Khamis Seif yeye amezungumzia kero za Muungano miaka hamsini haziishi tunajitahidi kuzifanya kazi. Lakini pia amesema mengine, Tanganyika kuvala koti la Tanzania, utungaji wa sheria na theluthi mbili kwenye Bunge. Haya yote naomba tuje tuyazungumze mwezi wa nane na siyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo yeye alikuwa na swali anasema kwa nini mambo au kero za Muungano zilizobaki hazimalizwi kwa haraka. Mfano; kero zinazohusu ajira, mgawanyo wa fedha na miradi kadhalika. Mheshimiwa Faith nikuambie tu kwamba tunajitahidi kuyafanya kazi, na hili la ajira kwa kiasi fulani tumelimaliza kwamba mwongozo wa mgao wa ajira umeshatoka na hata ukiangalia Rasimu ya mapendekezo ya Katiba kifungu cha 185 kinasema kwamba kuwe na uwiano wa ajira kwa Washirika wa Muungano, kwa hiyo hiyo inaonesha kwamba limetoka kwenye mazungumzo na sasa linakabiliwa Kikatiba.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khatib Said Haji Mbunge wa Konde yeye amesema kwamba Muungano umetimiza miaka 50, lakini uhai wake umepita kwenye misukosuko mingi. Ni kweli kuna malalamiko mengi kwa upande wa Zanzibar, niseme siyo Zanzibar peke yake hata upande wa pili wana malalamiko yao. Lakini alikuwa anauliza je, Zanzibar inashiriki vipi katika Afrika Mashariki? Labda nimjibu tu kwamba katika vikao vyote vya Afrika Mashariki Zanzibar inawakilishwa na matakwa ya Zanzibar yanazungumzwa kwa sababu Mawaziri wa wa Zanzibar wa sekta zisizo za Muungano wanashiriki wenyewe na wanapata nafasi ya kuzungumza mambo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anaendelea kuuliza kwamba je, mbona Tanzania Bara wana miradi ambayo imepelekwa Afrika Mashariki, mbona Zanzibar hakuna? Nimhakikishie tu kwamba kuna miradi minne ya Zanzibar iko kwenye hatua mbalimbali ndani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Khatibu pia ameuliza suala la Zanzibar kujunga na OIC, Tanzania iliahidi itafanya hivyo lakini haijafanya mpaka leo. Nimwambie tu kwamba mapendekezo ya Rasimu mpya ya Katiba kifungu cha 65(2) kinasema kwamba Washirika wa Muungano watakuwa na fursa ya kujunga na taasisi za kikanda na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Sululu Juma yeye amesisitiza kwamba elimu ya Muungano iendelee kutolewa. Tutafanya hivyo. Lakini pia vikao vya Kamati ya pamoja SMT na SMZ zishughulikie maamuzi ya vikao hivyo, kwa haraka tutajitahidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh yeye amezungumzia kwamba fedha zote zinazotoka SMT kwenda SMZ basi ofisi yetu izioneshe. Na niseme tu kwamba tunajitahidi kuonesha zile ambazo ziliwa zinapita ndani ya ofisi yetu, lakini tumeona kwamba kuna upungufu na tumejipanga kushirikiana na Wizara ya fedha na tumeshafanya mazungumzo kwamba fedha zote zinazokwenda SMZ kutoka kwenye maeneo tofauti tofauti basi tuelezwe ili nasi tuweze kuyaweka kwenye ripoti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, yeye ana masikitiko tu kwamba kero zimechukua muda mrefu na zinaleta vikwazo katika Muungano wetu. Nimwambie tu kwamba nyingi tumeshazifanyia kazi zimebakia chache ambazo kwa pamoja mimi binafsi huwiweka kwenye fungu la uchumi na ninaziita kero za uchumi. Kwa hiyo mara nyingine huwa ninasema kero tumezifanyia kazi, imebakia moja ya masuala ya kiuchumi. Sasa ninaposema hivyo wengine wanababaika, mbona umesema zimebakia moja lakini zikiandikwa zinaandikwa tatu au nne. Ukiwiweka pamoja zote zinakwenda kwenye masuala ya kiuchumi. Kwa hiyo zimebakia hizo na tutazifanyia kazi kadiri tutakavyoweza.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya TASAF: Mheshimiwa Mwanakhamis anasema kwamba iko haja wa Wabunge kujulishwa fedha na miradi ya TASAF inayoendeshwa katika maeneo yao. Niseme kwamba kama tulivyosema kwenye hotuba yetu kwamba kuna Wabunge wawili na wawakilishi wawili wanaingia katika Kamati ya Kitaifa ya TASAF kule Zanzibar au Kamati kuu ya TASAF kule Zanzibar na kwa hiyo nadhani tungewatumia Wabunge hao na wawakilishi kupata taarifa yanayoendelea ndani ya TASAF ingekuwa rahisi kwetu kujua kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nirudi tena kwa Mheshimiwa Khatib ambaye ametaka kujua vipi Balozi zetu za Tanzania zilizoko nje na ajira yake Mabalozi na Wafanyakazi mbona Zanzibar ina idadi ndogo! Nataka kukubaliana naye ni kweli na Mabalozi huwa idadi inakwenda inafika sita, inarudi inakuwa tatu kama sasa hivi. Lakini makubaliano tuliyozungumza, ajira katika Taasisi za Muungano ziwe 79 kwa 21, 79 kwa Tanzania Bara na 21 kwa Zanzibar. Kwa hiyo, pole pole formula hiyo itafanyiwa kazi na hasa kwa sababu suala la uwiano limeshawekwa kwenye mapendekezo ya Katiba kwa hiyo hakuna atakayeweza kukwepa, tutalitungia sheria na polepole tatizo hili litakuwa linaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Mnyika yeye ametoa ushauri anasema Ofisi yangu ni kiungo kizuri kati ya Serikali na masuala yanayozungumzwa kwenye Katiba ni masuala ambayo yananihusu kiasi kikubwa kwa hiyo amenitaka nichukue *initiative* za kuandaa vikao vya maridhiano ili kuona kwamba pande zote mbili tunazungumza, tunafikia muafaka na tunatunga Katiba yetu. Niseme tu kwamba hakuna anayekataa suluhu kama pande zote ziko tayari kufanya hili, sisi hatutaacha kuwa volunteer wa kukutanisha pande hizo ili mjadala wa Katiba uendelee na nchi yetu iweze kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, yeye amezungumzia Tume ya Pamoja ya Fedha kwamba yale mapendekezo yaliyoletwa hayajafanyiwa kazi. Nimuambie tu tunayafanyia kazi na muda si mrefu maamuzi yatatoka. Lakini pia amesema formula ya kugawana mapato ya Muungano ijulikane. Kwa kweli inajulikana formula ni 4.5 lakini ndani ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuna mapendekezo mengine maamuzi yatakayotoka 4.5 itabadilika.

Lakini pia kuna vigezo ambavyo vinatumika katika kufikia 4.5 au *five* au *eleven* na vigezo vyenyewe kwanza ni idadi ya watu ukilinganisha pande mbili za Muungano, lakini pia masawazisho au *investment*, uwiano wa mahitaji ya rasilimali, uzalishaji, biashara, matumizi ya bidhaa na huduma kwa pande zote mbili za Muungano, uwezo wa pato la Taifa na mapato ya Serikali, lakini pia

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

masawazisho ya mfumko wa bei hivyo ndivyo vigezo vinavyotumika ku-determine kama ni tatu, nne, tano au sita.

Mheshimikwa Mwenyhekikti, lakini pia aliuliza Ofisi ya Makamu wa Rais Tunguu lini itaanza kazi? Mheshimiwa Pindi na Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Rais Tunguu tayari imeanza kazi, kuna *private office* iko pale na mratibu wa mambo ya Muungano yuko pale na sisi tunapokwenda Zanzibar ndiyo Ofisi ambayo tunatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ametushauri kwamba tuweze kubuni miradi ili kuongeza kiwango cha fedha ili tuwe na upeo mkubwa wa kutekeleza mambo yetu, na ninakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwa Mheshimiwa Mnyaa ambaye amezungumzia kwanini kitabu cha hotuba asilimia 14 tu kimezungumzia Muungano na mambo yote yaliyobaki ni mazingira! Nimwambie tu kwamba anayeongoza Idara ya Muungano au sehemu ya Muungano ni mtu wa maneno machache lakini vitendo vingi, kwa hiyo sikuona haja ya kuweka porojo kubwa humu ndani, ila naomba uangalie yale ninayoyatendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Mheshimiwa Rashid ye ye amesema kwamba Muungano ni mzuri, unaleta nguvu ya kiuchumi na mshikamano lakini kero zilizopo katika Muungano unaleta sura ya mbaya. Nimhakikishie tu kwamba kero tutaziondosha, lakini uzuri zaidi wote tukikaa pamoja kuzijadili na kufikia pale tunapotaka kwenda kama alivyopendekeza vizuri Mheshimiwa Yusuph Salim amesema kwamba sasa ni wakati wa kuacha kutumia nguvu na ubabe wa Tanganyika kuitawala Zanzibar kitu ambacho hakipo, lakini amesema na badala yake tukae pamoja, tuyaweke wazi matatizo ya Muungano, tusameheane kwa yaliyopita na tuangalie mbele nini kinaweza kutupeleka pale tunapotaka katika kudumisha Muungano wetu. Haya ni mawazo mazuri sana na mimi namuunga mkono lakini tutayafanya wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo na misaada ya kibajeti limejibowi vizuri na Waziri wa Fedha. Lakini pia kuna masuala mengi yanayohusu Muungano, lakini niungane tu na Mheshimiwa Akunaay ambaye amesema kwamba haiwezekani Waziri wa Muungano kukaa hapa na kujibu yote yaliyoulizwa leo hapa kwa sababu siyo kikao husika na siyo mahali pake ila leo tunajadili bajeti. Lakini pia Mheshimiwa Mnyaa katika mchango wake wa maandishi ana *points* nzuri sana ambazo angesimama na kuzizungumza pengine angezifafanua vizuri, tungeweza kumuelewa na tukampatia majawabu, lakini aliposimama ametanguliza hamasa, kwa maandishi ametuandikia *point* nzuri, kwa hiyo tulishindwa kuzielewa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimejibu yote ambayo yameulizwa yanayohusiana na bajeti, yale yanayohusiana na hadhi ya Muungano, Katiba, nini, naomba tuje tuyazungumze baadae kwenye kikao husika na siyo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie na kijishairi kizuri ambacho ndugu yangu Yusuph ameniletea hapa. Kishairi kinasema "mwiba wa kifauongo ni mwiba usioshingo lakini watia vongo pale unapoingia". Sasa mimi nataka kumwambia, si mwiba tu wa kifauongo lakini kila kinachotoga kikiingia kinaacha vongo na kinaacha alama". (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaomba kutoa hoja. (Makofi)

### **WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Naafiki. (Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumekubaliana kwenye Kamati ya matumizi itakuwa ni dakika ishirini na tano kwa mujibu wa makubaliano na mujibu wa kanuni na kwenye vifungu saa moja. Tutatizama pale ambapo kuna nafasi basi tutajaribu kuongeza wajumbe. Isipokuwa wale ambao kwenye mshahara wa Waziri watakuwa na nia hiyo, basi mjaribu kupunguza mazungumzo ili kuwapa nafasi/fursa nyingine watu wengine waweze na wao kuchangia. Katibu!

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 26 – MAKAMU WA RAIS**

Kif. 1001 – Adminstration and  
HR Management.....Tshs.5,726,696,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na  
Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

#### **FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Kif.1001 – Adminstration and  
HR Management .....Tshs.2,930,465,000/=

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri, kama kawaida yetu kuna majina ambayo nilishapewa na vyama ikiwepo nafasi mkiweza kutumia muda vizuri tutaongeza Wabunge wengine, naanza Mheshimiwa Ali Kessy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika hotuba ya jana ya Mheshimiwa Celina Kombani alizungumzia kuhusu kero za Muungano kwamba Zanzibar watapata ajira asilimia 21 ya Wizara za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni asilimia 3 ya wakazi wote wa Jamhuri ya Muungano, vijana wetu wa Tanganyika wataenda kufanya kazi wapi kama watapata asilimia 21 mara saba zaidi? Hii ndiyo kero nyingine ya Muungano. Vijana wetu wanaosoma kuna vyuo vikuu zaidi ya 40, sekondari kila kata, watakwenda kufanya kazi wapi? Wawe kama watu wa Ethiopia wanaofia kwenye magari kule Morogoro? Nataka jibu. Hilo sitakubali, sikutakubali, sitakubali! Na ndugu zangu wa Tanzania Bara msikubali ajira asilimia 21 ziende Zanzibar, watoto wenu wataenda kufanya kazi wapi? Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika vikao tumekubaliana hilo, lakini Mheshimiwa Kessy, isimtishe kabisa asilimia 21. Kwa mfano, tukichukua Balozi zetu zote zilizoko nje zinazowakilisha Tanzania 34, asilimia 21 yake ni Balozi 7 tu ndiyo wanaotoka Zanzibar, kwa hiyo, wala siyo asilimia kubwa kiasi hicho na isimtishe.

Lakini lingine nataka akumbuke kwamba kwa muda mrefu Zanzibar haikuwa ikipata faida hii katika Muungano, kwa hiyo sasa tumeitetea tumekubaliana tumefikia hapo. Kwa hiyo unapoikataa kuliko kuwa na *rationale decision* itakuwa ni uchoyo tu Mheshimiwa Kessy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ubaguzi, tena ubaguzi. Kuna Wazanzibar wako Bara zaidi ya 800,000 na wenyewe utawaingiza wapi, wakapate ajira Zanzibar au watapata Tanzania Bara huku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli itabidi tupunguze vyuo vikuu, tufunge vyuo vikuu, songa mbele ya sekondari sasa itakuwa basi haitakubalika. Ajira asilimia 21 ni kubwa sana, na bado wako Wazanzibar zaidi ya 800,000 mpaka kule kwangu Nkasi wapo, hiyo haitakubalika, huu utakuwa ni ubaguzi tena ubaguzi wa tena wa hali ya juu. Sitakubali, mimi sitakubali, labda Wabunge wenzangu wakubali, lakini mimi najitoa. Wananchi wote mnisikilize mimi sikubali hilo wazo, sitakubali, sitakubali. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukukurupuka tu na asilimia hii bali kuna vigezo tulivitumia ndiyo maana tukafikia hapo. Sasa mnapofanya maamuzi kuna wanaokubali na wanaokataa lakini inategemea wengi ni wepi.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Shilingi kwa hilo jambo ipigiwe kura.

**MWENYEKITI:** Umechelewa Mheshimiwa Kessy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Lakini mimi nilishakataa sikubali, wananchi wanawasikia kule nyuma watajua Wabunge wengine wamekaa kimya bila kuniunga hoja hili jambo litaleta matatizo.

**MWENYEKITI:** Nakuomba uzime microphone yako. Mheshimiwa Mrema!

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa hii nafasi.

Nilitaka kumwambia Waziri wa Mazingira kwamba kule Vunjo, kule Njiapanda kuna kiwanda kina utata. Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi alimtuma Naibu Waziri wake akakitembelea na akasema yafuatayo:- Ujenzi wa kiwanda hicho umekiuka sheria za nchi, ikiwemo Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1969, Sheria ya Mipango Miji Na.8 ya mwaka 2007, Sheria ya Mamlaka ya Miji Na.8 ya 1982, Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira Na.20 ya mwaka 2004; na hivyo hakikustahili kupewa leseni kama ilivyofanyika. Akaendelea kwamba kitendo hicho kimesababisha usumbusu kwa wananchi wa Mji Mdogo wa Himo, hususan wananchi karibu na eneo la kiwanda.

Mimi nimeongea na Katibu Mkuu Wizara ya Mazingira jana akaniambia hajatoa leseni ya mazingira, nimeongea naye Januari akaniambia hajatoa leseni ya mazingira, hata jana akaniambia hajatoa leseni ya mazingira. Nikaongea na DED wa Moshi, akaniambia hajabadili matumizi ya ardhi ile kutoka kuwa ardhi ya makazi ya watu kuwa ardhi ya kiwanda. Sasa yule bwana anafanya biashara sasa hivi. Naomba kujua msimamo wa Serikali kwa sababu wale wananchi 148 wanaozunguka kiwanda hicho wanalamika, wanailani Serikali kwa kuwaletaa kiwanda katika mazingira yao wanayoishi. Sasa nini msimamo Mheshimiwa Waziri, kwanza hongera kwa kuteuliwa kwa sababu najua ni mtu muadilifu, unasema nini kuhusu jambo hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analoliongelea Mheshimiwa Mrema nalifahamu nimeliona pale ofisini. Kiwanda hicho kiliomba kifanyiwe tathmini ya athari ya mazingira, lakini watu wangu kupitia NEMC (Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira) lilikwenda pale, na ili mdau yejote afanyiwe tathmini ya athari ya mazingira lazima kwanza awe na hatimiliki ya ardhi ile. Kwa hiyo walipokwenda

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wakagundua kwamba hakuwa na kibali cha kumiliki ile ardhi, na NEMC wakafanya kazi zaidi ya kufutilia, wakagundua kama ni kweli hakuwa anamiliki lile eneo. Kwa hiyo, hakutakiwa kuanza kufanya zile shughuli, na kama anafanya hajapewa tathmini ya athari ya mazingira ambayo hutolewa na NEMC, atakuwa anafanya shughuli zake kinyume cha sheria.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa msimamo wako usiotetereka kwa sababu hilo jambo lilikuwa linatuletea mgogoro mkubwa sana watu kulaumu Chama cha Mapinduzi, kulaumu Serikali ya CCM wakiamini kwamba yule bwana amekwishapewa hati zote zinazohusika na kiwanda kile na yeze anatamba. Kwa hiyo, mimi nimeridhika na maelezo yako naomba sasa nitakapomaliza Bunge hili naenda kuwaambia wananchi wangu "hakijala kwao". Ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesimama kutaka kuomba ufanuzi kuhusu issue ya mazingira kwa sababu ni issue ambayo ni serious na kama tukileta mchezo baada ya muda mfupi nchi itakuwa na majanga na mvua zitakuwa hazinyeshi, tutaingia kwenye njaa na mambo mengine.

Naomba ufanuzi, kwa sababu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya ilioishia tarehe 31 Machi, 2012, ilisema Tanzania tunakata miti hekta 400,003 kwa mwaka. Ukurasa wa 25 wa ripoti inasema nchini Tanzania asilimia 4 tu ya misitu ina mipango ya usimamizi, na asilimia 96 inafanya kazi bila ya kuwa na mpango wowote. Kwa maana kwamba asilimia 96 ya misitu nchini kwetu watu wanakata, wanafanya vyovoyote na nini, hakuna mipango yoyote ya Serikali kuhusu rasimilia hii ya misitu.

Taarifa ya Mdhibiti inaeleza kwamba Wizara haina utaratibu mzuri wa kudhibiti utoaji wa leseni katika ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo nilibaini kuwa baadhi ya Wilaya zimetoa leseni za uvunaji bila kuwa na mipango ya usafirishaji wa mazao ya misitu, bila kuwa na mipango ya usimamizi wala ile ya uvunaji kwa mwaka. Kwa hiyo nchi hii ni kwamba hakuna mipango ya uvunaji misitu, na hapa tumeona hata kwenye taarifa ya Upinzani kwamba kwa mkaa peke yake tunatumia tani 2,650 kwa mwaka.

Sasa mimi ninaomba kupata ufanuzi, Serikali imefanya ripoti hii kazi gani? Itaendelea kuishi hivi bila kuwa na mipango ya misitu mpaka lini? Kwa sababu vitu hivi vinaisha, misitu inaisha? Mna mpango upi ninyi watu ambao tumewakabidhi toka mwaka 2012 mnafanya nini hapa? Natoa shilingi kwenye hili kama sijibowi vizuri. (Makofii)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mkosamali kwa kuguswa na suala la miti inavyozidi kupotea kwa kukatwa. Lakini nataka nimueleze kwamba utoaji wa vibali vya uvunaji wa miti asubiri kwenye hotuba itakayosomwa nadhani kesho, Maliasili na Utalii ndiyo wanaotoa vibali. Lakini niseme tu kwamba nadhani juhudzi za Serikali zipo za kuhakikisha kwamba wananchi hawatumii miti kwa ajili ya kuni wakawatafutia njia mbadala za kuweza kutumia kama nishati ambapo utaona kama alivyosema Mheshimiwa Masele kwamba tunasisitiza na tumeondoa VAT kwenye miradi yote au vifaa vyote vinatumia solar, wind ili ku-encourage tu kwamba watu watumie aina hiyo ya nishati ili wasiende kwenye kuvuna hiyo miti.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ni rahisi sana kujibu hivi na kusema kwamba subiri Wizara inayofuata. Hii Wizara kazi yake ni kutazama issues za mazingira, hii. Sasa unapoambiwa kwamba hekta 400,000 za misitu zinakatwa kwa mwaka ni kwamba baada ya miaka 10 tutakuwa na jangwa kwenye nchi hii, hapatakuwa na miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapoomba Serikali ilete mikakati yake ya kupambana na jambo hili ili tusije tukafikia sehemu kuna njaa, hakuna mvua hakuna nini, everything, baada ya miaka kumi tu unawaambia watupe mkakati mpango wao wa kunusuru jambo hili ili tusifike huko halafu tunajibiwa hivi. Wewe Mwenyekiti unaweza kuridhika kweli kujibiwa hivi wakati unaona kabisa jambo hili litatuathiri? Waziri rudia tena, jibu, mna mkakati gani wa kupunguza hii, kwa kipindi gani, kwa muda gani, kwa mikakati gani? Kwa sababu taarifa hii inasema hamna mpango wowote wa kushughulikia misitu ninyi na hii itatuathiri, sisi! Tujibu mipango yenu, hatujasikia mipango yenu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkosamali ana nia njema sana na ni kweli misitu inakatwa, lakini Kanuni zetu zinakataza kuwahisha shughuli. Sasa namuomba, nakuomba Mwenyekiti, kwa kuwa kesho utakalia Kiti, umruhusu aulize suala hili la mpango wa Serikali na namna inavyoweza kunusuru misitu na sera ya Serikali juu misitu aliulize keshokutwa wakati wa Bajeti ya Maliasili na Misitu. Kwa sababu kisera maana hapa tunazungumzia sera, hayo ni maswali ya kisera. Kisera, masuala ya misitu, upandaji wake, usimamizi wake, na uvunaji wake na kila kitu yanasmamiwa Wizara ya Maliasili. Nakuomba tu kama inawezekana umruhusu swali hili utakapokaa kwenye Kiti siku ya Maliasili apewa nafasi aulizwe. Kama litaingiliana na masuala ya mazingira, bado Waziri wa Mazingira atakuwepo atajibu, lakini kisera masuala haya ya ukataji na usimamizi wa misitu ni mambo ya misitu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, hoja yako ni ya msingi na unachosema ni sahihi kabisa, kama Taifa letu halikuanza kudhibiti mambo haya

tutaingia kwenye majanga makubwa sana. Hii hoja ni ya msingi na hakuna mtu anayeipinga na Serikali imekubali. Mimi nakuomba kesho Maliasili nipo, keshokutwa nipo, nitakuruhusu utoe hoja yako na kama unataka mshahara wa Waziri utaukamata kwenye Wizara inayohusika. Tunaichukua na nakuahidi tutalifanya kazi, ni issue ya msingi kabisa wala si suala la kubeza. Nashukuru sana kwa kuliona na naiomba Serikali m-take note kwenye hili kwa sababu *this is a very serious thing*, matokeo yake hata hizo Serikali tatu tunazozitaka hazitakuwepo vilevile. (Makofi/Kicheko)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru katika mchango wangu wa maandishi, ambapo Mheshimiwa Waziri alisema mzuri, lakini sikupata kufafanua. Ni kwamba katika Kamati ya Uchumi, Biashara na Viwanda nilimuuliza swali Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, ambalo linahusiana na deni la Taifa la trilioni 21 ambalo kila Mtanzania kabeba pamoja na sisi kule.

Halafu nikataka kujua thamani ya shilingi ya Tanzania inaposhuka, ambapo deni hili la Taifa na thamani ya shilingi ya Tanzania inaposhuka, inaathiri sana uchumi wa Zanzibar, sana kabisa kwa asilimia kubwa, na haya mambo yote yanababishwa na upande huu wa Jamhuri ya Muungano siyo Zanzibar. Nilitaka kujua tunafidiwa vipi Zanzibar katika masuala kama haya. Jibu lake ananiambia Zanzibar mnakopa Serikali kuitia Jamhuri ya Muungano na madeni hamlipi tunalipa sisi Jamhuri ya Muungano. Duu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo ndipo nilipokuwa nataka ufanuzi kwamba ikiwa jibu lake la mtu mzito kama huyo wa Wizara ya Fedha maana yake ni kama hisani tu tunafanyiwa Zanzibar, si haki yetu. Sasa kama ni hivyo ni hisani, basi tutizame mashirika yote ya Muungano ambayo Zanzibar hayajafaidika shilingi hata moja, tutizame sasa muda umefika wa miaka 50 hii ya Muungano, taasisi zote zile za Muungano zifanywe hesabu Zanzibar ilipwe haki na ilipe deni letu isiwe hisani hii ya kuwa tunasaidiwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, Hazina hapa inatoa fedha kuwekza katika mashirika na taasisi mbalimbali kama mtaji. Fedha zile zinapotolewa inakuwa gawio la Benki Kuu hiyo hiyo asilimia 4.5 ya Zanzibar bado halijafanywa zinatoka fedha ile na kwa maana hiyo fedha zile zinapowekezwa upande wa Tanganyika na fedha ya Zanzibar imo, kabisa. Kwa hiyo ina maana taasisi zozote, mashirika yote yasiyokuwa ya Muungano pia yanatumia asilimia 4.5 ya fedha ya Zanzibar hiyo hiyo wanayotaka, achia hiyo asilimia 11.02. Kwa maana hiyo sasa wakati umefika wa miaka 50 ifanywe hesabu ikiwa kuna Serikali tatu, ikiwa hizi mbili zilizopo, lakini zifanywe hesabu Zanzibar ifidiwe tuache kubewa tunakoonekana kama hisani. Naomba ufanuzi, la kwanza. Ngoja Mheshimiwa Lukuvi...(Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa moja tu!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Ni moja tu hili linaendelea la hesabu hizo hizo, la fedha.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Hayo ndiyo maneno!

Mheshimiwa Mwenyekiti, anatuambia Waziri bajeti hii anaomba bilioni 44.03 za kupelekwa Zanzibar, bajeti iliyopita bilioni 44.784 zilipelekwa Zanzibar. Ufafanuzi wa fedha hizo uko wapi? Kilichopo hapa ni bajeti *support* pamoja na CDCF, hizo nyingine zina matumizi gani? Nataka Waziri atupatie majibu ya hayo na kama sasa hivi wako tayari ili tusifadhiliwe kila siku. Ahsante. Na kama hatuna majibu leo kwa mara yangu ya kwanza katika Bunge hili natoa majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali lake la kwanza kuhusiana na vipi Zanzibar inafidiwa thamani ikishuka. Kawaida tunapochukua mikopo fedha ambazo hazijatumika kwa sababu tuna *implement* ile, fedha ambazo hazijatumika popote zilizopo, basi tunasaini *increment* zile fedha zinarudi zilikotoka. Tunakuwa na ile *component* ambayo sisi tumechukua. Kwa hiyo, inakuwa mara nyingi hakuna kufidiana. Mara nyingi kunakuwa hakuna kufidiana. Hilo moja.

Lakini la pili, sina uhakika kama tafsiri iliyokuwa imetolewa na Naibu Katibu Mkuu kwamba majibu yaliyotolewa ambayo yameletea tafsiri hiyo ya kuwa Zanzibar tunafadhiliwa, hapana, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa sababu kuna Serikali na *arrangement* zilizopo ni kwamba Zanzibar inachukua mikopo kupitia miradi mbalimbali yenyewe. Aidha, mradi ambao unakwenda *direct* Zanzibar, aidha kuna kuwa na miradi mingine ambayo inakuwa inatekelezwa katika sehemu ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania.

Kuna issue ya MIVAF nadhani juzi alizungumzwa. Ule ni mradi ambao unatekelezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na *component* ya Zanzibar. Kwa hiyo, pale tuna *implement* kutokana na mahitaji, Zanzibar inataka kutekeleza nini na upande wa pili wa Jamhuri unataka kutekeleza nini. Kwa hiyo, miradi kama hiyo tunakuwa tunaanza wakati wa *planning stage*. *Planning stage* very early mradi dhahiri MCC tumeanza katika hatua za awali

na katika component ambazo Zanzibar ilipata ni pamoja umeme na barabara. Huku kumetekelawa miradi ambayo ilikuwepo ya umeme na barabara na kule Zanzibar imetekelawa miradi hiyo.

Hivyo, hakuna ufadhili as such, hakuna ufadhili as such. Na tunapofanya debts sustainability assessments kama nilivyosema awali kwamba ni component yote ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekopa na si Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekopa, hususan deni la nje. Kwa hiyo, nadhani ni maeneo ambayo yanataka maelezo, lakini una hoja nzuri Mheshimiwa ambapo pengine tungeweza kukaa zaidi tukatafakari kwa umakini ili tuweze kuondoa hii migongano midogomidogo ambayo inaendelea kutokea na kwa sababu tu ya *misinformation*. Asante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, labda ungetusaidia hii sintofahamu waeleze Wabunge kutoka Zanzibar na waelezwe Wabunge wa hapa wajue hii kitu iwe clear. Hakuna sababu kila siku izungumzwe wakati majibu mazuri yapo kama hivyo ulivyosema. Just cristal clear kuwaeleza nchi nzima hali halisi ni hii toka miaka 50 contribution ni hii, mchango ni huu, Muungano wetu unakwenda hivi, mafanikio yetu yanakwenda hivi, changamoto zetu ni hizi, ili kila mtu ajue anaelwa vipi katika hili.

Mheshimiwa Waziri wa Mazingira una cha kuongeza? Muungano!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana sina kitu cha kuongeza. Nimshukuru Waziri wa Fedha kwamba ametoa maelezo mazuri. Lile ambalo umeliuliza sasa hivi, labda nieleze tu kwamba ofisi yangu kushirikiana na Wizara ya Fedha tutakuja na semina ya Wabunge hapa kuhusu mambo hayo. Kilichotoka, kilichokwenda, kilichotumika tutakuja na semina hiyo. Lakini nilikuwa nataka kuzungumzia lile la 44 billion ambalo Mheshimiwa Mnyaa ameuliza. Fedha zilizooneshwa kwenye kitabu cha bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais zilizokwenda Zanzibar ni za general budget support na contribution ya PAYE inayokwenda Zanzibar pamoja na Mfuko wa Jimbo.

Lakini, kuna fedha ambazo zimetajwa separately na hazikujumuishwa hapa na hizi ni fedha ambazo Mheshimiwa Waziri wa fedha amezizungumzia zile za miradi ya pamoja tunayofanya kama Tanzania, TASAF, Maendeleo ya Kilimo, Maendeleo ya Mifugo, Millennium Challenge Account. Ukisoma kitabu utaziona ziko peke yake peke yake. Kwa hiyo, hizo 44 billion kwa mwaka zina component hizi tatu, Mfuko wa Jimbo, PAYE na GBS.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa lile la fedha hoja ilikuwa deni hili la Taifa ambalo linakopwa na upande mmoja mkubwa wa Muungano ndiyo uanotumia, sisi kule ni component ndogo sana, sana kabisa *minimum*. Tunafidiwa vipi pamoja na devaluation, hilo halijajibiwa Waziri wa Fedha hajajibu. Ametoa maelezo ya mambo mengine kuhusu jibu la Naibu Katibu Mkuu. Hii hoja tunafidiwa vipi Zanzibar, tunaingia katika hasara ambayo haituhusu! Sasa tunafidiwa vipi Zanzibar? Hili linataka maelezo na hii ya bilioni 44 hii PAYE, PAYE ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zikiletwa katika miradi ya Zanzibar, tumesema hapa mara nyingi sana, Wabunge washirikishwe, hiyo miradi ya TASAF inayozunguzmwa, miradi yote hiyo ya MIVAF, kila aina ya miradi Wabunge hawajui wala hakuna ufanuzi. Hata katika randama imeandikwa tu mgawo wa kibajeti, PAYE pamoja na Mfuko wa Jimbo. Hii PAYE, PAYE gani na hizi ni shilingi bilioni 21, PAYE gani? Tunaomba ufanuzi, ufanue Mheshimiwa Waziri, PAYE gani hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kabla ya ufanuzi kwamba, Waheshimiwa Wabunge basi na sisi tuwe na *interest* ya kujua mambo. Hili la PAYE; PAYE ni pay as you earn, hii ni kodi ya mishahara inayokatwa kwa wafanyakazi wa taasisi za Muungano ambao baada ya makusanyo yote ya mwezi, 4.5 ya kilichokusanya kinakwenda Zanzibar. Huwa tunapeleka shilingi bilioni 1.75 kila mwezi na kwa mwaka zinakuwa kama shilingi bilioni 21, hiyo ndiyo PAYE. Nadhani nimesema vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa ngoja nikuite basi! Waziri wa Fedha!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Labda Mheshimiwa Mnyaa tuelewane jambo moja, Zanzibar imo katka sehemu ya lile deni na Zanzibar haichangi katika kulipa lile deni. Kwa hiyo, ile *principal* pamoja na *interest* inayolipwa ni pamoja na miradi ile ya Zanzibar iliyochukuliwa ambayo iko kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa napata shida kuelewa Zanzibar tunafidiwa vipi katika kitu ambacho kimebebwaa, yaani tunalipa pamoja na ile miradi ambayo tulikuwa tumechukua. Sasa hiyo fidia nakuwa napata tabu kuelewa, iweje, au pengine labda anaweza akatupa *insight* zaidi unavyotaka wewe iwe kama ndiyo *reality* yenyewe ilivyo. Kwa sasa deni linalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania pamoja na miradi yote ambayo ilikopwa kwa ajili ya Zanzibar, miradi yote ambayo imekopwa kwa ajili ya Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba Waziri hajajua fidia ipi inayohitajika mpaka hivi sasa na kwamba haelewi, na hapa hakuna haja ya miwani wala darubini. Kwamba uchumi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya ukubwa wa Tanganyika na kwa sababu ya kutumia fedha moja ya Tanzania, ni kwamba Zanzibar tunaburuzwa kiasi kwamba uchumi wa Zanzibar tukitaka kujitanua hatutanuki kwa sababu ya huku na ni kwa sababu ya deni la Taifa, ni kwa sababu ya thamani ya shilingi kudondoshwa kila siku.

Sasa hizi gharama ambazo sisi hatupati kujitanua kwa sababu ya kutumia fedha moja na uchumi mkubwa huku ndiyo unafanya kila kitu, sisi tutafidiwa vipi Zanzibar ili na sisi tuweze kutembea kwa miguu yetu wakati hizi adha zinazotufika siyo sisi tunaosababisha zinasababishwa na upande wa Tanganyika. Hujanielewa Mheshimiwa Waziri? Mshahara bado nazua, nataka ufanuzi wa kina ili miaka yote ambayo tumeathirika ya devaluation ya fedha, mwaka 1978/79 thamani ya shilingi za Tanzania shilingi saba ndiyo dola moja ya Kimarekani. Leo mwaka 2014 shilingi 1600 ni dola moja ya Kimarekani, hili lote limesababishwa na upande wa Tanganyika. Zainzibar tumeburuzwa tumesababishwa kuingizwa huko tutafidiwa vipi?(Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hebu jibu hiyo fidia iko vipi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa hatuwezi ku-calculate fidia, hayo ni mambo ya kisera ambayo pengine tungeweza kuyazungumza katika Bunge la Katiba na siyo hapa ambapo tunaweza tukajibu kwa sababu hilo zoezi halijafanyika, hilo zoezi halijafanyika na kwa sasa hatutaweza kuzungumza masuala ya fidia kwa sababu nadhani huko ndiko ambako tungeweza kitaalam, technically hasa kuweza kuzungumza masuala hayo, component hii ikaingia hasa katika Katiba mpya ambayo tungeweza kujadili. Si suala la Wizara ya Fedha, si suala la Muungano, lakini liwe ni suala la kikatiba zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage, dakika tatu!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tatu, nimesimama kuwasihhi Wabunge wenzangu especially Mr. Mnyaa, tusilete ajenda mpya. Hakuna mtu kamuumiza mwenzie, depreciation ya shilingi mimi nakubali Zanzibar najua, najua strength ya Zanzibar, sasa utujengee hoja utuonyeshe kwamba, Zanzibar kipi hicho kilichozalishwa ambacho kingefanya shilingi yako appreciate lakini utukumbushe kwamba Zanzibar karafuu yetu ya Zanzibar ilianguka kama ambavyo mazao yote yalianguka kwenye trade trap

ya mazao yote. Kitu gani ambacho kinakufanya wewe ungepata uchumi mkubwa. Uchumi wetu sisi ni wa Watanzania wote nafuu yote. Tusijiburuze kwenda kwenye suala ambalo halihusiki. Karafuu ilidondoka, kila mtu anajua, mbata zilianguka kila mtu anajua. Kwa nini mnatureleka nje ya ajenda? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa hitimisha hoja yako!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijahitimisha natoa shilingi sasa na ninawaomba...natoa shilingi katika mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Aha haa, Mheshimiwa Mnyaa, hebu kaa kwanza, please kaa. Mheshimiwa Mnyaa wewe ni mzoefu sana kwenye Bunge hili, umeishatoa shilingi, umesema nimemruhusu Mwijage ambaye siyo... hapa tunakwenda kwa kanuni lazima tuwe fair, wewe ni mzoefu sana humu ndani. Sasa hitimisha hoja yako. Unakamata shilingi au unairudisha shilingi ndiyo nililotaka kujua mimi hilo.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilikuwa natoa maelezo, sasa naikamata shilingi, naomba jambo hili lijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimwia Mnyaa, ulishatoa shilingi yako mapema. No no no no!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa usitubuluze!

**MWENYEKITI:** Sikuburuzi! Nakuheshimu sana Mheshimiwa Mnyaa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninakuheshimu. Unatuburuza sasa!

**MWENYEKITI:** Mimi sikuburuzi, hansards zipo, unaweza kwenda kwenye hansard, ulishatoa shilingi, na mimi hapa kazi yangu kama nilivyokuambia mimi siyo kocha mimi ni referee! (Makofi)

Mheshimiwa Mnyaa hitimisha hoja yako, unakamata shillingi au unairudisha?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakamata shilingi.

**MWENYEKITI:** Yamekwisha basi!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Hayajaisha, sasa nitoe maelezo si alitaka ufanuzi!

**MWENYEKITI:** Haya endelea, endelea!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nikisema suala hili la kiuchumu, Zanzibar imejaribu kutaka kujitanua kiuchumi, kikwazo imekuwa ni upande wa Tanzania Bara. Itakubukwa wakati wa Rais Salmin alitangaza bandari huru, alitaka kufanya offshore banking, alijenga uchumi kupitia EPZ, wawekezaji wakaja Zanzibar...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, toa hoja yako, unajua unaanza mjadala upya kabisa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si unataka nifafanue Zanzibarimeathirika vipi?

**MWENYEKITI:** Hitimisha, hapana. Mheshimiwa Mnyaa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mwijage alitaka nifafanue Zanzibarimeathirika vipi kiuchumi, sasa ndiyo nafafanua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa nakupa dakika mbili basi!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo viwanda vyote, viwanda vidogo vidogo katika EPZ kila biashara iliyotumika wakileta vitu kusafirisha upande wa Tanzania Bara TRA wanavizuia wakasababisha wawekezaji wale wote waondeke na EPZ matokeo yake ikazuiliwa kule ikafunguliwa huku Tanzania Bara.

Sasa hiyo ni mifano ambayo sisi kila uchumi unapokuja karafuu, imepanda bei na kama hajui Mheshimiwa Mwijage pishi moja ya karafuu sasa hivi ni pesa nyingi sana zaidi ya mara nne tano, lakini bado thamani ya pesa yetu inakuwa chini. Sasa hata karafuu ikipanda bei, tukijaribu kujinasua kiviwanda, kila tunachofanya hatuendi kwa sababu ya devaluation ya shilingi ya Tanzania ambayo prime mover ni upande wa Tanganyika. Sasa hivyo ndiyo Zanzibar tunavyoathirika. Tunahitaji na sisi kufidiwa na tatizo hili. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, umeelewa, kwenye semina mtaelezana zaidi. Sasa nitawahoji!

(Haja Ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu niliomba ufanuzi kuhusu mradi ambao haukuwa na namba na ulitengewa shilingi 2,893,755,000/=. Kwa hiyo, nilihitaji tofauti ya bilioni moja plus nipaye ufanuzi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuliangalia hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kilicho jitokeza ni kwamba wakati hizi randama zinaandaliwa Dar es Salaam tulikuwa hatujapata ile final ya ceiling ya fedha, lakini baada ya kupata ile final, ile fedha sasa, kile kipengele cha climate inakwenda kwenye shilingi 1,393,775,000/=. Aangalie kwenye randama ukurasa wa mwisho kabisa, page ya mwisho kutakuwa na table ambayo sasa ina figure ambazo ni sahihi ambazo zinalingana na kwenye kitabu cha Hazina.

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa ngapi huo? Kwenye randama ndiyo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Ukurasa wa mwisho.

**MWENYEKITI:** Sehemu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Kuna jedwali, matumizi ya maendeleo.

**MWENYEKITI:** Okay ni mradi upi? Sustainable finance environmental management!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Ndiyo Mheshimiwa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Natse!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijamaliza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Ngoja nimalizie. Ni Fungu 5301 - climate change adaptation programme jumla shilingi 1,393,755,000/=. Kwenye table mwishoni kule.

**MWENYEKITI:** Mbona hapa kwetu hamna?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Ngoja ngoja, sawa, ngoja twende pamoja. Endelea!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwenye jedwali la mwisho kabisa la randama.

**MWENYEKITI:** Hapa mezani hamna ndiyo maana tunapata tabu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Bahati mbaya hiyo.

**MWENYEKITI:** Tunapata tabu randama hakuna na kuna mbu hapa wanatusumbua...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi huo...

**MWENYEKITI:** Haya maradhi ya sasa hivi. (Vicheko)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo kwenye kitabu cha maendeleo ipo kwenye environment imeandikwa, hii ni vote 5301, ukurasa wa 31 - climate change adaptation programme una shilingi 1,393,755,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Natse, Meza ilikuwa inajaribu kuthibitisha na sisi tumesharidhika hapa, bado wewe.

**MHE. MCH. ISRAEL YOHANA NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Baada ya kuangalia randama yao ambayo ina tofauti sasa siyo bilioni moja tu. Ukifanya mahesabu ina tofauti ya bilioni moja na milioni mia tano. Kile kitabu cha maendeleo (*volume iv*) ambacho sasa Mheshimiwa Waziri ameeleza shilingi 1,393,755,000/= ukitoa shilingi 2,893,755,000/=, kuna un-accounted for ya fedha ya 1,500,000,000/=.

Sasa nina angalia randama hii ambayo ndiyo wameweka hapa na kufanya kazi, juu ya 2,893,755,000/= ukurasa wa 47 wa randama yao. Hii wamesema kiasi cha shilingi 2,540,755,000/= ni fedha za nje na 300,353,000/= ni fedha za ndani. Sasa hoja yangu ya msingi ambayo Mwenyekiti unasema unashawishika ukiangalia mwisho wa jedwali la mwisho randama hiyo hiyo, bado mimi inanipa mashaka ya mahesabu haya, kwamba kuna un-accounted for ya shilingi 1,500,000,000/= na nisipopata maelezo sahihi nitatoa shilingi, Mheshimiwa Waziri!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kukubaliana ukweli ulipo. Nasema kwamba, wakati tunaandaa randama tuliweka matazamio kabla ceiling ya mwisho ilikuwa haijatolewa na tuliamini kwamba itakuwa hivyo. Kwa hiyo, hicho anachokiona kwamba yeye kinazidi ilikuwa ni hayo matazamio.

Sasa nataka yeye na mimi, cha kutumia na ambacho tutakifuatilia kwenye utekelezaji, ni lile jedwali la mwisho kwenye randama, ambalo lipo kwenye Kitabu cha Maendeleo. Hiyo ndiyo concern ambayo nataka tukubaliane kwamba, tunatekeleza hii kwenye jedwali hili ambayo inaoana na hii hapa. Yale ya ndani tutakwenda kuyarekebisha ili yaweze ku-fit kwenye hizi fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Natse, nafikiri Mheshimiwa amejieleza vizuri tu.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa maelezo hayo, ninarudisha shilingi ya Waziri. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Ester Bulaya!

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu dakika 25 umekwisha kabisa, najaribu tu kuwaliza wale wote walioteuliwa na chama. Majina yote yaliyokuja hapa tutayamaliza, lakini hatutakuwa na nafasi ya Wajumbe wengine.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika Ripoti yetu ya Kamati, maana mimi ni-declare interest ni mjambe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, tulizungumzia na tuliishauri Serikali kuchukua hatua kwa watu wote waliokiu ujenzi katika fukwe au ujenzi usiozingatia taratibu za kisheria. Tulifanya hivi kwa sababu Kamati ilifanya ziara na tukaona athari ambazo zinajitokeza kwa baadhi ya watu kukiuka taratibu na kuvunja sheria za mazingira, kuziba, kujenga katika kingo za mito na ndani ya mita 60, kinyume na taratibu na Sheria ya Mazingira. Kamati ikatoa agizo, nyumba hizo zivunjwe, lakini mpaka leo agizo hilo halijatekelezwa.

Moja ya athari ya kuacha watu kujenga nyumba ovyo kweye maeneo ambayo hayaruhusiwi ni mafuriko na lingine lipo Jimboni kwako, Mtaa wa Indir Ghandi ambapo watu wamekufa. Moja ya sababu ambazo Mheshimiwa Waziri ametuambia, kwamba, kesi zipo mahakamani na akasema tunafuata utaratibu wa kisheria; ni utaratibu gani ambaa unafuatwa kwa upande mmoja?

Bunge hili nalo ni Mhimili mwengine na lina jukumu la kutunga sheria na sheria zinazotungwa na Bunge hili ndiyo zinazosimamiwa na Serikali. Sasa iweje

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutekeleza sheria kwa upande mwingine iwe kosa, lakini wengine kuacha kutekeleza sheria kwa sababu ya Mhimili mwingine iwe sahihi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanataka kutumia nyadhifa zao vibaya, kuona wao wako juu ya sheria kwa kigezo cha mahakama. Hilo mimi siliafiki, pamoja na Wajumbe wa Kamati hawaliafiki, kwa sababu kuacha watu watumie uhuru wa mahakama vibaya, madhara yake ni makubwa.

Tumeona watu wamekufa pale, mahakama imetoa amri, jengo lile la Indira Ghandi livunjwe na nisipopata majibu mazuri nitaondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, *with due respect*, Waziri amejibu vizuri tu, wamelifuatilia, issue ipo Mahakamani. Bunge linatunga Sheria, Mahakama inatekeleza Sheria, *simple as that*. Sasa hata sioni kama kuna argument kweli ya kumfanya Waziri umtolee shilingi *for nothing!* Wewe msomi, kijana, you know these things. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nafahamu concern ya Mheshimiwa Ester Bulaya pamoja na Wajumbe kwamba, ni kweli haipendezi kwamba, mtu amevenja sheria, lakini mnapotaka kwenda kuvunja nyumba inaonekana wengine wanakubali na wengine hawakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba, NEMC wanatekeleza sheria na pale walipobaini haya matatizo walivunja zile nyumba, lakini bado wale watu waliokuwa wanavujiwa, wengine walikimbilia Mahakamani akiwepo na huyo ambaye nimemsema. Akikimbilia Mahakamani, katika utaratibu wa utawala bora huwezi ukamzuia na alipokwenda mahakamani, sisi tulishinda, lakini akaenda ku-appeal. Kwa hiyo, alipo-appeal, kesi iko mahakamani inasikilizwa tarehe 25 Juni.

Sasa hapa hatuna namna, lakini ninachotaka kumhakikishia ni kwamba, tutaendelea kusimamia na wale ambao wamekiuka tutatekeleza Sheria ya Mazingira kama inavyosema.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe muda Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni mgeni katika hii Wizara, lakini ajue kwamba, kuna haja ya suala hili kulifuatilia kwa kina. Hakuna mtu aliyejikuwa juu ya sheria na wala tusitumie mwanya wa watu kutumia Mahakama vibaya. Watu wote tunaiheshimu Mahakama, lakini vilevile hili Bunge lina mamlaka, linatunga sheria na lazima sheria zake zifuatwe.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, gawio la asilimia 4.5 la Zanzibar, naomba nifafanuliwe na ninaomba niseme yafuatayo ili nipewe ufanuzi sawasawa:-

Hapa nilipo nina maelezo ya Waziri Samia Suluhu Hassan na nina maelezo ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Waziri Samia Suluhu Hassan ameieleza Kamati, yeye aliileta kwenye Kamati kwamba, kuhusu mgawanyo wa fedha zinazotoka kwa wafadhili, upo utaratibu wa mgawanyo wake, ambapo kwa upande wa misaada na mikopo ya kibajeti, isiyokuwa na masharti maalum, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hupata gaiwo la asilimia 4.5. Haya ni maneno ya Waziri Samia Shuluhu Hassan, siyo ya Tundu Lissu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na akasema kwenye maelezo yake kwamba, kwa mwaka huu wa fedha, Zanzibar ilitengewa shilingi bilioni 32, imepata bilioni 27. Sasa ili tujue hizi zimetokea wapi, zimekuwa *calculated on what basis*, kwa sababu maelezo ya Waziri, hayajasema jumla ya fedha zote za misaada na mikopo ya kibajeti, inabidi twende kwenye maelezo ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Maelezo ya Waziri wa Fedha yapo kwenye ukurasa wa tatu wa Hotuba yake, inasema; misaada na mikopo nafuu ya kutoka nje, shilingi bilioni 1,163.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 20 wa maelezo ya Waziri wa Fedha na Uchumi, misaada na mikopo ya kibajeti shilingi bilioni 922. Hizi ndizo takwimu nilizotumia mimi, sijatumia zingine zozote. Sasa uki-*calculate* gawio la asilimia 4.5, kwa mujibu wa maelezo haya ya Waziri, unakuta kilichotolewa mwaka huu wa fedha, shilingi bilioni 32, Zanzibar imepunjwa shilingi bilioni 20. Zilizotolewa ni bilioni 27, ilitakiwa zitolewe bilioni 52.335. Zimetolewa bilioni 27, Zanzibar imepigwa bao shilingi bilioni 25 za mwaka huu peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maeneo hayo ya Mawaziri; mwaka ujao wa fedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi anasema, misaada na mikopo ya kibajeti itakuwa shilingi bilioni mia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, umejieleza vizuri na una hoja ya msingi, nakubaliana na wewe. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tupe majibu kama kuna upungufu umepungua hesabu nini, warudishieni au kama hakuna majibu tuambieni. (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hakuna upungufu wa hesabu, nilitoa maelezo kwamba, wakati tunatoa maelezo kibajeti, tunasema misaada na mikopo ya kibajeti ambayo tunatarajia kuipata ni fedha kadhaa, general. Tukumbuke kwamba, hii ni commitment ya donor, yaani donor anaji-commit, lakini most of the time inakuwa actual disbursement siyo sawasawa na ile commitment. Kwa hiyo, hiyo kwanza tuone tofauti.

Tofauti nyingine, katika ile jumla ya *commitment*, kuna portion, yaani mikopo na misaada ambayo ina masharti maalum, tunasema earmarked, haiendi Zanzibar. Kinachokwenda Zanzibar ni ile *unearmarked*; yaani katika ile *list*, kwa mfano, una 900, ndani yake unaondoa ile ambayo earmarked unaweka pembeni na ile *total* ya *unearmarked* ndiyo asilimia 4.5 inakwenda Zanzibar. Kwa hiyo, hiyo ni hesabu sahihi, umechukua *calculations*, lakini umechanganya na mambo mengine.

Kuna jambo ambalo tunaita misaada na mikopo nafuu, hii inakuwa siyo ya kibajeti, ambayo hakuna utaratibu wa kupeleka 4.5 Zanzibar. Isipokuwa kama kuna misaada na mikopo ambayo ipo inatekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo ambayo inakwenda Zanzibar na hii inakwenda based on the needs, yaani na mahitaji. Nimetoa mifano Miradi kama MIVAF, ndiyo ambayo based on the needs, ndiyo inakwenda Zanzibar. Nadhani, nakuelewa, lakini kuna vitu viwili ambavyo umevichanganya. Kwa hiyo, kinachokwenda hapa ni asilimia 4.5 ya general budget support ya unearmarked general budget support, nayo mpaka hivi tunapozungumza, kuna asilimia kubwa sana bado haijatolewa. Once ikitolewa, kinachokwenda Zanzibar, kitakwenda Zanzibar.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme nitatoa shilingi kwa sababu hizi ni porojo. Kwenye maelezo ya Waziri Mkuya, kuna misaada na mikopo ya kibajeti, halafu kuna misaada na mikopo ya Miradi, kuna misaada ya mikopo ya basket fund, sijagusia huko. Nazungumza mikopo na misaada ya kibajeti, ambayo kwa maneno yake ni shilingi bilioni mia tisa ishirini na mbili, kwa mwaka ujao wa fedha. Ambayo kwa maneno yake, kwa takwimu zake, kwa mwaka huu unaoisha tumeletewa, hajasema hii ni commitment, amesema hizi ni za mwaka huu ambazo zimekuja, bilioni 1,163.

Sasa anasema hapa kwamba, hii ni commitment; kama ni tofauti na actual disbursement, my point is, kama ni commitment, hiyo actual disbursement ni kiasi gani, ambayo hamjaionesha hapa, kwa sababu haipo hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye hoja hii hii na ni very important, kama matazamio ya mwaka ujao ni bilioni 922, then matazamio ya gawio la Zanzibar liwe asilimia 4.5 ya hilo tazamio la the total sum. Ukiangalia kwa utaratibu huo, asilimia 4.5 ya bilioni 922, ni bilioni 44, lakini maelezo ya Waziri Samia Suluhu anasema, mwaka ujao Zanzibar itapata bilioni 21! Inatakiwa ipate on the basis ya asilimia 4.5 ya bilioni 922, inatakiwa ipate bilioni 44, haitapata hiyo. (Makofi)

Last year haikupata na ndiyo maana tumesema,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, sasa toa hoja yako ili na wengine wachangie.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, watuambie, hii ya mwaka huu unaoisha, *actual disbursement* iliyoletwa ni kiasi gani ili tujue kama Zanzibar imepata fedha yake halali? (*Makofij*)

La pili, kwa nini hawajaweka asilimia 4.5 kwa hii inayotazamiwa mwaka ujao wa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, kama nilivyokwambia mwanzo, una hoja ya msingi, issue ya kuondoa shilingi hapa ni kupitisha bajeti, itakuwa haina tena presidency yoyote huko mbele. Wewe una hoja ya msingi, cha msingi hoja yako Serikali imeisikia itaichukua, wewe kaa nao hakikisha hii kitu inapatikana. Subirini, wewe Matiku kaa kimya! (*Kicheko*)

Kwa sababu tutapiga kura hapa, *and then the end of it*, hii siyo sahihi. Una kitu cha msingi, kama kuna kitu ambacho kinapungua na labda upande wa Serikali wamepitwa, umewaonesha jamani, kuna kitu hiki bado hakijafanikiwa, kinatakiwa kiwe hivi na hivi!

Sasa hii haina sababu tusimame tuenze kujadili kitu, mimi nakuomba na mimi nina-guarantee kuwa nitazungumza na Kamati ya Bajeti, nitazungumza na Serikali, hoja yako ipokelewe, itazamwe upya, *and then*, kama kuna pungufu ambayo ilikuwa haiendi Zanzibar, iende! *This is what is government is for!* Sawa umekubali? Nakuruhusu, mrudishie Waziri akatumie fedha yake na mumewe.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nirudishe shilingi, lakini kama ambavyo nimeomba kwenye maelezo yangu ya msingi na Waziri amesema, tunahitaji Bunge lako liletewe takwimu za fedha zote za *budget support* za Jamhuri ya Muungano na fedha zote ambazo zimepelekwa Zanzibar kwa kipindi cha miaka kumi, ili tujue kama hakujawa na wizi hapa. (*Makofij*)

Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, nafikiri Waziri wa Fedha umesikia, lipokee hilo. Wewe kaa tu huna haja ya kujibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit .... .... Sh. 326,113,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003-Policy and Planning Division ... .... Sh. 828,198,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Nipo kwenye Kasma 270700 - *Rental Expenses*, ambayo mwaka jana ilitengewa shilingi milioni 31 na ushee na mwaka huu...

**MWENYEKITI:** Samahani, hebu rudia tena hicho kifungu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Kasma 220700 - *Rental Expenses*, gharama za kodi ya pango. Mwaka jana ilitengewa shilingi milioni 31, mwaka huu imeongezewa zimefika milioni 51, yaani milioni 20 zimeongezeka kwenye masuala ya pango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye maelezo sasa ya kina, pango maana yake nini? Kwa tafsiri ilivyotafsiriwa pango kwa minajiri ya Ofisi ya Makamu wa Rais hapa, kwenye kifungu hiki, ni pamoja na kulipia gharama za kumbi za mikutano, kwa ajili ya warsha mbalimbali zinazoendeshwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Wanasema kwamba, fedha zimeongezeka kwa sababu safari hii Ofisi ya Makamu wa Rais itaongeza viwango vya warsha hizo kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira.

Sasa niliomba ufanuzi kwa maandishi na nilitoa rai kwa Wizara kwamba, katika mapitio hayo ya Sera ya Mazingira, nipewe hakikisho ya mazingira maalum ya Dar es Salaam, ambapo kutokana na mabadiliko ya tabianchi sasa hivi, Dar es Salaam limekuwa ni Jiji la maafa ya mafuriko. Mazingira maalum ya Dar es Salaam, kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu, uwezo wa Halmshauri kuhimili usafi wa mazingira umekuwa dhaifu. Mazingira maalum ya Dar es Salaam, kutokana na ongezeko kubwa la viwanda, kumekuwa na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikataka nihakikishiwe kwamba, kama hii nyongeza itatumika kufanya hayo na kwamba kama hii nyongeza haitatumika kufanya hayo, nitaomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi, hizi fedha zitoke kutoka kwenye warsha zisizokuwa na tija, badala yake zielekezwe kwenye kazi halisi ya usimamizi wa mazingira. Kwa hiyo, naomba ufanuzi na kama sitaridhika nitaondoa shilingi katika sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna ongezeko kutoka milioni 31 kwenda 51. Kiasi hiki kimeongezeka kutokana na kazi zilizopangwa mwaka huu, ikiwemo mchakato wa mapitio ya Sera ya Mazingira. Sehemu kubwa ya kazi inafanywa nje ya ofisi, kwa hiyo, tunahitaji kuwa na maeneo ya kufanya kazi (kumbi). Kama unavyofahamu, kazi ya kupitia Sera ya Mazingira, lazima ushirikishe wadau mbalimbali ili muweze kukubaliana maeneo kwa maeneo na hasa eneo hili gumu ambalo analiongelea Mheshimiwa Mnyika la madadiliko ya tabianchi ambayo yamesabisha matatizo mengi, hasa kwa Dar es Salaam miundombinu kuharibika na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii siyo kazi ya siku moja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nisiondoe shilingi katika eneo hili, ninaomba *commitment* ya Waziri, kwamba, katika huo mchakato wa *consultation* ya wadau, kwa sababu ya mazingira maalum ya Dar es Salaam na ninazungumza hili kwa uzito; Dar es Salaam inachukua takribani zaidi ya asilimia kumi ya Wananchi wote wa Tanzania Bara. Kwa hali ilivyo, kama Dar es Salaam haitapewa nafasi maalum katika masuala ya mazingira, ni majanga. Majanga ya Dar es Salaam kutopewa mazingira maalum kwenye masuala ya mazingira, ni makubwa kweli kweli.

Nikihakikishiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba, Wabunge wa Dar es Salaam na wadau wa Dar es Salaam, katika *consultation* hiyo ya Sera ya Mazingira tutahusishwa, niko tayari kuachia shilingi katika eneo hilo. Naomba *commitment* yako Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sema tu kuwa umemkubalia. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala moja muhimu sana na mimi nitafurahi kwamba, idadi kubwa ya wadau ihusike, akiwemo ye ye mwenyewe Mheshimiwa Mnyika na Wataalam wengine. La msingi ni kwamba, mabadiliko ya tabianchi hayaathiri tu Dar es Salaam, yanaathiri dunia nzima, Tanzania nzima, Afrika nzima, kwa hiyo lazima tuyaangalie kwa upana wake si kwa kusema tu Dar es Salaam, lazima tuyaangalie kwa nchi nzima.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1004 - Government Communication Unit ....Sh. 259,256,000  
Kif. 1005 - Internal Audit Unit ... ... ... ... Sh. 239,685,000  
Kif. 1006 - Procurement Management... ... ... Sh. 251,521,000  
Kif. 1007 - Information and Communication  
Unit... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 244,371,000  
Kif. 1008 - Legal Services Unit... ... ..... Sh. 160,840,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila  
mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - Union Secretariat... ... ... ... Sh. 44,845,791,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Program 20 inayohusu Union Coordination kwa maana ya uratibu wa masuala ya Muungano, Kasma 221000 – Travelling-in-Country. Kiwango cha fedha kimeongezwa kutoka shilingi 126,000,000 mpaka Shilingi 158,000,000 na kwenye maelezo, pamoja na kuwa kwenye maeneo mengi vifungu vya Wizara hii havijaongezwa kwa sababu ya ukomo wa bajeti, lakini hii imeonekana ni muhimu kwa sababu ya safari za kuratibu masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimetishwa kidogo na hii nyingeza, katika mazingira ambayo Ofisi ya Makamu wa Rais kuitia kwa Makamu wa Rais, wakati wa uzinduzi wa mbio za Mwenge imesema kwamba itaratibu, itashiriki, kwenye masuala ya kura ya maoni juu ya jambo la Katiba mpya. Katika jambo hili, tayari Makamu wa Rais anajulikana msimamo wake na msimamo wa ofisi yake unajulikana.

Naomba nipate ufanuzi ni kwa nini katika kipindi hiki tete ndipo pesa za kuzunguka Makamu wa Rais zimeongezwa? Kwa vyovypote vile, kama sitapewa ufanuzi wa kuridhisha, nitaondoa shilingi kwenye eneo hili kwa sababu bila hivyo pesa hizi zitatumika kujaza mafuta ya kwenda kufanya propaganda kwa kisingizio cha kuratibu masuala ya Muungano. Naomba ufanuzi. (Makof)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ziko kwenye Fungu 31 na si *Private Office* ya Makamu wa Rais. Fungu 31 ujisoma Kitabu chetu cha Bajeti, kwa mwakani tumeji-commit kufanya kazi na RCCs na Mabaraza ya Ushauri ya Wilaya. Kwa hiyo, hiyo italazimisha Maafisa katika Kitengo changu kufanya safari nyngi za ndani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafahamu tofauti kati ya fungu binafsi la Makamu wa Rais pamoja na Idara ambazo bado ziko chini ya Makamu wa Rais. Kwa heshima ya Makamu wa Rais sikushika kifungu

kule, ningeliweza kushika kule lakini nimeshika kwenye idara kwa sababu hawa ndiyo watendaji wataoratibu masuala haya.

Majibu ya Mheshimiwa Waziri ndiyo yametisha zaidi, kwa sababu iko vilevile kwenye Hotuba yake, anasema bayana kwamba; masuala hayo ya Muungano watakenda kuyafanya. Ukishasema unakwenda kutumia RCC maana yake unakwenda kutumia Chombo kinachoongozwa na Mkuu wa Mkoo. Chombo hiki katika maeneo ambayo kuna wabunge tofauti kinaweza kikawa na mwafaka, lakini katika maeneo ambayo ni Wabunge wa Chama kimoja, unakwenda kutumia Baraza la Chama kimoja, Mkuu Mkoo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama cha Siasa, kwenda kupenyeza propaganda za kisasa kwa mwaka mzima kuelekea kura ya maoni. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halikubaliki na ninaomba nipewe nafasi ya kutoa hoja ya kuondoa shilingi. Afadhali kama ni elimu, kama ni uratibu wa masuala ya Muungano, tutengeneze mfumo, kuna kero nyangi za Muungano zinahitaji Makamu wa Rais. Watu wa Idara ya Makamu wa Rais wasafiri washughulikie kero hizi ambazo kuna mgongano wa kauli namna ya kuzishughulikia. Sasa badala ya kushughulikia kero za Muungano, mnakwenda kuzunguka kufanya propaganda za Muungano wa Serikali Mbili. Jambo hili haliwezi kukubalika kufanya kwa kutumia fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa shilingi jambo hili lijadiliwe pesa hizi zihamishwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, nimekuelewa. Ukitosha hii randama inajieleza vizuri tu, Kasma hii ilitengewa Shilingi 126,030,000. Kiasi hicho kimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kutoa elimu kwa umma, *simple as that*. Sasa Mheshimiwa Mnyika ndugu yangu toka jana, juzi, ni hela za CCM, leo umekuwa mwenge na Serikali mbili. Jamani samahanini, nikisema mimi naomba mkae kimya wote. Ninachokuomba mimi, tunaye CAG anayekubalika Kimataifa na anakagua hesabu zote hizi, akiona popote pale pesa imekuwa *missused* na tumeona kwenye ripoti yake pesa ambazo zimetumiwa vibaya, anaandika na anaikemea Serikali.

Mimi nakuomba Mheshimiwa Mnyika, kubaliana na kifungu hiki kipite na urudishe shilingi yako, tutashirikiana mimi na wewe Wabunge wa Dar es Salaam, kufuatilia. Hii ni elimu wala siyo kampeni, nakuomba.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakuheshimu sana na kule Dar es Salaam kwenye RCC mambo kama haya ni wazi tutayazuia, lakini hatuna uwezo wa kuzuia kwenye mikoa mingine na maeneo mengine. Sasa kwa manufaa ya watu wengine, kwa manufaa ya nchi...

**MWENYEKITI:** Mimi nakushukuru umeshatoa tahadhali na sasa Serikali imesikia...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa ufupi sana; mtu aliyeng'atwa na nyoka akiona unyasi hufanya nini? Sawa sawa, tayari Ofisi ya Makamu wa Rais imeendesha makongamano ya wanafunzi wa vyuo vikuu imefanya propaganda, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendesha makongamano ikitumia pesa za walipa kodi wa nchi hii, ikialika watu kwa kuangalia vyama vya siasa, kwa kufanya propaganda. Sasa kama kwenye makongamano tayari tumeshaona dalili, itakuwaje nchi nzima kwenda kukaa na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kwenda kutengeneza mtandao nchi nzima kufanya propaganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi hii ina mambo ya muhimu zaidi, pesa za mazingira zipo chache, pesa za kushughulikia kero za Muungano zipo chache, hakuna sababu ya kuendelea kuingiza pesa za kufanya propaganda. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika nimekuelewa, nakuomba, labda ungemwomba Waziri akupe *commitment*, kwa sababu mimi nafikiri tutashirikiana wote kuhakikisha pesa hizi zinafanya kazi ya elimu kwa umma, zisiende kufanya kazi yoyote nyingine. CAG naye anasikia vilevile na auditors wa Makamu wa Rais wanasi kudhibiti hiyo. Nakushukuru kwa uungwana wako. Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naongelea Subvote 2001, kifungu kidogo 220800 - *Training Domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka ...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa, kifungu kipi?

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sub-vote 2001, kifungu kidogo 220800 - *Training Domestic*.

**MWENYEKITI:** Okay! Yes, kuna milioni tatu hapa.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka unaoishia ilitengwa shilingi 18,000,000. Mwaka huu kifungu hiki kimetengewa shilingi 3,000,000. Mheshimiwa Waziri, katika Hotuba yake amekazia sana kwamba elimu zaidi inahitajika na kifungu hiki nadhani kinazungumzia kuhusiana na mafunzo. Kwa nini kipindi kilichopita ni zilitumika shilingi 18,000,000 sasa hivi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kimewekewa shilingi 3,000,000 tu; shughuli ambayo ni muhimu sana? Naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka wa jana tulikuwa na milioni 18 kwa *training domestic*, lakini ya *staff* ndani. Mwaka huu tungependa kuwa na nyingi zaidi, lakini kwa sababu ya ukomo wa bajeti tumepata hizi. Ukiangalia mpango wetu wa mafunzo, hatutaathirika sana kwa mwaka huu kwa *training domestic*. Kwa hiyo, elimu anayoizungumzia Mheshimiwa riziki ni ile elimu ya umma ambayo ndiyo tumeweza pesa nyingi, lakini hii ni elimu ya ndani ya *staff*.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hata kama ni hawa *staff*, kwa sababu tunachozungumzia hapa ni *training* na hawa wakipata *training* nzuri nadhani na ofisi yake inaweza ikafanya kazi vizuri. Anasema ni ukomo wa bajeti ndiyo uliofanya kutengewa bajeti hii ndogo sana, lakini sikatai nakubaliana naye, Mheshimiwa Waziri, aone kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kitengo hiki kutengewa fedha za kutosha ili kuweza kufanya kazi inayohusika kufanyika. Wao wakiweza kupata *training* ndivyo ofisi yake inavyoweza kufanya kazi vizuri na *training* ikaweza kwenda vizuri pia hata kwa umma. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Sawa sawa. Mheshimiwa Waziri umesikia hoja hiyo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 5001- Environment... .... .... .... .... .... .... .... 6,114,479,000

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nipo katika sub-item 220100, inayohusu *Office and General Supplies and Services...*

**MWENYEKITI:** Samahani, soma tena.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo sub-item 220100, inayohusu *Office and General Supplies and Services*.

**MWENYEKITI:** 108?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Tuko Subvote 500.

**MWENYEKITI:** Si ndiyo total 108,000,000.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Okay, tuendele.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana kulikuwa na fedha *almost* 35,800,000, lakini mara hii imeombewa 108,000,000, ni ongezeko la mara tatu ya fedha ambayo ilitengewa mwaka wa jana. Nataka maelezo ya ufanuzi kwa nini imezidi kiwango kikubwa kama hiki?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha pale zinaonekana zimeongezeka, sababu kubwa ni kwamba, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inaagiza uanzishwaji wa Mfuko wa Mazingira na Baraza na Rufaa. Tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha ili tuweze kuanzisha Baraza la Rufaa na Mfuko wa Mazingira, ndiyo maana pale pana fedha nyingi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, inawezekana anafahamu umuhimu wa uwepo wa Mfuko wa Mazingira ambao umeombwa sana na Waheshimiwa Wabunge hapa.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsuhukuru kwa majibu yake, lakini amezungumza kwa jumla, naweza kupata uchambuzi kidogo?

**MWENYEKITI:** Semeni Mabaraza ya Mazingira Wilaya ya Unguja, Pemba, Zanzibar, Dodoma, Mwanza. Majibu rahisi tu jamani haya. (Kicheko)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nichukue Mfuko wa Mazingira; tunatakiwa kwanza tuwe na Bodi ambayo itatakiwa kuwa na vikao; tunatakiwa tuwe na ofisi kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira, kwa hiyo, kuna shughuli ambazo zimetengwa ili iweze kufanya kazi. Inatakiwa vilevile Mfuko wa Mazingira hiyo Bodi yake ikae na iainishe namna huo Mfuko unavyoweza kufanya kazi ili hatimaye uweze kutekelezwa. Vilevile kwenye Baraza la Rufaa ambalo kama utafahamu, watu wengi wamekuwa wakilalamika baada ya kukosa *Environmental Impact Assessment*, hakuna kwa *ku-appeal* baada ya Waziri kutoa rufaa. Tunadhani Baraza hili ni muhimu liwepo ili kutekeleza sheria.

Kwa hiyo, kuna mahitaji mengi ambayo Mheshimiwa Mbunge akihitaji tutayaainisha ili aweze kuyaona wakati wa utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Pamoja na *compliance*, watakaoharibu mazingira wote wanakamatwa wanapelekwa mbele ya sheria. (Kicheko)

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapitisha fedha na ninashangaa kwa nini Mheshimiwa Waziri hana randama, matumizi yote yamewekwa *break-down!* Kwa nini anashindwa hata kutoa *figure* ya huku tunatoa kiasi gani na huku tunatoa kiasi gani, anatoa mambo ya jumla tu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mnayo randama hapo? Soma.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mhesihmiwa Mbunge kuwa tutampatia kwa sababu itahitaji *details* ambazo sasa hivi sina. La msingi ni hilo kwamba, Vyombo vyaa Mfuko wa Mazingira ni vikubwa na vinahitaji maandalizi na Baraza la Rufaa nalo ni kubwa. Ningedhani pengine angetupongeza kwamba, toka sheria imeanza mwaka 2004, leo ndiyo tumefanikiwa kuanzisha Mfuko wa Mazingira na Baraza la Rufaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid nafikiri ni...

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana Mheshimiwa Waziri anakuja hapa hayuko kamili. Tunapitisha fedha, huenda fedha hizi hazina matumizi, kwa hiyo, mimi naondoa shilingi mpaka atuhakikishie kwamba fedha matumizi yake ni nini. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya, umetoa Shilingi, hakuna mchangiaji, ninawahoji. Mheshimiwa Waziri, hebu mjibu halafu ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe mchanganuo kama ifuatavyo:-

Kutakuwa na office consumables ambayo ni 45,000,000, kutakuwa na vifaa vya computer na accessories kwa ajili ya kazi hiyo kwa hayo Mabaraza mawili shilingi 11,100,000, kutakuwa na masuala ya newspapers na magazines shilingi 4,770,000, tutakuwa na masuala ya printing and photocopy machines shilingi 43,500,000, tutakuwa na masuala ya clean supplies kwenye hizi ofisi mbili 4,000,000. Jumla 108,976,000. (*Makofii*)

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna newspapers mimi nadhani zinakwenda katika masuala ya information kwa nini anaiweka kule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid, wewe Kiongozi mkubwa sana humu ndani na una heshima yako humu ndani na jamii; kwa hiyo umeridhika? Mheshimiwa Mnyaa! (*Kicheko*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye Subvote 5001, Kifungu 270200 - Current Grant to International Organization na Kifungu 270800 - Current Grant to non-Financial and Public Units.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza katika vifungu hivi, nimejaribu kutazama ufanuzi wake wa kina ndani ya randama havimo kabisa. Sasa inakuwaje huku kuna maelezo, kuna pesa mwaka wa jana zilizotumika, kuna pesa zinazoombwa ambazo ni shilingi 3,832,091,000 lakini sasa kwenye randama hazionekani kabisa? Wakati huo huo katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna huu Mfuko wa Mazingira ya Dunia (*Global Environmental Facility*), kuna shilingi 649,629,929,000 ambazo matumizi yake zimekwenda kwa vikundi vidogo vidogo vya mazingira, ambavyo vimetajwa 35. Halafu akatupeleka kwenye Kiambatisho Namba Mbili cha Hotuba yake, nimetazama pesa hizo hakuna hata Shilingi moja iliyopelekwa popote Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye maelezo yake Zanzibar imo na ukizama katika Kiambatisho Namba Mbili hatuzioni zimekwenda wapi? Sasa mimi nilitaka ufanuzi, atupatie ufanuzi wa kutosha; katika uharibifu wa mazingira ukanda kutoka Makunduchi, Jambiani, Paje, Bwejuu, Chwaka, Urowa, kote ukanda wa Pwani unaharibika kila mwaka takribani mita moja bahari inakula kule, hatukuona kinachofanyika kwa miaka kumi zaidi sasa hivi.

Ukienda Pemba makaburi Kisiwa Panza ya kale yote yameng'olewa baharini na bahari inakuja juu. Hii *environmental* kwa nini itumike upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano? Yale yale kila siku tunayoyakataa, atuambie fedha ngapi zimekwenda anzibar? Mimi nataka maelezo, ahsante. (*Makofij*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu lake dogo tu, mwambie Zanzibar zinakwenda ngapi, Pemba zinakwenda ngapi na Bara zinabaki ngapi. Mheshimiwa Waziri (Muungano)! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nisiwe na *figure* hapa za ngapi zimekwenda wapi, lakini katika Mfuko wa GEF Zanzibar Nungwi wamefaidika Miradi ya Maji, lakini pia Pemba kuna miradi ya Mfuko huu wa GEF. Kwa hiyo, naweza nikawa sina *figure* ngapi na ngapi lakini Mfuko huu unatumika maeneo yote. Inawezekana katika randama sijui kwa nini haionekani au hizi ni fedha ambazo zinapitia UNDP hazionekani hapa.

**MWENYEKITI:** Hizi ni katika zile *international donors*. Ehee, Mheshimiwa Mnyaa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hizi story za kwamba, Pemba, wapi, Zanzibar zimefungwa, ukiacha hiyo aliyoitaja physically, kuna Miradi mwaka wa 15 tunatajiwa ya Mkumbu, hakuna chochote kinachofanyika. Haya ni maneno kila siku tunaambiwa! Sasa kwa nini asitueleze na kwa nini vitu kama hivi visiwemo kwenye randama na huku kwa nini kiwepo huku kwenye kifungu lakini maelezo katika randama hakuna?

Sasa hii Miradi mingine inaathiri kwa muda mrefu. Huo Ukanda wa Pwani ninaousema wa Urowa, Pwaje na Bwejuu, unaathirika kwa muda mrefu sana. Zipo process nyngi sana za kufanya, kwa nini pesa za environment siku zote Makamu wa Rais huyu zitumike upande mmoja; huyu Makamu wa Rais wa upande mmoja tu? (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nafikiri kuna wataalam wanaweza kutoa msaada, hebu jaribuni kuwaliza. Ninashangaa wataalam, wanaacha mnateswa wao wamekaa tu pale.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema kile kifungu cha 270800, ambazo ni fedha za ruzuku ya NEMC. Tunapozungumzia fedha za GEF, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mnyaa kwamba, pesa hizi hazitumiki upande mmoja. Katika Hotuba yangu, tulisema kwamba, fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya Miradi midogo midogo. Sasa hivi ofisini kwetu kuna Miradi mitatu kutoka Zanzibar; Mradi kutoka Kaskazini maeneo ya Matemwe na Pwani Mchangani kuna Mradi kutoka Pemba na kuna Mradi kutoka Kusini ya Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ufundi wa fedha hizi ni kuombwa. Ukiomba na Mradi ukitimiza vigezo fedha hizi zinakwenda. Ninataka niseme kwamba, kwa mwaka 2013, kuna fungu kubwa la fedha lilikwenda kwa ajili ya Mradi wa Kujenga Ukuta Eneo la Kikwajuni mjini Zanzibar, fedha zile hazikutumika. Baada ya kufika SMZ, fedha zile zikabadiishiwa matumizi na zikatumika katika Miradi mingine hasa katika Kisiwa cha Pemba. Kwa hiyo, fedha hizi zinatumika pande zote.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimwia Mwenyekiti, hizi ni hadithi za halikudiki, kwa sababu Kisiwa Panza imetajwa zaidi ya miaka minne, mitano, uharibifu wa mazingira uliong'oa makaburi ya kale. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimwia Mnyaa, katika hatua hii sasa hatuna mjadala. Tuwapo katika hatua hii ni kusema tu wewe umeyakataa maelezo ya Waziri na unaikamata shilingi yako, tumtafute mtu mwengine naye achangie kama hakuna tunahoji Bunge.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Wapo wachangiaji tele.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa Panza, si Mradi ambao umetajwa katika Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kama umetajwa basi umetajwa katika SMZ, lakini kwetu hatuna Mradi wa Kisiwa Panza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyaa. Vilevile ninasema kwamba, kama alivyoanza yeye kwamba, hizi ni hadidhi kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza mwanzo kwamba, kuna hadithi za halikuniki. Inaonekana halikuniki, ni yeye mwenyewe katika hili. Kutokana na hilo na yale yote ambayo tumeongea hapa. Kwa kweli hizi fedha ni lazima zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyaa. (Makofij)

**MHE. DKT. TEREZYA P.L. HUVISA:** Mheshimwia Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafsi hii. Mimi ninaomba niwaambie wenzangu wa Zanzibar kwamba, Mfufo wa GEF uko mara mbili; kuna Mfuko mkubwa amba Mheshimiwa Fatma Fereji anajua, kuna pesa zilizopelekwa Zamzibar kwa ajili ya kujenga hizo kuta ufukweni. Hizi zilizosemwa hapa ni Miradi midogo midogo ya GEF, inayotangazwa kwenye Magazeti, mnatakiwa msome magazeti muombe. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha!

**MHE. JOHN J. MNYIA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika kaa.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Fedha!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika kaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata mchanganuo wa Miradi ya GEF. Katika mchanganuo huo unaonesha kwamba, Zanzibar kuna ukarabati wa ukuta wa mita 400 wa Kisiwa Panza hiyo anayoisema na Bwawani mita 119 pale Zanzibar, ambayo ni shilingi 261,900,000. Kuna uboreshaji wa Mikoko, hekta 50 Tumbe, hekta 100 Ukele na 260 Kisiwa Panza huko anakokusema, hekta 50 Bwawani pale Unguja ambayo ni shilingi 62,104,000.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kusema kweli sijaridhika na haya majibu. Kwa sababu gani?

**MWENYEKITI:** No, no, kama hujaridhika unakaa tu na tunahoji Bunge.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nikueleze basi, la hutaki niseme basi nitakaa.

**MWENYEKITI:** Kama hujaridhika kaa tulihoji Bunge. Hujaridhika ukaanza na maneno, ndiyo utaratibu ulivyo. Jamani mimi msinihukumu hapa, unapohukumiwa kwenda kunyongwa, nikiwa ninanyonga unanilalamikia mnyongaji, hapana, mimi ninafuata kanuni. *I am guided by these rules na ninazifuata na nitaendelea nazo. (Makof)*

Sasa nitawahoji muiamue hoja kwamba, Mshahara wa Waziri uzuiwe. (Kicheko/Makof)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 - Administration and General ... ... Sh.1,530,000,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kila mwaka huwa ninajohi kuhusu hiki Kifungu na ni kwa sababu majibu huwa hayaridhishi. Huu ni Mradi, uko Kifungu cha Utawala, lakini unahu ujenzi wa Ofisi za Makamu wa Rais na kuna Kasma mbili; Kasma 6309, ambayo mwaka 2012 ilitengewa shilingi 50,000,000, mwaka 2013 ilitengewa shilingi 500,000,000 na mwaka 2014 shilingi 400,000,000.

Kasma nyingine iko pale, mwaka 2012 ilitengewa shilingi bilioni 1.6, 2014 shilingi bilioni 2.1, mwaka 2011 bilioni 2.4, jumla shilingi bilioni 5.0. Kwa hiyo, ukijumlisha shilingi bilioni 5.0 na hizi bilioni nyingine moja nukta kadhaa, unakuta pesa zinazotengwa kila wakati kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Ofisi Makamu wa Rais ni zaidi ya shilingi bilioni 7.0 au milioni 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungelipenda kuelezwaa inawezekana tunapotenga pesa mwaka fulani, pesa hazitoki. Kwa hiyo, kama hazitoki, maana yake sasa itabidi tuihoji Wizara fedha kwa nini fedha hazitoki. Kama tunapotenga pesa zinatoka, itapaswa Serikali ijieleze, Ofisi ya Makamu wa Rais; hizi ni ofisi gani zisizoisha? Ofisi gani, matengenezo hayakamiliki tukafikia hatua tukasema kiwango cha pesa ambacho tunatenga kwa ajii ya ujenzi wa hizo ofisi sasa kipungue. Maana yake tusipodhibiti hapa kila mwaka tutaletewa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

bajeti ya ujenzi kumbe kuna watu wanakula cha juu kila wakati kwenye ujenzi. Kwa hiyo, ninaomba ufanuzi na kama hautaniridhisha nitaondoa shilingi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hoja iliyopo ni kwamba, pesa hizi zinatoka miaka yote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, unapoomba Bajeti ni Bajeti, kuna miaka ambayo pesa hii hatupati. Mwaka 2012/2013, pesa hii hatukupata. Miradi hii iko miwili; kuna Mradi wa Tunguu na kuna Mradi wa Ofisi ya pale Luthuli, ambayo tumemaliza. Fedha zilizotengwa mwaka huu ni *mainly* kwa Luthuli kulipa *instalment* ya mwisho ya Mkandarasi baada ya kukubali kupokea jengo. Pia kuna 400,000,000 alizozitaja ni kwa ajili ya manunuvi ya samani ya Ofisi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, pesa hazikutoka!

**MHE. JOHN JOHN MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kurudisha shilingi ya Waziri. Tungeliomba *commitment* kutoka Wizara ya Fedha, hii Miradi tunapojenga taratibu gharama za Mradi zinazidi kupanda kwa gharama za walipa kodi wa nchi hii. Kwa nini tusijenge tukamaliza tukafanya kazi nyininge?

Wizara ya Fedha watupe *commitment* kwamba, sasa ni kama vile Makamu wa Rais haheshimiwa hivi, Ofisi yake ndiyo ambayo inachukua muda mrefu kweli. Ofisi ya Rais hapa tuliona, ukarabati wa Ikulu. Ikulu ya wapi, kiwango cha pesa kilichokuwa kinatolewa *compliance* yake iko juu. Kwa nini kwa upande wa Makamu wa Rais *compliance level* haiko kwa kiwango hicho tumalize hii kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *commitment* ya Wizara ya Fedha au Sera, Uratibu na Bunge, ninaona Mheshimiwa Lukuvi amenyoosha mkono ili tupate *commitment* ya upande wa utoaji wa pesa.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Fedha, kuna *commitment* mtajitahidi Wahisani? (Kicheko)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani fedha zinazopopatikana kama zilivyo tuna-disburse; ukiona hapa kuna division ya fedha na hii si kwa sababu ya Ujenzi tu wa ofisi.

**MWENYEKITI:** Nimesema hivyo, maji, hospitali. *This is the problem we are facing.*

**WAZIRI WA FEDHA:** Exactly, sisi wote tumesikia. Kwa hiyo, ndiyo tunaona kwamba ile consequence ina-cut across.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru.

**WAZIRI WA FEDHA:** Tunapopata tunatoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru. Kifungu hiki kinaafikiwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana.

(Kifungu kilichotajwa hapa juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - Policy and Planning Division ... ... ... Sh 600,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 5001 - Environment ... ... ... ... ... Sh.4,432,746,00

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Kasma 5301 – Climate Change Adaptation Program. Mwaka huu wa fedha kimetengewa Shilingi 353,000,000 fedha za ndani na shilingi bilioni moja fedha kutoka UNDP, fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ni kwa ajili ya kufanya mipango ya kuingiza masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mikakati na Miradi ya Nchi. Miradi iliyotajwa, ambayo wanasema tume-stream climate change ni Miradi ya Kilimo na Miradi ya Ufugaji. Sina tatizo na Miradi ya Kilimo na Ufugaji, kwa maana ya Climate Change kuwa mainstreamed, kwa sababu wafugaji na wakulima wanaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari kubwa zaidi ya mabadiliko ya tabianchi ni kwenye Sekta ya Maji na Sekta ya Nishati ambazo ndiyo roho ya Taifa hili. Sasa hivi tunavyozungumza, Dar es Salaam kuna shida kubwa sana ya maji. Sababu zinazosababisha Dar es Salaam, kuwa na shida ya maji ni kwamba *line* yote hiyo ya Ruvu Chini na Ruvu juu, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, *flow* ya maji kuingia katika Miradi ya Ruvu Juu na Ruvu Chini imepungua. Ndiyo maana

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

sasa hivi tunafikiria kujenga Bwawa la Kidunda Morogoro ili walau kuyashikilia maji kwa muda na kuyasukuma kuelekea katika maeneo hayo.

Nimeshangazwa na Mradi huu muhimu, kutokuweka kabisa Sekta ya Maji na Sekta ya Nishati. Pamoja na kuwa tunasema tuna mgao wa umeme, tuna matatizo ya umeme, kutokana na matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi. Vyanzo vya Miradi ya Umeme wa Maji, vinaathirika. Ningelipenda kupata commitment ya Waziri kwamba, watakwenda kurekebisha ili Sekta za Maji na Sekta ya Nishati ziingizwe kama sehemu ya Mradi huu wa ku-mainstream suala la mabadiliko ya tabianchi katika utekelezaji wa Miradi na upangaji wa Miradi. Ninaomba ufanuzi kuhusu jambo hili na kama sitaridhika nitaondoa shilingi.

**MWENYEKIT:** Inahitajika commitment kutoka kwako Mheshimiwa Waziri na ni hoja ya msingi vilevile.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaongelea maji na ukatatua tatizo la wafugaji, maana yake umetatua tatizo la maji. Kama unaongelea maji na ukaweka vizuri suala la kilimo, maana yake umelinda vyanzo vya maji. Kwa hiyo, ni mikakati ambayo inategemeana. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, hatuchagui maeneo, tunachukua maeneo yote. Sasa hivi tumefanya kazi na wenzetu wa Nishati na Madini ili kuandika Policy ya namna ya kutumia hizi bio-fuel na vitu vingine na tumetoa fedha. Kwa hiyo, tunafanya maeneo yote kulingana na upatikanji wa fedha pamoja na Sekta hii ya Maji. Kwa hiyo, sioni kama kuna tatizo lolote lile kwenye hili.

**MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina kifungu kingine kidogo cha mambo ya Ozone Layer.

**MWENYEKITI:** Wewe si ulikuwa huko huko jamani, haya tuendelee!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nime...

**MWENYEKITI:** Hapana, subiri tu Mheshimiwa Mnyika. Mheshimiwa Huvisa!

**MHE. DKT. THEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza nikachangia kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba, Miradi inayohusu Maji ipo kwenye Sekta ya Maji na wao wana vipengele vya kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, siyo lazima vifungu vyote vitokee hapa. Ofisi ya Makamu wa Rais, inafanya kazi na Sekta nyingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika umeridhika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sehemu ya Mradi. Ukiangalia Miradi mingine inayofuata, huu ndiyo Mfradi ambao umetengewa pesa nyingi kuliko Miradi mingine yote. Huu ndiyo Mradi ambao Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa maana ya UNDP, limeingiza mguu wake na mikono yake kwa kiwango kikubwa kuisaidia nchi yetu. Sasa haiwezikani Mradi mkubwa namna hii na mzito, nimesoma kwenye randama, ukurasa wa 46 wa randama unasema; kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika Sekta za Kilimo, Misitu na Mifugo. Maana yake ni nini? Mradi ukibakia hivi, bila kutaja Sekta nyingine, mtekelezaji wa Mradi atajikita peke yake kwenye kilimo, misitu na mifugo.

Ninakubaliana kuna maeneo ambayo uharibifu wa mazingira unaosababishwa na kilimo ama unaosababishwa na mifugo, una athari katika Miradi ya Maji na Miradi ya Umeme, lakini siyo sehemu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Dar es Salaam, sasa hivi tunapiga kelele Bwawa la Kidunda lililopo Morogoro, liharakishwe kujengwa, ili lihimili maji pale Kidunda Morogoro, maji yasukumwe Dar es Saalam, Dar es Salaam tupate maji kwa wingi. Pale Kidunda hakuna uhusiano wowote na suala la mifugo na kilimo. Sana sana kinachotakiwa ni Serikali kulipa fidia kwa Wananchi, Wananci waondolewe Bwawa lijengwe. Siyo suala la kilimo wala mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye vyanzo vingine vyaa umeme nchi hii, kuna vyanzo ambavyo encroachment ya wakulima na wafugaji siyo issue. *Issue ni mambo* mengine ambayo tunaihitaji Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kama sehemu ya mkakati wa mabadiliko ya tabianchi. UNDP wakitusaidia uzoefu wa Kimataifa, tuingize tu maneno hapa kirahisi tu, tuongeze sekta hapa tutaje Sekta ya Maji, tutaje Sekta ya Nishati, tumemaliza. Hilo tu ndiyo ninaloliomba. Nitamrudishia shilingi yake akitekeleza hilo.

**MWENYEKITI:** Yeye anataka commitment tu basi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna athari za mabadiliko ya tabianchi, ambayo inaendelea kuwa mbaya. Katika kila Mradi wa Maji, tunauanza baada ya kutathmini ni jinsi gani Mradi huu utaathiri mazingira na utakuwa wa kijamii. Tunafanya hivyo tuangalie pia na athari hiyo kwa jinsi mazingira yanavyobadilishwa na tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kidunda hivi sasa tunapitia upya athari za mazingira na athari za kijamii kwa sababu hiyo na Miradi yote tunafanya hivyo. Kisera, Baraza la Mazingira linatoa Sera ambayo Wizara zote sisi tunafuata na kuhakikisha kazi hizi zinatekelezwa kwa kuzingatia hali ya mazingira kwa sasa na huko mbele.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Maji, hata kwenye Miradi ya Nishati na Madini, Ofisi ya Makamu wa Rais ni Coordinator na sisi tunaweka Bajeti za Mazingira. Huwezi kuanzisha Mradi wa Nishati bila kufanya tathmini ya athari za mazingira na tunaweka Bajeti. Miradi ya Migodi ikianza lazima kuwe na Bajeti na athari za mazingira zinafanyiwa tathmini. Kwa hiyo, hii Bajeti iliyowekwa hapo kama coordinator na Wizara nyingine zote tunaweka bajeti kwa ajili ya kuangalia mazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, ninafikiri ni majibu wa kutosha tu hayo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshikiwa Mwenyekiti, ninasikitika Mawaziri hawa wawili, mimi nimetoa hoja ya kuwasaidia wao; wao wamejibu kitu tofauti kabisa. Waziri wa Maji na Waziri wa Nishati, wamejibu vitu tofauti. Wanazungumzia ....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, hitimisha hoja yako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Wanazungumzia, ninaomba nimalize.

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni kwamba, sijasema hapa kuhusu haja ya kufanya *Environmental Impact Assessment*, sijazungumzia hilo kabisa. Hilo siyo hoja yangu. Hoja yanugu ni nini? Kuna tatizo katika nchi yetu la mabadiliko ya tabianchi, hapa tumepewa mabilioni na wahisani na tumetenga pesa za ndani za walipa kodi, tunataka Miradi ya Maji na Miradi ya Nishati, nayo iwe mainstreamed. Katika utekelezaji wa Miradi, tunapopewa ushauri wa kitaalam na kila kitu hapa tutengewe pesa. Ninataka kuwasaidia hawa Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, muda wako umekwisha, una hoja ya msingi, majibu uliyopewa hukuridhika nayo. Sasa ninakupa haki ya kulihoji Bunge. Unless, kama Serikali mnayo commitment yoyote nyingine? Hamna. Sasa nitalihoji Bunge.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Hoja ya Mheshimiwa Mnyika ya kuondoa shilingi ilikataliwa na Bunge)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Fedha za Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 26 - Ofisi Binafsi na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na (Mazingira), kwa Mwaka wa Fedha 2014/205, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofii)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji kwamba, sasa Bunge likubali kupidisha Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na (Mazingira), kwa mwaka 2014/2015.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais  
(Muungano) na (Mazingira) kwa Mwaka 2014/2015  
yalipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Bajeti imepita. Mheshimiwa Esther Bulaya!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

## MAELEZO BINAFSI YA MHESHIMIWA MBUNGE

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Sasa naomba nisome maelezo yangu binafsi ya kuitaka Serikali kuchukua hatua ya dharura kukarabati mashine ya mionzi ya saratani katika Hospitali ya Ocean Road.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013, napenda kutoa maelezo binafsi juu ya tatizo la msingi la dharura katika nchi yetu kuhusu mashine mbili za mionzi ya saratani (*Computed Tomography Scan – CT Scan*) katika Hospitali ya Ocean Road kuharibika kwa takribani miezi miwili sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saratani ni tatizo kubwa sana ulimwenguni na hasa katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, ambapo takwimu za kimataifa zinaonesha kuwa kila mwaka zaidi ya watu milioni tano hugundulika kuwa na saratani na kufanya tatizo hilo kukua na kufikia 29% kila mwaka, huku wengi wao wakipatikana na Saratani ya Mlango wa Kizazi ambalo ni tatizo kubwa sana hasa kwa akina mama wa Tanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za magonjwa za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2010 zinaonesha kuwa, Ugonjwa wa Malaria uliuu watu 500,000, Kifua Kikuu uliuu watu milioni 2.1, UKIMWI uliuu watu milioni 1.8 na Saratani iliongoza kwa kuua watu milioni 9.9 Hivyo, Ugonjwa wa Saratani ni tatizo na tishio kwa sasa Duniani na katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua na ninapongeza jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuwa, matibabu kwa wagonjwa wa saratani yanapatikana bure hapa nchini. Uamuzi huo wa Serikali unatokana na ukweli kwamba, gharama za matibabu za ugonjwa huu ni kubwa na ghali kwa Mtanzania wa kawaida kuweza kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Ocean Road ndiyo kubwa na inayotegemewa kwa kutoa tiba bora za saratani hapa nchini. Pia natambua kuwa mashine za mionzi za Ocean Road ndiyo pekee zinazotoa tiba hasa kwa wagonjwa mbalimbali kutoka mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Ocean Road kwa sasa inakabiliwa na ongezeko la wagonjwa wa Saratani kuliko uwezo wake wa kuhudumia wagonjwa hao. Tatizo hili limepelekea mashine za mionzi ya Saratani kuharibika mara kwa mara, kwani hivi sasa mashine hizo mbili zenye gharama kubwa zimeharibika kwa takribani miezi miwili sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Ocean Road mwaka 2009 ilikuwa na uwezo wa kuchukua wagonjwa wasiozidi 120 kutokana na idadi ya vitanda ilivyonyavyo. Hivi sasa Hospitali hii imeanza kuzidiwa kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wapya kutokana na idadi ya wagonjwa hao kuongezeka kila mwaka na kufikia wagonjwa 40,000 wanaohitaji tiba hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya idadi kubwa ya wagonjwa, Hospitali ya Ocean Road imekuwa ikiwarudisha wagonjwa wengine nyumbani bila

matibabu kutokana na uhaba wa vitanda na kuwataka ndugu zao kuwafikisha hospitalini hapo kwa ratiba maalum ya kukutana na Daktari au kupata tiba ya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matibabu ya Ugonjwa wa Saratani kwa kupitia mashine za mionzi huhitaji wagonjwa hao kupata huduma ya mashine hizo kila siku ili mgonjwa apate nafuu. Kuharibika kwa mashine hizi katika Hospitali ya Ocean Road ni janga la kitaifa na linahitaji hatua za dharura zichukuliwe ili kuokoa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waathirika wakubwa wa ugonjwa wa Saratani hivi sasa ni Wanawake. Wanawake wengi wanaathirika na Saratani ya Mlango au Shingo ya Kizazi. Tafiti zinaonesha kuwa, Wanawake 6000 hugundulika kuwa na Ugonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa, takribani Wanawake 4000 nchini kupoteza maisha kila mwaka kutokana na ugonjwa huo ambapo ni sawa na wastani wa Wanawake 11 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuharibika kwa mashine hizi katika Hospitali ya Ocean Road; nini hatima ya wagonjwa wa Saratani? Je, ni wagonjwa wangapi wa Saratani wanapoteza maisha kwa siku kwa kukosa huduma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla takwimu kutoka Hospitali ya Ocean Road zinaonesha kuwa 40% ya vifo hivyo vinavyotokana na matatizo ya Saratani ni wagonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi, ambao wengi ni wanawake. Takwimu hizi pia zikionesha kuwa 80% ya wagonjwa wote wanaokwenda kwenye matibabu ya Saratani ya Mlango wa Kizazi hufika hospitalini kupata huduma hiyo wakati tatizo limekuwa kubwa, hivyo kusababisha wengi kupoteza maisha kutokana na huduma hii kutotolewa katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la Saratani ni kubwa hapa nchini hasa kwa akina mama, ni lazima Serikali ishughulikie suala hili kwa umuhimu wa hali ya juu na kuhakikisha matibabu ya uhakika yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tiba ya mionzi inapoanza kutolewa kwa mgonjwa wa Saratani haitakiwi kusitishwa, pindi inaposhishwa husababisha vijidudu kuzaliana na tatizo kuongezeka au mgonjwa kupoteza maisha; na kwa kuwa tatizo la mashine hizo kuharibika limesababisha usumbufu kwa wagonjwa wa Saratani na tatizo la ugonjwa kuongezeka; na baadhi ya wagonjwa kupoteza maisha kwa kukosa tiba ya kuchomwa mionzi kwa takribani miezi

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

miwili; ninaiomba Serikali kushughulikia ukarabati wa mashine hizi kama jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa gharama husika za ukarabati wa mashine hizi ni takribani Tsh. Bilioni 8 na ukizingatia suala la usalama na uhai wa wagonjwa wa Saratani uko hatarini, ni vyema Serikali ikaliangalia kwa umuhimu wake hasa katika kipindi hiki cha bajeti ya Serikali kama jambo linalohitaji umuhimu na ucharaka wa pekee katika kunusuru maisha ya Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa idadi ya wagonjwa wa Saratani inazidi kuongezeka siku hadi siku katika Hospitali ya Ocean Road na mashine zilizopo kuelemewa, ninaiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kununua mashine nyingine kwenye mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la saratani linazidi kukua na wagonjwa kuongezeka ambapo wengi wao wanatoka mikoani; hivyo, kupelekea wagonjwa wengi kufika Hospitali ya Ocean Road wakati saratani imeishasambaa sana mwilini na kuleta madhara na hivyo kupoteza maisha, niishauri Serikali kununua mashine hizi za mionzi na kuzipeleka katika Hospitali Kuu za Kanda ili wagonjwa wa mikoani wapate huduma za matibabu katika mikoa yao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lukuvi!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali ningependa kusema kwamba, tumepokea hizi taarifa zote za Waheshimiwa Wabunge wawili kuanzia ile ya asubuhi; Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni na Mheshimiwa Esther Bulaya.

Hili jambo la mashine za X-ray tunalifahamu na tutafanya yote mawili, tutakuja kutoa taarifa, lakini wakati huo huo tumeshaanza kuchukua hatua. (Makof)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla hajaja hapa ameishakutana na wote wanaohusika, ameishajua tatizo, lakini Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, atakuja kutoa taarifa kuhusiana na hoja zote za Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni. Kwa hiyo, tumeipokea na tutakuja kuitolea maelezo na wakati huo huo hili la mashine za X-ray tunaendelea kulishughulikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika, dakika tano!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitaomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, nimeshakupa dakika tano, achana na mambo ya miongozo tena, wewe sema taarifa yako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kutoa taarifa ya dharura kwa Serikali juu ya dharura inayoendelea hivi sasa Dar es Salaam na Pwani katika maeneo yote yanahudumiwa na DAWASA kwa Chanzo cha Maji cha Ruvu Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi mitatu sasa, maeneo yote yanayohudumiwa na chanzo cha Ruvu Juu, nikisema hivyo ninamaanisha maeneo ya kutoka Chalinze, Mlandizi, Kwembe, Kibamba, Msigani, Kimara, Saranga, Ubungo, Makuburi, Segerea, Tabata na vitongoji vyake. Zaidi ya Wananchi wa Dar es Salaam na Pwani milioni moja wana shida kubwa sana ya maji. (Makofii)

Sasa maelezo ambayo yanatolewa na wanaoendesha shughuli ya maji Dar es Salaam kwa niaba ya DAWASA kwa maana ya DAWASCO ni kwamba, kumekuwa na uharibifu wa pampu katika chanzo cha Ruvu Juu, lakini kila wakati wanatoa maelezo hayohayo uharibifu wa pampu, uharibifu wa pampu Ruvu Juu, huku Wananchi wakiwa na shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki kabla ya mafuriko walikuwa wakitoa maelezo kwamba, kuna kina cha maji kimepungua. Baada ya mafuriko shida ya maji ikaongezeka zaidi, wakatoa maelezo kwamba mafuriko yamesababisha shida ya maji. Sasa Wananchi wa maeneo ya Chalinze, Mlandizi, Kibamba, Kwembe, Kiluvya, Saranga, Ubungo, Makuburi, Tabata na Segerea, wanashindwa kupata uelewa kabisa na kukubali kwamba, ni vipi ongezeko la maji ambalo lingepaswa kuwa neema ya kupata maji zaidi kwa Wananchi sasa ndiyo inakuwa sababu ya kuelezwu kwamba kuna shida kubwa ya maji katika kipindi cha miezi mitatu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la dharura kwa sababu Wananchi wa maeneo yote haya wanunua maji kwa gherama kubwa sana kwa sababu ya matatizo ya maji ambayo yanaendelea. Naomba katika hatua hii, Serikali itoe kauli Bungeni juu ya matatizo haya ya maji, chanzo halisi cha matatizo ya maji kujirudia rudia na kuwa makubwa kwa upande wa chanzo cha Ruvu Juu kinachohudumia maeneo haya niliyoyataja, chanzo halisi ni nini hasa? Kama chanzo hicho ni sababu inayotolewa ya kuharibika mara kwa mara kwa pampu, nini kinachofanya kwamba pampu inayoharibika mara kwa mara ni ya Ruvu Juu na siyo ya Ruvu Chini? Kuna nini hapo kilichojificha Serikali

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

iweze kutoa majibu ya kina kwa sababu Wananchi hawaelewi kabisa maelezo ambayo yanatolewa na DAWASCO upande wa nje ya Bunge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo Serikali inapaswa kutoa kauli kwa mujibu wa Kanuni ya 49. Kama maelezo ya ziada yatahitajika juu ya undani wa tatizo hili, niko tayari kuiandikia Ofisi ya Spika nipewe nafasi ya kuwasilisha maelezo binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 50. Jambo hili kuna ambao wanaamini kwamba, kuna mgogoro ndani ya DAWASCO hivi sasa na hivyo kuna hujuma katika mpango huu wa maji katika mtambo huu wa Ruvu Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili mambo yote haya yaweze kubainika, Serikali itoe kauli na kama haiko tayari kutoa kauli, basi nipewe nafasi ya kuwasilisha maelezo binafsi, niweze kuwasilisha undani wa jambo hili na vielelezo kutoka kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi!

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi yetu sisi kutoa ufanuzi kama Serikali pamoja na kwamba Kanuni aliyoitumia hairuhusu kusema hayo aliyosema, hii ya 68 aliyoitumia.

Mzee tunakuheshimu kwa sababu tunajua jambo lenyewe ni la maana na sisi Serikali tunaheshimu maelezo yake kwa sababu kama Serikali tunaosimamia utekelezaji wa huduma hizi, tuko tayari kutoa maelezo ndani na nje ya Bunge wakati wowote.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Maji atatoa maelezo ndani ya Bunge lako, lakini pia atapata nafasi ya kufafanua wakati wa bajeti yake.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Lukuvi si ungesema tu Waziri atatoa ufanuzi? (Kicheko)

Jamani kuna wageni wa Mheshimiwa Wasira, Ndugu Malagila na ujumbe unaojumuisha Wenyeviti wa vijiji vitatu vya Tahamu, Nyatwali na Serengeti, Wilayani Bunda. Hao ni wageni wa Mheshimiwa Wasira, wamekuja jioni; karibuni sana Dodoma.

Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

(Saa 1.53 usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 13 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)